HISTORIA YA MAPAMBANO YA MWAFRIKA



H. Mapunda

Boston
Public Library

Purchased with State Funds

T2 1986SP
35

HISTORIA YA MAPAMBANO YA MWAFRIKA

Lit
History of
Contact-or collisions
in Africa

includes explorers,
capitalism, etc...

DT 31
.M337

Historia ya Mapambano ya Mwafrika

H. Mapunda

TANZANIA PUBLISHING HOUSE
DAR ES SALAAM
1976

TANZANIA PUBLISHING HOUSE
S.L.P. 2138, Dar es Salaam

© H. Mapunda 1976

Chapa ya Kwanza 1976
Chapa ya Pili 1978
Chapa ya Pili 1979
Chapa ya Tatu 1980

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili kutafsiri, kupigisha chapa ama kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila ya idhini ya Tanzania Publishing House.

KUTABARUKU

Kwa wanamapunda, wanaAfronodi na wana-Afrika wote kwa mfungamano; na pia kwa wanaMapinduzi wote wanaojiingiza katika mapambano ya kutokomeza ubeberu, ukoloni na aina zote za unyonyaji kwa shabaha ya kuondoa unyonge na kuleta maendeleo na ustawi wa jamii katika dunia.

YALIYOMO

Sura *Ukurasa*

Dibaji ..... **ix**
Shukrani ..... **xi**
Utangulizi ..... **xiii**

1. Njia za kupatia maarifa ya historia za Waafrika 1
2. Mtu na mazingara yake 8
3. Suala la Afrika kuingiliwa na wageni 14
4. Suala la uhamiaji na uvamizi wa Kiafronodi 23
5. Suala la uvamizi katika Afrika ya Kusini 34
6. Mapambano ya Mfecane 41
7. Maendeleo ya jamii duniani kimfumo 53
8. Jamii za Kiafrika kabla ya ukoloni 70
9. Biashara ya watumwa na maendeleo ya Waafronodi .. 79
10. Ubepari ni chanzo cha ubeberu, ukoloni na mgawanyo wa Afrika 95
11. Utawala na siasa ya kikoloni 111
12. Wamisionari na ukoloni: Viongozi wa dini wananchi na ujenzi wa mataifa yao 120
13. Uafronodi na juhudi za Waafrika kujikomboa kitaifa .. 136
14. Uhuru na maendeleo ya mataifa huru ya Kiafrika 155

Nyongeza A **174**
Nyongeza B **177**
Nyongeza C **178**
Nyongeza D **179**
Nyongeza E **181**

DIBAJI

Nimekubali kuandika dibaji kwa kitabu hiki kwa sababu kubwa mbili. Kwanza kabisa nilifurahia kitendo cha Ndugu Mapunda kuthubutu kuangalia somo la historia ya Afrika kwa jicho tofauti na jinsi ambavyo limeangaliwa na wataalam wengi mpaka sasa. Uamuzi wake haukuwa rahisi kwa sababu zinazojulikana. Mwanadamu kwa kawaida hupendelea kufuatia njia ya zamani kwa sababu haimlazimishi kufanya mabadiliko makubwa ama katika maisha yake na katika fikara zake. Lakini pia mwanadamu huyo huyo huwa tayari kupambana na mazingara yake iwapo usalama wake uko hatarini. Jitihada ya Ndugu Mapunda imeonyesha kwamba bado ipo nafasi kubwa ya kuchimbua zaidi historia ya bara letu na hasa kupata msimamo unaoambatana na maslahi ya watu wake. Msomaji anaweza asikubaliane na mwandishi wa kitabu hiki lakini hawezi kupuuza jitihada hii.

Na sababu ya pili inatokana na uamuzi wa kuandika kitabu hiki katika lugha yetu ya Taifa—Kiswahili. Kuna vitabu vingi vya mambo muhimu yanayowahusu Waafrika. Lakini karibu vyote viko katika lugha za kigeni. Hivyo wananchi wengi ambao hawajui lugha hizo ila Kiswahili hawana nafasi ya kusoma na kujifunza yaliyoandikwa katika vitabu hivyo. Ndugu Mapunda ametoa mchango wake katika Kiswahili. Hii ni jambo la kupendeza na ni tumaini langu kuwa wanachuoni wengi nao watajitokeza kuandika katika Kiswahili. Kukua kwa lugha yetu kama chombo cha elimu na utaalam kutatokana na kuthubutu kwa uzito huo.

Napenda kutoa pongezi kwa mwandishi kwa juhudi na mchango wake wenye shabaha ya kukuza na kuendeleza historia ya Mwafrika ambayo kwa miaka mingi imekuwa ikipotoshwa, kudhalilishwa au kupuuzwa na wanahistoria wengi. Kusema hivyo hakuna maana kupuuza au kudharau kipindi cha ukoloni katika bara letu. Kipindi hicho ni kifupi sana sana katika jumla ya

historia ya mwanadamu katika Afrika. Ni wazi uzito uliotolewa kwa ukoloni, ingawa ni kipindi muhimu sana, ulipotosha historia kamili ya bara la Afrika.

Mwandishi ametoa uchokozi wa hali ya juu kwa matumaini kwamba wanafunzi wengine wa historia ya Afrika watasukumwa kufuata nyayo zake au kubishia juu ya msimamo wake na hivyo kuendeleza mjadala katika somo hili muhimu. Iwapo itatokea hivyo, jitihada ya mwandishi haitakuwa imepotea bure.

Uandishi wa historia umechukua njia au mikondo mingi ya fikara. Mkondo moja wa fikara hufuatia msululu wa matukio katika nchi na kujaribu kutoa tafsiri ya tawala mbali mbali kuanzia mwanzo hadi kipindi wanapokomea.

Jitihada wakati wote katika mkondo huu wa fikara ni kuonyesha ushindi au kutofaulu kwa mtawala fulani na sababu zake. Na bado kuna mkondo mwingine wa fikara ambao hujihusisha sana na mabadiliko ya msingi katika maisha ya jamii. Mkondo huu huangalia jinsi mwanadamu anavyoyakabili mazingara yake kwa vipindi mbali mbali; na zaidi ya hayo jinsi kiumbe huyo alivyoweza kujenga msimamo wakẹ wa fikara za mapambano. Mkondo huu wa fikara unazingatiwa sana na wafuasi wa siasa ya ujamaa. Kuna mkondo mwingine wa fikara. Lakini kwa shabaha ya kuangalia kitabu hiki mikondo hii inatosha. Mwandishi wa kitabu hiki amejaribu kutumia msimamo wa mkondo huu wa tatu. Si rahisi kuwa mwaminifu kabisa ukitambua kwamba kila mtu hawezi kukwepa ukweli wa kuhusika na mazingara yake hata kama msimamo wake ni safi.

Ni matumaini yangu kuwa kila atakayepata nafasi ya kusoma kitabu hiki atashawishika kutafuta kujua zaidi juu ya somo hili muhimu. Na kwa Ndugu Mapunda ni matumaini yangu kwamba huu ni mwanzo tu katika safari ndefu ya kuandika historia ya bara letu na watu wake kwa undani zaidi.

D.N. MWAKAWAGO.

SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu, kwanza kabisa, kwa wanangu na marafiki kwa kunihimiza kuandika kitabu hiki. Shukrani za pekee nazitoa kwa Ndugu D.N. Mwakawago kwa ushauri wake wa daima ambao ulinipa moyo na msukumo wa kuendeleza kazi hii; na pia namshukuru kwa kibali chake kuandika dibaji ya kitabu hiki katika uwezo wake kama Katibu Mwenezi wa Chama cha TANU na pia kama Waziri wa Habari na Utangazaji wa Jamhuri ya Tanzania.

Miongoni mwa ndugu na marafiki wengine wanaostahili shukrani zangu ni Ndugu G. Mapunda. kwa mazungumzo na ushauri wa uchokozi; pia shukrani ziwaendee kwa wingi wapiga mashine wa Chuo cha TANU cha Kivukoni, hasa Bibi. C. Asenga, Bi. N. Rose na Bi. V.A. Maira. Vile vile napenda kumshukuru Ndugu R. Utukulu, Mwalimu katika Chuo cha TANU cha Kivukoni, kwa ushauri wake katika mambo mengi muhimu. Na mwisho napenda kuwashukuru wale wote walioniruhusu kudondoa au kutumia sehemu za maandishi yao.

H. Mapunda

UTANGULIZI

Kitabu hiki kidogo kimeandikwa kwa shabaha moja kubwa; nayo ni kutoa mawazo na fikara mpya za uchokozi. Uchokozi wa mtungaji utahusu mambo kadhaa; nao, utakuwa ni wake kama mwanahistoria na wala usichukuliwe kama msimamo wa siasa ya nchi. Kwa mfano, kutakuwa na uchokozi juu ya mikabala mbali mbali ya kihistoria na matatizo yanayowakabili wanahistoria wa leo wa historia ya Afrika.

Papo hapo kijitabu hiki kinakusudia kusawazisha na kufutilia mbali baadhi ya fikara na imani zenye kasumba za waandishi wa kikoloni kuhusu nadharia mbali mbali za kihistoria. Pamoja na hilo, mtungaji anajaribu kutoa fikara na nadharia mpya, pengine kwa hivi sasa hatakuwa na ushahidi wa kutosha wa kisayansi kumwezesha, yeye mwenyewe na wanahistoria wengine, kujenga na kuiratibu upya historia ya Afrika. Hata hivyo, mtungaji anaamini kuwa nadharia hiyo mpya itakuwa ndio msingi halisi wa uchokozi kwa wanahistoria wengine.

Kwa maneno mengine, kazi ya mtungaji ni kuchokoza hasa kwa njia ya maswali ambayo hayana budi kujibiwa na yeye mwenyewe au na wanahistoria wengine lau kama si leo, basi, siku yoyote kuanzia leo. Na kwa kufanya vile mtungaji ana shabaha ya kutoa aina mpya ya mkabala kwa madhumuni ya kuendeleza juhudi za wanahistoria wakimapinduzi wa historia ya Afrika ambazo kwa hivi sasa zaonyenya hali ya kudumaa na ku-kwama. Na kwa sababu hiyo hiyo mtungaji wa kijitabu hiki amejaribu kuepukana na utoaji wa majibu kwa maswali mengi ya uchokozi na ya kinadharia. Hata hivyo, mtungaji amejaribu kutoa majibu kwa baadhi ya maswali kama: Nini maana ya historia? Nini maana ya usemi 'Waafrika hawakuwa na historia; na kwamba historia yao inaanzia baada ya kuja kwa watu weupe tu, yaani, wakoloni? Hizo ni baadhi tu za fikara ambazo, kusema kweli hazina msingi wowote wa kibusara. Historia ni matokeo ya

mapambano ya mtu na mazingara yake. Ni dhahiri kwamba Waafrika, kama watu, wamekuwa na historia yao ambayo inaweza kurudi nyuma mpaka wakati wa mtu wa kwanza. Utovu wa 'historia ya Afrika' kama somo, hauwezi kuwa sababu ya kiakili ya kudai kuwa Waafrika hawakuwa na historia.

Waandishi wengi wameandika juu ya historia ya unyonge wa Mwafrika. Ingawa mtungaji wa kitabu hiki anakusudia kuandika juu ya somo hilo hilo anaogopa kusisitiza juu ya historia ya unyonge wa Mwafrika. Mtungaji anatarajia kuonyesha kuwa unyonge haukuwa wa Mwafrika peke yake na wala haukusababishwa na rangi yake. Jamii zote duniani zimepata kukabiliwa na unyonge; na kwamba unyonge wa mtu ulisababishwa, kwanza, na mazingara mbali mbali ijapokuwa mabaa ya biashara ya watumwa na ukoloni uliopata kuendeshwa katika Afrika umesababisha na kuifanya historia ya Waafrika, hasa Waafronodi, ionekane tofauti na historia ya unyonge na mapambano ya jamii nyingine duniani. Unyonge wa Mwafronodi haukusababishwa na rangi yake. Pia ikumbukwe kuwa kila palipo na mapambano ya kuondoa unyonge pana maendeleo ya aina fulani. Na kwa sababu hii mtungaji anasita kusisitiza juu ya neno unyonge ambalo linampa Mwafronodi fikara za kudumu kuwa yeye daima ni mnyonge; na kwa hiyo, kuendeleza unyonge wake. Hivyo, mtungaji anapenda kutilia mkazo juu ya mapambano ya maendeleo ya Waafrika. Kusema kweli unyonge leo upo hata katika nchi zilizoendelea. Tofauti ni kuwa katika nchi za kibepari unyonge huo unatokana na mfumo wa jamii ambao huruhusu wachache kuwatawala, kuwatumikisha na kuwakandamiza walio wengi.

Nadharia ya mgawanyo wa watu au jamii za Kiafrika kama ilivyotolewa katika mjadala juu ya 'Afrika kuingiliwa na wageni' ni mpya; nayo imebuniwa na kupendekezwa na mtungaji mwenyewe kwa shabaha ya kusaidia uchokozi na ufasaha wa maelezo yake. Nadharia hiyo siyo tu kwamba inafuta 'kasumba ya Kihamati' bali hata kasumba ya Kinigrodi na Kibushimanodi* maneno ambayo yana kasumba ya kashfa na dharau kwa Mwafronodi ndani yake japokuwa pengine nia ya mwandishi ilikuwa njema. Badala yake mtungaji wa kitabu hiki anapendelea kuwapanga Waafrika katika makundi makuu matatu:

* B.A. Ogot, (ed) *Zamani*, Nairobi, Uk. 69 – 99

Waafronodi[2], Wasanodi[3] na Wayuronodi[4]. Kundi la Waafronodi hugawanyika katika vikundi vingine viwili, yaani, kikundi cha Wakansanodi[5] na Wakaprinodi.[6] Neno Wakakasadi[7] pia linafutwa maana lina maana kuwa mtu mweupe ni bora kuliko Mwafronodi. Kuhusu jamii waliyoita Wabushimeni' mwandishi anapendekeza kuita watu wa jamii hiyo 'Wakalahari'. Hawa ni watu wanaoishi sasa katika sehemu za jangwa la Kalahari; na neno: 'Wakalahari' linatokana na neno 'Kalahari'. Maelezo zaidi ya ufafanuzi wa suala la watu wa Afrika yametolewa katika sura ya nne juu ya suala la Afrika kuingiliwa na wageni ambamo pia kielelezo chake kimetolewa.

Maneno yaliyotumika hayana uhusiano na kitu chochote na wala hayana msingi wa kisayansi bali ni mapendekezo ya mtungaji. Maneno: Wakansanodi na Wakaprinodi yanatokana na mistari ya kijografia ya tropiki ya 'Kansa na ya Kaprikoni' maneno ambayo yana maana mistari iliyo kaskazini na kusini ya mstari wa ikweta. Vikundi hivyo vya Waafronodi vimependekezwa ili kuelezea hatua tofauti za maendeleo ya watu tangu angalau miaka 6,500 iliyopita.

Uchokozi mwingine unamhusu mtungaji na mwanafunzi wa historia. Nini kazi ya mwanahistoria? Kueleza au kufasiri historia tu au yote mawili? Na iwapo hivyo ndivyo, yaani, yote mawili, basi, swali litabaki kuwa shabaha ya kufanya vile ni nini? Na iwapo kama historia ina shabaha ya kuleta msukumo wa maendeleo ya jamii sharti ielezwe, pasipo kupotosha ukweli, kwa jinsi kwamba italeta maana ya kweli. Pasipo kuwa na lengo hilo la mwisho, basi, somo la historia halitakuwa na maana yoyote, hasa kwetu sisi watu wa Afrika ambao tumepitia katika janga la kuuzwa utumwani na katika mpango wa ukoloni; na ambao historia yetu imepotoshwa na wakoloni kwa shabaha ya kuteremsha hadhi yetu ya kiutu, kutudhulumu, kututawala na kutunyonya. Kuhusu utumwa na biashara ya watumwa mtungaji anatarajia, kwanza, kuonyesha jinsi mfumo wa kitabaka uliokuzwa na kuendelezwa na baadhi ya watu wachache katika

---

2. Waafronodi – Waafrika wa asili ambao waliishi katika bara hili kabla ya wageni wa kutoka Ulaya na Asia.
3. Wasanodi – Watu wenye asili ya bara la Asia.
4. Wayuronodi – Watu wenye asili ya bara la Ulaya ambao wameishi hapa kwa karne nyingi kama walowezi.
5. Wakansanodi – ni Waafronodi wanaoishi kaskazini ya Ikweta na kusini ya Sahara.
6. Wakaprinodi – ni Waafronodi ambao maskani yao yamekuwa kusini ya Ikweta.
7. Wakakasadi – neno hili lilitumiwa na wanahistoria wa Kiyuronodi kueleza watu wenye asili ya Ulaya na Asia.

jamii ulivyoweza kusababisha aina mpya ya unyonge wa umma wa wanajamii popote duniani. Pili, mtungaji amejaribu kulikabili suala zima la biashara ya watumwa kwa msingi wa mfumo wa kitabaka — mfumo ambao chanzo na dosari zake pia zimeelezwa. Mkabala wa mtungaji pia umekuwa wa kitabaka katika sura zote. Ingawa mkabala huu si mpya sana lakini jinsi ulivyotumika unaweza kuonekana mpya hasa katika kuelezea suala la biashara ya watumwa.

Nadharia nyingine mpya ambayo mtungaji ameitoa ni kuhusu suala la Uafrika na Uafronodi. Fikara za uafrika, yaani, umoja wa Waafrika wa Afrika na watu wenye asili ya Kiafrika katika mabara mengine, pia zimepewa nafasi kubwa ya mjadala. Kwa maoni ya mtungaji fikara hizo zilizosemekana mpaka sasa kuwa ni fikara za uafrika, fikara ambazo zilikuzwa kwa mara ya kwanza na watu wa asili ya Kiafrika huko ugenini, zilikuwa, ni fikara za uafronodi. Watu hao walioanzisha fikara hizo bila ya kuwafikiria kuwa walikuwa na moyo wa ubaguzi, walikuwa Waafronodi kwa asili. Na wakati walipopigania kurudi katika Afrika ni dhahiri pia kuwa Afrika ni Afrika ya Waafronodi ambako ndiko babu zao walichukuliwa na kuuzwa huko ugenini. Mtungaji pia amejaribu kuonyesha dosari na ugumu wa utekelezaji wa fikara au azimio la watu wenye asili ya Kiafronodi kupigania kurudi Afrika. Vile vile mtungaji amejaribu kutoa maoni yake kuhusu uafrika, yaani, umoja wa Waafrika (Waafronodi, Wasanodi na Wayuronodi) na watu wote wenye asili ya Kiafronodi popote walipo duniani na wanyonge wengine wote katika juhudi zao za kujikomboa kutokana na unyonyaji, ubeberu na ukoloni.

Wamisionari wa madhehebu mbali mbali wamepewa nafasi yao kuhusu wajibu na jukumu walilochukua kuandalia, kuhudumia na kuendeleza ukoloni katika Afrika. Mtungaji amejaribu kutofautisha suala la imani na waenezi wa imani hizo katika Afrika. Pia amesisitiza kuwa maelezo juu ya wamisionari hayana makusudio ya kuunda chuki na uhasama. Shabaha ni kukumbushana juu ya makosa ya kihistoria yaliyofanywa na wamisionari; na pia kujaribu kuona sababu zilizowafanya wamisionari kujiingiza katika makosa hayo ambayo wengi wao wangerudi tena Afrika wasingeyarudia tena. Kusema kweli baadhi yao ambao wamo bado Afrika wamejaribu sana kuonyesha fikara za kimapinduzi za kupigania haki na uhuru wa wanyonge – Waafrika na mataifa mengine yaliyonyonywa na kuachwa maskini baada ya kujikomboa kitaifa. Vile vile,

mtungaji amejaribu kutoa kijimwongozo cha kuwaelekeza viongozi wazalendo wa madhehebu mbali mbali ili kuwawezesha kuendeleza fikara za kimapinduzi na kuwasaidia wananchi wa mataifa yao kujikomboa kutokana na umaskini, maradhi, na ujinga; mambo ambayo ni msingi wa unyonge wetu. Shabaha kubwa ya juhudi na mapambano hayo ya kuondokana na unyonge ni kustawisha na kuendeleza maisha ya Waafrika na wanyonge wengine wote katika dunia. Mwisho kabisa mtungaji anajadili juu ya mbinu mpya za mabeberu na wakoloni. Papo hapo mtungaji anajaribu kutoa maoni yake kuhusu mbinu na tahadhari za ulinzi ili kujikinga na kupambana na ubeberu na ukoloni — mambo leo. Pamoja na suala la ulinzi mtungaji amesisitiza juu ya ujamaa kama njia ya pekee ya kukomesha unyonyaji na unyonge kwa shabaha ya kuleta amani, furaha na ustawi wa jamii.

Kwa hiyo, pasipo kuomba msamaha, msomaji atalazimika kuiona kazi hii ambayo ni ndogo kwa kurasa zake kama ni uchokozi mkubwa. Tatizo letu Waafronodi ni kasumba ya utovu wa imani ya kuwa sisi Waafronodi hatuna uwezo wa kufanya jambo lo lote la maana pasipo msaada wa Wayuronodi au Wasanodi. Kwa maneno mengine, kasumba ya aina hiyo imekuwa pingamizi kubwa kwa maendeleo yetu kinadharia, kifikara, kisayansi, kitamaduni, kiuchumi na kadhalika. Na tukitaka kujiendeleza, basi, hatuna budi kwanza kuzindukana na kasumba za aina yote pamoja na baadhi ya mila na desturi ambazo huzuia maendeleo ya jamii kwa wakati wetu na ujao.



Mipaka ya jamii hizi haina uhalisi sana; imewekwa kwa shabaha ya kurahisisha maelezo ya somo, hasa ikikumbukwa uingiliano wa jamii.

Sura ya 1

NJIA ZA KUPATIA MAARIFA YA HISTORIA ZA WAAFRIKA

Katika sura ya pili mtungaji anatueleza kuwa historia ni somo lenye uhai linaloeleza, kwa ujumla, maisha ya watu wa jamii mbali mbali na katika vipindi mbali mbali. Na kwamba ni watu tu ndio waliojaliwa uwezo wa kazi na kujenga utamaduni ambao ndiyo hasa msingi mkuu wa maendeleo. Papo hapo mtungaji anatuomba kuzingatia muda wote kuwa historia hii tunayoiongelea siyo historia ya vitu bali ni historia ya mtu na jamii.

Bara la Afrika limekaliwa na watu kwa miaka ipitayo 2,000,000 ambao, kusema kweli, ndio umri unaosadikiwa wa mtu katika dunia hii.

Ni dhahiri kuwa Waafronodi kwa sababu ya utamaduni wao, wamekuwa na historia. Ukweli ni kuwa historia ya Waafrika kusini ya Sahara ukiondoa pia historia ya Wahabeshi haikupata kuandikwa. Hata hivyo, maandishi ya kihistoria sicho ndicho kitu kinachozifanya jamii za watu kuwa au kutokuwa na historia. Bali maandishi ni moja tu ya njia za kuhifadhia historia za jamii za watu. Kwa tahadhari mambo yafuatayo yapaswa kuzingatiwa.

Sehemu kubwa ya historia ya watu wanaoishi kaskazini ya Sahara, kama Wamisri na Wahabeshi, imehifadhiwa na wao wenyewe katika maandishi. Jambo muhimu linalowapasa kufanya ni kuitazama vipya historia yao na kuiratibu vipya katika msimamo wa kisasa. Hata hivyo, iko haja kufanya uchunguzi zaidi.

Pia kuna suala la kuchagua mahali au tarehe ya kuanzia. Lazima ifahamike kwa kila mwandishi wa historia kuwa, ingawa historia ina umri sawa na binadamu, uwezekano wa kuipata historia yote ya jamii kuanzia miaka 2,000,000 haupo. Na pengine si jambo muhimu sana. Juhudi za kupata maarifa ya kutosha na kwa kipindi kirefu kutosha hutuwezesha kufasiri historia za jamii zetu na kuzipa maana zaidi.

Mara nyingi sehemu au tarehe ya kuanzia hutegemea sana tukio au matukio muhimu katika maisha ya jamii japokuwa tukio au matukio yenyewe ni mambo tu yanayoweza kutokea na kupita; na mara nyingi bila ya watu wenyewe kuazimia au kuyapangia.

Leo tunasema umri wa mtu ni miaka ipatayo 2,000,000, ni kwa sababu fuu la Zinjantropasi ambalo ni fuu la 'mtu' lililo na umri mkubwa zaidi kuliko masalia yote ya watu yaliyopata kugunduliwa mpaka sasa linakadiriwa kuwa na umri huo. Leo tunaongea juu ya mwaka huu. Hii ina maana kuanzia wakati Yesu wa Nazareti, katika Uyahudi, alipozaliwa. Hivyo, basi, tunapoongea juu ya historia, kwa mfano, ya Waafrika kusini ya Sahara tunaweza kuanzia wakati wa ujio wa wakoloni na kurudi nyuma kwa kiasi uchunguzi utakavyotuwezesha. Pia tunaweza kuanzia kipindi hicho hicho cha ujio wa wakoloni hadi leo kupitia kipindi chote cha ukoloni, kipindi cha mapambano ya wananchi ya kujikomboa na baada ya ukoloni kwa baadhi ya nchi ambazo zimepata kujitawala kisiasa.

Baada ya maarifa hayo machache kuna haja ya kuanza mazungumzo kuhusu njia mbali mbali za kukusanyia maarifa ya kihistoria; tukijadili papo hapo juu ya ubora na matatizo au upungufu wa kila moja.

Kumbukumbu zilizohifadhiwa katika maandishi ni za kuaminika zaidi ingawaje suala la tafasiri na mchanganuo wa kihistoria laweza kubaki tatizo.

Pili, kama ilivyodokezwa hapo juu sehemu kubwa ya historia ya Afrika, hasa kusini ya Sahara, ukiondoa sehemu za mwambao, haikupata kuandikwa mpaka baada ya mwaka 1800 B.K. Mwaka huu umependekezwa kwa sababu ni mwanzo wa kipindi cha maingilio ya wakoloni na mapambano baina yao na wananchi, hasa wa sehemu za bara.

Uzuri wa maandishi ni kuwa tarehe na matukio muhimu huweza kuhifadhiwa na kudumishwa kwa miaka mingi bila kubadilika. Hata hivyo, ifahamike wazi kuwa siyo maandishi yanayojenga historia za jamii za watu. Bali historia hujengwa na watu wenyewe kwa wakati wote wa maisha ya jamii. Maana kila jamii ina uhai na hujimudu wakati wote. Na kama tutakubaliana kuwa watu ndio wenye uwezo wa kujenga historia yao, basi, ni dhahiri kwamba Waafrika wana historia zao ndefu zaidi kuliko zile zilizopata kuandikwa, ukisahau suala la

upotoshaji wa makusudi na wakoloni.

Hivyo, basi, kuna haja ya kusahihisha fikara fulani fulani za kikoloni kuhusu historia ya Waafrika. Kwanza kabisa, si kweli, kufuatana na maelezo yaliyotolewa hapo juu, kwamba Waafronodi hawakuwa na historia kabla ya kufika watu weupe, yaani, Wasanodi na Wayuronodi na maandishi yao. Walikuwa nayo!

Pili, kuongea juu ya "kipindi kabla ya historia", hakuleti maana yoyote. Haiwezekani kuzungumzia juu ya wakati kabla ya historia kwa sababu mbili. Kwanza, ina maana kuwa hapakuwepo na watu katika Afrika kabla ya kufika watu weupe na maandishi yao ambao walifikia kiwango cha utu kamili cha kuwa na uwezo wa kujiendeleza.

Pili, fikara za namna hiyo ni hatari kwa sababu ni wazimu kwa watu kuongea, kudadisi na kujadili juu ya jambo ambalo kusema kweli halipo au halijawahi kutokea. Badala ya kuzungumza juu ya kipindi kilichoitwa "kabla ya historia ya Afrika" tuanze kuzungumza juu ya kipindi cha historia ya Afrika kabla ya maandishi. Kwa maneno mengine, tutakuwa tunaongelea juu ya mapambano ya Waafrika katika kipindi kabla ya ukoloni ambao uliingia Afrika baada ya miaka ya 1800 B.K.

Maandishi mbali mbali ya wakoloni kuhusu maisha ya Waafronodi yaweza kupatikana katika idara za serikali za kuhifadhia mambo ya kale, katika maofisi ya serikali: mikoani na wilayani; na katika maparokia ya dini.

Pia itabidi mkusanyaji wa maarifa ya kihistoria kutembelea maofisi ya wakoloni wanaohusika katika nchi zao, ili kupata baadhi ya makala ambayo "wapelelezi" na maofisa katika makoloni waliandikiana na serikali au jamaa wa kwao. Na kwa tahadhari ni kuwa makala za maandishi ya wakoloni hayana budi kusomwa na kutumiwa kwa makini sana. Hii ina maana kuwa kwanza yatupasa kuelewa shabaha na msimamo wa wakoloni kuhusu watu wa makoloni ambao habari zao waliziandika. Baada ya kukubaliana kuwa Waafronodi, kama watu wengine, wana historia ndefu zaidi kuliko ile iliyopata kuandikwa, kuna haja ya kutafuta njia zitakazotuwezesha kuikusanya historia hiyo.

Katika jamii nyingi za Kiafronodi kulikuwa na watu ambao tutawaita wataalam wa historia. Kazi yao muhimu ni kukumbuka na kuieleza historia ya ukoo, jamii au ya ukoo wa utawala Huko Afrika Magharibi watu hao hujulikana kama 'Griots'. Wanahistoria hao huendeleza historia ya jamii kizazi hata kizazi.

Vile vile katika kila ukoo wazee walikuwa wanawasimulia watoto wao hadithi kuhusu asili ya ukoo, utawala, jamii na mpango wa maisha ya watu kwa ujumla. Kwa kuwa watoto ndio wazee wa kesho, nao pia waliendelea kuwasimulia watoto wao na hatimaye wajukuu wao na kadhalika. Hata hivyo, njia hii ya kutunza kumbukumbu kwa masimulizi haiwezi kuaminika sana.

Kwanza, uwezekano wa kusahau mambo muhimu na pengine hata kupotosha ukweli wa habari ni mkubwa sana. Pili, kuna hatari ya kutia chumvi zaidi katika kuikuza na kuitukuza habari kwa sababu ya watu wenyewe kutaka kujipa ufahari. Tatu, ni vigumu sana kukumbuka tarehe za matukio muhimu kwa kipindi kirefu. Hivyo, njia hii inaweza tu kuturudisha nyuma kwa kipindi cha miaka michache.

Ubora wake ni kuwa njia hii inatuwezesha kujua angalau asili ya watu wa jamii mbali mbali, mpango na mfumo katika vipindi maalum. Hivyo, basi, ni juu ya mwanahistoria kuyatumia "mapokezi" hayo na kuyachanganua pamoja na maarifa yanayotokana na njia nyingine kama maandishi, uchimbuzi na kadhalika.

Kwa mfano, kutokana na masimulizi ya Wangoni na ya watu wa Zimbambwe sasa inafahamika kuwa Zwangendaba, kiongozi wa Wangoni kutoka Afrika ya kusini, aliuvuka Mto Zambezi mnamo 1835 kuelekea Tanzania.

Masimulizi yanatueleza kuwa Zwangendaba alikuwa kiongozi shujaa sana; na enzi yake ilitambuliwa sana, sio na watu tu bali hata na vitu vilivyomzunguka. Hivyo, basi, wakati akivuka Mto Zambezi, ng'ombe wengi walikufa kwa maji, ambayo kusema kweli yalikuwa ni mafuriko ya ghafla, na kwamba nchi nzima ilikuwa katika giza japokuwa ilikuwa mchana. Ndiyo kusema, kwa sababu ya enzi aliyokuwa nayo Zwangendaba hata jua liliweza kusalimu amri yake.

Wataalam wa mambo ya anga wamerekodi kuwa mwaka huo 1835, kulikuwa na kupatwa kwa jua. Hivyo, basi, kutokana na maarifa hayo pamoja na masimulizi ya . watu wenyewe tunafahamu tarehe ambayo Zwangendaba na wafuasi wake walivuka Mto Zambezi. Na kwa kuwa tunaambiwa kuwa mara tu baada ya kuvuka mto huo mke mkubwa wa Zwangendaba alimzaa Mbelwa, na kwamba mwanae mwingine, kwa jina Mpezeni, alizaliwa yapata miaka mitano kabla katika nchi ya Zimbabwe, tumepata kufahamu pia umri wa wana hao wawili wa Zwangendaba. na mahali walipozaliwa.

Kwa sababu ya kukosa ujuzi wa kusoma na kuandika jamii nyingi za Kiafronodi ziliweza kuhifadhi kumbukumbu zao kwa njia ya michoro. Vitu walivyochora vilieleza aina ya utamaduni, ukiwa ni utaratibu wa maisha kwa ujumla ambao jamii hizo zilikuwa nao. Michoro mingi ya jamii za Kichembe* imegunduliwa miongoni mwa Wasandawe na Watindiga wa huko Kondoa katika Tanzania. Michoro hiyo hufanana sana na michoro ya Wakalahari na Wahotentoti wa huko Afrika Kusini. Vile vile rangi iliyotumiwa na jamii hizo nne ni aina moja. Hii peke yake inaweza kutufanya tufikiri kuwa pengine watu hao asili yao ni jamii moja.

Picha walizochora huonyesha watu, vyombo, kama mishale, na aina fulani za wanyama waliowinda; na pengine aina ya matunda na mizizi ya porini waliyoichimbua na kutumia kama chakula.

Ingawa michoro hutupa maarifa ya uchumi na utamaduni wa jamii hizo haiwezi kutufahamisha zaidi. Ni vigumu sana kujua kama watu hao walikuwa na 'dini' au serikali. Na kama walikuwa na utamaduni wa aina hiyo kuna tatizo bado la kufahamu miundo na utaratibu wa kuendesha shughuli mbali mbali. Pia ni vigumu kujua kama michoro na picha hizo zinawahusu watu wa jamii ya karne zipi. Hata hivyo ni wazi kuwa wanahistoria wataitumia michoro hiyo ili kuwawezesha kuweka nadharia fulani kwa shabaha ya kufikia lengo maalum la kihistoria.

Lugha ni sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii. Ukubwa na uhafifu wa msamiati wa jamii husababishwa na ukubwa au upungufu wa maendeleo ya kitekinologia na utamaduni wa jamii. Kwa sababu hiyo hatuna budi kwanza kukubaliana kuwa kila "lugha" ni kamilifu kwa watu inaowahusu; na kwamba lugha ina falsafa yake.

Lugha ndicho chombo muhimu cha kuelezea fikara za jamii kuhusu mipango ya kazi zao za kila siku, vyombo mbali mbali wanavyotengeneza na kuvitumia, mila na desturi zao, imani na thamani za maisha, serikali pamoja na uchumi wao.

Watu wanaoishi kando ya mito na maziwa au bahari wana msamiati mkubwa zaidi kuhusu shughuli za uvuvi kuliko wawindaji na watu waishio milimani. Na hii ni kweli kwa jamii zote zenye utamaduni tofauti.

Kwa vile lugha ni sehemu muhimu ya utamaduni, maarifa

---

* Maelezo zaidi yametolewa katika sura ya pili.

yanayotokana na 'elimu ya lugha' yanatuwezesha kujua asili ya mpango wa maisha, kwa ujumla, wa jamii za watu mbali mbali[1]. Elimu ya lugha imesaidia sana kufuta kasumba ya wakoloni ya kuwagawanya Waafrika katika matabakatabaka na kusisitiza juu ya fikara isiyo na msingi kuwa watu weupe ni bora na wenye uwezo zaidi wa kufikiri na kufanya maendeleo yao kuliko Waafrika ambao walielezwa kuwa ni nusu watu.[2]

Kama ilivyoelezwa hapo awali sehemu kubwa ya historia za jamii za Kiafronodi haikuandikwa. Na ili kuziandika imelazimu kutumia njia mbali za kukusanyia maarifa. Baadhi ya njia hizo ni 'masimulizi, 'michoro' na 'elimu ya lugha! Ubora na upungufu au uhafifu wa njia hizo pia umeelezwa.

Njia nyingine ambayo inaweza kutupatia maarifa ya kihistoria ni uchimbuzi wa masalia ya watu wa kale na utamaduni wao ambao huendelezwa leo katika sehemu mbali mbali za dunia.

Kwa upande mwingine, Afrika Mashariki peke yake imebahatika kuwa na sehemu ambayo inawawezesha wataalam wanaoshughulikia suala la maendeleo ya watu duniani kuyapata masalia yao (watu) katika mfululizo wa matabaka mbali mbali ya ardhi. Hivyo, basi, katika Bonde la Olduvai Daktari L.S.B. Liki amegundua fuu la mtu, mtu kufuatana na tafasiri yetu, ambaye anasadikiwa kuwa na umri wa miaka ipatayo 2,000,000. Mafuu na mifupa mingine ya watu yameonekana katika mfululizo huo huo wa matabaka ya ardhi mpaka kufikia tabaka la mwisho.

Matabaka ya ardhi.



Kimaumbile na kitamaduni masalia ya watu wa tabaka la mwisho, yaani, tabaka la IV katika kielelezo, hufanana sana na watu wa siku hizi. Kwa ufupi, walikuwa wamefanya maendeleo makubwa hasa kuanzia miaka ipatayo 10,000; wakati, kwa mara ya kwanza watu walipoanzisha kilimo na ufugaji; na baadaye

1. Kwa maelezo zaidi soma utangulizi na sura ya tano.
2. Maelezo zaidi yametolewa katika sura ya pili.

kujiendeleza katika ufundi na utaalam mbali mbali, wakiishi katika vijiji na miji na kuendelea kubadilishana maarifa na ujuzi.

Huko Kilwa, katika Tanzania, kwa mfano, mtaalam mmoja ajulikanaye kwa jina la Chitiki na kikundi chake wamo katika shughuli ya kuchimba masalia ya utamaduni wa kale. Utamaduni huo unahusu majengo ya magofu na vitu au vifaa ambavyo wakale walivitumia kama bidhaa katika biashara.

Kutokana na masalia ya vyombo vya kitamaduni vya wakale tunaweza kujua mambo kadhaa. Na kwa sababu katika baadhi ya vyombo hivyo kuna maandishi na tarehe tunaweza kufahamu utamaduni wa jamii za wakale katika vipindi mbali mbali. Vile vile tunaweza kupata tarehe za vyombo hivyo kwa kutumia njia za kisayansi za kutolea tarehe.

Vyombo vingi vyenye utamaduni wa asili ya Kisanodi yaani, Kiarabu, Kichina na kadhalika, vimegunduliwa. Baadhi ya vyombo hivyo ni vikombe, sahani na bakuli za udongo, vyombo vya kusafiria na aina ya fedha ambayo iliweza kutumika kama njia ya kubadilishana mali. Baadhi ya masalia yaonyesha bidhaa za kutoka sehemu za bara za Afrika, kwa mfano, vipusa na dhahabu ambayo migodi yake imeenea huko Zimbabwe. Hii pia imethibitishwa na maandishi ya Wasanodi juu ya biashara ya dhahabu kati ya Waafronodi na Waarabu iliyoendeshwa huko Sofala katika Msumbiji.

Hata hivyo, ieleweke kuwa njia ya uchimbuzi ina upungufu wake. Haiwezi kutupatia maarifa ya kutosha kuhusu watu wa kale. Hatuwezi, kwa mfano, tukajua aina gani ya chakula (nafaka) jamii za kale zilikuwa zinakula. Na kama walikuwa na serikali na dini, kwa mfano; bado ni vigumu kujua muundo na madhehebu yake au mfumo wa jamii za wakale wanaohusika.

Lakini iwapo maarifa yanayotokana na uchimbuzi wa masalia ya utamaduni wa wakale yatatumika pamoja na maandishi, masimulizi na michoro, yatamsaidia sana mwandishi wa historia kuiratibu historia ya jamii za wakale. Na, kusema kweli, jamii za wakale ndizo zilizokuza, kustawisha, kuendeleza na hatimaye kuturithisha utamaduni ambao, kwa maneno mengine, ni historia zetu.

Kwa kumaliza somo letu hapana budi kukumbukwa kuwa kila njia ina ubora na upungufu wake. Ili mwanahistoria aweze kupata picha kamili ya maendeleo na utamaduni wa jamii za watu wa kale njia zote hizo ni muhimu sana; na kwamba hazina budi kutiliwa mkazo na kuimarishwa na vyama vyote vya siasa na serikali zao popote katika Afrika.

Sura ya 2

MTU NA MAZINGARA

Ili kulielewa vizuri somo la historia itapasa kwanza kutoa ufafanuzi kuhusu maana ya historia na umuhimu wa kujifunza somo hili. Pili, kuna haja ya kutoa maelezo machache kuhusu mapambano ya 'mtu' na mazingara yake.

Historia ni somo lenye uhai kwani linatupa maarifa ya mapambano baina ya 'mtu' na mazingara yake. Shabaha kuu ya mapambano hayo ni jitihada ya mtu ya kuendeleza kizazi chake. Shabaha ya pili ya mapambano ni kuyafanya maisha hayo ya 'mtu' kuwa bora zaidi na zaidi. Na kwa kuwa lengo ama shabaha hizo mbili hufikika tu wakati 'mtu' anapoyashinda na kuyatawala mazingara ni dhahiri kuwa 'mtu' huondokana na 'unyonge' wa aina mbali mbali.

Mapambano ya 'mtu' na mazingara yana historia ndefu sana. Kusema kweli, urefu wa mapambano ya aina tunayozungumzia unalingana na umri wa 'mtu' katika dunia hii ambao unasadikiwa kuwa kiasi cha miaka ipatayo 2,000,000. Lakini jambo la kufahamu ni kuwa mazingara ambayo 'mtu' amelazimika kupambana nayo yametofautiana kutegemea vipindi mbali mbali vya wakati katika maisha ya 'mtu'.

Kwa kuwa historia ni somo linalohusu mapambano ya 'jamii za watu' na mazingara umuhimu wake unaweza tu kuonekana iwapo maarifa yatokanayo na somo hilo yatatumika katika kutatua matatizo ya wakati wetu na kusaidia kutoa mwangaza kwa siku za mbele. Katika kuyakabili matatizo mbali mbali wakati mwingine mtu au jamii hukosea lakini papo hapo 'mtu' hujifunza somo maalum kutokana na makosa yake. Kwa jinsi hiyo, 'mtu' huwa na uwezo mkubwa sana wa kuepukana na baadhi ya makosa ya siku za nyuma; hasa anapotengeneza mipango ya maendeleo ya wakati wake na ya wakati wa siku za mbele. Uwezo huu wa kukusanya maarifa ni kipaji ambacho mtu peke yake amejaliwa kuwa nacho.

Iko haja vile vile ya kutoa maelezo machache ya kimsingi kuhusu 'mtu' ambaye ndiye somo la historia linamhusu. Mtu ni mmoja wa wanyama wa daraja la juu na ambaye peke yake ndiye amepata kufikia upeo wa juu tangu miaka 2,000,000 iliyopita. Upeo huo unamwezesha mtu kupambana na kuyatawala mazingara kwa shabaha ya kujiendeleza. Kwa kuwa ni yeye ndiye mwenye uwezo huo wa kujiendeleza, basi, ni dhahiri kwamba ni yeye tu, miongoni mwa wanyama wengine wote, ndiye anayestahili kuitwa mtu; na kwa hiyo neno mnyama laweza kuondolewa.

Mtu popote duniani, aweza kutambuliwa kuwa ni mtu kwa sababu ya uwezo alionao wa kujiendeleza. Kujiendeleza maana yake kwanza kuwa na maarifa pamoja na uwezo wa kuyatumia maarifa, yaani, kufikiri, kupanga na kuratibu kwa shabaha ya kufikia lengo maalum ambalo yeye mwenyewe hujiwekea. Pili kuwa na uwezo wa kuunganisha maarifa na juhudi. Na sifa ya tatu ni kwamba mtu ana uwezo mkubwa wa kutumia mali ya asili ambayo imo katika mazingara anamoishi kwa masilahi yake. Ukimwondoa mtu, wanyama wengine wote waliobaki: wanyama wa nchi kavu, samaki, ndege na kadhalika, hawana sifa hizo; na kwa kuwa hawana sifa hizo hawawezi kujiendeleza; na kwa kuwa wanashindwa kujiendeleza wao hawataitwa watu au nusu watu. Neno wanyama ndilo litakalotumika kwa ajili yao. Kutokana na maelezo yetu juu ya maana ya mtu ni dhahiri kwamba mtu popote duniani ni kamili kuhusu utu wake. Kwa kuwa watu wote ni kamili, ni kweli pia kuwa watu wote, kama watu, ni sawa kuhusu utu na uwezo wao kutegemea mazingara wanamoishi. Na kwamba mahitaji yao muhimu ya maisha ni sawa. Wote wahitaji chakula, mavazi, malazi, hakika na usalama wa maisha na wa mali zao na kadhalika.

Ingawaje mahitaji hayo ya mtu ni ya msingi kwa watu wote bado ni mahitaji ya msingi kwa wanyama pia. Kwa hiyo, kufuatana na maelezo ya mwandishi juu ya mtu kuna haja ya kutoa maelezo ya hali ya juu zaidi kuhusu mahitaji ya mtu. Mtu akiwa tofauti na wanyama na mimea, ameendesha mapambano kwa shabaha ya kupata maarifa na vyombo muhimu na bora zaidi vya kurahisisha kazi zake ambazo zitaweza kumpatia chakula kwa wingi, chakula bora zaidi, mavazi bora zaidi, malazi bora zaidi na afya bora zaidi ili kuondokana na unyonge na kuwa mtu mwenye furaha anayeshangilia maisha yake kikamilifu hapa duniani. Na, kwa hiyo, mambo yote hayo yatategemea sana maazimio yake, ubora wa mipango yake ya maendeleo ya jamii

na uwezo wa kuangaza mbali zaidi katika siku za mbele. Na ili kuleta maendeleo ya haraka zaidi huenda jamii za watu leo zitahitaji mipango mikubwa zaidi ya elimu ya kiufundi, na pia kujiunga pamoja kwa shabaha ya kujumlisha maarifa na juhudi zao. Na ili maendeleo yasiwe ya wachache au ya mtu mmoja mpango mzuri wa kujiunga ni kujiunga kijamaa ili kuhakikisha kuwa maendeleo ya haraka yatakuwa kwa jamii nzima.

Sifa hizo tatu zilizoongelewa hapo juu ndizo sifa zinazomtofautisha mtu na mnyama. Kutokana na sifa hizo mtu anao uwezo wa pekee wa kuazimia lengo la maisha yake kulingana na mazingara yake.

Kazi ni matokeo ya jumla ya sifa hizo tatu za mtu: maarifa na uwezo wa kufikiri, kutumia juhudi na mali ya asili kwa shabaha ya kuendeleza kizazi na kufanya maisha yawe bora zaidi na zaidi.

Mazingara ni vitu au nguvu mbali mbali za asili ambazo huonekana katika sehemu zinamoishi jamii za watu. Vitu na nguvu hizo ni maji, milima, mabonde, mimea, misitu, wanyama, madini, hali ya hewa, mipango ya uchumi na pamoja na mifumo ya jamii za watu. Sehemu ya pili ya mazingara ni ulimwengu wa fikara na mawazo. Vitu hivyo kama vinavyoonekana katika mazingara vyaweza kuwa ni vipingamizi kwa maendeleo ya watu. Kwa mfano, maji, katika nchi ya Waeskimo, kwa sababu ya hali baridi ya hewa ya huko, maji huwa ni tatizo kwa maisha ya Waeskimo. Lakini kwa kuwa Waeskimo ni watu kamili, kama watu wengine, wakiwa na sifa zote tatu wameweza kulikabili tatizo hilo kwa kuyatumia mazingara yao hayo ili kuhakikisha usalama na maendeleo yao kama watu. Juhudi hufanywa siku hata siku kubadilisha mazingara ili kuyafanya maisha yao yawe bora, ya kuvutia na ya kupendeza zaidi.

Mfano mwingine ni kuwa mito inaweza kuwa ni tatizo kwa maendeleo ya watu. Lakini watu wameweza kuitumia mito kwa kuzalisha umeme ambao ni kitu muhimu sana katika kumwendeleza mtu. Pia watu wanapoona nguvu ya maji ya mto inawaletea uharibifu hugeuza mkondo wa mto ili wajipatie ardhi ya kutosha ya kulima; na kiasi tu cha maji ya mto huo yakaachiliwa kupitia katika mashamba kwa shabaha ya umwagiliaji wa mimea. Na pengine mfano mzuri ni jinsi watu wa Misri walivyoweza na wanavyoendelea kutumia maji ya Mto Nilo ili kuweza kuendeleza kizazi chao.

Kwa muda mrefu sana wa maisha ya mtu 'anga' ilikuwa ni haki ya pekee ya ndege (wanyama) kuitawala. Lakini kwa sababu ya uwezo wake mtu ameweza leo kutengeneza vyombo vyake

(ndege) vya kusafiria katika anga. Uvumbuzi wa ndege ni baadhi ya ushindi mkubwa ambao mtu ameupata katika kupambana na baadhi ya mazingara yake. Kwa njia hii mtu anaweza leo kutawala anga na maji; na kuifanya dunia na ulimwengu mzima uonekane mdogo zaidi kuliko hapo awali. Vile vile kutokana na ushindi huo mtu amefaulu kuufikia mwezi na kuufanya sehemu ya dunia yake kwa kutumia maroketi.

Katika ulimwengu wa mawazo au fikara mtu ameweza kupiga hatua kubwa sana japokuwa mapambano makubwa bado yanaendelea. Hapo zamani kila ulipotokea umeme na radi watu walikimbilia mafichoni. Hawakufahamu kitu gani kiliweza kusababisha nguvu hizo. Mara nyingi umeme, radi, hata mvua zilisadikiwa kusababishwa na uchawi. Lakini kutokana na maendeleo ya kisayansi, ingawaje katika jamii nyingi duniani imani hizo bado zinashikiliwa, mtu ameweza kugundua chanzo cha nguvu hizo na amegundua jinsi ya kuepukana na hatari itokanayo na nguvu hizo kwa kutumia maarifa ya kisayansi. Pia amefaulu kuzitumia nguvu hizo hizo kwa kuzalisha nguvu nyingine ambazo zinawezesha kuendesha vyombo muhimu vya kumwendeleza mtu. Hivyo, badala ya kukimbia umeme, na kadhalika, mtu huutawala na kuutumia umeme. Kifikara mtu ameondokana na imani za uchawi ambazo zilimfanya awe mnyonge kwa muda wote.

Aina nyingine ya mazingara ambayo mtu analazimika kupambana nayo ni mfumo* wa kitabaka wa jamii. Mpango au mfumo wa kitabaka wa jamii umewawezesha wajanja wachache kuwanyonya walio wengi kwa maslahi yao. Matokeo ya mpango huo ni kuwa hao wachache wamejiona kuwa wao ndio watu bora na wenye haki zaidi za maisha kuliko umma ambao hukandamizwa, hutumikishwa, hudhulumiwa, hunyanyaswa na kupuuzwa. Hivyo utaona kuwa mazingara ya aina hiyo ambayo, kama tulivyosema, husababishwa na mfumo wa kitabaka wa jamii husababisha uhusiano wa bwana na mtumwa. Lakini kwa kuwa mtu amejaliwa uwezo wa kupambana, kuyashinda na kuyatawala mazingara yake, kama si leo bali kesho, ameweza kugundua kuwa mpango au mfumo wa kitabaka wa jamii ndio chanzo cha unyonge wa walio wengi.

Ili kujikomboa kutoka unyonge wa aina hiyo mtu amebuni mfumo wa kijamaa ambao huzuia aina zote za dhuluma, matabaka, na huwapa watu wote haki na heshima sawa za kiutu.

---

* Soma sura ya nane kwa maelezo zaidi.

Maendeleo ni nini? Na kwa ajili ya nani? Haya ni maswali magumu sana. Maendeleo msingi wake mkuu ni kazi, kama ilivyoelezwa hapo juu. Kazi hufanyika wakati mtu anapopambana na aina fulani ya mazingara yake. Na kila mtu anapofanikiwa kupambana na mazingara, au kutatua matatizo yake kwa maneno mengine, huwa amepiga hatua fulani ya maendeleo. Wakati mwingine kazi huwa ya pole pole, na pengine ikawa na matokeo yakumrudisha mtu hatua moja nyuma. Hiyo bado ni safari ya kusonga mbele kwa sababu kutokana na kutokufanikiwa katika kutatua tatizo fulani mtu hulazimika kurekebisha mipango yake na kutafuta mbinu mpya na bora zaidi. Matokeo yake ni kupiga hatua mara dufu mbele. Na hapo mtu huwa ameendelea maana tatizo la aina ile hatalipata tena. Kusema kweli tatizo hilo ambalo limepata kutatuliwa huingizwa katika sura mojawapo ya historia ya maendeleo ya mtu.

Kwa mfano, suala la usafiri na mawasiliano leo si tatizo tena. Mtu amevumbua njia ya kurahisisha suala hilo kwa kutengeneza vyombo kama ndege za kurukia angani magari ya kusafiria katika nchi kavu na mwisho vyombo mbali mbali vya kusafiria majini kama vile mashua, meli na kadhalika. Vile vile simu za mdomo na upepo zimerahisisha suala la kupelekeana habari kati ya watu wa sehemu mbali mbali. Hayo yote ni maendeleo maana yanarahisisha kazi ya mtu; nayo leo ni sehemu ya historia ya ushindi wa mtu aliojipatia katika kupambana na mazingara yake. Hata hivyo, maendeleo ya watu wa sehemu mbali mbali hutofautiana kwa sababu ya tofauti ya mazingara yao.

Iko haja leo ya kukuza na kuratibu vipya historia yetu. Historia ni somo muhimu sana kwa jamii au taifa lolote. Somo la historia hutupa maarifa mbali mbali kuhusu mapambano ya mtu, mbinu na zana za aina mbali mbali ambazo mtu amepata kuzitumia katika mapambano yake kwa nyakati tofauti na katika mazingara tofauti.

Vile vile tunajifunza mambo yaliyomletea mtu ushindi na sifa katika maisha yake. Kwa sababu katika mapambano hutokea ushindi au kushindwa; pia tunajifunza kwa nini, kwa mfano, katika mapambano ya aina fulani mtu au jamii ilishindwa kujipatia ushindi. Na ili kuepukana pengine na makosa ambayo jamii zilipata kuyafanya katika mapambano ya wakati fulani itatulazimu kuwa waangalifu zaidi na kuwa na maarifa zaidi juu ya mazingara ya wakati.

Katika historia ya mapambano ya Watanzania na ukoloni wa Kijerumani wananchi wapigania uhuru, wana-Majimaji

walishindwa. Lakini kutokana na kushindwa kwao viongozi wa TANU walijifunza somo la maana sana. Nalo ni kuhakikisha kuwa kufaulu kwa mapambano ya TANU kulitegemea sana umoja wa kitaifa miongoni mwa wananchi na uongozi thabiti wa Chama cha TANU. Wana-Majimaji walishindwa kwa sababu hawakuungana katika mapambano na wala hawakuwa na kiongozi. Kinjikitile ambaye angeendelea kuwaunganisha na kuwaongoza wananchi kama kitu kimoja alikamatwa mateka na mabeberu, yasemekana, na hakuna ajuaye majanga yaliyompata kiongozi huyo wa wapigania uhuru, wana-Majimaji.

Kwa kuwa somo la historia ni fahari ya taifa hapana budi kutolewa wito. Na wito huo ni kuwa vyama vya siasa na serikali havina budi kuimarisha shughuli za utafiti wa maarifa ya historia zetu na kuziratibu katika msimamo unaokubalika. Vile vile kwa kuwa historia ya Waafrika, kwa ujumla, imepuuzwa, kukashifiwa na kupotoshwa, vyama vya siasa vya mataifa mbali mbali ya nchi huru za Kiafrika vina wajibu mkubwa wa kuimarisha shughuli ya uchunguzi wa historia za jamii za Kiafrika. Wakoloni walikashifu na kupotosha historia za Waafronodi kwa sababu walitaka kuonyesha uhalali wa kufundisha historia ya kwao ambayo sote tulilazimika kujifunza, kukariri, kuisifu na kuitukuza. Papo hapo tukalazimishwa kuamini kuwa Afrika haikuwa na historia!

Sura ya 3

SUALA LA AFRIKA KUINGILIWA NA WAGENI

Suala la wageni katika Afrika ni kubwa sana na wala siyo rahisi kulieleza. Pili, ili mjadala wowote kuhusu suala la wageni uweze kuwa wa manufaa hauna budi kuwa na shabaha ya kuleta na kusukuma maendeleo ya Waafrika.

Neno 'wageni' linatupa mara moja fikara kwamba katika Afrika kulikuwa na watu ambao ni wenyeji wa asili; na kwamba katika kipindi fulani cha historia kulikuwa na watu wa asili ya sehemu nyingine nje ya Afrika ambao walilivamia bara hili. Na iwapo fikara hiyo ni kweli, basi, kutakuwa na maswali kadhaa ya msingi ambayo yatapaswa kujibiwa. Yafuatayo ni baadhi tu ya maswali mengi ya kujiuliza: Nani Waafrika wa asili? Wageni ni akina nani? Wapi waliweka maskani yao? Vitambulisho ni nini? Kuwepo kwao katika Afrika kumesaidiaje kuharakisha au kuzuia maendeleo ya Afrika?

Afrika ikiwa ni moja ya mabara matano imekuwa na watu wake kwa nyakati zote za maendeleo ya mtu katika dunia. Ushahidi mzuri umetokana na maarifa ya masalia ya watu wa vipindi mbali mbali yaliyochimbuliwa huko Olduvai. Ni kweli pia kuwa Afrika kwa muda mrefu sana ilikuwa na uhusiano na mabara mengine. Watu wa Afrika waliweza kuhamia sehemu nyingine duniani, kadhalika watu wa mabara mengine kuhamia Afrika kutegemeana na tofauti ya mazingara katika vipindi vya kijografia. Lakini 'kwa mtu wa kawaida' mwenyeji wa asili wa Afrika ni mtu mweusi. Fikara hiyo ni nzuri na ni rahisi kueleweka. Lakini tatizo hutokea wakati tunapowaona watu weusi miongoni mwa wenyeji wa huko Bara Hindi, visiwa vya Fiji katika Pasifiki, Australia na kadhalika. Vile vile, kuna watu miongoni mwa Waafronodi ambao wana ngozi, kwa kiasi fulani, nyeupe. Kwa hiyo, jambo la msingi linalomfanya Mwafrika kuwa Mwafrika siyo rangi yake. Hakuna mtu aliyepata kuthibitisha kuwa Afrika tangu miaka 2,000,000 iliyopita ya

historia ya mtu imekaliwa muda wote na watu weusi. Kadhalika haijapata kuthibitishwa kuwa wenyeji wa mabara mengine kama Ulaya na Asia wamekuwa nyakati zote hizo watu weupe au wekundu.

Afrika kwa miaka mingi sana, inasadikiwa, iliunganika na Ulaya na Asia. Hii ina maana kuwa watu wa Afrika waliweza kuhamia sehemu nyingine za dunia kwa urahisi sana kila ilipoonekana haja ya kufanya vile. Kadhalika watu wa Ulaya na Asia waliweza kutembelea na kuhamia Afrika kila ilipobidi kufanya vile kwa sababu ya tofauti za kimazingara katika vipindi mbali mbali vya kihistoria.

Jangwa la Sahara, ambalo lilianza kujitokeza yapata miaka 5,000 au 6,000* iliyopita, liliwafanya Waafrika waishio kusini yake wasiingiliane tena kwa urahisi na Waafrika kaskazini yake, au na watu wenye asili ya Kiyuronodi na Kisanodi. Hayo ni maelezo ya baadhi ya wanahistoria.

Wanahistoria wa karne yetu wanastahili kupongezwa kwa hatua kubwa waliyopiga katika jitihada ya kuondokana na sehemu kubwa ya mikabala mbali mbali ya wanahistoria wa kale. Hata hivyo, iko haja ya kuendelea kulitazama suala hilo la mikabala kikamilifu na kwa makini zaidi. Jangwa la Sahara lenyewe lilikaliwa na watu na wala halikuwa kipingamizi kikubwa kuweza kuzuia maingiliano ya kawaida kati ya watu wa kaskazini na kusini yake. Ukweli ni kuwa mara nyingi Wabeba waliendesha biashara na watu wa kusini ya Sahara. Pia watumwa wengi kutoka sehemu ya kusini ya Sahara walichukuliwa kwa karne nyingi sana, na kupelekwa Misri, Uarabuni na Ulaya ya Kusini. Hivyo, basi, uhusiano wa aina fulani uliendelea kuwepo.

Swali linabaki sasa ni kuwa: Kwa nini watu kusini ya Sahara wamekuwa weusi na wale wa kaskazini na mashariki ya kaskazini wamekuwa weupe? Ili kulijibu swali hili kimaarifa zaidi, na hasa kwa sababu ya utovu wa uthibitisho wa kisayansi, hapana budi kwanza kuwepo na ukubaliano juu ya suala zima la rangi. Suala la watu kuwa na rangi mbali mbali si suala la msingi la kiutu. Rangi hasa ni matokeo ya tofauti ya mazingara katika vipindi fulani vya historia ya mendeleo ya mtu katika dunia. Kipindi hicho maalum hakiwezi kukadiriwa kwa idadi ya miaka kwa vile hapana njia ya kujua hata rangi ya mtu wa kwanza ambaye anasadikiwa aliishi miaka ipatayo 2,000,000 iliyopita.

---

* A.J. Wills, *Introduction to the History of Central Africa*, London, Uk. 12

Jambo jingine linalopaswa kupata kibali cha awali cha wasomaji ni kuhusu suala la uenyeji. Suala la uenyeji linaambatana sana na suala la mipaka ya maeneo ya watu. Masuala ya rangi za watu na mipaka yanatufikisha mahala ambapo tunaweza kutoa uamuzi ufuatao:

Kwanza kabisa, Afrika, kama Bara, ilikuwa na watu wake ambao tutawaita Waafronodi. Idadi kubwa ya watu wa Afrika waishio sehemu ya kusini ya Sahara na magharibi sehemu ambazo hazikuwa rahisi kufikiwa na Wayuronodi na Wasanodi ni weusi. Uweusi wao unaweza kuwa ni kithibitisho kuwa wenyeji wa asili wa Afrika, kuanzia kipindi fulani cha historia, ni watu ambao walikuwa na rangi nyeusi. Hata hivyo, ifahamike kuwa uweusi siyo msingi wa uenyeji au uafronodi bali ni moja tu ya ushahidi kuhusu uasilia wa watu wa Bara hili. Uenyeji na uasilia wa watu wa Afrika umo katika uafrika wao. Uafrika huo wa watu wa Afrika huonekana katika utamaduni, fikara, thamani za maisha, mipango na katika shughuli mbali mbali za mapambano na maendeleo yao kama watu wa Afrika.

Wayuronodi, kama watu wa asili ya Ulaya, sehemu kubwa, hufikiri, hujiona, hujihisi na hujimudu kama watu wamoja; kadhalika Wasanodi na watu wa mabara mengine. Na ndiyo maana walowezi wa Zimbabwe na Makaburu hujiona siku zote kuwa wao si Waafrika bali Wayuronodi. Kama ilivyoelezwa hapo juu uasilia wao hutegemea sana utamaduni, shughuli za kiuchumi, na fikara na mfungamano wao katika mapambano ya maendeleo yao kama watu wa moja.

Iwapo maelezo ya hapo juu yanatosheleza na kukubalika kama msingi wa mjadala, basi, Waafronodi, ambao ni watu weusi ni Waafrika wa asili wa Afrika. Na kwamba watu waishio kaskazini ya Sahara na sehemu ya mwambao wa Afrika mashariki na visiwa vyake wengi wao ni wageni. Utamaduni wao, kujimudu kwao, na fikara zao katika mapambano, kwa shabaha ya maendeleo yao kwa ujumla, huzitambulisha jamii hizo kuwa na asili moja na watu wa Asia na Ulaya, jamii zinazoizunguka Bahari ya Mediteraniani, ambao hujulikana kama Wasanodi na Wayuronodi.

Hata hivyo, tatizo la tarehe ya kuja kwa wageni hao, yaani Wasanodi na Wayuronodi, halijapatiwa ufumbuzi. Kutokana na ushahidi wa kimaandishi wageni kama Wamisri, Wabeba na baadhi ya Wahabeshi walikuwa wamekwisha kufanya maskani yao humu Afrika hata mnamo karne ya kwanza baada ya Kristo (B.K.). Ushahidi wa kihistoria, ambao unatokana na maarifa ya

masalia ya utamaduni, lugha na tekinologia – wa watu wa sehemu hizo: maandishi, majengo, vyombo na kadhalika, unathibitisha kuwa watu hao waishio leo Afrika kaskazini ya Sahara na katika Uhabeshi, pengine hata Wasomali, walikuwapo katika sehemu hizo yapata miaka 2,500 au zaidi iliyopita. Hata hivyo, suala la utamaduni na utaalam linaweza kuwa bado ni sehemu ya mjadala. Inawezekana kabisa wanahusika na asili ya utamaduni na tekinologia hiyo na baadaye kueneza katika sehemu za Uarabu na Ulaya ambako ukaendelezwa mpaka wakati wetu. Ukweli mwingine ni kwamba Wasanodi na Wayuronodi wamehamia kwa wingi katika sehemu hizi katika kipindi cha baada ya Kristo.

Suala la msingi sasa hivi ni kujaribu kuona jinsi gani wageni hao tunaowaongelea habari zao waliingia katika sehemu hizo za Afrika. Kwanza kabisa, ieleweke na kukubalika kwamba 'historia kama sayansi' ni kitu kichanga sana japokuwa historia yenyewe kama mjumlisho wa matokeo ya kazi ya mapambano na maendeleo ya mtu ina umri upatao miaka 2,000,000 ambao ni umri unaosadikiwa sasa hivi kuwa ni umri wa mtu katika dunia hii. Na hapo awali ilikubaliwa kuwa watu wa asili wa Bara hili lote ni Waafronodi. Na hao walijiona na kujihisi kama kitu kimoja. Pia walijawa – ingawaje waligawanyika katika makundi mengine madogo madogo ya kitawala na kitamaduni – na fikara ya kuona kuwa Afrika ni nchi yao; imani ambayo hata watu wa Ulaya, Marekani, Asia walikuwa nayo na kuishikilia mpaka leo. Hivyo, basi, jamii yoyote ambayo haikuwa na asili ya Kiafronodi, na ambayo ilijaribu kuingia katika Afrika ilichukuliwa kama wavamizi.

Matokeo yake ni migongano. Na katika migongano ya aina hiyo mara nyingi wenye nguvu hupishwa. Na kwa sababu leo sehemu nzima ya kaskazini ya Sahara na pwani ya Afrika mashariki kaskazini imekaliwa na watu wenye asili ya Kisanodi kuna uwezekano wa aina mbili kuhusu matokeo ya migongano; uwezekano mmoja wapo ni kuwa huenda wageni waliwashinda nguvu Waafronodi ambao wakalazimika kukimbilia na kuhamia sehemu ya kusini ya jangwa. Na uwezekano wa pili ni kuwa huenda Waafronodi wa sehemu hiyo waliuawa kwa wingi na wageni; na kwamba wachache waliosalimika walimezwa na jamii ya Kisanodi ambayo ilivamia na kuteka sehemu hizo. Na vile vile ikumbukwe kuwa uvamizi huo ulikuwa wa mara kwa mara na wala siyo wa mara moja au kikundi kimoja.

Suala la Waarabu kuzivamia sehemu za mwambao wa Afrika

mashariki, na uvamizi wa jamii za Kiindonesia katika visiwa vya Komoro na Madagaska pengine si tofauti sana na suala la uvamizi katika sehemu iliyoongelewa. Maandishi ya kwanza kuhusu kuwepo kwa Wasanodi wa Kiarabu na Kihindi katika pwni ya Afrika mashariki yanaturudisha nyuma kiasi cha miaka iisiyopungua 1,000. Lakini maandishi ya Waindonesia ambao walivamia sehemu ya mrima ya kisiwa cha Madagaska ni ya kati ya karne ya nne na karne ya saba B.K.

Maandishi hayo pamoja na masalia ya utamaduni wa Wasanodi hayatuelezi lini hasa Wasanodi walifika katika sehemu hizo na jinsi walivyoziingilia: iwapo kwa kuvamia na kuteka au kwa njia ya amani. Dhana ambayo ni ya kuaminika zaidi, kwa mtu yeyote mwenye akili timamu, ni kuwa sehemu hizo ziliingiliwa kwa uvamizi na kutekwa. Hii ina maana kuwa sehemu hizo zilichukuliwa tu baada ya mapambano makali na watu wa asili wa sehemu hizo ambao ni Waafronodi. Ikiwa hivyo ndivyo, basi, ni kweli pia kuwa 'ukoloni wa Kisanodi' katika Afrika ni wa siku nyingi sana na kwamba umekuwa wa mafanikio makubwa zaidi kuliko hata ukoloni wa Kiyuronodi wa karne ya kumi na tisa na ishirini.

Ni muhimu kutoa tofauti kati ya ukoloni wa Kisanodi (Waarabu katika Afrika kaskazini, mwambao wa pwani ya Afrika mashariki na visiwani; na Waindonesia katika Madagaska) wa kipindi hicho cha mwanzo ambacho imeshindikana kukitolea tarehe maalum; na utawala wa kikoloni wa Kiarabu katika Zanzibar na wa Kiyuronodi katika Bara zima la Afrika na Visiwa vyake baada ya 1800.

Hatua za maendeleo kati ya jamii za Kiafronodi na za Kisanodi zilikuwa tofauti hata mnamo karne ya kwanza baada ya Kristo. Wasanodi kwa ujumla, walikuwa wamepiga hatua kubwa zaidi hasa katika ulimwengu wa sayansi, tekinologia na biashara. Waliweza kutengeneza vyombo ambavyo viliwawezesha kusafiri katika bahari toka kwao hadi pwani ya Afrika ya mashariki na kuweza kuendesha biashara na Waafronodi wa mwambao. Matokeo ya biashara hiyo ilikuwa ni kukua kwa miji, ambayo kusema kweli ilikuwa ni masoko katika sehemu za mwambao. Kuondoa sehemu ya kaskazini ya Sahara, Uhabeshi, Zanzibar na Madagaska, Waarabu na Waindonesia hawakuingia sehemu za bara za Afrika ya Waafronodi mpaka karne ya kumi na tisa wakati biashara ya watumwa ilipokuzwa na kustawishwa na mataifa dhalimu ya Kiyuronodi na Kisanodi.

Wayuronodi ndio waliokamilisha mzingiro, yaani mzunguko,

wa ramani ya Afrika mnamo 1500. Afrika ya kaskazini na sehemu ya mwambao ya Afrika mashariki zilifahamika kwa Wayuronodi tangu karne ya kwanza. Ushahidi mkubwa unatokana na maandishi ya Myunani mmoja ambaye aliandika kijitabu cha 'Masimulizi juu ya biashara katika Bahari ya Shamu na Bahari ya Hindi'.

Wayuronodi, mara tu baada ya kuwasili kwao, wakaanza kuingilia siasa na utamaduni wa Waafronodi hasa huko Afrika magharibi, kusini na pwani ya Afrika mashariki na visiwa vyake.

Wareno kwa muda mrefu walikuwa katika mstari wa mbele katika kuingilia shughuli mbali mbali za Waafronodi. Lakini baadaye Wareno walifuatiwa na mabeberu wa mataifa mengine ya Kiyuronodi kama Wadachi, Waingereza na kadhalika. Katika sehemu ya mwanzo ya kuingia kwao Wayuronodi walitumia mbinu za unyenyekevu, ushirikiano wa kinafiki, udanganyifu na wa kiitifaki, yaani, wa kiprotokali pamoja na kasumba za dini na elimu. Yote hayo yalikuwa na shabaha ya kununua nyoyo, fikara na miili ya Waafronodi ili kukuza utamaduni wao na kuwatumikisha Waafronodi huko Ulaya na Marekani. Mpango huo ulifanywa kwa utaratibu sana; na ukawa mwanzo wa mpango maalum wa kuteremsha hadhi ya Waafronodi na kuwafanya, kwa makusudi mazima, waonekane mbele ya wengine, pia wajione na kujihisi, kuwa wao ni nusu watu kiutu. Na huu ulikuwa ndio mwanzo wa ubaguzi wa rangi.

Jambo muhimu la kukumbuka ni kuwa Wayuronodi hawakulivamia bara hili katika kipindi hiki kwa mabavu. Vile vile hawakufanya maskani ya kudumu hasa ukiondoa Angola, Msumbiji, Afrika ya Kusini na visiwani, mpaka mnamo karne ya kumi na tisa walipoingia ukoloni wa mabavu katika Tanzania Bara na Visiwa vyake.

Wasanodi na Wayuronodi katika Afrika, wote kwa ujumla, walizitumikisha jamii mbali mbali za Kiafronodi. Licha ya kuwanunua, kuwatesa, kuwapuuza kuwadharau na kuwauza utumwani katika nchi za kigeni, wakakuza kasumba ya kashfa kwa Mwafronodi. Wakahubiri imani kadhaa za kumfanya Mwafronodi ajione kuwa yeye ni nusu mtu, yaani, yu njiani katika safari ndefu ya kufikia upevu wa kiutu. Kasumba hizo zilikuwa na shabaha ya kumfanya Mwafronodi asiwe na imani juu ya utu na uwezo wake. Mpango huo ulikuwa ni kumwandaa Mwafronodi kuupokea utawala wa kidhalimu wa kikoloni kwa madhumuni ya kumgandamiza na kumnyonya.

Usambamba wa mjadala huu unatufikisha kwenye amuzi

kadhaa. Uamuzi wa kwanza ni kuwa Waafrika wa 1800 walikuwa ni mjumlisho, japokuwa si kifikara, wa Waafronodi, Wasanodi na kidogo Wayuronodi, hasa katika Afrika ya magharibi na mashariki, na pia katika Afrika kaskazini ya Sahara.

Uamuzi mwingine tunaofikia ni kuwa kuingia kwa wageni kulidhoofisha na kurudisha nyuma maendeleo ya aina yote ya Waafronodi wakati ambapo Wasanodi na Wayuronodi wa Kiafrika na wa mabara ya asili zao walikuwa wanajiendeleza katika mambo mbali mbali. Uamuzi wa tatu ni kuwa wageni hao kwa kutumia kasumba mbali mbali hasa kasumba ya 'Kihamati,' walijenga na kuimarisha utengano na uhasama baina ya makundi hayo mawili ya Waafrika, yaani, Waafronodi kwa upande mmoja na wao wenyewe, yaani, Wasanodi na Wayuronodi. Na ili leo Waafrika waweze kujiendeleza kama wamoja ni lazima kwanza kusafisha na kuondokana na kasumba ya Kihamati ambayo inamfanya Msanodi na Myuronodi kwa sababu ya rangi yake, ajione yeye ni bora kuliko Mwafronodi ambaye ni Mwafrika mwenzake. Na kwa upande mwingine Mwafronodi naye aondokane na kasumba ya kuwa yeye amezaliwa mnyonge; na kwamba Afrika ni kwa ajili ya Waafronodi tu, yaani, watu weusi ambao wameenea sehemu kubwa ya kusini ya Sahara. Afrika ni moja, na kwamba Waafronodi na wageni ambao wameishi humu Afrika kwa mamia na maelfu ya miaka hawana budi kutambuliwa; na wao wenyewe, yaani, Wasanodi na Wayuronodi sherti wajione na kujihisi kuwa wao ni kitu kimoja na jamii moja na Waafronodi; na kwamba leo wote ni Waafrika. Kasumba ya Kihamati ambayo ni ya ubaguzi ni kizuizi kikubwa sana kwa juhudi za kuleta umoja kwa madhumuni ya kuendeleza ukombozi wa Bara zima la Afrika. Kasumba nyingine ambazo zimevunja moyo na kurudisha nyuma juhudi za umoja wa watu wa Afrika zimejengwa juu ya msingi wa imani za dini ambazo tumeletewa na wageni wa Kisanodi na Kiyuronodi. Usemi huu hauna maana kuwa imani zenyewe ni mbaya bali wageni wenyewe wamezitumia imani hizo vibaya ili kujinufaisha wenyewe binafsi.

Jambo muhimu la kuzingatia ni kuwa si shabaha ya mwandishi kutukuza fikara ya rangi ambayo mara nyingi imeonyesha ubaguzi na mtengano. Shabaha ni kujaribu kuondoa kasumba hiyo ya rangi ambayo wakoloni wameitumia katika kuwatenga na kuwagawanya Waafrika. Na vile vile ifahamike kuwa maneno: Yuronodi, Asanodi na Afronodi hayana msingi wa

JAMII KUU ZA AFRIKA KIASILI



JAMII KUU ZA AFRIKA.

Jamii kilugha	Kikundi cha asili	Jamii kiasili
Wakushito	Wasanodi	Wasanodi (Waafrika wageni)
Wabantu Wanilo	Wakansanodi	
Wakichembe	Wakaprinodi	Waafronodi

kuwagawanya watu katika msingi wa rangi au maumbile bali rangi yaweza kuwa moja ya ushahidi wa asili za jamii. Maana si kweli kuwa watu wote weupe ni Wasanodi na Wayuronodi na wala si kweli pia kuwa watu wote weusi ni Waafronodi. Ili kukamilisha suala la mgawanyo wa jamii za Kiafrika budi tutumie ushahidi utokanao na maarifa ya lugha. Na kwa kufuatia maarifa yaliyotolewa na mtaalam wa lugha za Kiafrika, Greenberg, Waafrika, hasa tukiongea juu ya Waafrika waishio leo kusini ya Ikweta, wamegawanyika katika makundi ya Wakushito, Wabantu, Wanilo na Wakichembe.

Sura ya 4

SUALA LA UHAMAJI NA UVAMIZI WA KIAFRONODI

Maendeleo ya mtu kwa muda mrefu sana yalikuwa ya pole pole sana. Hatua kubwa na za haraka za maendeleo ya mtu zimepigwa kuanzia miaka 10,000 iliyopita, yaani, baada ya mapinduzi ya kwanza ya kilimo. Kabla mtu hajagundua maarifa ya kilimo na ufugaji mtu aliishi kwa kukusanya matunda, mizizi na uwindaji wa wanyama wa porini. Maisha yalikuwa magumu, na ya kutangatanga. Hapakuwa na uhakika wa maisha. Jamii za watu zilikuwa ndogo ndogo; na idadi ya watu kwa ujumla haikuwa kubwa.

Kilimo kilileta sura mpya ya maisha. Jamii ambazo zilifikiwa au zilizopata kuvumbua maarifa ya kilimo zilianza kuishi pamoja kwa 'wingi' na maskani yao yalikuwa ya 'kudumu'. Neno kudumu lisichukuliwe kwa maana ya wakati wetu. Jamii za leo kwa sababu ya maendeleo ya kitaalam, kitekonologia, kisayansi na kadhalika, zinajenga majengo ya kudumu; zinatumia njia mbali mbali za kurutubisha ardhi iliyochoka na kwa jinsi hiyo kuweza kuongeza uwingi wa mazao kutokana na eneo dogo. Jamii za kale hazikuwa na utaalam huo.

Kwa hiyo, ingawa kilimo kiliziwezesha jamii kuishi pamoja katika vijiji, mara nyingi jamii zilikuwa zikihama-hama hasa kila ilipoonekana ardhi ya mashamba yao imechoka. Kilimo ambacho kiliwapa watu hakika ya maisha kiliwafanya watu waongezeke kwa wingi na kwa haraka. Kwa sababu ya uhaba wa ardhi bora ya kilimo na ya mifugo wakati mwingine baadhi ya watu ilibidi wapungue kwa kuhamia sehemu nyingine ambazo zilifaa kwa kilimo na malisho. Uhamaji wa aina hii haukuwa wa mbali sana. Watu au jamaa zilihamia sehemu za ujirani na mara nyingi waliendelea kuwa ni sehemu ya jamii watokanayo au jamii wanayojiunga nayo.

Lakini inafahamika kihistoria kuwa mara nyingi, hasa katika Afrika, kama ilivyofanyika katika mabara mengine, watu

walihama katika makundi na kwenda kuanzisha maskani na tawala mpya katika sehemu za mbali. Afrika, kama inavyoonyesha ramani yetu ilikaliwa na watu sehemu zote. Hivyo, basi kila ilipotokea kundi la watu wa jamii fulani kuhamia sehemu nyingine ilipaswa wapambane na wenyeji wa sehemu hiyo. Ushindi katika mapambano ulitegemea maendeleo ya kifundi na kitekinologia hasa zana. Ilipotokea wageni kuwashinda wenyeji wao, wageni hao walianzisha makazi na tawala juu ya wenyeji wa asili wa sehemu hiyo.

Kutegemeana na idadi ya watu utamaduni wa jamii mpya uliweza kuwa ni wa wageni au wa wenyeji; na pengine ni mchanganyiko wa tamaduni za jamii zote mbili. Lakini fikara na mpango mzima wa mfumo: uchumi na utawala, ulikuwa ni wa jamii inayoteka na kutawala.

Kwa mfano, Wangoni kutoka Afrika ya Kusini walipofika Songea wakapambana na wenyeji wa asili wa sehemu hiyo na kuwateka. Jambo lililofuata ni kujenga utawala wa Kingoni. Lakini kwa kuwa Wangoni walikuwa wachache walichukua sehemu kubwa ya utamaduni wa wenyeji wa sehemu hiyo. Wenyeji nao waliiga mengi kutoka kwa wageni wao. Hivyo, lugha na mila ambazo leo zinatumika huko Songea hadi sehemu za Ziwa Nyasa, kwa sehemu kubwa, ni za jamii za asili za sehemu hizo.

Katika Afrika ya Waafronodi inasadikiwa kuwa makundi ya wahamiaji na wavamizi, wa miaka 3,000 iliyopita, yalitokana na jamii za Kikansanodi. Mara nyingi, hasa katika hatua za mwanzo za uhamiaji, makundi ya Wakansanodi yalihamia na kuziteka sehemu zilizokaliwa na Wakaprinodi. Hali hiyo yasadikiwa ilisababishwa na tofauti ya hatua za maendeleo tangu yapata miaka 6,500 iliyopita. Wakansanodi walikuwa ni wakulima na wafugaji. Maarifa ya kilimo yalivumbuliwa huko Afrika Magharibi na watu wa jamii ya Wamande na baadaye kuenezwa katika sehemu nyingine za Afrika. Maarifa ya kilimo na ufugaji yalienezwa pia katika sehemu nyingine za Wakaprinodi na Wasanodi kutoka kaskazini (Misri) kwa njia ya mto Nile na pia kutoka Afrika ya kaskazini Mashariki. Pia inasadikiwa kuwa yapata miaka 3,000 iliyopita Wakansanodi walikuwa na maarifa ya uhunzi na ufuaji wa zana na vyombo vya chuma. Wakaprinodi, kwa upande mwingine walikuwa bado na maisha ya kikarne ya mwisho ya mawe. Wao, inaaminika, walijifunza ufuaji na matumizi ya vyombo vya chuma, siyo maarifa ya utengenezaji wa chuma, kutoka kwa Wakansanodi na Wayuronodi

kwa upande wa Wakaprinodi wa Afrika ya Kusini.

Kutokana na maarifa ya chuma ni dhahiri kuwa Wakansanodi walikuwa na nguvu zaidi ya kudiriki kuwavamia na kuwashinda Wakaprinodi ambao zana na vyombo vyao vilikuwa bado vya mawe na hafifu. Kutokana na ushahidi mbali mbali tuliopata uvamizi wa Wakansanodi kwa Wakaprinodi ulianza yapata miaka 500 k.k. na kuendelea hadi karne ya kumi na mbili wakati Wanguni na Wasutu walipoingia sehemu iliyo kusini ya Mto Limpompo.

Ili maelezo ya uvamizi na mapambano ya Wakansanodi yaweze kuwa na ufasaha itabidi kuzigawa jamii zilizohusika na uvamizi kusini ya Ikweta kuanzia miaka 3,000 iliyopita katika jamii za Kilugha au Kiisimu. Makundi hayo ya lugha ni: Wabantu, Wanilo, Wakichembe na Wakushito. Kwa sababu Wakushito ni wachache sana katika Afrika ya Waafronodi, na kwamba wanakomea Kenya tu na Tanzania hapana haja ya kuzungumza sana habari zao katika sura hii. Kiasili Wabantu na Wanilo ni Wakansanodi. Wakichembe ni Wakaprinodi na Wakushito, kwa sehemu kubwa, ni watu wenye asili ya Kisanodi. Kabla ya kueleza hatua mbali mbali za uvamizi wa Kikansanodi ni busara kwanza kuzungumza juu ya watu ambao waliishi katika sehemu hiyo ya Afrika ambayo iliingiliwa na kutekwa na jamii za Kikansanodi. Kwa ufupi, waliotekwa ni Wakichembe.

Wakichembe ambao ni wakaprinodi ni watu wa asili wa Bara la Afrika walioishi kusini ya Ikweta. Wakichembe ni watu wasemao lugha za Kichembe, yaani, hugongagonga ulimi. Idadi yao leo katika Afrika ni ndogo sana. Watu hao walikuwepo hapa nchini tangu zama zote na kwamba Wabantu walipohamia sehemu hizi kutoka katika nchi yao ya asili huko Katanga ya Kaskazini, kama inavyosadikiwa, waliwakuta.

Kwa vile Wakichembe wanasadikiwa kuwa hawakuwa wameendelea sana kiuchumi, kisiasa na kitamaduni kama Wabantu hawakuweza kushindana na wahamiaji wa Kibantu. Wengi wao huenda waliuawa na wengine kufukuziwa katika sehemu za kusini. Leo Wakichembe wanaonekana hasa katika sehemu za jangwa la Kalahari. Wahotentoti na Wakalahari* wa Afrika ya kusini; Wasandawi na Wahadizapi au Watindiga katika Tanzania Bara ndizo jamii pekee za Kichembe katika Afrika nzima.

---

* Wakalahari–jamii za Kichembe zinazoenea katika sehemu za Kalahari.

Kwa upande wa utamaduni Wakichembe popote katika Bara hili, hujulikana sana kwa uchoraji wa picha katika miamba ya mawe na mapangoni walimokuwa wakiishi. Wakichembe hawakuwa na vibanda vya kuishi kama vile Wabantu. Masikani yao yalifanywa chini ya ardhi au katika mapango kati ya miamba ya mawe. Na wengine wanaendeleza maisha ya aina hiyo mpaka leo japokuwa juhudi, hasa katika Tanzania, zinafanywa kuzikomboa jamii zao.

Wakichembe hawakuwa wakulima kabla ya kuja kwa Wabantu katika nchi hii. Maisha yao yalitegemea mawindo ya wanyama na ukusanyaji wa matunda na mizizi ya porini kwa chakula chao. Vyombo na silaha zao pia zilikuwa bado za kipindi cha tatu cha mawe. Hii inaonyesha kuwa hawakuendelea sana na kwamba hawakuweza kuishi mahali pamoja kwa vile iliwabidi kuwafuata wanyama huku na huko. Tukiwaondoa Wahotentoti wa Afrika ya Kusini, ambao walifuga ngo'mbe na kondoo kabla ya kukutana na Wabantu na Wayuronodi, Wakichembe hawakuwa na mifugo. Na jambo la kukumbuka ni kuwa Wakichembe daima walikuwa ni watu wa kuvamiwa. Hata hivyo, haina maana kuwa Wakichembe walinyamaza tu. Mara nyingi walionyesha, kama watu huru, upinzani japokuwa mara nyingi yaelekea ushindi umekuwa wa Wabantu.

Jamii iliyohusika na uvamizi wa kwanza kwa Wakapirinodi ni jamii ya Kibantu. Neno Bantu katika vitabu vingi limeelezwa na kupewa maana mbalimbali ya upotovu. Wengine wamewahi kukazia kuwa Wabantu ni watu ambao asili yao ni mchanganyiko wa jamii za Kisanodi na Waafronodi; nao wakapangwa kadiri ya maumbile yao.

Kusema kweli hakuna mtu anayeweza kumwonyesha mwenzake au kikundi cha watu kuwa yeye au wao ndio au sio Wabantu kutokana na rangi au maumbile yao. Wabantu ni watu gani basi? Wanahistoria wa kisasa hukubaliana kwa ujumla kuwa Wabantu ni 'jamii za watu ambao huzungumza lugha zenye asili moja'. Hii ina maana kuwa hapo zamani za kale palikuwa na kikundi cha wananchi katika Afrika ambacho kilionngea lugha maalum; na wala lugha hiyo haikuitwa Kibantu bali ilijulikana kwa neno la lugha ya jamii hiyo. Wataalam wa lugha wamependekeza kuziita jamii zote zinazotumia lugha ambazo asili yake, kama ilivyoelezwa sasa hivi, ni huko Katanga ya Kaskazini: 'Wabantu'. Uvamizi wa Kibantu unagawanywa katika hatua kuu nne.

Yapata miaka 500 au 1,000 K.K. kikundi cha watu kutoka

Afrika magharibi, hasa katika sehemu ya Kameruni kama ilivyoandikwa na wengi, kilisafiri hadi kufika Katanga ya Kaskazini ambako kilianza kufanya maskani yake. Pia inakisiwa kuwa watu hao walisafiri kwa mitumbwi kupitia bahari ya Atalantiki hadi kwenye mdomo wa mto Kongo na baadaye kusafiri katika mto Kongo wenyewe mpaka kufikia sehemu hiyo ya Katanga. Mazingara ya nchi ya Katanga yalifanana sana na mazingara ya nchi yao ya asili. Pia katika Katanga kulipatikana, kusema kweli mpaka hivi leo, shaba nyekundu na chuma kwa wingi sana. Kwa vile wasafiri hao walikuwa ni wakulima, wafugaji na wafua chuma Katanga palionekana ndipo mahali pa kufaa kufanya maskani yao mapya. Hivi wakaendelea na kilimo cha aina mbali mbali cha mtama na ulezi, na ufugaji. Kama wafua chumawaliweza kuchimbua mawe ya chuma, kuyayeyusha na hatimaye kutengeneza vifaa mbali mbali vya kilimo na shughuli nyingine pamoja na zana za vita.

Tofauti za kiuchumi kitekinologia na kitamaduni ndizo zilizowawezesha Wabantu kuziteka zile sehemu za Wakichembe maana silaha za chuma ni bora kuliko silaha za mawe na ambazo wakati wake ulikuwa umepita pia. Hivyo, basi, Wakichembe wengi huenda waliuawa katika mapambano na wengine kufukuziwa katika sehemu kame zisizotakiwa na wakulima wa Kibantu. Na kwa sababu ya wingi wa chakula Wabantu waliweza kuongezeka kwa haraka sana wakati wote. Kuongezeka huko ndiko kulikosababisha tena baadhi ya watu kuhamia na kuziteka sehemu zaidi zilizokaliwa na Wakichembe.

Kutokana na tafasiri yetu ya Wabantu tuliyoitoa hapo juu mababu wa Wabantu hawakuwa Wabantu kwa sababu hawakuwa wanaongea lugha ambayo wataalam wa elimu ya lugha leo wamependekeza kuiita Kibantu. Kwa maana kufuatana na maelezo ya hapo juu, lugha ya Kibantu iliundwa na kukuzwa kwa mara ya kwanza katika Katanga. Hivi, basi, Wabantu wa kwanza ni wale ambao walianza kuongea lugha ya Kibantu nao wakiwa wakazi ama wananchi wa Katanga ambao, kwa kusema kweli, asili yao ilikuwa ni Kameruni. Huko Kameruni walikuwa wanaongea lugha za aina nyingine ambazo wataalam wa lugha wameziita majina tofauti.

Hivyo basi, katika hatua yao ya pili Wabantu hao wa kwanza walihamia kutoka Katanga kuelekea magharibi na kusini na kufanya maskani yao katika sehemu za mrima za pwani ya Bahari za Atalantiki na Hindi. Uhamiaji huo ulifanyika kati ya karne chache kabla ya kuzaliwa Kristo na karne za mwanzo

baada ya kuzaliwa Kristo. Na kama ilivyodokezwa hapo juu sababu zilizowafanya wahame nchi yao ya Katanga ilikuwa ni mwongezeko wa idadi ya watu ambao ulisababishwa na 'neema' ya chakula kutokana na mapinduzi ya kilimo. Hivi, basi, kwa jinsi idadi ya watu ilivyoongezeka na ndivyo ardhi bora, kwa kawaida ardhi mpya, ilivyozidi kuadimika. Kwa hiyo, baadhi ya watu ilibidi waondoke ili kutafuta ardhi mpya katika sehemu nyingine. Pia hatuna budi kukumbuka kuwa uhamaji huo haukuwa wa mara moja bali ulikuwa ni jambo la daima na kila shida ya ardhi ilipotokea. Uhamaji na uvamizi wa Kibantu unaweza pia kuelezwa katika msingi wa harakati ya mapambano baina ya jamii zilizoendelea na zisizoendelea. Huo haukuwa ubeberu wala si ukoloni hasa tukizingatia maana ya ubeberu na ukoloni ambao hueleweka vema katika msingi wa mpango wa uzalishaji mali na uhusiano wa watu.

Huko katika pwani ya mashariki Wabantu walipata kukutana na wafanyabiashara kutoka Uarabuni na Bara Hindi. Yasadikiwa pia kuwa Wabantu walikutana na jamii za kutoka Mashariki ya Mbali kama vile Indonesia. Wasanodi wa kutoka Indonesia waliwahi kupitia katika pwani ya Afrika mashariki kati ya karne ya kwanza na ya nane B.K., kama inavyosadikiwa na wana-historia wengi. Wasanodi hao wa kutoka Indonesia yasadikiwa, waliingiza mazao mapya mawili katika Afrika mashariki, nayo ni: ndizi na viazi. Kati ya mazao hayo mawili ambayo yalipokelewa na Wabantu wa mrima kama inavyosadikiwa, migomba ambayo huhitaji kazi ndogo sana iliweza kustawishwa kwanza katika sehemu za pwani. Kwa kuwa mgomba ni mmea wa kudumu na unaojiongeza wenyewe muda wote idadi ya Wabantu wa pwani na mrima iliongezeka kwa haraka na hatimaye kuleta tena shida ya ardhi kwa ajili ya kilimo na malisho. Basi baadhi yao ilibidi wahamie sehemu nyingine ambako migomba ingeweza kustawi vema.

Kwa vile migomba hustawi sana katika sehemu za joto jingi na zenye mvua nyingi, Wabantu, katika hatua yao ya tatu ya uhamaji, walichagua kuhamia katika sehemu ya nyanda za juu za Afrika. Na hii ndiyo sababu leo Wabantu wanaolima zao hilo kwa wingi na kulifanya chakula kikuu huonekana katika sehemu za nyanda za juu, kwa mfano, Uchagani, Upare, Usambara, Bukoba, Tukuyu na kadhalika, katika Tanzania. Katika Uganda zao hilo limeenea sana hasa katika sehemu ya Buganda.

Katika hatua yao ya nne na ya mwisho ambayo iliendelea hadi mnamo karne ya kumi na tisa baadhi ya Wabantu waliopatwa na

shida ya ardhi waliweza kuhamia sehemu ambazo ziliachwa wazi au hazikujazwa sana na watu katika hatua ya pili na ya tatu. Hii haina maana kuwa Afrika leo imejaa na kufurikwa na watu.

Sehemu nyingi sana bado ni mapori. Lakini kwa jinsi idadi ya watu inavyozidi kuongezeka kwa upesi upesi kutokana na chakula bora, afya bora, kutokana na utabibu wa kisasa, ndivyo jamii zitakavyoona haja ya kuhamia na kwenda kufungua makazi mapya. Lakini jambo la kukumbuka ni kwamba safari hizo za uhamiaji zilzofanyika katika hatua hii ya nne na zile zinazofanyika sasa na zitakazofanywa kwa siku za usoni haziwezi kuwa tena ndefu kama zile za hatua ya kwanza hadi ya tatu au za jamii za Kinguni kutoka Afrika ya Kusini hadi Afrika ya Mashariki katika karne ya kumi na tisa. Habari za Wanguni zimeelezwa kwa kirefu katika sura ya sita na saba. Jambo la kuzingatia ni kuwa mpaka mnamo karne ya kumi na mbili Wabantu walikuwa wameteka karibu sehemu zote za Wakichembe, kuanzia Ikweta mpaka kusini ya Mto Limpompo isipokuwa sehemu ya Jimbo la Rasi ya Afrika ya Kusini, jangwa la Kalahari, na kwa kiasi fulani kwa sababu zisizofahamika, wilaya ya Kondoa katika Tanzania Bara.

Wabantu ambao walivamia na kuziteka nchi za Wakichembe walifuatiwa na jamii za Kinilo kati ya miaka 1300 na 1500 B.K. Wanilo ambao waliishi kwa mifugo na mashambulio walizishambulia sehemu ambazo sasa zilikaliwa na jamii za Kibantu. Huko wakaanzisha tawala zao za kifalme na Wabantu wakafanywa raia. Wanilo, inasadikiwa, hawakupambana na Wakichembe hata mara moja.

Wanilo ni watu wanaozungumza lugha ya Kinilo. Asili yao ni katika nchi ya Sudani ambako ndiko mababu zao waliishi kwanza na kustawisha aina ya lugha zisemwazo na jamii za Kinilo. Neno 'Nilo' limebuniwa na kupendekezwa na wataalam wa lugha ili kueleza jamii zinazozungumza lugha za aina hiyo katika Afrika, hasa, Afrika Mashariki.

Wanilo hugawanyika katika makundi matatu kama ilivyoonyeshwa hapo chini. Wengi wao huishi huko Uganda na Kenya na baadhi yao katika Tanzania Bara. Wanilo hawakuweza kupenyeza na kuvamia sehemu ya kusini ya Ikweta zaidi ya Tanzania kaskazini. Makundi hayo matatu ya Kinilo katika Tanzania ni:—

Kikundi	Mifano
1. Wanilo wa sehemu za mito na ziwa	Wajaluo
2. Wanilo wa Nyanda za juu	Watatoga
3. Wanilo wa nyika	Wamasai

Wahamiaji wengine ambao ni kundi la mwisho kutokea kaskazini, yaani, Sudani ya kusini ni Wahima au Watusi. Asili ya kundi hili la wavamizi katika Afrika mashariki haifahamiki sana kadiri ya maelezo ya wanahistoria wengi. Watu hao, mara nyingi kwa sababu ya umbile na rangi yao, hufikiriwa kuwa wana asili ya Kisanodi au Kiyuronodi. Na kwamba wanahistoria wengi wamediriki kutamka kuwa huenda Wahima asili yao ni Uarabuni, au Uyunani, au Ureno, au Misri au Uhabeshi. Hizo zote ni fikara za kupotosha zitokanazo na kasumba ya Kihamati.

Kwa fikara za uchokozi wa mwandishi wa kitabu hiki, Wahima ni moja ya makundi ya Waafronodi wa asili ya Kikansanodi ambao walihamia na kuzivamia sehemu za Wabantu kuanzia karne ya kumi na sita hivi.

Kutegemea maarifa ya lugha ni vigumu sana kuamua kuwa Wahima walikuwa ni watu wa asili ya jamii ipi. Maana Wahima leo huongea katika sehemu zote walizoziteka lugha za wenyeji wao ambao ni Wabantu. Umbile na mjengo wa watu hao pia hautuwezeshi kufikia uamuzi unaokaribiana na ukweli. Maumbile ya watu hubadilika haraka sana kutegemea aina ya maisha, chakula, shughuli hata fikara za watu. Wahima kwa muda mrefu wameishi kwa nyama na maziwa na baadaye wakiongezea ndizi na aina nyingine ya vyakula vya aina ya nafaka kama vyakula vya sunaa. Vile vile baada ya kuzivamia jamii za Kibantu Wahima wakajifanya ndio watawala.

Matokeo yake ni kuwa Wahima walikuwa na fikara huru zaidi kuliko jamii za Kibantu walizozitawala, kuzikandamiza na kuzinyonya. Kwa jinsi hiyo Wabantu walikuwa wanyonge, vyombo vya kuzalisha mali kwa ajili ya tabaka la makabaila wa Kihima. Unyonge na uhuru wa fikara una uhusiano mkubwa sana na maendeleo ya mjengo wa maumbile ya jamii yo yote ile. Wanyonge mara nyingi huwa na fikara duni na hukubali kila lisemwalo na wakubwa; na hali hiyo husababishwa na woga ambao ni matokeo ya kukandamizwa, kutumikishwa na kunyonywa kwa muda mrefu. Vile vile katika jamii ya kitabaka utu wa wanyonge hauthaminiwi bali utu wa tabaka la wastahiki. Afya bora, chakula bora, shibe, malazi bora, furaha, faraja na heshima vyote huwa kwa ajili ya tabaka hilo. Haya yote huwaletea wastahiki hao maendeleo bora ya kiumbile, kifikara, kisiasa na kitamaduni.

Wanyonge hulazimishwa kuupokea utamaduni wa tabaka hilo la watawala ambao ni wa kigeni.

Kutokana na mjadala huu mmoja anaweza kudiriki kutamka kuwa Wahima ama Watusi, kwa jina jingine, walikuwa na asili ya Kinilo. Kwa kuwa walitokana na koo zenye asili moja, tena siyo karne nyingi zilizopita, na kwa sababu ya mpango wao wa uchumi na maisha Wahima walimudu kuendeleza mjengo wa umbile lao popote walipoanzisha maskani yao katika Afrika Mashariki. Na kwa sababu ya uchache wao kikundi hiki cha Kinilo kililazimika kupokea lugha za Wabantu ambao ni wenyeji wao. Hivyo, basi, hakuna sababu ya kuzidi kuzingatia mkabala wa kale ulio na kasumba ya kihamati. Jambo muhimu la kukumbuka ni kuwa tawala zilizojengwa na Wahima zilikuwa za kifalme na kikabaila kiumbile.

Kwa ujumla, Wanilo mpaka karne chache tu zilizopita hawakuwa na makao maalum. Maisha yao ama chakula chao kikuu kilikuwa ni maziwa na nyama. Kilimo kwao hakikuwa jambo la kuthaminiwa. Kwa maneno mengine wao walikuwa na wanaendelea kuwa wafugaji.

Kwa sababu ya kuishi jirani na Wabantu, Wanilo wamepata kutambua umuhimu wa kilimo; na kwamba wengi wao sasa hufanya maskani ya 'kudumu' na kulima chakula huku wakiendelea na mifugo yao. Mfano mzuri wa Wanilo waliotulia ni Wajaluo na Waarusha. Wanilo ni miongoni mwa jamii ambazo zilikuwa na maarifa ya chuma. Hata hivyo, Wanilo wanajulikana sana kwa kuunda serikali za muungano wa jamii nyingi. Licha ya kuunda serikali za utawala msonge—Wanilo walikuwa na zana na vyombo vya chuma kwa vile walijua jinsi ya kufua chuma. Hivyo basi, kwa mambo ya vita waliweza kushindana na Wabantu ambao, kama ilivyoelezwa, walikuwa wahunzi na wafua chuma. Lakini kwa kuwa Wanilo walitegemea mifugo tu hawakuweza kuwa na maskani ya kudumu kama Wabantu. Walikuwa na tabia ya kuhamahama japokuwa uhamaji huo ulikuwa katika maeneo maalum ambayo yalijulikana kama ni ardhi yao. Mara nyingi Wanilo walihama na kuzivamia sehemu za Wabantu kama ilivyoelezwa hapo awali. Tabia hiyo ya kuhamahama na uvamizi iliwafanya Wanilo wajiendeleze zaidi katika mambo ya vita kuliko Wabantu ambao walikuwa sasa na tabia ya kutulia mahali pamoja na kuendeleza maisha ya amani pasipo wasiwasi. Hata hivyo, uvamizi wa Kinilo ulizuiwa na kupingwa kwa mafanikio sana na jamii za Kibantu katika Tanzania mnamo karne ya kumi na tisa baada ya baadhi ya jamii hizo za Kibantu

kuungana. Ilikuwa ni jamii ya Kigogo iliyopambana na Wamasai na kuzuia kabisa jamii za Kinilo kusonga kusini zaidi katika miaka ya 1830 B.K.

Wakushito ni jamii nyingine ya Kiafrika, kadiri ya tafasiri yetu ya Mwafrika, ambayo watu wake huzungumza lugha zenye asili moja. Kiasili sehemu kubwa ya Wakushito ni Wasanodi, na kwamba kilugha wana uhusiano sana na Wasanodi wa Kiarabu. Hata hivyo maelezo ya Daktari J.E.G. Satoni kwamba Afrika Mashariki, 'wakati fulani ilikaliwa na watu wenye asili ya Kisanodi, kwa sababu ya maumbile yao ni ya kupotosha. Kadhalika maelezo yake juu ya kujitokeza kwa 'Waswahili' katika pwani ya Afrika Mashariki; wakiwa ni matokeo ya mchanganyiko kati ya Wabantu na Wasanodi ni ya kuhatarisha.

Ili kupata picha nzuri juu ya Wakushito kuna ulazima wa kulikabili suala la watu hao kwa njia ya mjadala. Inawezekana kabisa kuwa Wakushito walikuwa ni wahamiaji katika Afrika kutoka mabara ya Ulaya na Asia. Maelezo na mjadala wa kutosha juu ya fikara za mtungaji umetolewa katika sura ya tatu juu ya 'suala la Afrika kuingiliwa na wageni'. Wakushito ilikubalika kuwa ni wageni waliolivamia Bara hili tangu miaka mingi kabla hata ya Kristo. Hata hivyo, idadi kubwa ya wavamizi hao wa Kisanodi imehamia katika Afrika ya kaskazini na mashariki katika kipindi cha miaka 2,000 iliyopita.

Kwa kuwa watu hao wameishi mamia kwa maelfu ya miaka katika Afrika ilikubaliwa pia kuwa wao ni Waafrika halisi kama Waafronodi kwa vile hawana tena sehemu nyingine, ukiacha kifikara, ambayo wanaweza kuiwekea madai kuwa ni makwao.

Lakini kufuatana na mjadala juu ya Wahima, ambao tumewaita Wanilo, Wakushito wa Afrika ya mashariki kaskazini na kusini inawezekana kabisa kuwa ni Waafrika wenye asili ya Kisanodi.

Suala la Waswahili bado ni tatizo kubwa. Watu wa mwambao wa Afrika Mashariki hujulikana kwa majina mbali mbali ya kijamii na kwamba wote ni Wabantu. Kiswahili, kama lugha, hakitokani na Kiarabu au lugha za jamii nyingine bali hutokana na lugha za Kibantu. Kama lugha za mataifa mengine katika dunia Kiswahili kina maneno kadhaa ya kuazima kutoka Kiarabu, Kireno, Kiingereza, Kijerumani, Kiyunani na kadhalika. Karibu msamiati wote na sarufi nzima ya Kiswahili msingi wake ni lugha za Kibantu. Kwa hiyo, 'Waswahili' kama jamii katika Afrika hawajapata kuwepo bali Kiswahili kama lugha iliyokuzwa katika mwambao kwa madhumuni ya jamii mbali mbali za

Kibantu na kigeni kuelewana katika kuendesha biashara, kipo. Vile vile si kweli kwamba kulikuwa na kuoleana kati ya wageni na Wabantu kiasi hata kusababisha jamii mpya ya machotara, yaani, Waswahili.

Ukweli ni kuwa baadhi ya Waarabu na Wahindi waliwavamia mabinti wa Kibantu na kuzaa nao. Lakini machotara hao hawakuwa wengi kiasi cha kusababisha kuundwa kwa jamii mpya. Na kama kungekuwa na kuoleana katika maana halisi ya neno, suala la kuoleana baina ya Waafronodi na Wasanodi leo lisingekuwa tatizo tena bali lingekuwa jambo la kawaida, na la mazoea.

Wakushito kama Wanilo walitegemea mifugo; na chakula chao kikuu kilikuwa maziwa. Kwa sababu ya mifugo yao Wakushito walipendelea kuishi katika sehemu za nyika zisizo na mvua nyingi. Kwa upande mwingine, Wabantu, kwa sababu ya kilimo, walipendelea kuishi katika sehemu za milimani na zenye misitu na mvua kwa wingi. Kisiasa Wakushito walijenga serikali za kifalme; na kwamba kimfumo jamii za Kikushito zilikuwa za kitabaka.

Sura ya 5

SUALA LA UVAMIZI KATIKA AFRIKA YA KUSINI

Karibu asilimia tisini na tisa ya watu waishio leo kusini ya Ikweta ni Wabantu. Neno 'Bantu' limeelezwa kwa kirefu katika sura ya nyuma. Ili kuelewa vyema matatizo yanayowakabili ndugu wa huko Afrika ya Kusini na Namibia maarifa machache hayana budi yatolewe kuhusu jamii, asili, desturi, uchumi na siasa zao za jadi; na kadhalika. Jamii za leo za huko Afrika ya Kusini ni kama zifuatazo:—

Kama ilivyopata kuelezwa hapo awali, Wakichembe ni watu wenye kuongea lugha za kugongagonga ulimi kama wafanyavyo Wasandawi na Watindiga wa huko Kondoa. Wakichembe wa huko Afrika Kusini ni Wahotentoti na Wakalahari. Watu hao ni wenyeji wa asili wa Afrika Kusini; nao ni wana wa Wakaprinodi ambao ni Waafronodi.

Tukiwaondoa Wakalahari, Wahotentoti peke yao ndio walipata kuwa wafugaji wa ng'ombe na kondoo kwa miaka mingi kabla ya kuingiliwa na Wabantu ambao ni Wakansanodi na Wayuronodi kutoka Ulaya kwa mujibu wa maelezo ya walowezi wa Kiyuronodi. Kwa upande mwingine Wahotentoti walifanana na Wakalahari kwa vile wote "hawakuwa na maarifa ya kilimo na ya kutengeneza vyombo na zana za chuma". Hivyo, waliishi kwa kuwinda wanyama na kuokota matunda na mizizi ya porini; na kwa jinsi hiyo, idadi yao haikuweza kuongezeka kama Wabantu walivyopata kuongezeka kwa sababu ya chakula kingi na cha kutosheleza.

Kama ifahamikavyo, Wakichembe mpaka karne za karibuni hivi walikuwa bado watu wa nyuma katika maendeleo ya kiuchumi, kiufundi na kisiasa. Kisiasa hawakuwa wameunganika. Kila ukoo ulikuwa na watu wachache tu na mkuu wa ukoo ndiye aliyekuwa na mamlaka yote juu ya ukoo uliohusika. Alikuwa msuluhishi na mtoa mashauri. Wakichembe hawakuwa na maskani ya mahali pamoja, maisha ambayo waku-

lima, waliishi na kuyafurahia. Hata hivyo, Wakichembe kwa ujumla walikuwa na mipaka maalum kuhusu umilikaji wa ardhi, jambo ambalo halikupata kufahamika kwa wageni wa Kiyuronodi hapo mwanzoni.

Kila ukoo au kikundi kilikuwa kinatangatanga katika eneo maalum ambalo lilikuwa ni mali ya ukoo huo. Kwa upande wa Wahotentoti kizizi, ambamo mifugo ilikusanywa, kilikuwa ndicho kitu kilichounganisha ukoo ama baadhi ya koo zenye asili moja. Lakini kutokana na kutoelewana kulikotokana na kukua kwa zizi na kuongezeka kwa watu jamii iliweza kugawanyika. Kila kundi liliweza kumchagua mzee ambaye aliweza kuliongoza kundi kwa kushauriana na wazee wengine. Kwa ufupi, Wakichembe hawakujenga serikali za pamoja na wala hawakuunganika. Hivyo basi, ilikuwa vigumu sana kwa upande wao kujilinda na kujikinga kutokana na maingilio—uvamizi na mashambulio ya Wabantu na hasa Makaburu ambao ni Wayuronodi.

Kutokana na maarifa ya wataalam wa lugha, Wabantu wamesemekana kuwa asili yao ni katika jimbo la Katanga la Jamhuri ya Zaire. Kuanzia karne za mwanzo za kipindi cha Kikristo waliweza kusambaa na kwenda sehemu nyingi za Afrika mashariki, magharibi, na kati. Mnamo karne ya kumi na mbili Wabantu walipata kufika na kuishi katika sehemu ya kusini ya Afrika, yaani, kusini ya Mto Limpopo. Uthibitisho wetu unatokana na masalia ya utamaduni wao, viwanda vya chuma na madini mengine. Vyombo au masalia ya vyombo vyao baada ya kupimwa na wataalam wa sayansi kwa kutumia kaboni 14 na vipimo vingine vimeweza kutupatia tarehe hizo. Babu zetu hawakutuachia kumbukumbu zo zote za maandishi kwa vile hawakupata kugundua alama za maandishi za aina yetu.

Wabantu walikuwa wakulima, wafugaji na wafua chuma. Uchumi wa aina hii uliwafanya waweze kuishi pamoja katika vijiji na mahali pamoja kwa muda mrefu. Hivyo waliweza kubadilishana mawazo kuhusu utamaduni na siasa ingawaje tawala zao hazikuwa kubwa sana, ukiondoa zile za Manikongo na Mwenemutapa, zikiunganishwa na zile zilizokuzwa na kustawishwa na Wahima katika sehemu za kuzunguka maziwa ya Victoria, Kyoga na Alberti. Ng'ombe walithaminiwa sana kama chakula na hasa kama chombo cha kuolea. Zizi lilijengwa karibu na mtemi tena katikati ya makazi.

Koo chache ziliunganishwa chini ya mtemi mmoja ambaye aliongoza kwa kushauriana na wazee wengine wa kijiji. Tawala

hizo za kitemi zilikuwa ndogo kieneo na shughuli zake zilikuwa ndogo japokuwa ni kamilifu. Ushirikiano kati ya tawala moja na nyingine ulikuwa kidogo sana. Kadhalika dunia ya jamii mbali mbali haikuwa kubwa.

Wabantu waliendeleza ufundi mbali mbali. Walitengeneza vifaa mbali mbali vya kazi pamoja na zana za vita kama vile: mikuki, marungu na kadhalika. Pia Wabantu wa Afrika kusini walikuwa na desturi ya unyago — kutia jando vijana na kuwapa elimu ya maisha — desturi ambayo Dingiswayo akaikomesha katika karne ya kumi na nane kama ilivyoelezwa katika sura ya sita.

Wabantu wa Afrika kusini waligawanyika katika makundi makuu mawili kutegemea lugha walizoongea. Makundi hayo yalijulikana kama Wanguni na Wasutu. Wanguni waliishi katika sehemu ya mashariki kati ya Bahari ya Hindi na Milima ya Drakensberg. Huu ulikuwa ni uwanda mwembamba, wenye mvua nyingi rutuba ya kutosha. Kwa hiyo, sehemu hiyo ilikuwa ni ya kuvutia sana kwa wakulima na wafugaji.

Wasutu walienea sehemu za nyanda za juu za mfululizo wa milima ya Drakensberg na katika nchi ya Boswana. Makazi ya Wasutu hayakukaribiana kama yale ya Wanguni. Wasutu walisambaa katika sehemu kubwa sana kwa sababu walikuwa na eneo kubwa. Ingawa Wasutu na Wanguni walitofautiana kwa lugha kwa kiasi fulani makundi hayo mawili yalikuwa na uchumi, siasa, utamaduni na desturi za aina moja.

Katika nchi ya Namibia waliishi Waherero na Wavambo. Jamii hizo pia zilikuwa za Kibantu. Waherero, huenda kwa sababu ya mazingara ya sehemu waliyoishi, waliacha kilimo na badala yake kushughulika na ufugaji wa ng'ombe tu. Wavambo walikuwa wakulima. Jamii hizo mbili zilihamia sehemu hiyo kwa kupitia Afrika ya kati (Waherero) na Afrika magharibi (Wavambo). Wagrikwa kama jamii ya tatu walihamia Namibia kutoka Afrika ya kusini katika karne ya kumi na nane na hasa ya kumi na tisa. Mnamo karne ya kumi na tisa Waherero walikuwa wameunganika chini ya uongozi na mamlaka ya mtemi mmoja aliyejulikana kwa jina la Maherero. Waherero walipatwa na baa kubwa sana la kuangamizwa na wakoloni wa Kijerumani katika vita ya ukombozi iliyodumu tangu mwaka 1904 hadi 1907. Huu ni wakati wazalendo wa Tanzania Bara walipopambana na ukoloni wa Kijerumani katika vita vya ukombozi vya Maji Maji! Mpaka mnamo miaka ya 1770 Wabantu wasadikiwa kuwa hawakuwa wamefika sehemu ya Jimbo la Rasi, yaani, Kusini ya

mto wa Fishi; kadhalika Wakaburu walikuwa hawajaifikia sehemu hiyo wala kupambana na Wabantu.

Mnamo 1497 Mreno mmoja aitwaye Vasco da Gama alipita katika Rasi hiyo ya Afrika Kusini, ambayo aliipa jina la 'Rasi ya Matumaini Mema', katika safari yake ya Bara Hindi. Baada ya msafara wa Da Gama meli nyingi za Wayuronodi zilipita sehemu hiyo ili kupata maji baridi na nyama mbichi kutoka kwa Wahotentoti. Ushahidi ni maandishi ya Wayuronodi wenyewe. Lakini mnamo mwaka 1652 kampuni moja la Kiholanzi lililojulikana, kama, 'Kampuni la Kiholanzi la India Mashariki', liliamua kuwapandikiza ndugu zao wa Kiholanzi katika sehemu hiyo ya Rasi. Hao walikuwa ni Makaburu, maana yake, wakulima. Makaburu wakawa ni jamii ya tatu kwa huko Afrika ya Kusini.

Makaburu hawakuwa tofauti na Wabantu. Walikuwa wakulima wa kawaida na pia, kama Wahotentoti, walikuwa wafugaji wa ng'ombe na kondoo. Na mpaka mnamo mwaka 1895 Makaburu walikuwa wanatawaliwa na kampuni hilo la Kiholanzi kwa njia ya Gavana ambaye makao yake yalikuwa India.

Tangu mwanzo Makaburu walionyesha siasa yao mbaya ya ubaguzi. Waliamini na kuendeleza imani ya kuwa Waafronodi ni wana waliolaaniwa wa Hamu. Hawafai ila kuwa watumishi tu wa watu weupe na kwamba kwa kuwatumikisha Waafronodi walikuwa wanatimiza na kutekeleza mpango maalum wa Mwenyezi Mungu. Imani hiyo bado wanaishikilia mpaka siku hizi. Hivyo, basi, wakaanzisha mpango wa kuwaua Wakalahari ili kuwamaliza kabisa na kuchukua ardhi yao. Wahotentoti waliingizwa utumwani kwa kuajiriwa kama watumishi wa ndani na mashambani. Makaburu, ambao idadi kubwa sana hawakuwa na wake, walianza kuwachukua mabinti wa Kiafronodi wa jamii ya Kihotentoti na kuwaweka vimada. Baada ya karne chache jamii mpya ya nne ikawa imezaliwa huko Afrika Kusini, nayo ni ya machotara ambao hujulikana kama Wagrikwa.

Wagrikwa huongea lugha ya Makaburu, yaani, Kikaburu. Wagrikwa hawakuwa na tawala za nguvu na wala hawakuwa na umoja sana. Kwa muda mrefu Wagrikwa walikuwa wanapendelewa na serikali ya Makaburu ya huko Afrika ya Kusini. Leo Wagrikwa hubaguliwa katika mambo yote, hudhulumiwa na kukandamizwa na serikali ya Makaburu ya huko Afrika ya Kusini kama Waafronodi. Ubaguzi huo ni katika sehemu za starehe, mashule, vyuo na makanisani pia hunyimwa haki ya kushiriki katika serikali ya nchi yao. Makazini hunyimwa kazi za ujuzi

hata kama wangekuwa na ujuzi na utaalamu wa kazi na sifa zote nyingine ambazo ni muhimu. Kazi za ujuzi ni kwa ajili ya Wayuronodi tu na Mwafronodi ni mtu wa kazi ngumu za mikono ambazo ni mwiko kwa Myuronodi kuzifanya. Siasa hii ni kinyume cha siasa ya usawa wa binadamu na heshima kwa kazi za aina yoyote kwa vile kazi ndio hasa msingi wa maisha na maendeleo ya mtu na jamii. Hata hivyo, iko haja ya kusisitiza kuwa msingi wa ubaguzi huu ni kuhalalisha suala zima la unyonyaji wa Kiyuronodi.

Koloni hilo la Rasi lilitawaliwa na kampuni la Kiholanzi kuanzia 1652 mpaka 1795. Makaburu hawakupendezwa na siasa ya kampuni. Wakaamua kupambana mnamo 1795 ili kujinyakulia uhuru kwa nguvu. Wakati wa ghasia hizo Waingereza wakaingilia kati na kuteka koloni hilo na kulitawala mpaka mnamo 1803. Mwaka huo Waingereza walilirudisha tena koloni hilo kwa serikali ya Waholanzi ambao walilitawala mpaka 1806 ndipo Waingereza wakalichukua tena kuliendesha kama koloni lao mpaka wakati wa kuwakabidhi madaraka walowezi wachache wa Kiyuronodi mnamo mwaka 1910. Serikali ya kwanza ya walowezi hao iliongozwa na Botha, ambaye ni Mkaburu. Jambo la kukumbuka ni kuwa mnamo 1820 serikali ya Kiingereza iliamua kuwaleta na kuwapandikiza huko Afrika ya Kusini wakulima au walowezi wa Kiingereza. Kitendo hicho, na hasa kwa sababu ya upendeleo waliopata walowezi hao wa Kiingereza, kiliwaudhi sana Makaburu. Walowezi hao wapya wa Kiingereza wanaunda jamii ya tano katika Jamhuri ya Afrika ya Kusini.

Jamii ya sita ya huko Afrika ya Kusini ni Wasanodi kutoka Bara Hindi na Mashariki ya Mbali. Wasanodi hao waliletwa huko na serikali ya Waingereza ili kufanya kazi za kujenga njia za reli na uchimbuzi wa madini kama vibarua. Leo idadi ya Wasanodi hao ni kubwa kuweza kustahili kuhesabiwa kama moja wapo ya jamii sita za Afrika ya Kusini.

Maelezo ya jamii katika taifa yanaweza kusababisha hatari ya kuimarisha na kuendeleza tabaka za kihasama miongoni mwa jamii zinazounda taifa hilo. Lakini maelezo hayo yanaweza kusaidia kueleweshe sababu za migongano na tabaka za kihasama katika taifa. Katika Jamhuri ya Afrika ya Kusini migongano ya kihasama ni kati ya Wayuronodi kwa upande moja; na Waafronodi, Wasanodi na Wagrikwa kwa upande mwingine.

Wayuronodi ambao ni walowezi wachache katika Afrika ya

Kusini walinyakua mamlaka ya kitawala na kuanza kuwakandamiza Waafronodi katika ardhi yao. Waafronodi wakiunganishwa na Wasanodi hubaguliwa, hudhulumiwa haki zao zote za kiutu, hupuuzwa na kutumikishwa katika shughuli mbali mbali za kuzalisha mali ambazo zahitaji mitulinga zaidi.

Ili kuleta ueleano wa dhati Wayuronodi hawana budi kwanza kuondokana na ile kasumba mbaya ya kihamati ambayo imemfanya Msanodi na Myuronodi ajione kuwa yeye ni bora kuliko Mwafronodi kiutu, kifikara na kadhalika. Vile vile wanapaswa kutambua kuwa, ingawa ni wageni katika ardhi ya Waafronodi, wao ni Waafrika kwa sababu wameishi humo vizazi na kwamba hawatazamiwi kuwa siku moja wataihama nchi hiyo; na kwa jinsi hiyo hiyo Wabantu ambao kwa asili wanasadikiwa kuwa ni Wakansanodi hawategemei kuwa wana mahali pengine ambapo wangeweza kuamua siku moja kurudi. Tofauti ni kuwa Wabantu si wageni kama Makaburu kwa vile wao kama Waafronodi walikuwa wamehamia sehemu ambayo ni yao kwa asili.

Sasa hivi tatizo kubwa la Wayuronodi wa huko Afrika ya Kusini ni kujitambulisha na Waafronodi. Kufanya hivyo kutakuwa na maana kuwa wamekubali ukweli juu ya usawa wa watu katika maana zote ikiwa ni pamoja na uhuru wa mtu kuchagua kuishi po pote. Na baada ya kuupokea ukweli huo, ambao kusema kweli wanautambua, Wayuronodi wanakabiliwa na suala la kutambua na kutoa haki sawa za kiutu kwa watu wa jamii za asili mbali mbali. Kwa maneno mengine, Wayuronodi watakuwa wamejenga na kukuza fikara halisi za kizalendo na kitaifa badala ya kuimarisha ubaguzi na utengano kama wanavyofanya hivi sasa.

Kufuatana na siasa ya Waafronodi wa huko Afrika ya Kusini na wa Afrika nzima walowezi wa Kiyuronodi hawana sababu ya kuhofu kuwa huenda siku moja watafukuzwa kutoka humo nchini au kukandamizwa na Waafronodi. Kwa upande huu Waafronodi wamepevuka sana; na kusema kweli wamefikia kiwango cha juu zaidi cha upevu kuliko Wayuronodi. Suala la msingi kwa Waafronodi siyo suala la uenyeji au ugeni. Suala la msingi ni kuona kuwa jamii zote za Afrika ya Kusini zinaunganika kama taifa moja, likiwa na shabaha na lengo moja la kutoa nafasi sawa za maendeleo kwa watu wa asili zote.

Hali ilivyo sasa hivi huko Afrika ya Kusini ni ya kusikitisha na kuhuzunisha sana. Siasa ya walowezi wachache wa Kiyuronodi inaimarisha ubaguzi na utengano; na wakati huo huo ikiendelea kudumisha hali ya utumwa wa Waafronodi na Wasanodi ambao

wamelazimishwa kuishi katika mazizi ambayo kwa lugha yao yajulikana kama nzavu. Kwa Myuronodi taifa la Afrika ya Kusini ni watu wenye asili ya Kiyuronodi tu; na kwamba Wayuronodi wenyewe sio moja ya jamii sita zinazopaswa kuunda taifa la Waafrika wa Afrika ya Kusini. Kwa kuwa fikara hiyo ya Wayuronodi ni kongwe sana na kwamba wakati wake umepita, ni dhahiri kwamba kiwango chao cha fikara kimedumaa; na kwamba Waafronodi wanao wajibu mkubwa wa kuwapa msukumo na mzinduko jamaa hao wa Kiyuronodi ili kuwapatia mwamko mpya wa fikara za kimapinduzi kulingana na maendeleo ya dunia ya leo.

Kufuatana na ukweli wa kihistoria walowezi wa Kiyuronodi wa Afrika ya Kusini ni Waafrika wala si wamoja tena na Wayuronodi wa Ulaya ingawa kwa asili ni Wayuronodi. Walowezi wote wa Kiyuronodi walipandikizwa huko Afrika ya Kusini na tabaka la kinyonyaji la matajiri wa Kiyuronodi. Koo zilizopandikizwa zilikuwa ni za watu wanyonge waliokataliwa huko Ulaya na tabaka la wanyonyaji. Hivyo, basi, jambo la maana kwa walowezi wa Kiyuronodi si kujaribu kujiona wao ni Wayuronodi wakati Wayuronodi wenyewe wa huko Ulaya hawawatambui. Na watakapoamua kurudi Ulaya wataonekana ni wageni zaidi kuliko wanavyojifikiria.

Wayuronodi, katika maana halisi ya neno, huwatambua walowezi hao kwa shabaha moja kubwa. Nayo ni kuhakikisha maendeleo ya Ulaya na Marekani na wala siyo ya taifa la Waafrika wa Afrika ya Kusini ambao walowezi wa Kiyuronodi ni sehemu moja. Kama ilivyoelezwa hapo awali suala la maelezo ya jamii lilikuwa na shabaha ya kueleza chanzo cha asili ya uhasama kwa madhumuni ya kujenga fikara za kitaifa miongoni mwa wananchi kwa kubomoa misingi hiyo ya uhasama, ubaguzi wa rangi na asili ya jamii. Pia ieleweke kuwa Afrika ya Kusini, kama nchi, haiwezi kupata heshima inayostahili kama nchi huru mpaka suala la usawa wa utu limetatuliwa. Sasa hivi uchumi wa nchi hiyo hautumiki kwa maendeleo ya watu bali kwa kununua silaha kutoka Marekani na Ulaya kwa shabaha ya kuendeleza uhasama, udhalimu na kuvuruga maendeleo ya jamii mbali mbali katika Jamhuri hiyo; na kwamba walowezi wa Kiyuronodi huridhika tu na makombo wapatayo kutoka kwa mabepari na mabeberu wa Kiyuronodi wa Ulaya na Marekani.

Sura ya 6

MAPAMBANO YA MFECANE

'Mfecane' ni neno la Kinguni ambalo limetumika kueleza vita vilivyotokea huko Afrika ya Kusini mwishoni mwa karne ya kumi na nane na kuendelea mpaka karne ya kumi na tisa. Mapambano au vita hivyo vilikuwa ni baina ya tawala za jamii mbali mbali za Kinguni ambazo ziliishi katika uwanda mdogo kati ya milima ya Drakensberg na Bahari ya Hindi.

Mpaka mnamo 1800 Wanguni waligawanyika katika makundi mengi. Baadhi ya makundi makubwa na yenye nguvu ni kama yafuatayo:

Kundi la jamii	**Mtemi**
Watetwa	Dingiswayo
Wandandwe	Zwide
Wakoza	—
Wangwane	Sobuhusa
Wajere	Zwangendaba
Wakumalo	Msilikazi
Wazulu	Chaka

Miaka michache kabla ya 1800 jamii hizo zikaanza kugongana na kupambana zenyewe kwa zenyewe. Jamii ya Watetwa chini ya uongozi wa Dingiswayo ndiyo iliyopata ushindi mara nyingi. Washindani wakubwa wa Dingiswayo walikuwa Zwide, mtemi wa Wandandwe; na Sobuhusa, mtemi wa Wangwane ambao sasa ni Waswazi.

Kwanza kabisa Dingiswayo alianza kumshambulia Sobuhusa na watu wake. Baada ya kuona ameelemewa na kuchoshwa na vita vya muda mrefu, Sobuhusa, na sehemu kubwa ya watu wake, aliihama nchi yake. Alielekea magharibi akivuka milima ya Drakensberg. Huko milimani alipambana na Wasutu ambao aliwatimua na kuwatia msukosuko mkubwa sana. Wasutu na

watu wa jamii nyingine ndogo ndogo wakatawanywa huku na huko katika kuogopa vurumai ya wakimbizi hao wa Kinguni. Wasutu na makundi mengine ya sehemu hizo za magharibi wamesemekana hawakujiunga chini ya tawala maalum na zenye nguvu. Waliishi kwa amani kwa sababu hali ya mazingara iliimarisha amani. Hivyo, basi, mpaka wakati huo, haja ya kuzuka tawala kubwa na zenye nguvu haikuwepo.

Wakimbizi hao waliendelea na safari yao huko wakipiga vita, wakinyang'anya mifugo, chakula na mali nyingine mpaka walipofika katika sehemu ambayo leo hujulikana kama nchi ya Swazi. Hapo wakaanza kufanya maskani yao. Wenyeji wa nchi ya Swazi ni mchanganyiko wa Wangwane, ambao asili yao ni Uzulu, na watu wa jamii mbali mbali za Kisutu ambao walichukuliwa mateka njiani na wengine ambao walikuwa wakazi wa asili wa sehemu hiyo.

Baada ya Sobuhusa na watu wake kutorokea katika nchi ya Swazi ugomvi ulizidi kuendelea kati ya Dingiswayo na Zwide. Kama kawaida Dingiswayo alipata ushindi mara nyingi. Safari moja Dingiswayo alipokuwa akiongoza majeshi yake vitani aliviziwa na majeshi ya Zwide. Akakamatwa mateka na kufikishwa mbele ya Zwide. Bila ya huruma, yasemekana, Zwide akamnyonga adui yake akitegemea kuwa atamaliza ugomvi na uhasama baina yake na Watetwa.

Dingiswayo alikuwa ni mtu mwenye fikara za juu sana na asemekana kuwa ndiye aliyepata, kabla ya Mbantu mwingine yeyote huko Afrika ya Kusini, kutambua umuhimu wa watu kuungana chini ya utawala wa pamoja na wenye nguvu. Ili kutekeleza wazo hilo, Dingiswayo alipaswa kukamilisha mambo fulani fulani katika jamii yake kabla ya kuanza kufanya mashambulio yoyote.

Kwanza kabisa, alikomesha ile desturi ya Wanguni ya kutia watoto jando. Unyago, kwa fikara za Dingiswayo, ulipoteza wakati wa vijana ambao wangeweza kupewa mafunzo ya kijeshi. Hivyo, basi, badala ya unyago Dingiswayo akaamuru kuwa vijana wote watengwe kadiri ya umri au rika na kupewa mafunzo ya kivita. Vijana mateka wa jamii nyingine pia waliingizwa katika vikosi hivi kwa kufuata umri wao. Hata hivyo Dingiswayo hakuanzisha jeshi la kudumu. Majeshi yalikusanywa wakati wa vita tu na baadaye kuachiliwa. Utaratibu huu baadaye uliigishwa na jamii nyingine za Kinguni.

Baada ya Dingiswayo kunyongwa na Zwide, mnamo 1818, Watetwa wakawa wanashindana wao kwa wao katika

kupendekeza jina la mtemi mpya. Watu waliofikiriwa na kupendekezwa ni kati ya ndugu wawili wa hayati Dingiswayo. Baada ya kushindwa kukubaliana, Watetwa wakawa wamegawanyika.

Chaka, Jemadari hodari wa Dingiswayo na kisha mtemi wa jamii ndogo ya Wazulu iliyoshirikishwa chini ya dola ya Dingiswayo, alijitokeza na majeshi yake ya Kizulu na kuwabwagilia mbali watawala wapya wa jamii ya Watetwa.

Chaka alijifunza kazi ya uaskari katika jeshi la Dingiswayo. Tangu ujana wake Chaka alionyesha uhodari wake katika mambo ya vita kiasi hata cha kutambuliwa na Mtemi Dingiswayo ambaye alimpandisha cheo na kumfanya Jemedari wa kikosi kimoja wapo. Mwaka 1816 baada ya kifo cha Senzangakona, baba yake Chaka, Dingiswayo alimpatia Chaka msaada wa kijeshi ili kupambana na nduguze kwa shabaha ya kutwaa madaraka ya utemi. Chaka akawashinda nduguze na akawa mtemi wa Wazulu.

Chaka alitayarisha jeshi lake kwa njia ya pekee sana hata likaonekana lenye ufundi na uwezo wa pekee kabisa kwa mambo ya vita. Hivyo, basi, mara tu baada ya kujinyakulia madaraka na kujitawalisha kijeshi kama kiongozi mpya wa Watetwa Chaka akaamuru kuwa watu wa jamii zote zilizopata kuwa chini ya dola ya Dingiswayo watajulikana kwa jina la 'Wazulu'. Kwa kufanya hivyo Chaka aliitukuza sana jamii yake ya Kizulu ambayo, kama ilivyoelezwa hapo juu, ilikuwa ndogo sana na kutojulikana. Hata hivyo, hatua zilizochukuliwa na Chaka zilikuwa za muhimu na za kimapinduzi kwa vile zilibadili mpango mzima wa maisha ya jamii kimuundo, kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, kiufundi, kifikara na kiulinzi.

Baada ya kujitangaza kuwa yeye ndiye kiongozi mpya, Chaka alitengeneza utaratibu mpya wa kuendesha nchi yake. Kwanza kabisa, watawala wajadi waliondolewa madaraka yote na kuachwa kama wasuluhishi wa wazee na watoto. Chaka alianzisha mpango mpya wa kuwa na jeshi la kudumu. Vijana ambao walifikia umri wa kwenda jando walikusanywa na kuwekwa pamoja ili kujifunza mambo ya vita. Kutokana na kila kikosi Chaka aliweza kuteua viongozi au majemedari wake kutegemea uwezo wa mtu bila kujali kama wazazi wa kiongozi huyo walikuwa wa asili ya kitemi. Uwezo na uhodari ndizo sifa zilizoweza kumpandisha mtu cheo. Wakati wa Chaka watu wote wenye umri kuanzia miaka kumi na zaidi walipaswa kutumikia kama wanajeshi. Wasichana nao walikuwa na vikosi vyao. Shughuli zao muhimu ni kuwapa moyo askari na kuwastare-

hesha nyakati za vita na mapumziko kwa nyimbo, ngoma na kadhalika. Vile vile wasichana hao walikuwa na kazi ya kuangalia shughuli za nyumbani: kuchunga ng'ombe wa kikosi, kukamua maziwa na kutayarisha chakula cha wanajeshi iwe wakati wa amani au vita mamoja.

Vijana, wavulana na wasichana, hawakuweza kuoana isipokuwa kwa ruhusa maalum ya Chaka tu. Na mara nyingi ruhusa hiyo ilitolewa kama zawadi baada ya kutumikia kiaminifu kwa muda mrefu katika jeshi na kupata ushindi mwingi. Hivyo, Chaka aliweza kukiruhusu kikosi kizima, wavulana na wasichana, waoane na kuishi maisha ya kiraia lakini wakiendelea kuwa askari wa akiba. Mali yote katika Uzulu ilifanywa mali ya umma na Chaka mwenyewe akiwa ndiye mdhamini wa mali hiyo. Ardhi, vijana, mifugo, mashamba na kadhalika yote yalikuwa chini ya mamlaka na usimamizi wa Chaka. Wazee wasiojiweza kwa shughuli za kijeshi walikuwa na wajibu wa kulima, kulisha mifugo na kubeba mizigo ya askari wakati wa vita. Hivyo, kila mtu alikuwa na wajibu maalum wa kutekeleza kwa taifa lake. Sheria kuu ya Chaka ni kwamba kikosi kinapoishinda jamii nyingine kikosi kilipaswa kutekeleza masharti kadhaa. Miongoni mwa masharti hayo ni:

(a) Wazee wote wa jamii iliyotekwa ambao hawafai kwa kazi ya uaskari ilibidi wauawe mara moja kwa kuwa wangeleta hasara na usumbufu wa kuwatunza badala ya kuleta manufaa kwa taifa. Pengine waliachwa kufa kwa njaa.

(b) Vijana wote ilibidi wachukuliwe wazima kama mateka wa vita na kujiunga na vijana wenzao wa umri wao katika majeshi ya Chaka. Wasichana pia waliwakilishwa kwa Chaka na kuwekwa chini ya ulinzi wake. Chaka mwenyewe, yasemekana, hakupata kuoa katika maisha yake yote. Wasichana mateka nao walipelekwa kujiunga na wasichana wenzao wa jamii ya Kizulu wa rika yao katika makambi ya kijeshi.

(c) Mali na mifugo, hasa ng'ombe, ambayo ilichukuliwa kutoka kwa maadui ilibidi iwakilishwe kwa Chaka ambaye aliigawa, kama zawadi, kwa vikosi mbali mbali kadiri ya matakwa yake. Hivyo, basi, kila kikosi kilipewa zizi ambalo kusema kweli lilikuwa ni mali ya taifa. Jemedari aliyeshindwa kutekeleza masharti hayo mara yote alikabiliwa na adhabu ya kifo. Na hii inaeleza kwa nini baadhi ya majemadari wake kama vile Msilikazi, kiongozi wa jamii ya Kumalo, waliweza kutoroka na kukimbilia katika nchi za ugenini.

Kwa upande wa kijeshi Chaka alianzisha utaratibu mpya kabisa ambao hakuna mtu duniani alipata kuufikiria. Kwanza kabisa, alileta wazo la kutumia mikuki mifupi ya kumchomea adui (kuchoma na kuchomoa) kwa karibu, kama vile askari wa kisasa wafanyavyo kwa kutumia singe ya bunduki zao wanapokabiliana ana kwa ana na adui zao. Mkuki huu wa aina mpya uliitwa 'assegai' nao ulitumika badala ya mkuki wa jadi wa kutupa. Taabu ya mkuki wa aina ya kwanza ni kuwa askari hubaki bila silaha baada ya kutupa mkuki wake na hakuna jambo jingine analoweza kufanya tena isipokuwa kukimbia au kujisalimisha. Vile vile Chaka alibuni mwondoko au mtindo mpya kabisa wa kumsogelea adui. Askari wanapomkabili adui ilibidi wajipange na kumsogelea adui kwa mfano wa pembe za nyati na kisha kumkabili kutoka pande zote.

Kwa kufanya utajiri wote wa nchi kuwa mali ya umma chini ya udhamini na mamlaka yake Chaka aliweza kuongeza heshima na utukufu wake na wa taifa zima mara dufu. Majemedari aliowachagua waliweza kuonyesha uaminifu wao kwa mtu mmoja; na kwamba kubaki kazini na kupandishwa cheo zaidi kulitegemea uaminifu na uhodari wa kazi kwa kiasi cha kuona Chaka anaridhika. Uvivu, utegaji na uhaini viliadhibiwa vikali sana.

Kwa vile majeshi yote yalikuwa chini ya mamlaka yake hapakuwa tena na haja ya mashauriano baina yake (Chaka) na Baraza la Watemi ambalo alilivunja. Kulikuwa na demokrasi iliyomwezesha kila mtu katika jamii kuonyesha uwezo wake na kufikiriwa kwa madaraka na uongozi ingawa utawala ulikuwa wa 'kijeshi' na kwa jinsi fulani wa kiimla ambao uliweka mamlaka mikononi mwa mtu mmoja, Amiri Jeshi. Hata hivyo, Chaka alijitahidi sana kufungamana na wakuu wa vikosi na kupata ushauri wao. Na wakati wowote Chaka alipotaka kuishambulia jamii fulani aliweza kufanya hivyo kwa kukiamrisha kikosi chochote. Na kwa kuwa ilibidi kikosi kinachoshindwa kuleta ushindi kiadhibiwe vikali na kwa ukatili, kila kikosi kilijitahidi kuleta ushindi wa sifa. Hata hivyo, matokeo ya nidhamu hiyo ya kijeshi ni kujengwa kwa moyo wa kizalendo.

Na kwa mpango wa kuwakusanya vijana wa jamii mbali mbali katika makambi ya kijeshi Chaka aliweza kuvunjilia mbali ubaguzi wa kijamii na kukuza moyo wa kitaifa. Kwa kuwa watu wote walionekana 'sawa' mbele ya Chaka kila kijana aliweza kufanya bidii na jitihada ili kuleta ufahari wa taifa na kuvutia upendo wa Chaka. Hapakuwa na matabaka ya wastahiki na

kabwera. Na kwamba, Wazulu walikuwa ni mchanganyiko wa jamii mbali mbali za Kinguni, yaani, Wazulu wa asili na wale waliotekwa kutoka jamii nyingine. Vile vile kwa kuwa na jeshi la kudumu Chaka aliweza kulitayarisha jeshi la nguvu sana ambalo liliweza kumhakikishia ushindi wakati wote. Hali kadhalika uvumbuzi wa silaha mpya na maarifa ya vita, kwa ujumla ulisaidia sana kuyaletea ushindi mkubwa majeshi ya Chaka. Hata hivyo, yapasa kukumbuka kuwa jamii zote za Kinguni baadaye ziliiga utaratibu huo mpya wa jamii ya Kizulu. Chaka aliweza kukuza jeshi lake kwa njia ya kuwashirikisha vijana mateka ambao walipata haki sawa na wale wenye asili ya Kizulu.

Vita vingi vilipigwa kati ya Chaka na Zwide. Baadaye majeshi ya Chaka yaliyashinda majeshi ya Zwide baada ya kuyachosha na kuyadhoofisha kwa muda mrefu kwa njaa na kadhalika. Zwide alitorokea katika nchi ya Wangwane ambao hapo mwanzoni walikuwa maadui. Huko akakamatwa mateka na kuuawa kwa amri ya mtemi wa nchi, Mtemi Sobuhusa.

Baada ya kushindwa kwa Wandandwe na kuuawa kwa Zwide jamii nyingi zilizoshirikishwa katika dola ya Wandandwe zilijinyakulia uhuru na kujitenga. Moja ya jamii hizo zilizojitangazia uhuru mnamo 1819 ni Wajere ambao walitawaliwa na mtemi ajulikanaye kwa jina la Zwangendaba na ambaye baadaye aliwaongoza watu wake mpaka Mapupwe, huko Ufipa, katika Tanzania mnamo 1840.

Wanahistoria wengi wa Kiyuronodi kama ilivyo kawaida yao, wamepotosha ukweli wa mambo kwa kusema eti Dingiswayo alijifunza fikara ya umoja na utaifa kutokana na Myuronodi mmoja ambaye asemekana alipata kukaribishwa nyumbani kwa Dingiswayo wakati fulani. Pili, mabadiliko yote ya kivita yaliyoletwa na Chaka yalikuwa ni mambo aliyojifunza kutoka kwa Makaburu. Tatu, ni kwamba ilikuwa ni kwa sababu ya kupambana kwao na Makaburu wa kutoka katika Koloni la Rasi. Madai hayo yote hayana ukweli. Kwanza, hakuna ushahidi wowote kuhusu mkutano kati ya Dingiswayo na huyo Myuronodi. Pili, Chaka hakuwahi hata mara moja katika maisha yake kufika katika sehemu ya Rasi na kutazama gwaride la wanajeshi wa Kiyuronodi kama ilivyodaiwa.

Kuna mambo mawili ambayo yaweza kukanusha madai hayo. Kwanza, vita hivyo vya Wanguni vilianza na kupigwa katika sehemu za Natali na kisha kuenea katika sehemu nyingine za Uzulu. Ingekuwa kwa sababu ya kukutana na kushambuliwa na Makaburu, basi, mfecane ingeanzia katika jamii ya Wakoza am-

bao walikuwa sehemu ya mpakani na ndio waliopambana na Makaburu. Vile vile kutokana na muundo tofauti wa serikali na jeshi, pamoja na maarifa tofauti ya vita, ni dhahiri kwamba yote yalitokana na kichwa cha Mwafronodi mwenyewe, yaani, Dingiswayo na Chaka. Kwa hiyo, swali la kujiuliza ni kuwa mambo gani yaliweza kusababisha misukosuko hiyo?.

Bwana Omer-Cooper*anaeleza kuwa 'vita hivyo vilisababishwa na mazingara ya asili katika jamii ya Wanguni wenyewe'. Kwanza kabisa, katika Unguni kulikuwa na msongamano wa watu. Hivyo, basi, ardhi ilionekana haba kwa kilimo na malisho. Wanguni walishindwa kusonga upande wa kusini kwa sababu walizuiliwa na Wayuronodi, yaani, Makaburu. Matokeo yake ni vita. Mwenye nguvu alibakia na asiye na nguvu alipoteza maisha yake au kukimbilia nchi ya kigeni, kama ilivyotokea, na kuishi huko kama mkimbizi wa vita akimpisha mwenye nguvu. Hapakuwa na njia nyingine ya kuongeza ardhi kwa vile Wanguni walizibwa pande zote isipokuwa baadhi ya watu kulazimishwa kutoka nje kwa kuvuka milima ya Drakensberg au kuuawa. Kwa upande mwingine Dingiswayo alitaka kumiliki njia ya biashara baina ya nchi yake na Msumbiji ambako Wareno waliendesha shughuli mbali mbali za kibiashara. Na mwisho kabisa ni jambo la kawaida kwa jamii au taifa kutaka kupanua eneo la dola yake. Hayo yamepata kutokea kati ya jamii mbali mbali za Ulaya na sehemu nyingine za dunia.

Kuanzia wakati wa Dingiswayo hadi kufikia wakati wa Chaka 1818-1828, makundi mengi ya Kinguni yalitoroka na kukimbilia nchi za kigeni ili kutafuta usalama. Kuhama kwa watu na wengi wao kupoteza maisha yao, kulisababisha upungufu wa watu katika nchi ya Wazulu.

Mfecane ilisababisha kuundwa kwa taifa moja la nguvu la Kizulu katika nchi nzima ya Unguni ambako hapo awali wenyeji wake waligawanyika katika vijamii vidogo vidogo visivyoungana. Kufuatana na jinsi umoja huo ulivyoletwa serikali ya Kizulu ilipasa kuwa ya muundo na mwongozo wa Kijeshi. Baadaye Wazulu waliendeleza tabia ya kuishi kwa kushambulia na kunyang'anya mifugo ya jamii nyingine, tabia ambayo ilifuatwa na jamii zote za Wanguni popote walipokimbilia katika nchi za kigeni. Vijana wenye umri kati ya miaka 18 na 30 au 40 walitumia muda wao wote kwa mafunzo ya kijeshi. Kilimo kiliachwa kushughulikiwa na wazee wenye umri zaidi ya miaka

---

* J.D. Omer – Cooper, *The Zulu Aftermath*, London, 1966.

30 ambao ni wanajeshi waliostahafu. Kwa jinsi hii kilimo hakikuthaminiwa sana.

Vita hivyo vya mfecane vilivunja tawala za jamii nyingine zenye nguvu za Waafronodi katika Afrika ya kati na Afrika Mashariki. Hata hivyo, itakuwa ni makosa kufikiri kwamba vita vya mfecane vilileta hasara peke yake. Kusema kweli vita vya mfecane katika sehemu nyingi vilisaidia sana kuleta mwamko wa 'siasa wa kitaifa'. Vilizifanya baadhi ya jamii ziungane ili kujilinda na mshambulio ya maadui wao. Jamii hizo zilizopata kutambua faida ya umoja pia zilitambua umuhimu wa kuigisha mpango wa kijeshi wa maadui wao Wanguni. Baadhi ya wanahistoria huamini kuwa muungano wa Wahehe chini ya Mwinyigumba na baadaye chini ya mwanae, Mkwawa, Wasangu chini ya uongozi wa Merere na Wanyamwezi, chini ya Mtemi Mirambo, ulitokana na vituko vya Wangoni. Hata hivyo mwandishi anapenda kuacha suala hili wazi kwa wanahistoria kulifanyia utafiti zaidi.

Hivyo, basi, jamii hizo zilizopata kuungana kama vitaifa, ziliweza kujilinda wakati wa mashambulio; pia watu wake walipata kujisalimisha kutoka kwa wachuuzi au wafanya biashara ya watumwa. Baadhi ya vitaifa vilivyopata kuundwa na wakimbizi wa Kinguni nje ya Uzulu ni kama vifuatavyo:

a. Waswazi:

Waswazi walikuwa ni jamii moja wapo ya Kinguni ambayo mtemi wake alikuwa Sobuhusa. Waswazi walikimbilia sehemu hiyo ya Uswazi baada ya kupigwa na kushindwa na majeshi ya Dingiswayo, mtemi wa Watetwa, kabla ya mwaka 1818. Leo Swazi ni nchi inayojitegemea katika kuamua na kuendesha shughuli zake za maendeleo ya jamii kama taifa huru.

b. Wamatabele:

Wamatabele ambao leo wanaishi huko Zimbabwe walijulikana kama Wakumalo, wakiwa moja ya jamii za Kinguni. Wakumalo walitoroka kutoka Uzulu chini ya kiongozi wao Msilikazi mnamo 1821. Msilikazi alikuwa ni mmoja wa majemadari hodari wa Chaka. Safari moja alipotumwa kuishambulia jamii ya jirani Msilikazi alivunja moja ya sheria za Chaka. Nayo ni kuwa mwaminifu na kuwakilisha mali yote aliyoweza kuiteka kutoka kwa maadui wake. Kwa kuvunja sheria ya Mkuu wake, Msilikazi alitambua kuwa alikuwa anakabiliwa na adhabu ya kifo. Hivyo, akaamua kuwaongoza wafuasi wake, ambao walimwamini na kumpenda sana, hadi katika nchi ya Transivala. Njiani, katika sehemu za Lesutu na Transivala waliwababaisha sana watu. Siku

zote waliishi kwa kunyang'anya chakula na mifugo. Hivyo, waliondokana pia na shughuli za kilimo.

Lakini baadaye walipoingiliwa na Wakaburu katika miaka ya 1830 Wazulu hao ambao sasa walijulikana kama 'Matabele' kwa maana ya wanyang'anyi, waliamua kukimbilia na kuhamia kaskazini na kuishi kati ya mito ya Limpompo na Zambezi. Hii ni nchi ya Wamashona ambao hapo awali walitawaliwa na Warozwi. Wamashona ambao ni Wabantu pia walitekwa na kuwekwa chini ya mamlaka ya kijitaifa cha Matabele ambacho kiliendelea kuwatawala mpaka mwaka 1893 wakati wakoloni walipokivamia na kukiteka. Lakini Lobengula, mwana wa Msilikazi na mtemi wa Wamatabele wakati huo, kama Mkwawa, hakujiruhusu kukamatwa mateka. Alitoroka na mpaka leo yasemekana, hakuna mtu aliyeweza kushuhudia maiti yake au kujua mambo yaliyompata kiongozi huyo shupavu wa Wamatabele na Wamashona. Na huo ukawa ndio mwanzo wa uvamizi na utawala wa kikoloni wa Kiyuronodi katika Afrika ya Kati.

c. Wamakololo:

Wamakololo ni watu wa jamii mbali mbali za Kisutu ambazo zilishambuliwa na kutawanywa na jamii za Kinguni ambazo zilikuwa zinatoroka utawala wa kijeshi wa Chaka ambao ulidai nidhamu ya juu sana. Wakumalo walijikusanya chini ya Sebetwane ambaye alipatà kujitokeza kama kiongozi. Sebetwane aliwaongoza watu wake kupitia nchi ya Wagrikwa na katika nchi ya Boswana ambako Padure Roberti Mofati, mkwe wa mpelelezi Daudi Livingistoni, alikuwa anaendesha kazi za dini; na kisha kuelekea sehemu ya kaskazini. Wakaanzisha makazi ya kudumu katika nchi ya Barose ambayo leo ni moja ya majimbo ya Zambia. Mara tu baada ya kuwasili katika sehemu hiyo Wasutu hao wakapewa jina la 'Makololo'. Baadaye walishambuliwa na kuteketezwa (wanawake tu waliobakizwa) na wenyeji wao, yaani, Walozi chini ya uongozi wa Sipoya. Hata hivyo, utamaduni, desturi, mila n.k. bado wanaendeleza ule ule wa Kisutu kwa sababu ya akina mama waliosalimika.

d. Wangoni:

Wangoni ambao walitoka huko Afrika ya Kusini hawakupata kushirikishwa katika taifa la Wazulu. Wao walikuwa ni moja ya jamii za Kinguni. Walijulikana kama Wajere na kiongozi wao alikuwa Zwangendaba ambaye alijiunga na utawala wa Wandandwe. Mara tu baada ya majeshi ya Zwide kupigwa na kushindwa na majeshi ya Chaka, na Zwide mwenyewe kukimbilia Uswazi na kisha kuuawa, Zwangendaba alijinyakulia uhuru na

kutoroka mnamo 1820.

Zwangendaba aliwaongoza watu wake kupitia nchi ya Wasutu na kisha akaingia sehemu ya kusini ya Msumbiji. Baadaye aliendelea kuwaongoza watu wake kuelekea kaskazini. Mnamo 1835 Zwangendaba alivuka mto wa Zambezi baada ya kuiteketeza dola moja ya nguvu na ya zamani sana. Hiyo ilikuwa ni dola ya Kirozwi huko Zimbabwe. Mambo ambaye alikuwa mtemi wa Kirozwi katika Zimbabwe, yasemekana, alikamatwa na kuchunwa kikatil sana akiwa bado yu hai. Baadaye kikosi hicho cha Zwangendaba kiliendelea na safari yake ya vitisho kupitia Malawi hadi kufika Ufipa, katika mkoa wa Rukwa, Tanzania mnamo 1840 na ambako Zwangendaba alifariki mnamo, inakisiwa, mwaka 1845 au 1848. Kundi hili la Wanguni lilipewa jina la 'Wangoni' wakati likiwa njiani kuja Tanzania. Inawezekana wlipewa jina la Wangoni wakiwa Afrika ya Kati ambako baadhi ya jamii pia hujiita Wangoni.

Mara tu baada ya Zwangendaba kufariki Wangoni ambao sasa idadi yao ilikuwa kubwa sana kwa sababu ya mateka waliowakusanya njiani walianza kufarakana na kugawanyika. Baadhi yao wakamfuata jemedari mmoja aliyeitwa Gama ambaye aliwaongoza kusini hadi Unyakyusa na kisha kusini mashariki ya Ziwa Nyasa hadi kufikia Songea. Kundi hilo la Wangoni lajulikana kama Wangwangara japokuwa asili ya jina hili yatatanisha. Wangoni hao walipofika huko Ruvuma waliwakuta Wangoni wengine waliowahi kufika huko kwa kupitia kusini ya Ziwa Nyasa. Hao walijulikana kama Wamaseko. Kwanza, waliishi kwa kushirikiana lakini baadaye wakaanza kupambana wao kwa wao na ndipo Wamaseko wakaamua, baada ya kuelemewa, kurudi tena walikotoka na kuanzisha maskani katika nchi ya Malawi ambako wanaendelea kuishi mpaka leo.

Kundi jinginc la Wangoni liliendelea kutoka Ufipa kuelekea kaskazini hadi Unyamwezi na Usukuma magharibi. Hilo lilikuwa kundi la Watuta. Jambo la kukumbuka, kama inavyosadikiwa, ni kuwa Watuta walimchukua mateka Mirambo na baada ya kuachiliwa Mirambo aliunda jeshi lake la Ruga-Ruga kwa muundo wa majeshi ya Kingoni; na mara tu akaanza kazi yake kubwa ya kuangusha temi nyingine katika Unyamwezi na kuwaunganisha Wanyamwezi chini ya uongozi moja. Inawezekana kabisa kuwa Mtemi Mirambo hakuwa na fikara za kimapenduzi au za kiitikadi katika kuwaunganisha Wanyamwezi. Huenda shabaha yake kubwa ni kujijengea sifa na kujitajirisha

kwa kuwatoza ushuru wafanya biashara ya watumwa, yaani, Waarabu. Suala hilo linaachwa wazi kwa mjadala.

Kikundi kingine kilimfuata Mpezeni, mwana wa Zwangendaba, hadi huko mpakani mwa Zambia, Malawi na Msumbiji, na kuendelea kuishi huko hadi leo. Baadhi yao walimfuata Mwombera au Mbelwa, mtoto mwingine wa Zwangendaba, hadi nchi ya Malawi na kuanza kujenga utawala wao huko.

Wangoni Gwangara ambao wasifika sana kwa mashambulio yao katika sehemu kubwa ya Tanzania Bara, hasa sehemu zilizo kusini ya Reli ya Uhuru, hawakushiriki katika biashara ya watumwa. Hii ilikuwa ni kwa sababu wao wenyewe walikuwa wanahitaji mateka kwa shughuli za kijeshi. Hivyo, basi, badala ya kuwauza mateka wao Wangoni, waliwashirikisha mateka hao katika jamii yao kama ndugu.

e. Wasutu.

Baada ya kutimuliwa na wakimbizi kutoka Unguni, Wasutu wali tawanywa huko na huko. Ili kujikinga na mashambulio ya maadui wao kijana mmoja kwa jina Moshweshwe au Mosheshe akajitokeza, kwa mfano wa Mtemi Mirambo, na kuwaunganisha watu wa jamii mbali mbali za Kisutu katika taifa moja imara lijulikanalo leo kama 'Wasutu'. Kwa sababu ya muungano huo wa kitaifa Wasutu walijipatia ushindi mara nyingi katika mapambano ya kupinga ukoloni wa Kikaburu na Kiingereza. Baadaye Wasutu wenyewe waliamua kuomba ulinzi wa serikali ya Kiingereza, kwa kuogopa kuwa hatimaye wangetekwa na mabeberu wa Kiyuronodi wa Adrika Kusini.

Jambo muhimu la kukumbuka ni kwamba vita hivyo vya mfecane viliendelea kupigwa wakati wote wa miaka ya 1820 hadi 1830. Mara nyingi Wazulu waliweza kuwafuata maadui wao hata ng'ambo ya pili ya milima ya Drakensberg walikokimbilia. Hivyo, tawala za Kiafronodi zilibaki katika hali ya uhasama na uadui; na hii ilikuwa ni sababu mojawapo ya kushambuliwa na kupigwa kwa Waafronodi na wakoloni kutoka Afrika Kusini, maana, mataifa ya Kibantu au ya Kiafronodi hayakuweza kusahau ugomvi uliokuwa baina yao wenyewe na kushirikiana katika vita vya kumpiga adui moja — ukoloni. Pili vita hivyo vya Waafronodi kwa Waafronodi vilidhoofisha sana nguvu ya Waafronodi. Na kwa kuwa vita hivyo vilifanya sehemu nyingi ziachwe bila watu kwa wingi ilikuwa ni kumfungulia njia Kaburu kutoka Afrika Kusini katika miaka ya 1830 na kuziteka tawala nyingi za Kibantu katika sehemu za kaskazini.

Vita vya mfecane vilikuwa ndiyo sababu ya Wabantu wa

jamii ya Kinguni kuzivamia na kuziteka sehemu za Wabantu wengine katika Afrika ya kusini, kati na mashariki katika karne ya kumi na tisa. Vile vile tunaweza kutoa hoja ya msingi kuwa mfecane ilisaidia sana kuleta mwamko wa juu wa siasa wa kitaifa miongoni mwa jamii nyingi za Kibantu kusini ya Ikweta na hasa kukuza moyo wa kizalendo.

Sura ya 7

MAENDELEO YA JAMII DUNIANI KIMFUMO

Suala la maendeleo ya mtu limezungumziwa sana katika sura ya pili na katika sura nyingine zinazofuata. Jambo ambalo mtungaji anapenda kuongelea katika sura hii ni kuhusu maendeleo ya jamii duniani kimfumo na kitaasisi. Ili kutoa picha kamili kwa msomaji mtungaji anakusudia kusisitiza mapema juu ya mambo mawili ambayo ni muhimu sana.

Jambo la kwanza ni kuwa maendeleo ya aina yote ya jamii duniani msingi wake ni maendeleo ya maarifa katika ulimwengu wa sayansi na tekinologia. Kwa jinsi hiyo ni wazi kuwa kadiri jamii itakavyopiga hatua zaidi katika maarifa ya sayansi na utengenezaji, yaani, kitekinologia ndivyo maendeleo ya jamii hiyo kimfumo, kitaasisi na kadhalika, yatakavyozidi kudhihirika. Jamii ambazo hazijajiendeleza vyakutosha kisayansi na kitekinologia taasisi zake hubaki ndogo ndogo na kimfumo jamii hubaki nyuma.

Jambo la pili la kuzingatia ni kuwa karibu jamii zote duniani zimepata, kwa namna moja au nyingine na kwa vipindi mbali mbali vya kihistoria, kupitia au kuingizwa katika mifumo zaidi ya moja. Wakati, kwa mfano, jamii ya Kiingereza na jamii nyingine za Ulaya zimejiendeleza kupitia mifumo yote ambayo punde itazungumziwa jamii nyingi za Afrika na za sehemu nyingine za dunia zimeingizwa au zimesukumizwa katika baadhi ya mifumo. Kwa mfano, Waingereza wamejiendeleza kutoka mfumo wa ujima kupitia mifumo ya utumwa, ukabaila na ubepari. Jamii nyingi za Kiafrika zimeanza na mfumo wa kijima na kisha kuingizwa moja kwa moja ama katika mfumo wa ukabaila au katika mfumo wa ubepari wa kidunia au katika mfumo wa kijamaa kama itakavyoonekana katika maelezo yafuatayo.

a. Mfumo wa kijima:

Historia ya mtu duniani inaonyesha kuwa karibu jamii zote duniani zilianza na mfumo wa maisha ya kijima; na kwamba

kuna jamii duniani ambazo zinaishi bado maisha ya kijima. Katika mfumo wa kijima watu wote huwa sawa. Wote huwa na haki sawa. Watu hukabidhiwa madaraka ya uongozi katika taasisi mbali mbali kutokana na uwezo wao ikiwa pamoja na sifa ya kukubalika kutokanako na tabia ya kuthamini utu wa wengine na mchango wa mtu kwa jamii.

Ni vigumu sana kusema lini mfumo wa ujima ulianza. Ujima kama mfumo wa maisha ya jamii unadhihirika zaidi katika jamii zinazoishi maisha ya pamoja. Kihistoria watu wameanza kuishi pamoja kijamii hasa kuanzia miaka 10,000 iliyopita. Kwa ufupi, maisha ya kijamii yalidhihirika katika jamii nyingi baada ya mtu kupata maarifa ya kilimo. Kilimo ni mjumlisho wa ufugaji wa mimea ya chakula mashambani na ufugaji wa wanyama mbali mbali. Hapo awali aina zote za chakula na wanyama vyote vilikuwa vinatafutwa na kuwindwa na watu maporini. Hivyo, kabla ya kilimo ilikuwa vigumu sana kwa jamii kufanya maskani ya mahali pamoja.

Kilimo kilisaidia jamii kupiga hatua za haraka za maendeleo katika misingi mingi na kwa jinsi hiyo kuondokana na unyonge ambao, kwa asili, husababishwa na mazingara. Kilimo, licha ya kuongeza idadi ya watu katika jamii, kiliwezesha watu wa jamii kujiendeleza katika ulimwengu wa sayansi, ufundi, tekinologia na mawazo. Kutokana na maendeleo hayo muhimu watu katika jamii hutaalamika katika taaluma mbali mbali. Wengine huwa wataalam wa uganga na utabibu, muziki, uwindaji, uvuvi na kadhalika.

Taasisi mbali mbali pia hukuzwa. Taasisi hizo ni pamoja na serikali, biashara na madhehebu ya imani na kadhalika. Kama ilivyo kawaida, maendeleo ya mtu yamekuwa ni matokeo ya kazi au mapambano; na kwamba mara nyingi matokeo ya mapambano hayo huwa na sura mbili. Sura ya kuendeleza na sura ya kurudisha nyuma maendeleo ya jamii. Sura hizi mbili ambazo hujenga tabaka zenye mgongano wa kihasama huwa ndiyo hasa msingi wa mwendelezo wa mapambano; na, kwa hiyo, ni msingi wa maendeleo na ustawi zaidi wa jamii.

Jamii ya kijima ambayo watu wake ni sawa na hushirikiana bega kwa bega katika shughuli zote, hasa za kuzalisha mali, baadaye hugawanyika katika matabaka mawili katika hatua ya pili: tabaka la wanyonyaji na tabaka la wanaonyonywa. Katika hatua hii ya pili maendeleo ya tabaka la walio wengi huvurugika kwa kila hali. Maendeleo ya jamii huwa yamekatishwa na kurudishwa nyuma. Kwa upande mwingine, tabaka la

wanyonyaji ambao ni wachache huneemeka zaidi na zaidi. Kwa jinsi hii tabaka hili la wanyonyaji litakuwa linajiendeleza. Hata hivyo, kama ilivyodokezwa hapo juu, huo huwa ndio mwanzo wa mapambano ya kitabaka katika jamii na wakati huo huo huwa ni mapambano ya hali ya juu zaidi ya mtu kujiendeleza kisayansi, kiufundi na kitekinologia.

b. Mfumo wa kitumwa.

Utumwa kama mfumo wa maisha ni hatua ya pili katika maendeleo ya jamii duniani. Mfumo huu, kama mifumo mingine itakayoongelewa punde, ni mfumo wa kitabaka na kihasama kwa vile kiuchumi unaruhusu unyonyaji na kimaisha unaruhusu uka damizaji na ubaguzi. Utumwa humfanya mtu au tabaka la watu katika jamii kumilikiwa na mtu au na kikundi cha watu. Umilikaji wa mtu au watu na mtu au kikundi cha watu huhalalishwa na sheria za tabaka la wanaomiliki. Kwa kuwa wanaomilikiwa huwa wanyonge na wasiojiweza mfumo huu wa stumwa huonekana kama kwamba ni mfumo wa maisha ambao umekubaliwa na jamii nzima kama mpango rasmi wa jamii.

Mtu anayemiliki mtu mwingine au kikundi cha watu ni bwana na yule anayemilikiwa huitwa mtumwa. Mtumwa akisha milikiwa hupoteza haki zote za kiutu, yaani, hadhi yake kama mtu, haki zote za kiraia, uhuru wa kufikiri na kupanga maendeleo yake ikiwa pamoja na uhuru wa kutekeleza mipango yake mwenyewe ya binafsi. Mfumo huu ni matokeo ya ubinafsi na tamaa ya baadhi ya watu katika jamii kutaka kunyonya wengine. Mtumwa au watumwa hunyonywa na bwana wake au mabwana wao kwa kutumikishwa pasipo ujira katika shughuli zote za kiuchumi. Mtumwa au watumwa ambao hadhi yao imeteremshwa kutokana na kumilikiwa kama zana huwa ni vyombo vya kuzalishia mali ya bwana au mabwana.

Asili ya utumwa kama ilivyoongelewa hapo juu ni ubinafsi, yaani, tamaa ya watu wachache kujitajirisha na kujiendeleza wao wenyewe dhidi ya umma kwa kutumia jasho la watu wengine. Bwana, kama kawaida, mwenyewe hafanyi kazi, bali kazi moja tu ya kuhakikisha kuwa utumwa kama mfumo wa maisha unadumishwa na kuendelezwa. Licha ya kutumikishwa katika shughuli za kiuchumi watumwa walitumiwa sana kama vinyago vya kumfurahisha bwana au mabwana zao. Kufurahisha huko hakukuwa kwa nyimbo tu na michezo bali pia kwa kutendewa vitendo vya kiovu na kinyama. Furaha ya bwana ni kuona kuwa watumwa wanadhihakiwa, wanateswa kikatili, wanadhulumiwa, wananyanyaswa na kudharauliwa kwa kila hali.

Jambo la kukumbuka ni kuwa hata katika hatua hii ya utumwa, ambao tutauita pia utumwa-mkongwe, jamii huwa imo muda wote katika mapambano. Moja ya mapambano ni taraji ya wanaonyonywa na kukandamizwa kubomoa mfumo. Pambano jingine ni la mtu kujiendeleza katika misingi iliyoelezwa hapo awali kwa kupambana na mazingara. Kwa jinsi hii, hata kama maendeleo ya watu yatakosekana maendeleo ya vitu na maendeleo ya maarifa ya sayansi, utengenezaji na ufundi, kwa ujumla, huongezeka siku hata siku.

Inafaa ifahamike pia kuwa maana ya pili ya utumwa ni 'hali ya unyonge', hali ambayo ni matokeo ya mfumo wa kitabaka. Utumwa kama hali ya unyonge unaweza kuonekana katika mifumo yote ya kitabaka. Kwa ufupi, hali ya utumwa huonekana chini ya utumwa-mkongwe, ukabaila na ubepari.

Jambo jingine muhimu la kuzingatia ni kuwa unyonge wa mtu ni wa asili, yaani, unaanzia tangu mtu wa kwanza. Unyonge wa asili unatokana na utovu wa maendeleo ya kutosha ya mtu au jamii katika vipindi mbali mbali. Mipango ya uchumi ambayo hutoa umbile la mifumo ya kitabaka huongeza tu uzito wa unyonge huu wa asili na pia hubadili umbile la unyonge wenyewe. Maelezo kamili yatatolewa chini ya kila mfumo na mpango wa uchumi.

c. Mfumo wa kikabaila

Mpaka sasa mjadala umekuwa juu ya maendeleo ya jamii kuanzia maisha ya ujima hadi kufikia haua ya pili ya maendeleo ya jamii duniani ambayo ni utumwa. Jambo jingine lipaswalo kuzingatiwa ni kuwa utumwa kama mfumo wa maisha ya kijamii ulisababisha aina ya pili ya unyonge wa mtu na mapambano zaidi ya ukombozi wa tabaka la watumwa dhidi ya mabwana kama tabaka au, kwa maneno mengine, dhidi ya utumwa kama mfumo. Kadiri jamii zilivyozidi kuendelea kimaarifa, kiuchumi na kifikara mfumo huo wa utumwa ulianza kufa pole pole katika baadhi ya jamii. Badala ya utumwa-mkongwe jamii nyingi za huko Ulaya, ikiwa pamoja na duingereza, ziliingia katika mfumo wa ukabaila. Katika Afrika pia baadhi ya jamii zilifikia hatua hii ya tatu ya maendeleo ya jamii ambayo ni hatua ya ukabaila: Misri, Ethiopia, Buganda, Bukoba na Tanzania visiwani ni baadhi tu ya jamii zilizokuza ukabila.

Tofauti na mabwana, makabaila ambao huunda tabaka la wanyonyaji hawakumiliki watu. Wao waliwatumikisha watu ambao tutawaita 'watwana' katika shughuli zote za uzalishaji mali. Makabaila walimiliki ardhi ambayo ndio msingi mkuu wa

uchumi wao. Umma wa watu ulinyimwa haki ya kumiliki ardhi. Umma huo wa watu, yaani, watwana, ukalazimika kuwategemea makabaila kuwapatia ardhi. Papo hapo watwana walilazimishwa kuwalipa makabaila sehemu kubwa sana ya mazao ya jasho lao, kiasi kwamba wao wenyewe wanakuza, siku hata siku, utovu wa maendeleo yao. Wakati huo huo makabaila wanazidi, siku hata siku, kuimarisha mpango wao wa kinyonyaji kwa njia ya 'milisha', yaani, majeshi ya kulinda maslahi ya kabaila.

Ukabaila kama mpango wa kinyonyaji huwaondolea watwana haki zao nyingi za asili; na kwamba kisiasa hawaruhusiwi kuwa na sauti. Kimaisha hubaguliwa. Kiuchumi huwa ni vyombo vya kuzalisha mali ya makabaila wao. Kutokana na kunyonywa, kukandamizwa na dhuluma nyingine nyingi tabaka la walio wengi huingizwa katika utwana. Utwana ni hali ya utumwa katika hatua yake ya pili. Tofauti ni kuwa katika mfumo wa utumwa watu humilikiwa kisheria. Chini ya mfumo wa ukabaila, kisheria watwana ni watu huru. Nguvu za watwana hutawaliwa na makabaila, kwa maana watwana hulazimishwa kuzalisha mali ya aina itakiwayo na makabaila; na kwamba sehemu kubwa ya mazao ya jasho la watwana hutolewa kwa makabaila kama ushuru.

Watwana, kinyume cha watumwa, huwa huru zaidi kufanya majaribio mbali mbali ya kinadharia, kisayansi, kitekinologia na kiuchumi, kwa mfano, ustawishaji wa mashamba, uendelezaji wa viwanda mbali mbali na uendeshaji wa biashara ndani na nje ya nchi zao. Kadiri ukabaila ulivyozidi kukomaa ndivyo tabaka la tatu lilivyojitokeza na kudhihirika. Tabaka hili la tatu ambalo lilidhihirika sana katika Uingereza kati ya miaka 1500 na 1800 hujulikana kama tabaka la watu wa kati ambao ni 'vibepari vidogo'. Katika kundi hili hujumuika wafanya biashara ya ndani na nje, wataalam wa taaluma mbali mbali na kadhalika. Makabaila hujitahidi sana kukinunua na kuimarisha shughuli za kikundi hiki cha vibepari vidogo kwa kuwapatia misaada ya kifedha na ya aina nyingine kwa madhumuni ya kuendeleza viwanda vidogo vidogo; pia kwa kuendeleza utafiti wa maarifa ya kisayansi, kiufundi na kitekinologia.

Kutokana na kupanuliwa kwa maarifa ya kisayansi, ufundi na tekinologia jamii za Kiyuronodi ziliweza kutengeneza vyombo vya kusafiria mabaharini na kuweza kusafiri hadi mabara ya Marekani, Afrika na Asia. Matokeo yake ni 'ubeberu-wa-kibiashara'. 'Ubeberu wa kibiashara' una maana mbili. Maana ya

kwanza ni uwezo wa kitekinologia wa jamii za Kiyuronodi, hasa za Yuropa, uliowawezesha kufika Afrika, Asia na Marekani katika miaka 1440 na 1500. Tukio lililofuatia ni kuingizwa na kuenezwa kwa ukoloni-mkongwe katika mabara ya Marekani, Asia na katika sehemu za Afrika kati ya miaka 1500 na 1800. Kwa hiyo, maana ya pili ya ubeberu wa kibiashara ni kuwa, ubeberu huu uliendeshwa kabla ya kipindi cha mapinduzi ya kisayansi na viwanda ya karne ya kumi na nane na kumi na tisa kufikiwa huko Ulaya, hasa katika Uingereza.

d. Mfumo wa kibepari.

Kama utumwa na ukabaila, ubepari ni mfumo wa kitabaka unaoruhusu unyonyaji. Unyonyaji wa kibepari ni wa kisayansi zaidi. Ubepari ni mfumo ambao umetokea wakati mtu amepiga hatua ya juu sana katika ulimwengu wa nadharia, hasa, katika ulimwengu wa maarifa ya kisayansi, ufundi na kitekinologia, yaani, maarifa ya utengenezaji na utumiaji wa mashine na kadhalika katika kuzalisha mali. Tofauti kati ya ukabaila na ubepari ni katika misingi ya unyonyaji. Kabaila na bepari wote hunyonya watu. Lakini bepari hutofautiana na kabaila kwa vile bepari hutegemea mtaji katika kuendeleza shughuli zake za kinyonyaji kinyume cha kabaila ambaye msingi mkuu wa unyonyaji wake ni ardhi na siku hizi majumba katika miji. Ili kuelewa vema jinsi mfumo wa ubepari ulivyokuwa inafaa kuanza na maelezo mafupi ya historia ya ubepari.

Uingereza ilikuwa ni nchi ya kwanza kukuza mfumo wa kibepari katika historia ya mtu duniani. Mfumo huo uliletwa na mapinduzi ya viwanda ambayo ni matokeo ya maendeleo makubwa ya mtu katika ulimwengu wa sayansi, ufundi na utengenezaji wa zana na mashine za aina mbali mbali. Mapinduzi haya ya viwanda hayakupangiwa wala hayakutokea ghafla bali yalikuwa ni matokeo ya majaribio ya kisayansi na kitekinologia ya kipindi kirefu sana.

Chini ya 'ubeberu-wa-kibiashara' mabeberu wa Kiyuronodi walitegemea na kunufaika sana na jasho la watumwa wa Kiafronodi waliochukuliwa kwa wingi sana na kutumikishwa kikatili katika mashamba na machimbo ya madini hasa katika Bara la Marekani na katika Visiwa vya Karibiani. Makabaila na mabeberu wa kipindi hiki waliweza kulimbikiza mali nyingi; na kutokana na mali hiyo ya kulimbikiza makabaila na mabepari walipata uwezo mkubwa wa kuendeleza mipango ya maarifa ya kisayansi, ufundi na kitekinologia kwa kuajiri wataalam ambao kimaisha hali yao ilikuwa bora kushinda ya watwana katika

mashamba ya kabaila.

Maarifa ya kilimo yakaongezeka. Utumiaji wa mbolea na umilikaji wa ardhi kwa njia ya uwigo ni miongoni mwa mambo muhimu yaliyoleta mabadiliko katika kilimo. Viwanda vidogo vidogo vikaanza kumezwa na viwanda vikubwa ambavyo vilianza kujitokeza, hasa katika Uingereza. Uingereza, ikiwa ni nchi ya kwanza katika dunia kukuza viwanda, ilifikia ubepari kuanzia nusu ya pili ya karne ya kumi na nane na miaka ya mwanzo ya karne ya kumi na tisa. Dunia ya viwanda ilibaki ni utawala wa Waingereza kwa muda wa miaka isiyopungua thelathini. Baadaye jamii nyingine za Kiyuronodi zilifuatia. Viwanda hivyo vya mwanzo vilikuwa vya aina nyingi. Lakini viwanda vya chuma, pamba, nguo na kadhalika, vilikuwa miongoni mwa viwanda vikuu. Muhimu zaidi kwa kusukuma na kuharakisha mapambano ya mendeleo ni kukuzwa kwa viwanda-mama. Viwanda-mama hutoa bidhaa ambazo husaidia kuendeleza uzalishaji wa mali au bidhaa zaidi na za aina iliyotayari kwa matumizi ya binadamu. Kwa mfano, kiwanda cha chuma, kama kiwanda-mama, hutengeneza chuma cha aina mbali mbali. Chuma hicho huwa tena ni bidhaa-asili ambayo huweza kutumika katika kiwanda cha zana za kilimo, kiwanda cha cherahani, kiwanda cha nguo, kiwanda cha vyombo vya uchukuzi na mawasiliano, kiwanda cha zana za vita na vifaa vya kujengea viwanda vingi vingine.

Kukuzwa kwa viwanda kulileta mabadiliko kadhaa katika maisha ya jamii ya Kiingereza na katika uhusiano wake na jamii nyingine duniani. Papo hapo, viwanda vikawa ndiyo msingi mkuu wa maendeleo ya haraka ya mtu katika dunia. Viwanda vilifanya Uingereza na baadaye mataifa mengi ya Ulaya kuanza kuvitegemea zaidi kimaisha badala ya kilimo. Kwa sababu ya vyombo bora vya kilimo vilivyotengenezwa viwandani, ikiwa pamoja na maarifa mapya ya kisayansi, makabaila waliweza, licha ya kupanua, kuendeleza mashamba yao na kiasi cha mazao.

Matumizi ya zana bora za kilimo, yaani, mashine yaliwafanya makabaila kupunguza idadi ya watwana. Wengi wa watwana hao walilazimika kutafuta kazi za kuajiriwa kama vibarua katika viwanda. Viwanda, licha ya kuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha mali kwa wingi katika muda mfupi, viliwezesha miji mingi kujitokeza. Baadhi ya watwana au wakulima wadogo wadogo ambao mashamba yao yalimezwa na makabaila walihamia mijini kama mafundi wa taalauma tofauti, wengine kama wafanya biashara na wengine kama waendeshaji mabenki.

Maisha ya mijini yalileta sura tofauti na kujenga fikara mpya katika jamii. Matabaka ya wafanyakazi na mabepari yakaanza kujitokeza na kudhihirika kadiri viwanda vilivyozidi kukuzwa na kuendelezwa. Idadi ya mabepari ikawa inakua siku hata siku. Papo hapo idadi ya watu waishio mijini kwa kutegemea viwanda na biashara ikawa kubwa zaidi kuliko idadi ya wakulima wa mashambani. Idadi kubwa ya wafanyakazi pamoja na nguvu ya kiuchumi ilimpa bepari sauti kubwa, na kwa hiyo, nguvu kubwa ya kutawala siasa ya nchi. Uingereza, na baadaye ikifuatiwa na nchi nyinginezo za Ulaya Magharibi, ilikuwa imeingizwa katika mpango tofauti wa uchumi na maisha ya kijamii ambao ni ubepari.

Ubepari ukiwa ni hatua ya tatu ya kinyonyaji iliyopata kufikiwa na mtu au jamii za watu duniani kwa njia ya mapinduzi ya ndani ya viwanda au kwa njia ya ubeberu na ukoloni, una uwezo mkubwa sana wa kunyonya. Unyonyaji wa kibepari ni wa kisayansi, kama ilivyoelezwa hapo kwanza, na kwa hiyo, huwa ni unyonyaji wa hali ya juu sana. Wafanyakazi viwandani walikamuliwa sana jasho lao. Walilipwa ujira ambao haukuwawezesha hata kupata sembe ya kutosheleza jamii zao hata kwa mlo wa siku moja. Kwa jinsi hiyo wafanyakazi walilazimika kuwaandikisha watoto na wake zao kama wafanyakazi.

Hali ya wafanyakazi wa viwanda wa huko Uingereza ilizidi kuwa mbaya siku hata siku. Tofauti ya hali ya maisha baina ya mabepari na wafanyakazi ilizidi kuwa kubwa na mbaya muda wote.

Wafanyakazi walilazimika kuishi mapangoni. Hali ya hewa humo mapangoni ilikuwa mbaya sana; na wengi walipoteza afya pamoja na uhai wao. Afya ya wafanyakazi pia ilidhoofishwa na muda mrefu wa kazi. Kwa muda wa masaa kumi na nane wafanyakazi walitakiwa kuwa kazini kila siku. Kwa jinsi hii wafanyakazi walikosa muda wa kupumzika na kujiburudisha au kufurahia maisha, jambo ambalo ni muhimu sana; na hasa ndio shabaha ya mtu kama mwendeshaji wa mapambano ya maendeleo.

Wafanyakazi walinyimwa haki ya maisha. Hapakuwa na mpango wo wote kuhusu akiba ya uzeeni, matibabu wala elimu ya watoto wa wafanyakazi. Papo hapo wafanyakazi hawakutazamia kustaafu bali kila walipofikia umri wa uzee walitupwa na mabeberu kama vile chombo cho chote ambacho kimezeeka na kutofaa tena kwa matumizi ya mtu hutupwa kwenye jalala.

Ubepari hauna huruma wala haujali utu. Kwa bepari thamani ya wafanyakazi huonekana tu katika huduma yao, yaani, kama vyombo vya kuzalishia mali. Kwa jinsi hii wafanyakazi viwandani katika viwanda vya mabepari hawakuwa tofauti na watumwa chini ya mabwana au watwana chini ya utumishi wa makabaila. Watwana na wafanyakazi viwandani, kinyume cha watumwa, walihesabika kisheria kuwa ni watu huru. Kimaisha wote hao walimilikiwa pasipo wenyewe kutambua. Wafanyakazi viwandani nao waliwekewa masharti magumu ya kazi na mabepari. Masharti yote yalikuwa na lengo la kuwakandamiza wakulima na wafanyakazi ili wapate kunyonyeka vema. Hawakuwa huru kuacha kazi ya kabaila au ya bepari maana hawakuwa na njia nyingine ya kuhakikisha uhai wao, japokuwa siyo kuuendeleza, ila kuendelea kuuza hata tone la mwisho la jasho lao kwa makabaila na mabepari. Kwa jinsi hii, japo si kisheria, walimilikiwa kama watumwa.

Mabepari na makabaila waliokuwa na sauti kubwa katika serikali waliweza kuyatawala na kuyatumia majeshi kwa kulinda mpango wa kibepari na mfumo mzima wa jamii dhidi ya mapinduzi ya watwana na wafanyakazi.

Makabaila na mabepari walikuwa na mambo kadhaaa yaliyowahusisha. Wote walikuwa wanyonyaji. Wote walishika hatamu ya kuongoza serikali na kutawala. Kiuchumi wote waliweka faida mbele dhidi ya utu na hali bora ya wafanyakazi wao. Wote walipinga maendeleo ya watu. Wote walijawa na moyo wa kikatili na, kwa hiyo, ubinafsi. Wote walipigania maendeleo yao wenyewe kama tabaka dhidi ya vibepari vidogo na wakulima wadogo. Wote waliongea lugha ya ubwana mkubwa. Wote wakadhulumu, wakanyanyasa, wakakandamiza na kuongeza unyonge wa tabaka la wanaonyonywa. Hata hivyo, makabaila na mabepari walitofautiana katika mambo fulani fulani. Kwanza kabisa, ukabaila ambao msingi wake mkuu ni ardhi na katika miji majumba ya kupangisha ulikuwa wenyewe unagongana na ubepari ambao msingi wake mkuu ni mtaji na viwanda.

Tofauti nyingine ni kuwa ukabaila, ambao pasipo shamu ukaandaa na kuzaa ubepari, haukuwa mfumo wa kimaendeleo licha ya kunyima maendeleo ya walio wengi. Kwa upande mwingine, ubepari ambao ni matokeo ya maendeleo ya sayansi na maarifa ya kitekinologia, ambayo ni matunda ya mapambano ya mtu na mazingara, ulikuwa na uwezo mkubwa sana wa kuleta maendeleo ya vitu maendeleo zaidi ya maarifa na kinadharia,

kisayansi na kitekinologia ambayo yamekuwa mchango, hazina na urithi mkubwa wa mtu au jamii po pote duniani. Ubepari kwa kuunda tabaka la wafanyakazi ulitoa mwamko mkubwa miongoni mwa wafanyakazi. Mwamko huo wa kisiasa wa wafanyakazi pia umefanya tabaka la wanyonyaji, yaani, makabaila na mabepari kuungana nguvu dhidi ya wafanyakazi kama tabaka.

Mapinduzi ya wafanyakazi katika nchi hizo, kinyume cha matabili ya Kalo Maksi, hayana nafasi sana. Mabepari siku zote hubuni mbinu na siasa mpya ya kuwatuliza wafanyakazi. Hii haina maana kuwa mapinduzi ya wafanyakazi hayawezekani kabisa. Mapinduzi ya wafanyakazi katika nchi zilizokomaza ubepari yanawezekana tu baada ya wafanyakazi wenyewe kupata mwamko wa kutosha wa kimapinduzi.

Kwa sababu ya uwezo mkubwa wa kuzalisha mali ya aina zote, siyo kwa kufuatia mahitaji ya watu wao, mabepari walikabiliwa na matatizo kadhaa ambayo ilibidi wayatatue. Kwanza kabisa, sheria za Uingereza ziliwataka mabepari na wafanya biashara kuuza bidhaa zao za viwandani katika Uingereza yenyewe na katika makoloni au himaya yao tu.

Bei ya bidhaa ndani ya Uingereza na katika makoloni, kwa kiasi fulani, zilipangwa na serikali. Japokuwa viwanda havikuweza kutosheleza mahitaji ya Waingereza na watu wa makoloni yao mabepari walikuwa na tuhuma na shauku kubwa ya kupata faida kubwa kutokana na mauzo ya bidhaa zao kwa bei ya juu. Hii ilikuwa na maana ya kupigania kubadilishwa kwa sheria za biashara ili kuwawezesha kuendesha biashara, yaani, kununua na kuuza bidhaa zao po pote walipoweza kupata bei ya juu. Hivi vilifahamika kama vita vya uhuru wa biashara'.

Makabaila ambao kwa miaka mingi walitawala soko la mazao ya chakula kama vile mahindi na ngano walipinga sana maendeleo ya viwanda na hasa mpango wa 'uhuru wa biashara'. Makabaila hao walitambua kuwa mpango huo ungeharibu soko lao kwa kuingiza mahindi na ngano kutoka nje ambayo ingeuzwa kwa bei ya chini zaidi. Vita hivi vya uhuru wa biashara vilikuwa vikali sana katika kipindi cha kuanzia mwishoni mwa nusu ya pili ya karne ya kumi na nane na mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Katika vita hivi mabeberu walisaidiwa sana na watu wa makoloni kama vile Kanada, Australia na nchi ya Marekani ambayo ilikuwa imekwisha kujinyakulia uhuru wake mnamo 1776 na baadaye kukuza viwanda vyake yenyewe. Vile vile juhudi za mabeberu za kupigania uhuru wa biashara ziliungwa mkono na

serikali za mataifa mengine ya Ulaya ambayo yalihitaji pia bidhaa za viwandani kutoka Uingereza; na pia kuweza kuwauzia mabepari wa Kiingereza bidhaa-asili.

Viwanda vilihitaji bidhaa-asili kuviwezesha kuzalisha mali. Pia mabepari walihitaji sana mafuta ya chikichi kwa ajili ya kulainishia mitambo ya mashine viwandani. Papo hapo mabepari wa Uingereza, na baadaye wakiungwa mkono na mabepari wengine wa Ulaya, walitaka kuendeleza nadharia ya kuwa na wafanyakazi wa gharama ya chini. Mambo hayo yote yalipatikana Afrika.

Kwanza, ilibidi kufufua biashara ya zamani ya mafuta ya chikichi ambayo iliharibiwa na biashara ya watumwa huko Afrika Magharibi kama itakavyoonekana hapo baadaye. Pili, Afrika iliweza kutoa jawabu kwa suala la kupata wafanyakazi wa gharama ya chini. Afrika ilikuwa na watu ambao kwa muda mrefu walichukuliwa na kutumikishwa kama watumwa katika nchi za ugenini. Bidhaa-asili: madini na mazao ya kilimo, ambazo zilihitajika kuendeshea viwanda pia ziliweza kupatikana kutoka Afrika. Makoloni mengi ya zamani, yaani, yaliyovamiwa wakati wa ubeberu-wa-biashara yalikuwa yamejiingiza katika mpango wa 'uhuru wa biashara'. Pia ardhi ya makoloni hayo ilikuwa imechoka. Haikuweza kukuza tena baadhi ya mazao yaliyohitajiwa na mabeberu. Papo hapo baadhi ya makoloni yalijitawala na kukuza viwanda vyake. Jawabu ambalo mabepari walikuwa nalo ni kupambana na mpango wa utumwa-mkongwe pamoja na biashara ya watumwa ili kuweza kuwapata na kuwatumikisha Waafronodi humu humu Afrika. Vile vile Afrika ilikuwa katika hali ya kuweza kutatua suala la upanuzi wa soko la biashara la mabepari.

Kwa ufupi, masuala hayo yalitatuliwa kwa mpango wa ubeberu-wa-kibepari. Ubeberu huu umeitwa wa kibepari kwa sababu msingi wake ulikuwa ni ubepari uliokuzwa huko Ulaya katika karne ya kumi na tisa. Ubeberu-wa-kibepari wenyewe ulikuwa ni ubepari katika hatua ya juu sana. Ubepari ulianza kuvuka mipaka ya nchi za Ulaya na kusambaza mirija yake katika nchi za Kiafrika katika mpango wa ukoloni. Hivyo, kifungu cha maneno 'ubeberu-wa-kibepari' kimetumika pia kwa shabaha ya kutofautisha ubeberu wa karne ya kumi na tisa na ule wa kibiashara ulioendeshwa kati ya 1500 na 1800, yaani, kabla ya ubepari kukomaa.

Kutokana na matatizo yaliyoelezwa hapo juu ni dhahiri kwamba mabepari wa Kiingereza, na baadaye mabepari wa

mataifa mengine, walilazimika kutafuta makoloni mapya. Katika nchi nyingi za Ulaya ubepari ulikuzwa kati ya miaka ya 1800 na 1880. Lakini kwa kuwa karibu nchi zote za Ulaya zilikuza viwanda na kuendeleza ubepari ilibidi mabepari wa Uingereza kutafuta makoloni mapya. Uwezakano wa kupata makoloni mapya ulibakia tu katika Bara la Afrika, na katika sehemu nyingine za dunia ambapo ubepari haukukuzwa. Inafahamika kihistoria kwamba viwanda vingi katika baadhi ya nchi za Ulaya kama vile Urusi na Ujerumani vilikuwa vya mabepari wa kigeni kama vile Waingereza na Wayahudi. Wananchi, ingawa kisiasa walitawaliwa na viongozi wao wa jadi, yaani, wafalme, walikuwa wanyonge kwa sababu ya kukandamizwa, kupuuzwa, kunyanyaswa na kunyonywa na wadhalimu hao wa kigeni. Kufanikiwa kwa wanyonyaji hao wa kigeni kulitegemea sana kushirikiana kwao na tabaka la wanyonyaji wa ndani.

Kutokana na vitendo hivyo vya udhalimu vya mabeberu wa kigeni wananchi wa Urusi ilibidi wachukue hatua za kupindua serikali ya kifalme na mpango mzima wa kiuchumi na wa maisha ya jamii mnamo Oktoba, 1917. Hatua hiyo ilichukuliwa ili kukomboa umma wa Warusi na kuwarudishia hadhi yao ya kiutu. Hayo yalikuwa ni mapinduzi ya kwanza ya kijamaa katika dunia.

Wajerumani, kama taifa, waliungana mnamo 1870. Baada ya muungano wao Wajerumani walipiga hatua za haraka sana za kiuchumi wa 'kitaifa'. Viwanda-mama vilikuzwa na kuendelezwa. Hata hivyo, mabepari wa Ujerumani walikuwa bado ni mchanganyiko wa kikundi tajiri cha wananchi wakishirikiana na mabepari wa kigeni. Hatua za kuweka viwanda na njia nyingine za uchumi mikononi mwa mabepari wananchi na serikali zilichukuliwa tu kati ya miaka 1930 na 1940. Jambo la maana ni kuwa kuchelewa kwa kuzaliwa kwa taifa la Ujerumani kunatosha kuwa maelezo kamili ya kuchelewa kwa Ujerumani kujiingiza katika suala la ukoloni. Wajerumani walilazimika tu kutafuta makoloni mnamo miaka ya 1880. Hii ina maana kuwa wakati huo ubepari katika Ujerumani ulikuwa umefikia kiwango cha juu sana.

Ubepari wa Kiingereza ulikomaa na kupevuka sana kati ya miaka 1700 na 1850. Hivyo, umuhimu wa makoloni kwao ulianza kuonekana mapema zaidi kuliko miongoni mwa mabepari wa mataifa mengine ya Ulaya Magharibi. Na hii ni sababu ya kutosha kueleza kwa nini Waingereza walikuwa katika mstari wa mbele katika mapambano ya kukomesha biashara ya watumwa

na utumwa-mkongwe ambao kwa fikara za mabepari wakati wake ulikuwa umepita.

e. Mfumo wa kijamaa.

Ujamaa siyo ujima. Mifumo hiyo miwili hufanana katika jambo moja kubwa nalo ni utovu wa tabaka. Katika mifumo yote miwili kuna usawa wa watu, haki sawa, heshima sawa, na utovu wa aina zote za unyonyaji.

Hata hivyo, mifumo ya ujima na ujamaa hutofautiana katika misingi kadhaa. Ujima ni mfumo ambao jamii nyingi duniani zimekuza tangu kujitokeza kwao kama jamii siyo matokeo ya mapambano ya kitabaka. Pili, mfumo wa kijima huzuka wenyewe wakati ujamaa hupangiwa lengo na mbinu za kuujenga na jamii iliyoamua kukuza ujamaa. Lengo la ujamaa ni kuleta usawa wa jamii na kukomesha aina zote za unyonyaji kama vile ukabaila na ubepari kwa ajili ya maendeleo ya jamii.

Tofauti nyingine ni kuwa ujima ni mfumo unaoonekana katika jamii ambazo kinadharia, kisayansi, kiufundi, kitekinologia na kwa hiyo, kimaisha, hazijajiendeleza sana. Ujima una umri usiopungua miaka 10,000 wakati ambapo ujamaa leo una umri upatao miaka hamsini na tisa tu tangu mapinduzi ya kwanza. Ujamaa kama mfumo ni jawabu kwa mifumo ya kinyonyaji wakati ambapo ujima unakuwa ni hatua ya mwanzo ya maendeleo ya jamii kimfumo.

Ujima ulisaidia kuleta mabadiliko katika jamii baada ya kipindi kisichopungua miaka 1,690,000 ya maisha ya mtu duniani. Jamii nyingi zilianza kuishi pamoja na kushirikiana katika shughuli mbali mbali za kiuchumi na maisha kwa ujumla. Kwa jinsi hii, maisha hayo ya pamoja, yaani, maisha ya kijima yalisaidia, pasipo jamii yenyewe kupangia, kuleta mabadiliko makubwa katika ulimwengu mbali mbali wa maisha ya mtu.

Ujamaa ambao, kwa nafasi ya kwanza, unawataka watu kuishi kwa pamoja una lengo la kuleta maendeleo ya watu kama jamii na wala siyo maendeleo ya watu wachache waliojawa na ubinafsi. Kwa hiyo, ujima ulikuwa na upungufu. Utovu wa lengo na mipango; na kwamba katika ujima suala la 'mgawanyo wa kazi na mali' halikuwepo, kadhalika suala la maazimio makubwa ya mipango ya baadaye kwa ajili ya maendeleo zaidi ya jamii halikuwepo.

Katika kujenga ujamaa watu au jamii huzingatia sana suala la maarifa ya kisayansi, kitekinologia na kinadharia. Kwa msingi huo tu, tunaweza kusema, ujamaa ni mfumo wa kisayansi. Hata hivyo, kuna watu kama akina Kalo Maksi, Lenini na kadhalika

ambao huamini kuwa ujamaa, kama itikadi, ni mfumo wa kisayansi. Wanafalsafa hawa hutoa tafasiri yao katika misingi miwili. Kwanza, wana maana kuwa maendeleo yanaweza tu kutokana na maendeleo ya maarifa ya kisayansi na kitekinologia. Mpaka hapo mtungaji hukubaliana nao kabisa. Pili, wanafalsafa hao hao wameambatanisha suala la sayansi na imani ya Mungu na kujaribu kuonyesha kuwa imani juu ya Mungu huzuia ujenzi wa ujamaa. Hilo linahitaji mjadala.

Suala la kuondoa imani juu ya Mungu silo linalofanya ujamaa kama itikadi uonekane kuwa wa kisayansi. Imani za dini ni moja ya matukio ya maendeleo ya watu duniani. Kwa ufupi, mtu amejiendeleza kiuchumi, kimaarifa, kitamaduni: dini ikiwa ni sehemu yake, na kadhalika. Kama ilivyokuwa, mifumo yote iliyotangulia ujamaa, pamoja na ujamaa wenyewe, ni imani ambazo mtu ameshikilia kwa vipindi mbali mbali.

Kuwepo kwa imani juu ya Mungu hakuwezi kuhatarisha mapinduzi ya kijamaa. Kwa nini, basi, ndugu hao walileta suala la imani za dini katika mjadala wa itikadi ya ujamaa. Wanafalsafa hao wakitazamwa katika mazingara ya wakati wao wataonekana kwamba walikuwa na sababu ya kutoa nafasi ya hoja juu ya imani za dini katika mapinduzi ya kijamaa.

Imani ya dini, kama ilivyoelezwa katika sehemu nyingine ya kitabu hiki, haina dosari. Hata hivyo, kuna ukweli kuwa watu au viongozi wa dini kwa bahati mbaya walijitambulisha zaidi na tabaka za makabaila na mabepari. Mahubiri ya dini yalitetea maslahi ya wakubwa dhidi ya wanyonge. Kwa hiyo, dini zilionekana kuwa ni kipingamizi kwa mapinduzi ya ukombozi wa umma wa wanyonge.

Mwandishi angependa kusisitiza kuwa hii ilikuwa ni bahati mbaya kwa sababu dini si viongozi wa mambo ya roho bali ni imani ya jamii juu ya Mungu. Kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu hakuna uhusiano na utekelezaji wa itikadi ya ujamaa iwapo wahubiri wa dini hawapotoshi mahubiri yao juu ya ujamaa kwa ajili ya kuendeleza unyonyaji wa tabaka lao ikiwa pamoja na kulinda hadhi yao ya kimwinyi.

Si nia ya mwandishi wa kitabu hiki kulizingatia sana suala la nafasi ya dini katika ujenzi wa ujamaa. Lakini, kwa vile suala lenyewe limekwisha kutolewa uwanjani kama hoja, mtungaji naye, kwa vile msimamo wake ni wa kupendelea itikadi ya ujamaa, anaona ni muhimu kutoa maoni kuhusu nafasi ya dini; na ndio maana ameweza kutoa sura nzima juu ya wamisionari na wahubiri wa dini, katika kitabu hiki, ambao ni wananchi na

suala la kuleta mapinduzi ya jamii zao.

Ni kweli kuwa mahubiri mengi ya viongozi wa dini hayana msingi wa kimapinduzi na wala kurekebishwa kwake hakutahatarisha misingi ya imani za dini. Kinyume chake, mahubiri hayo huwa pengine kipingamizi kwa wanamapinduzi. Jambo muhimu ni kuwasaidia viongozi wa dini kuondokana na fikara za kikasumba, fikara ambazo hazina misingi hasa ya kiimani. Kutokana na hoja hii ni dhahiri kuwa tatizo la wanamapinduzi, halimo hasa katika msingi wa imani bali katika msingi wa kupotosha imani, yaani, katika msingi wa kasumba. Dini yo yote ambayo itaelezwa katika msingi wa kupinga maendeleo ya jamii kwa ajili ya kutetea maslahi ya wanyonyaji haina budi kupigwa vita na jamii yenyewe. Kitendo hicho ni tofauti na kuamini kuwa imani juu ya Mungu zinapinga maendeleo. Mungu, kama yupo, ameelezwa katika misahafu kuwa yeye ndiye asili na chemichemi ya uchaji wote. Hivyo, kwa mtu ye yote mwenye akili timamu, hawezi akawa na mgongano wa kihasama ndani yake mwenyewe. Mungu ambaye, kadiri ya imani, ni asili ya upendo, usawa na haki hawezi akawa wakati huo huo na tabia ya ubaguzi na upendeleo. Kinyume chake atatazamiwa kukamilika katika uchaji wake kwa kuwa mjamaa wa mstari wa mbele zaidi kuliko watu wote wanaohubiri na kuhubiriwa mapinduzi ya kijamaa. Na kama pasingetokea wahubiri wa kasumba za kupinga mapinduzi kwa kutumia imani za dini pasingepata kutokea suala la mjadala wa imani za dini miongoni mwa wanamapinduzi wa nyakati zote.

Hoja nyingine ni kuwa Angelo na Maksi walitabili kuwa jamii zingepitia katika hatua maalum za maendeleo ya jamii kimfumo kabla ya kufikia hatua ya ujamaa. Moja ya hatua hizo ni ubepari. Kwa fikara za Maksi ujamaa ni matokeo ya wafanyakazi, katika mfumo wa kibepari, kunyang'anya madaraka na kuyaweka mikononi mwao kwa ajili ya maendeleo ya jamii. Nini ukweli wa hoja hii hasa kwetu sisi Waafrika tukitaka, na kusema kweli ni lazima zaidi kwa upande wetu, kuamua kujenga ujamaa?

Ukweli ni kuwa Uingereza na Marekani ambako ubepari umekomaa sana matumaini ya wafanyakazi kubomoa mfumo wa ubepari yako mbali sana. Kwa upande mwingine Urusi, ambako ubeberu haukuendelea sana, mfumo wa ukabaila ulikuwa bado na nguvu sana, mapinduzi ya kijamaa kwa uongozi na mweleke-zo wa chama cha Bosheviki, chini ya ndugu V.I. Lenini, yalifanikiwa kwa mara ya kwanza katika historia ya ujamaa duniani mnamo 1917. Juhudi za wafanyakazi katika Uingereza

zinaonyesha kushindwa kuleta mapinduzi japokuwa ubepari katika nchi hiyo ulikuzwa miaka mingi kabla ya mapinduzi ya Oktoba 1917.

Kwa hiyo, nini basi, maelezo ya utabili huu? Mtungaji hana maana ya kupingana na falsafa hii ya Angelo na Maksi. Ukweli ni kuwa dhuluma za ubepari ni kubwa na mbaya mno kwa jinsi zinaweza kuharakisha mapinduzi. Hata hivyo, suala linabaki kuwa ni wapi mapinduzi hayo yanaharakishwa: nyumbani au ugenini ambako ubepari umepanukia? Kutokana na maarifa ya mapinduzi ya Urusi—ikifuatiwa na China, Kyuba, Korea na leo baadhi ya nchi za Kiafrika, mambo mawili yanaonekana kuwa dhahiri.

Kwanza kabisa, mapinduzi hayo yamesababishwa na mfumo wa kibepari ukiwa katika hatua ya ubeberu. Pili, mapinduzi yameanzia katika nchi ambako ubepari umepanukia. Hali hii inaelezeka kwa kuangalia tabia ya ubepari uliofanikiwa kufikia hatua ya ubeberu na ukoloni.

Dhuluma zitokanazo na ubeberu na ukoloni ni kubwa mno kiasi kwamba zinaharakisha mapinduzi. Wananchi katika makoloni au katika nchi ambako ubepari wa kigeni umestawi sana kwa kushirikiana na makabaila wa ndani huendesha unyonyaji na, hasa, ubaguzi wa hali ya juu zaidi kuliko nyumbani unakotoka. Kwa hiyo, wananchi wa nchi hizo kutokana na kukandamizwa, kudharauliwa, kubaguliwa na kunyonywa mno hulazimika zaidi kuchukua hatua za kimapinduzi za kupambana na ukoloni pamoja na ubeberu. Kwa upande mwingine, wafanyakazi katika nchi ambako ubeberu umetoka hununuliwa na mabepari na makabaila wao kwa kupewa makombo manene zaidi na kwa hiyo hunyamazishwa. Lengo lao la kuleta mapinduzi ya kijamaa huwa limepotoshwa!

Hoja hizo haziwezi kuridhisha zikikomea hapo. Kwanza, itaonyesha kuwa kubwaga ukoloni kunakwenda pamoja na kubwaga ubeberu na aina zote za unyonyaji. Hii si kweli. Kubwaga ukoloni ni tofauti na kubwaga ubeberu au na kukomesha aina zote za unyonyaji. Ukweli ni kwamba katika vita vya kupambana na ukoloni viongozi wa mapambano hayo hutumia lugha ya kimapinduzi. Baadhi yao huamini moja kwa moja kuwa ukombozi wa jamii au taifa hauwezi kukamilika mpaka aina zote za unyonyaji na dhuluma zimekomeshwa kwa shabaha ya kuleta maendeleo ya wanajamii ambao ndio hasa huendesha mapambano hayo ya kimapinduzi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya viongozi hutumia lugha ya

kimapinduzi wakati wa mapambano ya uhuru wa bendera pasipo wenyewe kuwa na imani ya dhati ya kimapinduzi. Wengi wao hununuliwa na kutayarishwa kama vibaraka wa kulinda maslahi ya mabeberu chini ya mpango wa ukoloni-mambo-leo. Watu kama hao mara nyingi huwahadaa wananchi kwa kuhubiri 'ujamaa wa kimsamiati'. Shabaha yao si kukomesha unyonyaji bali kuondoa unyonyaji wa kigeni na badala yake kujiweka wenyewe wakiendelea kuwanyonya wanajamii wenzao. Hali hii ni rahisi kuonekana katika nchi nyingi za Kiafrika ambazo hapo awali zilipata kutawaliwa na kunyonywa na mabeberu. Ukweli mwingine utokanao na maarifa hayo ya mapinduzi ya kijamaa katika nchi za Mashariki na Kyuba ni kuwa leo nchi nyingi za Dunia ya Tatu zinaendesha mapambano ya ukombozi kwa shabaha ya kuleta mapinduzi ya kijamaa. Nchi kama Msumbiji, Guinea Bissau na kadhalika, zinaendesha mapambano ya kujikomboa moja kwa moja kutokana na ukoloni-mkongwe, ukoloni-mambo-leo na pia kijamaa. Wakati huo huo nchi kama Uingereza na Marekani zinalazimika kubadili siasa yao ya unyonyaji wa ndani. Kwa maneno mengine, msukumo wa ukombozi wa tabaka la wafanyakazi katika nchi hizo utakuwa umetoka nje sehemu ambako ubepari ulipanukia na kurudi tena kujiua wenyewe katika nchi yake ya asili.

Maarifa hayo yanatoa matumaini kwa wanamapinduzi wote duniani kuwa ujamaa unaweza kujengwa hata pale ambapo ubepari wa ndani haukukuzwa sana na kwamba hata katika nchi zilizoendesha ubepari kuna matumaini bado ya kuwa siku moja nazo zitajikomboa kijamaa kwa mujibu wa maelezo ya Kalo Maksi. Lakini njia na mbinu zitakuwa tofauti kutegemea mazingara ambamo jamii inaishi. Uhuru ni ujamaa. Ujamaa ni hatua ya mwisho ya ukombozi. Ujamaa ni maendeleo ya haraka ya jamii.

Sura ya 8

JAMII ZA KIAFRIKA KABLA YA UKOLONI

Sura hii inakusudia kutoa maelezo, kwa ufupi tu, juu ya maendeleo ya jamii mbali mbali za Kiafrika kabla ya ukoloni. Kabla ya kuanza mjadala juu ya somo linalokusudiwa kuongelewa katika sura hii hapana budi, kwanza kueleweshwa mambo machache ya msingi. Kwanza kabisa, italazimu kuzingatia na kufahamu ramani yetu ya Afrika na watu wake ambao huunda jamii mbali mbali zinazotarajiwa kuongelewa. Pili, hapana budi kuzingatia maelezo juu ya maendeleo ya jamii duniani kimfumo.

Kwa upande wa wakoloni 'Afrika' ilikuwa ni sehemu ile tu iliyo kusini ya Jangwa la Sahara na ambayo ilikaliwa na watu wa ngozi nyeusi tuliowaita Waafronodi. Kwa upande mwingine, wananchi wa Afrika kaskazini ya Sahara na mashariki ya kaskazini kama vile Wamagrebu, Wahabeshi, Wasomali, na kadhalika hawakuhesabiwa kama Waafrika. Kulingana na siasa ya Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (OAU) wanahistoria wa kimapinduzi, hasa wale wenye asili ya Kiafronodi, wamechukua msimamo mpya baada ya kuitazama vipya historia ya Waafrika iliyoandikwa na wakoloni katika kipindi cha utawala wao.

Siasa ya wakoloni ni kuwagawanya wananchi wa Afrika katika makundi bila ya msingi wowote. Shabaha ni kujenga uhasama miongoni mwao ili utawala wao wa kidhalimu upate kudumishwa. Hivyo, basi, ili kurekebisha baadhi ya fikara za kikoloni itapasa kutoa maelezo juu ya jamii mbali mbali za Waafrika katika misingi ya lugha zao na mifumo yao. Mifano ya makundi au jamii mbali mbali za Kiafrika kutegemea lugha zao imetolewa na imeelezwa katika sura ya nne. Kwa hiyo, mazungumzo ya sura hii ni juu ya jamii mbali mbali kwa kutegemea misingi ya mifumo ya jamii hizo mnamo mwaka 1800 B.K. na kwa jamii nyingine mnamo 1900 B.K.

Kwa muda mrefu sana katika historia ya mtu; watu duniani kote waliishi kiukoo. Jamii zilikuwa ndogo ndogo sana. Kila

jamii ilikuwa imefungamana, imekamilika na imejitegemea. Uhusiano baina ya jamii za watu mbali mbali haukuwa mkubwa sana kama ulivyo siku hizi ijapokuwa hapakuwa na uhasama mkubwa. Kwa mfano, kale hapakuwa na haja ya biashara ya mbali wala umuhimu wa kuwekeana mabalozi. Kila jamii ilikuwa na kiongozi wake ambaye, akisaidiwa na halmashauri ya wazee, alikuwa ndiye mwenye kauri ya mwisho. Kwa mapendekezo ya mwandishi, kiongozi huyo wa jadi daima ataitwa 'mtemi'. Kazi muhimu ya mtemi ilikuwa kutoa huduma ya usuluhishi na ushauri wa uongozi kwa jamii yake. Papo hapo alikuwa na wajibu wa kuhakikisha amani, usalama wa jamii pamoja na mali ya jamii.

Jambo la maana kutia akilini ni kuwa jamii za watu, popote katika dunia zilikuwa zinajiendeleza siku hata siku. Habari za maendeleo ya mtu na jamii zimezungumziwa kwa kirefu katika sura zilizotangulia. Hata hivyo, inapasa kukumbuka kuwa maendeleo ya mtu yalikuwa ya kisayansi, kitekinologia, kiuchumi, kisiasa, kitamaduni, kifikara na kadhalika.

Jamii za watu zimepiga hatua kubwa na za haraka za maendeleo katika kipindi cha miaka ipatayo 10,000 ya nyuma, na hasa katika karne mbili za mwisho. Sababu ya kusema vile ni kuwa kuanzia miaka 10,000 iliyopita mapinduzi ya kilimo yamefanyika katika sehemu mbali mbali za dunia.

Mapinduzi ya kwanza ya kilimo, yaani, maarifa ya mwanzo ya ukulima na ufugaji, yalitokea katika Bara la Asia. Baadaye maarifa ya kilimo na ufugaji pia yalifanyika katika Bara la Marekani; na huko Afrika Magharibi miongoni mwa watu wa jamii ya Wamande yapata miaka 6,500 iliyopita; na baadaye maarifa hayo yakaenezwa katika sehemu nyingi za Afrika kuanzia miaka 2,000 au zaidi iliyopita. Maarifa hayo yalienezwa kusini ya Ikweta na jamii za Kibantu.

Yapata miaka 3,000 iliyopita wananchi wa Afrika kusini ya Sahara walijifunza ufundi wa kutengeneza chuma na vyombo vya chuma kwa matumizi mbali mbali. Maarifa ya kutengeneza chuma pamoja na uhunzi yalienea katika Afrika kaskazini ya Sahara yapata miaka 7,000 iliyopita. Maarifa ya uhunzi na ufuaji yalikuwa muhimu sana katika kuendeleza shughuli nzima ya mapinduzi ya kilimo. Mapinduzi ya kilimo yaliwawezesha watu kuishi pamoja kijamii katika vijiji. Maisha ya pamoja ndiyo yaliyoziwezesha jamii kujenga misingi halisi na dhahiri ya kisayansi na kitekinologia, ya kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, kifikara na kitaalam.

Haja ya jamii kuwa na serikali ilianza kuonekana mara tu maisha ya pamoja ya jamii yalipoanza. Watu walihitaji amani, usuluhishi, hakika ya usalama wao na wa mali zao. Jamii zilihitaji, kwa maneno mengine, chombo cha kurekebisha tabia mbali mbali za wanajumuiya. Chombo hicho ni serikali. Kimuundo serikali hizo za jadi zilikuwa ni ndogo ndogo kulingana na ukubwa wa jamii zilizohusika. Shughuli zake pia hazikuwa nyingi sana. Hata hivyo, serikali hizo za jadi zilikamilika tena zilikuwa za watu wenyewe. Kwa maneno mengine, kulikuwa na demokrasi kubwa sana; na kila mtu katika jamii ambaye alifikia umri wa utu uzima, ambao kila jamii iliweza kuukadiria, aliweza kushiriki katika shughuli mbali mbali zilizohusu siasa ya jamii. Serikali hizo za jadi, na ambazo ziliundwa na kudumishwa muda mrefu kabla ya ukoloni, hazikuwa na katiba au sheria zilizoandikwa. Msingi mkubwa wa katiba na sheria za jamii ulikuwa ni mila, desturi na thamani za maisha za kila jamii. Kwa jinsi jamii zilivyoendelea kukua tawala za jadi pia zilipanuka katika eneo la taathira au mamlaka; na pia aina mbali mbali kuhusu fikara za kisiasa zilikuzwa miongoni mwa jamii za wananchi. Vile vile, kwa jinsi jamii zilivyozidi kujiendeleza kulitokea mabadiliko ya mendeleo kwa upande wa miundo ya serikali kwa kutegemea pia mifumo na mipango ya kiuchumi ya jamii mbali mbali.

Kuishi pamoja kumewawezesha watu kubadilishana maarifa ya kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, kisayansi, kitekinologia na kifikara. Kutokana na mabadilishano ya maarifa watu wa jamii mbali mbali wameweza kujiendeleza kwa hatua na njia mbali mbali kutegemea mazingara ambmao jamii hizo mbali mbali zinaishi.

Kiuchumi watu waliweza kujifunza maarifa mengine ya kukuza na kuendeleza kilimo na ufugaji. Matokeo ni kuongezeka kwa chakula. Kutokana na kuongezeka kwa chakula idadi ya watu pia iliongezeka kwa haraka. Ili kupata chakula kutosheleza mahitaji ya maongezeko ya watu, njia mpya, vyombo bora na vifaa zaidi vya kilimo ilibidi vibuniwe. Kwa upande mmoja, tatizo hilo lilitatuliwa na maarifa ya ufuaji chuma na uhunzi wa vifaa kama majembe, miundu, mashoka, mapanga na kadhalika. Utaalam wa ufuaji na uhunzi ulikuwa ni siri na urithi wa koo maalum tu.

Kwa upande mwingine, umuhimu wa kubadilishana vitu kama vyakula, wanyama, chumvi, silaha, vyombo na vifaa vya kazi ulianza kuonekana. Na huo ulikuwa ndio chanzo cha biashara

Hivyo, kulikuwepo na mgawanyo halisi wa kazi katika jamii za Kiafrika. Baadhi ya watu waliishi kwa kutegemea matunda ya utalaam wao, kama vile: uganga, uhunzi, ufinyanzi, uwindaji, uvuvi na utengenezaji chumvi; na wengine walijitokeza kama wachuuzi au wafanya biashara. Mambo mawili ya kuzingatia kuhusu biashara inayoongelewa ni kuwa pesa haikutumika na kwamba masoko ya biashara yalikuwa kwa jamii za jirani tu. Biashara za mbali zingehitaji njia rahisi za mawasiliano na matumizi ya 'fedha' kama chombo cha kubadilishana mali. Kwa hiyo, badala ya fedha kulikuwa na biashara ya 'mali-kwa-mali'. Hata hivyo, biashara iliyoendeshwa na babu zetu ilikuwa ni kamili kwa vile iliwawezesha wananchi kujipatia mahitaji muhimu ya maisha kulingana na mazingara ya wakati wao.

Kwa sababu ya mgawano wa kazi za kitaalam; kwa mfano: ufundi, biashara, uganga na kadhalika, baadhi ya wataalam hao waliweza kuchuma na kulimbikiza mali kiasi kikubwa zaidi kuliko wakulima na wafugaji wa kawaida. Kwa sababu ya utajiri wao baadhi ya koo katika jamii katika vipindi mbali mbali zilianza kuheshimika na kutegemewa zaidi na wananchi kuhusu masilahi na uongozi. Baada ya kizazi au vizazi vichache koo hizo zikaanza kujifanya na kuaminiwa na umma katika jamii kuwa ndizo zenye haki ya pekee ya asili ya kuongoza na kutawala wengine. Hicho kilikuwa ni kitendo cha upotovu na udhalimu.

Katika baadhi ya jamii tabaka la watawala na matajiri lilijitokeza zaidi na kuanza kukandamiza na kunyonya tabaka la umma. Na katika jamii nyingine kikundi cha aina hiyo hakikujitokeza zaidi kiasi cha kunyang'anya haki za asili za umma wa watu. Kwa jinsi hiyo dhuluma na uhasama wa kitabaka viliweza kuepukika na wananchi wote wakawa na haki na heshima sawa za kiutu. Hizo zilikuwa ni jamii za kijima. Ujima ni ujamaa wa asili. Jambo la kuzingatia ni kuwa jamii zote zimepitia katika hatua hii ya ujima.

Maisha ya pamoja yamesaidia kukuza tamaduni za jamii mbali mbali. Nini maana ya utamaduni? Swali si rahisi kujibika. Hata hivyo, mambo ambayo ni sehemu muhimu ya utamaduni tunaweza kuyataja. Ikiwa ni mpango mzima unaoongoza maisha ya jamii utamaduni unajumlisha mambo mengi, kama si yote, yahusuyo maisha ya jamii; matendo, shughuli, fikara, uwezo na utaratibu wa kuratibu mipango ya maendeleo ya jamii, ukuzaji wa mila na desturi, ulezi wa vijana wa taifa la kesho, na kadhalika.

Baadhi ya mambo muhimu yaelezayo utamaduni ni lugha

ambazo jamii mbali mbali za watu huziunda na kuzitumia kama chombo mahususi cha kubadilishana mawazo, fikara na maarifa. Imani mbali mbali, mila, thamani za maisha, miiko, ngoma na nyimbo huwa ni maelezo ya fikara na shughuli za jamii kuambatana na mazingara ya kila jamii. Kwa mfano, mtu anaposhindwa kuelewa jambo kwa sababu ya ujinga huliwekea miiko; na hii ni dalili halisi ya unyonge ambao husababishwa na ujinga. Miiko hiyo hutoweka mara tu baada ya suala la ujinga kutatuliwa. Na jamii huwa imejikomboa kwa kiwango au hatua fulani.

Utamaduni, kwa maneno mengine, ni melelezo juu ya utaratibu wa maisha, mfumo na fikara za jamii, na pia ni kipimo cha upevu wa maendeleo ya jamii kuhusu kazi, siasa, uchumi, mfumo na thamani za maisha ya jamii. Na maelezo hayo huonekana, licha kwa njia ya vitu mbali mbali vinavyotengenezwa na jamii, katika nyimbo za furaha na masikitiko; na pia hukadiriwa na ukubwa wa msamiati wa lugha za jamii zenyewe.

Kuna aina kuu mbili za mifumo ya jamii. Kuna jamii ambazo watu wake waligawanyika katika matabaka ya mabwana ambao ni waheshimiwa, kwa upande mmoja, na watumwa au watwana ambao ni wanyonge, kwa upande mwingine. Aina ya pili ya mfumo wa jamii ni jamii zenye mpango wa ujima, yaani, ujamaa wa asili kama ulivyoonekana mpaka mnamo 1800 B.K. miongoni mwa jamii nyingi za Kiafrika.

Baadhi ya jamii za Kiafrika, kama vile Wamisri mpaka enzi ya Faruk, Wahabeshi, watu wa Mali ya kale, na katika Afrika Mashariki Wabaganda na Wahaya, pia zilikuwa ni jamii za kitabaka. Katika jamii hizi kulikuwa na kikundi kidogo cha watawala ambao walitumia madaraka na mamlaka ili kudhulumu umma wa walio wengi haki zao za kiutu ambazo ni haki za asili. Kwa upande mwingine, umma hutawaliwa pasipo uhuru, hukandamizwa, hudharauliwa, hupuuzwa, hunyanyaswa na hunyonywa jasho lao. Mbaya zaidi ni kuwa umma hupoteza hadhi ya utu wao na kugeuzwa watumwa. Mpango wa aina hii wa maisha ulionekana siyo katika baadhi ya jamii za Kiafrika tu bali katika jamii nyingi za watu wa mataifa mbali mbali ya dunia na jambo muhimu ni kuwa daima kuna uhasama mkubwa sana kati ya tabaka la wanyonyaji na wanaonyonywa. Uhasama huo ndio msingi wa mapambano ya tabaka la umma wa wakulima na wafanyakazi dhidi ya tabaka la wanyonyaji, yaani, mabwana, makabaila, na mabepari; pamoja na ukoloni ukiwa ni mpango muhimu wa kunyonyea.

Jamii za kijamaa hutofautiana na jamii za kitabaka kwa jinsi

ifuatavyo. Kwanza, watu wote katika jamii za kijamaa huamini kuwa wote ni sawa. Kwa maneno mengine, kuna tabaka moja tu ambalo ni tabaka la wakulima na wafanyakazi. Watu wote hubaki na haki na heshima sawa ya kiutu. Na msingi mkuu wa heshima ya watu na jamii nzima ni uhodari na uwezo wa kazi wa kila mwanajumuiya na jamii nzima. Madaraka ya uongozi hutolewa na umma kwa watu wenye uwezo, wanaokubalika na wenye sifa zote ambazo ni muhimu kwa kiongozi kwa mujibu wa sheria za jamii inayohusika.

Lakini tukizungumza juu ya jamii za kijima suala la kushirikiana na umilikaji wa mali sherti lipewe nafasi ya maelezo. Katika jamii za kijamaa za karne yetu, umma humiliki mali na njia zote za kuzalishia mali kwa pamoja. Watu huishi pamoja, hushirikiana katika kuzalisha mali; na matunda ya kazi yao huwa ni kwa faida ya wote. Kwa kufanya hivyo hakuna mtu wala kikundi cha watu kitakachoweza kunyonya umma wa wakulima na wafanyakazi. Na katika jamii za kijamaa ukoloni, kama moja ya vyombo muhimu vya kunyonyea, hauna nafasi. Hata hivyo, iko haja kwa nchi za kijamaa zinazoendelea kukuza uchumi huru wa kitaifa. Uchumi huru wa kitaifa utategemea mipango bora ya maendeleo ya uchumi ikitilia mkazo suala la utaalam, sayansi, tekinologia, viwanda mama na kilimo bora cha kisasa. Juu ya yote suala zima la ulinzi ni muhimu sana nalo huwahusu wananchi wote, maana, kuamua kujenga ujamaa ni kutangaza vita vya mapambano dhidi ya mabeberu na wanyonyaji wa ndani.

Katika Afrika, kusini ya Sahara, jamii nyingi zilikuwa za kijima. Umma wote ulikuwa na 'uhuru', heshima sawa ya kiutu; nao waliishi katika 'ujirani' wakishirikiana japokuwa si kwa manufaa ya wote. Lakini kwa kuwa jamii hazikuwa zimeendelea sana katika mambo mengi mfumo huo wa ujima ambao ndiyo msingi halisi wa ujamaa wetu, uliridhisha. Jamii za kisasa zimefikia hatua ya juu ya maendeleo kutokana na maendeleo ya kisayansi na tekinologia, ni dhahiri kuwa aina mpya ya ujamaa inahitajika. Ujamaa huu mpya ni ule ambao katika mipango yake ya maendeleo suala la utaalam na tikinologia hutiliwa mkazo sana. Jambo muhimu katika ujamaa wa kisasa ni uwezo mkubwa wa kupanga mipango ya maendeleo ya jamii kwa pamoja na kwa njia ya kisasa ili kuleta maendeleo ya haraka. Vile vile wajamaa popote katika dunia hujitambua kama ndugu; na muda wote hushirikiana katika mapambano ya kupinga na kutokomeza ubeberu, na aina zote za unyonyaji: ubepari, ukabaila, ubwenyenye, ukupe, uzurulaji, ujambazi na kadhalika, ili kuleta

maendeleo ya haraka ya umma wa wafanyakazi na wakulima. Kwa ufupi, wajamaa wote huupiga vita unyonyaji, ubeberu na ukoloni wa aina zote.

Katika Afrika kulikuwa na jamii za aina mbili. Jamii zenye mfumo wa kijima na jamii zenye mfumo wa kitabaka. Mifumo hiyo ilikuwa ni matokeo ya mipango ya kiuchumi ya jamii. Jamii ambayo mpango wake wa uchumi uliruhusu unyonyaji iliwagawa watu wake katika matabaka ya wanyonyaji na wanaonyonywa.

Watawala na wataalam kama vile: 'waganga', wahunzi, 'wapazi'*, yaani, wahubiri dini, na mabingwa wa uwindaji na uvuvi ndio hasa waliounda tabaka la waheshimiwa na hatimaye kuwa wanyonyaji. Watawala walitokana na koo zenye hali njema ya kiuchumi. Hali hiyo njema au utajiri wa koo hizo mara nyingi, mbali ya utaalam, ulitokana na dhuluma ya kunyonya jasho la umma; umma ambao, kwa kadiri kikundi cha wanyonyaji kilivyoendelea kutajirika, ulizidi kudhoofika kiuchumi, kiutu, kisiasa na hasa kifikara. Ili kulinda maslahi yake tabaka la wanyonyaji lilijenga mazingara ambayo yaliweza kuukandamiza umma kiasi umma usiweze hata kufurukuta na kujimudu wakati wote ulipokandamizwa. Kwanza kabisa, tabaka la wanyonyaji, ambalo ni tabaka la wachache, lilihakikisha kuwa serikali ilikuwa ni ya wachache tu ambao ni matajiri. Pili, kwa kutumia chombo hicho muhimu, yaani, serikali, tabaka la wanyonyaji lilijitungia sheria (isiyoandikwa) kuwa mali yote ya asili ilikuwa ni mali ya kiongozi mmoja ambaye kwanza kabisa tabaka lilimtambua. Huyo tutamwita kabaila mkuu – na ambaye kwa maneno mengine ameitwa mfalme katika maandishi ya wengi. Na mali ya asili tunayoizungumzia ni ardhi na vitu vingine vyote vilivyomo ndani yake – maji, misitu, madini na kadhalika.

Ni dhahiri kuwa kabaila mkuu asingeweza kuimudu ardhi yote. Alilazimika kuigawa miongoni mwa makabaila wa chini yake ambao walipaswa wajibu maalum kwa kabaila mkuu. Katika jamii nyingi kuendelea kwa makabaila hao katika nafasi zao za madaraka na uongozi wa kitawala kulitegemea sana jinsi walivyotekeleza wajibu wao kwa kabaila mkuu. Walipaswa kuwa waaminifu, kutoa kodi au ushuru kwa kabaila mkuu, na wajibu mwingine mkubwa ni kuweka majeshi yaliyoitwa militia (milisha) ambayo kazi yake muhimu ni kulinda mpango mzima wa ukabaila dhidi ya mapinduzi ya umma wa wanaonyonywa

*Wapazi – ni neno lililotumiwa na watu wa mwambao kuelezea wahubiri wa dini za jadi.

pamoja na mashambulio ya maadui wa nje. Milisha pia ilikuwa na wajibu wa kuvamia na kuteka nchi nyingine kwa shabaha ya kupanua milki ya kabaila mkuu. Kwa sababu hii TANU imependekeza kuanzisha 'ulinzi wa mgambo' badala ya milisha ambayo kihistoria ilitumika kulinda maslahi ya wakubwa. Hivyo, basi, ni yumkini kuwa tawala zilizojengwa na jamii za mfumo wa kitabaka zilielekea kuwa kubwa; na mamlaka yote hutoka katika ofisi ya kati, ofisi ya kabaila mkuu, ikishauriana na baadhi ya makabaila alioweza kuwaamini na kuwategemea. Hiyo ilikuwa taasisi ya utawala wa urasimu wa hali ya juu sana.

Tatu, kuufanikisha mpango huo wa uchumi wa jamii kabaila mkuu na wenzake wakajipa haki za pekee za kitawala. Hii ina maana kuwa hata kama watoto wa mtawala hawakuwa na sifa zifaazo kwa uongozi ilibidi warithi viti vya wazazi wao. Kinyume chake ni kuwa umma wa wananchi uligeuzwa watumwa ambao kazi yao muhimu ni kulima mashamba ya mabwana na makabaila na kutozwa ushuru mkubwa sana kwa njia ya mavuno; na pengine kupangiwa muda maalum wa kulima mashamba ya makabaila. Kisiasa, hata kama mmoja wa tabaka la umma angekuwa na sifa zinazohitajika kwa uongozi, asingeweza kuteuliwa maana madaraka na vyeo vilikuwa ni haki ya pekee ya tabaka la wanyonyaji, yaani, mabwana na makabaila.

Jamii nyingi za Kiafronodi zilikuwa za kijima kabla ya ukoloni. Hapakuwa na matabaka katika jamii za aina hii bali tabaka moja tu la watu waliosawa. Mtu yeyote ambaye alikuwa na uwezo pamoja na sifa muhimu za uongozi aliweza kuchaguliwa na umma kuwa kiongozi. Kudumu kwake katika madaraka au urithi wa madaraka ya uongozi ulitegemea jinsi kiongozi na wanae walivyoweza kuwaridhisha wananchi. Umma ndio uliokuwa na uwezo wa kujadili na kuamua kama mtoto wa kiongozi wao arithishwe mamlaka ya uongozi ama sivyo.

Ardhi, na pengine hata mifugo, ilimilikiwa kijima, yaani, kiukoo. Mkubwa wa ukoo au 'mtemi' wa jamii alikuwa ni mdhamini wa mali ya umma, ambayo pia ilitumika kwa manufaa ya umma. Msingi mkuu wa mfungamano wa wananchi katika jamii za kijima ni 'upendo wa kidugu', usawa na heshima. Na upendo ndio uliowafanya washirikiane katika shughuli zote za kiuchumi, kiufundi, kitamaduni na kiulinzi.

Hapakuwa na haja ya kuwa na majeshi ya kudumu ya aina ya milisha. Badala yake jamii nzima ilijiona ina wajibu wa kulinda na kupigania nchi yake kila la 'mgambo' lilipopigwa. Hivyo,

milki za jamii za kijima zilikuwa ndogo ndogo kwa eneo; na shughuli kubwa ya viongozi, yaani, watemi ilikuwa ni kuleta usuluhishi kila kutoeleana kulipotokea miongoni mwa wanajamii.

Lakini jamii nyingi za kijima zilianza kuunganika na kuimarisha umoja na tawala zake katika karne ya 19 kwa kujenga 'tawala za kijeshi', mpango ambao ulianzishwa na Dingiswayo wa jamii ya Watetwa wa huko Afrika kusini na baadaye kuendelezwa zaidi na Chaka, Mtemi wa Wazulu. Tawala hizo za kijeshi zilikuwa za kimapinduzi sana. Kwanza, zilishikilia suala la usawa wa kiutu na haki sawa kwa wote. Kiuchumi mali ilimilikiwa kwa pamoja na kiongozi ndiye aliyekuwa mdhamini wa mali yote ya umma ijapokuwa pengine ilitokea kuwa baadhi ya viongozi walionekana wakatili katika kutoa adhabu kwa wahalifu; hasa kwa makosa ya utovu wa uaminifu na nidhamu.

Kwa kuwa jamii hizo za kijeshi mara nyingi ziliishi kwa kuvamia jamii nyingine na kunyang'anya mali na chakula zililazimika kuwafanya wananchi wote kuwa ni askari wa kudumu kwa kipindi maalum. Kwa upande mmoja jamii za kijima ambazo zilijenga tawala za kijeshi zilidumisha na kuendeleza ujamaa wa asili hadi kufikia kiwango cha juu sana. Watu walijumulisha juhudi zao kwa manufaa ya wote. Ubinafsi na unyonyaji wa aina yote ulikuwa ni mwiko na marufuku. Lakini jamii haikuweza kulikabili suala la kupanga mipango ya maendeleo na kufanya ujamaa wao uwe na maana zaidi. Kwa maneno mengine, mpango huu ulifikia mahali ambapo haukuweza kuendeleza zaidi mapinduzi ya jamii. Hata hivyo, mwandishi anatoa kauli hiyo kwa wasiwasi maana kama wangepewa nafasi ya kutosha, yaani, kutoingiliwa na wakoloni huenda katika utulivu wangeweza kufanya maendeleo zaidi ya kiuchumi; kutokana na mwendelezo wa maarifa ya kisayansi, utaalam wa kitekinologia na kadhalika.

Sura ya 9

BIASHARA YA WATUMWA NA MAENDELEO YA WAAFRONODI

Kwa miaka mingi waandishi na walimu wa historia wamezungumza juu ya biashara ya watumwa. Jambo ambalo wanahistoria wameshindwa kujadili ni juu ya uhalali wa matumizi ya kifungu cha maneno: 'Biashara ya watumwa'. Ili ipate kueleweka vema hapana budi kwanza kutolewa maelezo ya msingi kuhusu maana ya kifungu hicho cha maneno. Awali ya yote wasomaji watapenda kufahamu maana ya biashara. Kinadharia biashara huonekana iwapo mambo matatu muhimu yakiwepo. Kwanza kabisa, katika kila biashara hapana budi kuwepo bidhaa. Kwa kawaida bidhaa huwa ni mali kama vile: madini, vipusa, pamba, mkonge, chai, mbao na kadhalika; ikiwa pamoja na mali iliyotengenezwa viwandani kama vile: vyombo vya mawasiliano, mavazi na vyakula vya makopo na kadhalika.

Pili, kuna suala la wauzaji na wanunuzi. Hii ina maana kuwa baadhi ya watu au jamii zitakuwa na baadhi ya mali hizo zilizotajwa hapo juu. Tatu kwa sababu si kila mtu au taifa laweza kujitosheleza kwa kila kitu suala la watu au mataifa kubadilishana mali kwa kukadiriana thamani huwa muhimu sana. Hivyo, basi, kubadilishana kwa mali, ambayo tunaiita bidhaa baina ya wauzaji na wanunuzi, ndiko kunakounda utaratibu wa biashara.

Biashara yaweza kuwa ya mali kwa mali. Kwa mfano, jamii nyingi katika dunia, na kwa miaka mingi ya historia ya mtu, ziliendesha biashara ya mali kwa mali. Fedha imeanza kutumika kama kitu cha kukadiria thamani ya mali katika biashara tangu karne chache zilizopita. Fedha, kwa maneno mengine, sicho kitu kinachosababisha kuwepo kwa biashara bali husaidia kurahisisha suala la biashara kati ya watu au mataifa. Hata hivyo, katika sehemu nyingi za Tanzania, kwa mfano, biashara ya mali kwa mali bado inaendeshwa mpaka wakati huu.

Je, udhalimu wa kuwachukua Waafronodi na kuwatumikisha katika nchi za kigeni ulikuwa ni biashara? Ukweli ni kuwa

udhalimu huo ulikuwa ni biashara kwa maana kamili ya neno biashara. Katika shughuli nzima kulikuwa na mambo yale muhimu, yaani, bidhaa, wauzaji, wanunuzi na kubadilishana kwa mali au bidhaa kwa thamani maalum.

Katika biashara ya watumwa Waafronodi, kutokana na tabaka la wanyonge, ndio waliogeuzwa kuwa bidhaa. Watumwa hao waliuzwa na watu wa tabaka la wanyonyaji la Waafronodi na wanunuzi walikuwa ni watu wa tabaka la wanyonyaji wa Kisanodi (wa asili ya Kiarabu) na Kiyuronodi. Hii ina maana kuwa si sahihi sana kuwa Waafronodi kama taifa au Waarabu na Wayuronodi kama mataifa walishiriki katika biashara hii ya udhalimu. Huko Ulaya na Uarabuni kulikuwa na watu ambao waliunda tabaka la wanyonge. Hao pia walidhulumiwa na makabaila wa kwao kama ndugu zetu Waafronodi walivyopata kudhulumiwa na tabaka la wanyonyaji kwa kuwauza utumwani. Hata hivyo, baada ya kuwauza na kuwatumikisha Waafronodi, Wayuronodi na Wasanodi (Waarabu) walipatwa na fikara ya ukubwa juu ya Mwafronodi kama mataifa.

Tabaka la wanyonyaji katika jamii mbali mbali za watu liliundwa na watu ambao walikuwa na hali njema ya kiuchumi. Kwa sababu ya utajiri wao vikundi hivyo vya wachache katika jamii za watu ndivyo vilivyoweza kustahili heshima ya kiutu. Hao walikuwa, miongoni mwa wengi: watawala na wataalam kama vile: wahunzi, waganga, pamoja na mafundi wa ujuzi mbali mbali. Vile vile walijumuika katika kundi hilo mabingwa wa uwindaji, uvuvi, michezo muziki na ngoma; na kadhalika.

Baada ya kuchuma na kulimbikiza mali kwa muda mrefu kundi hilo la watu wachache lilianza kukuza tabia na tamaa za kunyonya umma kwa madhumuni ya kujitajirisha lenyewe zaidi na zaidi. Hivyo, basi, ili kikundi hicho kipate kujitajirisha zaidi na zaidi ilibidi kwanza kibuni siasa ya kukandamiza umma wa walio wengi na kuwafanya watumwa, yaani, punda wa kuzalisha mali.

Biashara ya watumwa ilipata kuendeshwa kwa kame nyingi sana miongoni mwa jamii mbali mbali. Lakini biashara inayozungumziwa katika sura hii ni ile ambayo ilianzishwa na kustawishwa na tabaka la wanyonyaji wa Kiyuronodi na kuwahusisha wanyonyaji wa Kisanodi (Waarabu) na Kiafronodi. Ilikuwa ni rahisi kuyahusisha matabaka hayo kwa kuwa wanyonyaji wote katika dunia hutambuana, huzungumza lugha moja na hushirikiana katika vitendo vyote vya udhalimu.

Katika Afrika Magharibi 'biashara ya watumwa', kwa maana iliyotolewa hapo juu, ilianzishwa na kustawishwa na wanyonyaji

wa Kiyuronodi na Kiafronodi mnamo karne ya kumi na tano. Wayuronodi waliohusika kwanza walikuwa ni Wareno ambao ndio walikuwa Wayuronodi wa kwanza kufika Afrika Magharibi kama wapelelezi. Watumwa wa mwanzo walikuwa wachache sana nao walisafirishwa na kutumikishwa huko Ulaya kama watumishi wa ndani. Lakini biashara ambayo tunaiongelea katika somo hili ni ile iliyoanzishwa na kuendeshwa na Wayuronodi kuanzia karne ya kumi na sita.

Hii ilikuwa ni mara tu baada ya Wayuronodi kuigundua Marekani na visiwa vyake mnamo mwaka 1492. Ardhi ya Marekani na visiwa vyake iliwavutia sana makabaila na mabeberu wa Ulaya kwa rutuba na utajiri wa madini. Bila kupoteza muda wakaanza kuligawanya bara hilo katika makoloni, mgawanyo ambao hapo awali ulisimamiwa na Papa wa Roma kama kiongozi wa dunia ya Wakristo wa madhehebu ya Kikatoliki. Maelfu na maelfu ya makabaila na mabeberu wa Kiyuronodi wakaanza kumiminika huko Marekani. Shughuli yao ya kwanza ni kunyang'anya madaraka ya kitawala na ardhi kutoka kwa Wamarinodi ambao ni wenyeji wa asili wa huko. Pia kulifanyika jaribio la kutaka kuteketeza kizazi chote cha wenyeji hao, yaani, Wamarinodi. Jaribio hilo halikufanikiwa! Majaribio mengine kama hili yalipata pia kufanyika huko Afrika ya Kusini miongoni mwa Wakalahari na pia miongoni mwa Waastranodi na Wamorinodi wa huko Australia na Nyuzilandi. Mahali pengine kama vile Marekani na Australia jaribio hilo la mauaji lilifanikiwa zaidi. Na ndiyo maana wenyeji wa asili wa nchi hizo ni wachache sana leo ukilinganisha na idadi ya walowezi wa Kiyuronodi.

Makabaila hao walikabiliwa na suala la kupata vibarua wa kuwazalishia mali katika mashamba yao na katika shughuli za uchimbuzi wa madini hasa katika Marekani ya Kati. Watu wa kwanza kuvamiwa na kutumikishwa walikuwa Wamarinodi wakijumuika na makundi ya wanyonge wa Kiyuronodi. Wanyonge wa Kiyuronodi ni miongoni mwa watu ambao, kwa sababu ya kupigania haki zao za kiutu, walionekana machoni pa wakubwa ni wahalifu na adhabu yao kufukuzwa nchini na kutumikishwa huko Marekani.

Jambo la kukumbuka ni kuwa utumwa wa jamaa hao wa Kiyuronodi ulitofautiana na utumwa wa ndugu zetu wa Kiafronodi. Mwafronodi aliyeingizwa utumwani alibaki mtumwa yeye mwenyewe na vizazi vyake vyote. Utumwa wa Wayuronodi ulikuwa wa mkataba. Watoto wa Myuronodi

aliyetiwa utumwani walibaki kama watu huru.

Kwa maelezo ya wadhalimu wa kikoloni Wamarinodi hawakuwa na afya na nguvu ya kutosha ya kuzalisha mali kwa wingi. Kwa upande mwingine, watumwa wa Kiyuronodi hawakuweza kutosheleza mahitaji ya mabeberu na makabaila wa Kiyuronodi huko Marekani. Sababu iliyotolewa ni kuwa hali ya hewa ya joto haikuwafaa watu wa Ulaya. Dai hilo ni la kipuuzi kwa sababu Wayuronodi wengi leo wanastawi katika sehemu nyingi za joto bila ya hali hiyo kubadilika. Marekani yenyewe leo ni nchi ya watu weupe na watu wa asili ya Kiafronodi. Wamarekani wenye asili ya Kiafronodi, ambao babu zao ndio waliijenga Marekani, hubaguliwa na hata kupendelea wahame kutoka huko. Ubaguzi huo hufanywa na Marekani wenye asili ya Kiyuronodi ambao ndio wanaunda na kuendesha serikali ya Marekani na kumiliki mali yote.

Ni kweli tupu kwamba Afrika ilikuwa na majitu yenye nguvu na akili safi, afya bora na uwezo mkubwa. Wanyonyaji hao wa Kiyuronodi waliohamia Marekani wakaanza kuikodolea macho Afrika na watu wake. Walipofika Afrika waliwakuta jamaa ambao waliweza kuzungumza nao lugha moja, lugha ya kidhalimu. Hao walikuwa ni tabaka la wanyonyaji wa Kiafronodi.

Bila kufikiria matokeo ya siku za mbele wanyonyaji wa Kiafronodi, kwa sababu ya tamaa za kunyonya, wakakubali na kupendelea shauri la kuwauza wana-Afronodi utumwani. Hivyo, basi, mikiki mikiki ya kuwapata watu wa kuuzwa utumwani ikaanza. Wachuuzi wa Kiyuronodi mara nyingi walingoja na meli zao katika bandari zao. Mara nyingi pia walithubutu kuingia ndani sehemu za bara na kuwavamia wananchi. Wareno, miongoni mwa Wayuronodi, walihusika sana katika Zaire, Kongo na Angola. Baadhi ya Waafronodi walijiingiza kama wachuuzi wa kati. Hao ndio walioingia sehemu za bara na kuwanunua watumwa na kuwaleta pwani ambako wachuuzi wa Kiyuronodi waliwangojea na meli zao.

Jambo muhimu la kuzingatia ni kuwa biashara ya watumwa iliyoendeshwa huko Afrika ya Magharibi ilikuwa ni kati ya tabaka la wanyonyaji wa Kiafronodi na Kiyuronodi. Waarabu hawakuhusika na biashara hiyo ya Afrika Magharibi. Wareno waliokuwa katika mstari wa mbele baadaye walifuatiwa na wadhalimu wa mataifa mengine ya Ulaya.

Mara nyingi Wayuronodi walikuja na nguo kutoka Bara hindi na bunduki ambazo waliuziwa na kuzawadishwa baadhi ya watemi ili kuchochea vita baina ya jamii kwa shabaha ya

kuwapata mateka wa vita ambao waliuzwa utumwani. Biashara hiyo ya kidhalimu ilidumishwa huko Afrika Magharibi kwa muda usiopungua karne nne. Ilianza mnamo karne ya kumi na sita na kumalizika mnamo karne ya kumi na tisa. Watumwa wa kutoka Afrika Magharibi walisafirishwa katika makoloni ya huko Marekani, visiwa vya Pasifiki na vya Karibiani.

Makaburu walipandwa katika koloni la Rasi, ambalo leo ni Jimbo la Rasi, katika Afrika Kusini na Kampuni la Waholanzi la huko India mnamo mwaka 1652. Kaburu hao walitakiwa wafanye kazi wenyewe kama wakulima na wafugaji ili kuipatia misafara ya Kiholanzi, ikiwa njiani kwenda au kurudi kutoka India na Mashariki ya Mbali – nyama, mboga na vyakula vingine. Lakini, kwa kuwa wahubiri Biblia na wanahistoria wakikoloni waliwafundisha Kaburu nadharia ya kuwa Mwafronodi ni mtu wa chini aliyeumbwa na Mungu ili kumtumikia mtu mweupe, hawakuchelewa kuanza kuwatumikisha Waafronodi hasa wa jamii ya Kihotentoti na baadaye Wabantu kutoka Afrika ya Kati, Magharibi na Mashariki.

Hivyo, basi, ndugu wa Kiafronodi wa Afrika ya Kusini hawakuuzwa katika nchi za ng'ambo bali walinunuliwa kutoka kwa wanyonyaji wa ndani na kutumikishwa, na wanaendelea kutumikishwa, mumo humo nchini mwao. Na ingawa ndugu zetu wa Afrika Kusini hawakupatwa na janga la kuuzwa katika masoko ya dunia janga lililowapata ndugu hao ni kubwa mno. Kwa hali ilivyo na kwa jinsi siasa za akina Vosta wa Afrika Kusini na Smisi wa Zimbabwe zilivyo matumaini ya Waafronodi na wanyonge wengine ya kurudishiwa uhuru wa kikatiba zimeshindikikana. Njia iliyobaki ni ndugu hao kubeba silaha na kupambana na walowezi hao. Hata hivyo, yasikitisha kuona nchi nyingi huru za Kiafrika zinageuka vibaraka wa Makaburu, Smisi na Wareno – kama vile Malawi, Ghana, Ivori Kosti na kadhalika. Nchi hizo, iwapo hazibadili msimamo wao, hazitakuwa tu maadui wa maelfu ya Waafronodi wanaoteswa huko Afrika Kusini na Zimbabwe bali hudhoofisha sana juhudi za Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika ambazo moja ya maazimio yake muhimu ni kulikomboa Bara la Afrika.

Katika Afrika ya Mashariki biashara ya watumwa ilikuzwa na kupanuliwa sana katika karne za kumi na nane na kumi na tisa. Wanyonyaji wa Kireno na Kifaransa wakiwa ni Wayuronodi ndio waliohusika na biashara ya watumwa katika pwani ya Msumbiji na sehemu za bara za Afrika ya Kati kwa muda mrefu kabla ya wanyonyaji wa Kiarabu kujiingiza katika

shughuli hiyo katika sehemu ya Tanzania, Kenya, Uganda na Afrika ya Kati. Wareno waliwatumia machotara kutoka Msumbiji, ambako pia wamisionari wa Kireno waliishi kwa miaka mingi, kama watu wa kati. Wareno wenyewe, kama Wayuronodi wa mataifa mengine, hawakupenyeza sehemu za bara mpaka mnamo karne ya kumi na tisa wakati wa misafara ya upelelezi wa kijografia.

Makabaila wa Kifaransa walianzisha mashamba ya miwa katika visiwa vya Maurisiusi, koloni ambalo baadaye lilichukuliwa na Waingereza mnamo 1810. Wafaransa pia walijinyakulia kisiwa cha Madagaska na kukifanya koloni lao. Huko pia walowezi wa Kifaransa walihamia na kuanzisha kilimo cha miwa. Kama mabeberu na makabaila wa Kiyunorodi huko Marekani, walowezi wa Kiyuronodi katika Maurisiusi na Madagaska walihitaji Waafronodi wa kuwatumikisha. Watumwa hao ilibidi wachukuliwe na kuuzwa huko visiwani kutoka Afrika bara. Wanyonyaji wa Kireno na Kiarabu ndio hasa walikuwa katika mstari wa mbele katika kuvipatia visiwa hivyo watumwa kutoka Msumbiji na Afrika ya Kati. Machotara wa Kireno na Waarabu ndio waliohusika na ununuzi wa watumwa kutoka kwa tabaka la wanyonyaji wa Kiafronodi kama wachuuzi wa kati. Lakini kwa kadiri biashara ya kidhalimu ilivyozidi kustawi tawala nyingi ziliangushwa na watu wake wakaachwa pasipo usalama wakikabiliwa na hatari ya kuvamiwa na kuchukuliwa na wafanya biashara ya watumwa moja kwa moja. Pia ifahamike kuwa baadhi ya watumwa hao kutoka Afrika ya Mashariki walisafirishwa na Wareno katika koloni lao la Brazili. Jambo hilo kwa upande lilisababishwa na kampeni za mabepari wa Kiingereza za kukomesha biashara ya watumwa huko Afrika ya Magharibi kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na nane na kumi na tisa. Sababu ya pili ni upungufu wa watu katika Angola. Koloni la Angola lilikuwa kisima kikuu cha kupatia watumwa kuanzia karne ya kumi na tano.

Makabaila wa Kiarabu walisababisha kupanuliwa kwa biashara ya watumwa katika Afrika Mashariki na ya Kati katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa. Kisa cha kukuza biashara hiyo katika sehemu hii ni kilimo cha karafuu kilichokuzwa na kuendelezwa huko Visiwani Unguja na Pemba. Baadhi ya watumwa walipelekwa Uarabuni ili kuwahudumia makabaila wa huko katika kilimo cha tende na kama watumishi wa ndani. Ili pasitokee machotara huko Uarabuni wanaume wote wa Kiafronodi waliosafirishwa huko kama watumwa walilazimika kwanza

kuhasiwa. Ilipotokea kuwa mwanamke wa Kiafronodi, yaani mtumwa alizaa na 'bwana' ambaye ni Msanodi ilibidi hatua muhimu zichukuliwe kuhakikisha kuwa mtoto aliyezaliwa anafifishwa. Hizo ndizo sababu za kutokuwa na machotara huko Uarabuni kama walivyojitokeza huko Marekani na katika visiwa vya Karibiani.

Tabaka la wanyonyaji, matajiri na wenye tamaa ya kutajirika, wa Kiyao lilijishughulisha sana na biashara ya watumwa katika Tanzania ya kusini, Malawi, Msumbiji na Zimbabwe kama wachuuzi wa Kati. Njia yao Kuu ilianzia Kilwa na kuelekea bara hadi Ziwa Nyasa na hatimaye nchi ya Malawi. Watu wa jamii ya Kimang'anja katika Malawi ndio waliopata taabu sana na kuchukuliwa kwa wingi zaidi. Hii ni kwa sababu ya kubomolewa kwa serikali zao na Wangoni kutoka Afrika ya Kusini chini ya uongozi wa Zwangendaba. Njia nyingine za misafara ya watumwa zilianzia Pangani na Bagamoyo. Zote zilipitia nchi ya Wagogo hadi Tabora. Kutoka Tabora njia moja iliongoza Bukoba na kufikia Buganda hatimaye Wanga katika Kenya ambako biashara iliendeshwa. Njia nyingine kutoka Tabora iliongoza Kigoma hadi Ujiji na kuendelea mpaka nchi ya Wamanyema katika Zaire.

Kabla ya kupanuliwa kwa biashara ya watumwa njia hizo zilitumiwa na wachuuzi wa Kiafronodi ambao waliendesha biashara ya vitu kama pembe za ndovu, vipusa, ngozi za wanyama kama vile chui; pia waliendesha biashara ya chumvi, dhahabu na kadhalika. Miongoni mwa bidhaa za kigeni ni bunduki, baruti, nguo, shanga, bakuli na sahani za kauri na kadhalika. Lakini, baadaye hasa katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa Waarabu nao walianza kupenyeza sehemu za bara wakitumia njia hizo hizo. Huo ulikuwa wakati biashara ya watumwa ilipostawi na kufikia kiwango cha juu sana.

Misafara hiyo haikuweza kupitia katika sehemu za Umasai wala Ukikuyu. Jamii za Kimasai na Kikuyu hazikutaka wala kupendelea uhusiano wo wote na Waarabu. Na hii ni sababu ya kutosha kueleza kwa nini misafara ya Waarabu kwenda Buganda na Kenya magharibi ililazimika kuzikwepa sehemu za jamii hizo kwa kupitia Tabora na Bukoba.

Jambo la maana ni kuwa katika Afrika Mashariki, ambayo tunaizungumzia sasa hivi, jamii tatu za watu zilishiriki. Nazo ni wanyonyaji wa Kiafronodi kama wauzaji, Wayuronodi na Wasanodi kama wanunuzi. Waarabu, si mara nyingi waliwangojea watumwa katika masoko ya pwani kama

Wayuronodi walivyofanya huko Msumbiji na Afrika Magharibi. Bali mara nyingi waliingia sehemu za bara na kuwanunua watumwa na hata pengine kuwavamia wananchi moja kwa moja.

Kadiri biashara ya watumwa ilivyozidi kustawi makabaila wa Kiarabu pia walijipenyeza bara na kuendesha biashara moja kwa moja na tabaka la wanyonyaji wa Kiafronodi. Hata hivyo, kuna jambo moja la kukumbuka. Zao la karafuu lilitakiwa na makabaila na mabepari wa Ulaya. Hivyo, basi, ingawa biashara iliendeshwa na Waarabu chanzo chake ni ubepari wa Ulaya. Kwa maneno mengine, msingi wa biashara ya watumwa katika Afrika Magharibi ulikuwa ni ukabaila na ubepari wa Kiyuronodi katika Ulaya, Marekani na visiwa vyake; na katika Afrika Mashariki ulikuwa ni ubepari wa Kiyuronodi huko Ulaya ambao ulihitaji mazao maalum kutoka Afrika. Lakini, kwa sababu ya hali halisi ya wakati, mazao hayo ilibidi yazalishwe na mabeberu wa baadhi ya jamii za Kiyuronodi na Kiarabu kwa kuwatumikisha Waafronodi kwa mpango wa utumwa katika makoloni yao nje ya Afrika; na kwa kiasi fulani katika visiwa walivyoviteka vilivyomo katika Bahari ya Hindi.

Fikara za kupinga utumwa-mkongwe na biashara ya watumwa zilianzishwa na kusimamiwa na Waingereza kuanzia miaka ya 1770. Hata hivyo, iko haja ya kujiuliza iwapo Waingereza wote, kama taifa, walipinga utumwa na biashara ya watumwa. Pili, hapana budi kutolewa maelezo kuhusu hatua na juhudi za kupinga na kutaka kukomesha utumwa na biashara ya watumwa zilizochukuliwa katika kipindi hicho. Tatu, itabidi wasomaji waelimishwe juu ya sababu za Waingereza kuwa katika mstari wa mbele katika masuala hayo; na sababu zilizofanya mataifa mengine ya Ulaya na Asia kutojiingiza mapema na hata kudiriki kupinga hatua hizo. Na mwisho itapasa tupewe maelezo ya kuridhisha kuonyesha namna wadhalimu wa Kiafronodi walivyojimudu kuhusu uamuzi wa mabeberu wa Kiyuronodi.

Maelezo mengi yametolewa na waandishi wa historia wa kikoloni kuhusu sababu za kupiga vita biashara ya watumwa na utumwa. Sababu kubwa iliyotolewa ni kuwa baadhi ya wakristo wa Ulaya, hasa Uingereza, walianza kuwaonea huruma ya kiutu watumwa wa Kiafronodi. Maelezo hayo ambayo yameonekana kuwa ni ya kusadikika na kuridhisha kwa muda mrefu hayana budi kutazamwa vipya na katika mazingara halisi ya kipindi hicho. Ni dhahiri kwamba kulikuwa daima na watu wenye huruma ya dhati kwa watu ambao waliteswa na kutendewa

kinyama. Ukweli huo unatokana na fikara kwamba hata katika Ulaya kulikuwa na umma wa wanyonge; na kwamba miongoni mwao lazima pawepo kikundi ambacho kitapigania siyo ukombozi wao tu bali hata wa watu wengine ambao hukandamizwa na kudhulumiwa kama wao. Maelezo hayo yana maana kuwa si lazima tabaka la wanyonge katika jamii lione haja ya kujiunga na kuchukua hatua mahususi za kujikomboa kama tabaka. Kujikomboa kwa wanyonge kitabaka kuna maana moja kwamba wanyonge huzinduka na kujiunga pamoja ili kupambana na kulitokomeza tabaka zima la wanyonyaji kwa shabaha ya kujirudishia hadhi ya kiutu na kuleta maendeleo ya jamii kwa ujumla. Lakini ifahamike pia kuwa ingawa siasa ya kunyonya ni ya wachache, wengi miongoni mwa wanaonyonywa huwa na tamaa za ubinafsi; na kwamba kama wangepata nafasi ya kunyonya nao pia wangenyonya kwa kuwatumikisha wengine katika jamii. Kwa hiyo, basi, wanaonyonywa wanaweza tu kujiunga kama tabaka iwapo kama wenyewe watapata mwamko na mzinduko wa juu sana; na iwapo wanajikomboa kutoka unyonyaji wa tamaa, ambao ni unyonyaji wa kimawazo.

Shabaha ya nchi za kibepari ni kujenga na kuendeleza ubepari. Itikadi ya ubepari ni siasa ya wachache ambao ni wanyonyaji na wenye kauli ya mwisho katika taifa. Na kwa kuwa tabaka la umma wa wafanyakazi na wakulima hawajazinduka na kuunganika hugiribika na kufanywa kuwa sehemu ya waumini wa itikadi hiyo. Fikara za sehemu kubwa ya wanaokandamizwa na kunyonywa ni kutaka kupewa nafasi ya kunyonya. Wenye fikara zz kimapinduzi ni wachache sana; na kwa sababu njia zote za mawasiliano humilikiwa na wanyonyaji, wanyonge na wanamapinduzi hawana nafasi wala uwezo mkubwa wa kueneza fikara zao za ukombozi dhidi ya mfumo.

Kwa hiyo, na turudi tena kwenye mazungumzo yetu juu ya chama cha watu wenye huruma huko Uingereza. Watu hao walikuwa wakristo; na fikara ya huruma na utu si fikara ya ucha Mungu tu bali ni fikara halisi ya kimapinduzi kwa maana ni fikara ya ukombozi wa watu wanaodhulumiwa. Kanisa lenyewe huko Uingereza halikuwa limejikomboa; na pengine hata leo linahitaji hatua za kujikomboa ili liweze kuonekana la kimapinduzi katika muundo, mwenendo na mahubiri yake. Haja hii ya kanisa kujikomboa imekwisha onekana katika Marekani ya Kusini na Afrika, hasa katika Tanzania; na kwamba hatua za haraka zimeanza kuchukuliwa na viongozi wanamapinduzi wa Kiafronodi.

Ukabaila katika Uingereza uliendeshwa na watawala na matajiri pamoja na viongozi wa madhehebu. Mnamo 1967 mtungaji alitembelea sehemu moja, ya Uingereza. Sehemu hiyo ilikuwa imemilikiwa na shirika la kimadhehebu; nayo ina eneo kubwa sana la ardhi. Ndani yake kulikuwa na wakulima wengi na wafanyakazi; pia kulikuwa na mashine nyingi za kuendesha shughuli za kilimo na kadhalika. Kwa sababu hata serikali haiwezi kuingilia shughuli za humo ndani baadhi ya magari hayakuwa na namba na hii ilionekana halali na sahihi kwa vile magari hayo hayakutoka nje ya eneo hilo la shirika ambalo ni kubwa sana. Wakulima na wafanyakazi hawakuwa tofauti na watwana wa Kiafronodi chini ya kabaila wa Kiarabu huko Zanzibar kabla ya mapinduzi. Kama kulikuwa na tofauti, basi, tofauti hiyo ilikuwa ya kimizania tu. Mkulima katika eneo hilo la madhehebu la huko Uingereza aliweza kuonekana na hali bora zaidi ya kimaisha; mavazi, malazi na afya bora – kuliko mkulima wa Unguja na Pemba kabla ya mapinduzi. Lakini kuhusu utu na uhusiano wa kiutu na wa kimaisha hapakuwa na tofauti. Shabaha ya maelezo ya mfano huu ni kuthibitisha kwamba kanisa pia huko Uingereza, lilikuwa ni sehemu ya mfumo wa unyonyaji. Kwa hiyo, basi, huenda fikara hiyo ya huruma kwa utu, ambayo kusema kweli msingi wake ni usawa wa watu, ambayo baadhi ya waumini wa kikristo wa huko Uingereza walikuwa nayo haikutokana na kanisa, kama taasisi, bali na waumini wenyewe kama watu binafsi.

Uingereza kati ya miaka 1770 na 1800 ilikuwa imepiga hatua kubwa ya maendeleo ya kisayansi na kitekinologia. Moja ya matokeo makuu ya maendeleo hayo ya kisayansi ni mapinduzi ya viwanda kama ilivyoelezwa hapo juu. Viwanda vilisababisha, kwanza kabisa, mabadiliko katika mpango mzima wa uchumi na maisha ya kijamii katika Uingereza. Lakini mapinduzi hayo yalilazimika kuwa na matokeo mengi mengine katika jamii nyingi duniani – hasa katika Bara la Afrika.

Mabepari, kinyume cha makabaila, walihitaji mafuta ya kulainishia mashine yao. Mafuta hayo ni kutokana na michikichi ambayo iliota kwa wingi huko Afrika Magharibi. Vile vile, mabepari walihitaji mazao ya kilimo na madini kwa ajili ya kuendeshea viwanda vyao. Ardhi ya Marekani na visiwa vyake ilikuwa imechoka na Afrika ilikuwa na uwezo wa kutoa mazao ya kutosha kuweza kutosheleza mahitaji ya mabepari wa Uingereza na Ulaya.

Mabepari hawakupendelea mpango wa zamani wa utumwa

wa kuwatumikisha watu bila ujira angalau wa kudanganyia ingawa katika sehemu nyingine ujira wa kudanganyia ulianza kutolewa. Kwa kuwa ubepari msingi wake mkuu ni mtaji, yaani, pesa bepari alihitaji watu ambao ni maskini lakini wana uwezo mdogo wa kununua bidhaa za viwanda vyake. Na watu hao hawawezi kuwapata kutoka miongoni mwa watumwa wa aina ya kwanza, yaani, utumwa-mkongwe. Ilibidi bepari abuni mpango mpya wa uchumi na siasa ili kuendeleza mpango wake wa unyonyaji. Na siasa aliyobuni ni siasa ya ubeberu; na mpango ni ukoloni. Kwa ufupi, mabeberu na mabepari walianza kutafuta makoloni katika Afrika na sehemu nyingine. Ili kuzipata au kuziteka nchi za Kiafrika mabeberu walitumia mbinu na hila mbali mbali kama ilivyoelezwa katika sura ya kumi.

Kila walipofanikiwa kuivamia nchi mabeberu waliifanya nchi hiyo kuwa koloni. Walileta utawala wa kigeni. Wananchi wote kwa ujumla walipoteza uhuru na haki zote za asili. Ardhi na mali yote ya asili zilifanywa mali ya serikali na wafalme wa nchi ambako mabeberu walitoka. 'Majeshi', ambayo kwa wananchi yalikuwa ni kitu cha kigeni, yakawekwa. Shabaha ni kuwakandamiza na kuwatia hofu na msukosuko wananchi ili kurahisisha suala zima la unyonyaji. Wananchi ambao baadhi yao walishawishiwa na kushawishika kuhamia katika makoloni kama walowezi; baada ya kuchuma au kunyonya sana hustaafu na baadhi yao hurudi tena makwao kama mabwana mkubwa, waheshimiwa na mabepari wakubwa.

Shabaha ya mjadala huu ni kuonyesha kuwa utumwa-mkongwe na biashara ya watumwa havikukomeshwa na wanyonge wacha Mungu wa Ulaya kwa sababu ya huruma yao ya kiutu ambayo, kama ilivyoelezwa hapo juu, vigumu kuthibitisha. Vile vile ni vigumu kuamini kuwa waumini hao bila hata msaada wa Kanisa au nguvu nyingine wangeweza kufanikisha azimio lao la kukomesha utumwa na biashara ya watumwa.

Ikumbukwe pia kuwa hicho kilikuwa ni kipindi cha mapinduzi ya viwanda. Wananchi wengi wa Ulaya waliajiriwa viwandani huko huko Ulaya na kutumikishwa kinyama. Yasemekana walilazimika kufanya kazi kwa masaa kumi na nane. Watoto na wake wa wafanyakazi walilazimika kujiunga kama wafanyakazi kwa sababu ya kima cha chini mno cha ujira. Waliishi katika matembe mabaya kwa afya ya mtu chini ya ardhi. Hali yao kwa ujumla ilikuwa mbaya sana. Hivyo, kama juhudi za Waingereza zilikuwa na msingi wa uchaji, basi, pengine waumini hao

wangetazamiwa kwanza kutetea hali njema yao wenyewe na ya jamii zao ambao waliteswa, kukandamizwa na kunyonywa bila kifani na makabaila na mabepari wa nchi yao. Lakini kwa bahati mbaya hatua ya kimapinduzi kama hiyo haikupata kuchukuliwa. Vile vile, wakati wa biashara ya watumwa baadhi ya wamisionari wa kikristo, hasa huko Afrika Magharibi, walishiriki sawa na mabeberu wengine. Mnamo karne ya kumi na tisa wamisionari hao hao wa kikristo walifanya kazi kubwa sana ya kuliingiza Bara la Afrika katika ukoloni wa Kiyuronodi.

Kwa ufupi, suala la kukomesha utumwa-mkongwe na biashara ya watumwa lilikuwa ni suala la kiuchumi na wala si suala la uchaji wa Kimungu na wala si kitendo cha huruma kwa utu. Nyuma ya shughuli nzima alikuwa bepari ndiye aliyeifanikisha shughuli nzima ya kukomesha utumwa-mkongwe na biashara ya watumwa kwa sababu zilizotolewa hapo juu. Kwa upande mwingine wanyonyaji wa mataifa mengine kama: Wareno, Waarabu, katika Afrika Mashariki, na Waafronodi hawakupendelea sana kuunga mkono fikara ya kukomesha utumwa na biashara ya watumwa. Hivi si kwa sababu wao walikuwa na moyo wa ukatili na wa kinyama zaidi kuliko kikundi cha wenye huruma wa huko Uingereza. Bali upinzani wao unadhihirisha zaidi kuwa ubepari ndio uliokuwa sababu kubwa ya kupigania kukomeshwa kwa utumwa-mkongwe na biashara ya watumwa. Wanyonyaji wa Kireno, Kiafronodi na Kiarabu hawakuwa na viwanda ambavyo vingewafanya wawe na msimamo mmoja na mabepari wa Ulaya mnamo karne ya kumi na tisa. Uchumi wao ulitegemea sana biashara ya watumwa na utumwa-mkongwe katika kuzalisha mali.

Je, utumwa ulikomeshwa? Kwa fikara za mwandishi utumwa, kama mpango wa uchumi na maisha ya kijamii, haukukomeshwa bali ulibadili umbile au mfumo pamoja na mbinu. Katika Afrika wananchi, wote, chini ya mpango wa ukoloni, waligeuzwa watumwa wa ujira wa udanganyifu. Pamoja na umma wa wakulima na wafanyakazi wa huko Ulaya wananchi katika makoloni, wote kwa ujumla, waliendelea kukandamizwa, kunyanyaswa, kudharauliwa na kudhulumiwa haki zao na kunyonywa japokuwa kwa vilele tofauti. Kwa ufupi, moja kwa moja Waafronodi, kwa ujumla wao, waliingizwa katika utumwa wa hali ya juu sana. Ili kuhakikisha kuwa wananchi wanalazimika kuzalisha mali kwa mpango wa manamba au kwa mpango wa mtu binafsi, kama mkulima wa mazao ya biashara, wakoloni na serikali zao wakabuni mbinu ambayo iliwasaidia

sana kuwapata 'watumwa wa ujira'. Mbinu hii ilikuwa ni kodi ya kichwa ambayo wananchi walipaswa kulipa kwa pesa taslimu. Kodi haikuwa na shabaha ya kuwaletea kipato wakoloni bali kuwapatia 'watumwa', ambao tutawaita vibarua, na kutumikishwa katika shughuli zao mbali mbali za uchumi. Na kwa sababu ya kuwanyonya sana wananchi wa Afrika, mabepari waliweza kuendeleza nchi zao na kuinua hali ya maisha, kwa ujumla, ya wafanyakazi wao huko Ulaya. Kwa ufupi, ni dhahiri kuwa ukoloni ni mpango wa kielevu zaidi wa utumwa uliopata kubuniwa na mabepari kuchukua nafasi ya utumwa-mkongwe ambao uliimarisha biashara ya watumwa katika karne ya kumi na tisa. Na kwa kuwa kulikuwa na tabaka la wanyonyaji, yaani, wakoloni na wanaonyonywa ambao ni wananchi kwa ujumla; ukoloni kama mpango wa uchumi ulijenga mfumo wa kitabaka katika maisha ya jamii katika makoloni.

Afrika tangu zamani za kale ni nchi tajiri. Watu wake walikuwa wenye afya na nguvu. Lakini biashara ya watumwa iliiletea Afrika maafa mengi. Ikawahamisha Waafronodi vijana, wenye akili, afya bora na wenye nguvu za kufanya kazi na kuwapeleka katika nchi za kigeni. Huko walitumikishwa kama vyombo vya kuzalisha mali. Ni dhahiri kuwa wana Afronodi hao watumwa walijenga misingi ya maendeleo ya kiuchumi na kitamaduni katika Bara la Marekani, Ulaya na Uarabuni.

Kwa upande mwingine, Afrika ikaachwa inakabiliwa na suala la upungufu wa watu wenye afya bora, nguvu ya kuzalisha mali, na wenye akili timamu ya kufikiri mipango mipya ya maendeleo. Upungufu huo wa watu ndio uliokuwa sababu kubwa ya kuzorota kwa maendeleo ya Wafronodi kwa ujumla. Kama ilivyoelezwa hapo juu kuwa ni watu wenye afya, nguvu, uwezo na akili tu ndio waliochukuliwa ni wazi kwamba walioachwa ni wazee ambao ni dhaifu kwa kila hali. Hivyo, basi, maendeleo ya kwanza kuzoroteshwa yalihusu kuzaliana na kuongezeka kwa Waafronodi kama ilivyoonyeshwa hapa chini.*

—	1650	1750	1850	1900
Afrika	100	100	100	100
Ulaya	103	144	274	423
Asia	257	437	656	857

Hesabu hizi zinatuonyesha kuwa wakati watu wa mabara mengine wakiongezeka kwa idadi Waafronodi kwa muda wa

* W. Rodney, *How Europe Underdeveloped Africa*, Dar es Salaam, Uk. 106

miaka 300 hawakuweza kuongezeka. Idadi yao libaki pale pale. Na wale ambao walibakizwa kuendeleza kizazi cha Waafronodi walikuwa ni wazawa wa wazee na watu dhaifu. Hii ina maana kwamba maendeleo ya kimapinduzi katika sehemu zote za maisha yasingewezekana katika Afrika. Hasa ikikumbukwa kuwa maendeleo ya haraka huletwa na wingi wa watu wanapojumlisha juhudi zao. Mtu mmoja mmoja hawezi kuleta maendeleo ya kimapinduzi. Na hii pengine ni sababu ya kutosha kutoendelea kwa sehemu nyingi za Afrika na hasa katika sehemu ya Tanzania ya Kusini ambako karibu theluthi moja ya wananchi walikufa wakati wa Vita vya Maji-Maji vya 1905 - 1907. Wengi walikufa katika mapambano na Wajerumani lakini wengi zaidi walikufa kwa njaa, kuliwa na wanyama wakali na maradhi, Wajerumani walichoma moto mashamba, ghala za chakula, nyumba, na misitu. Pamoja na hayo yote, wananchi hawakuweza kulima kwa sababu ya misukosuko ya vita na ukosefu wa mbegu.

Biashara ya watumwa imeendeshwa kwa muda wa miaka zaidi ya 400. Waafronodi ndio waliofanywa bidhaa na kuuzwa utumwani. Matabaka ya wanyonyaji wa Kiafronodi na mabeberu wa Kiyuronodi na Kisanodi (Waarabu) ndio waliohusika katika kuwauza, kuwanunua na kuwatumikisha Waafronodi wanyonge. Lakini kwa sababu ni wanyonge wa Kiafronodi tu walifanywa bidhaa ni dhahiri kwamba hadhi ya Waafronodi, kama taifa, ilishuka. Wasanodi na Wayuronodi wakawaeleza Waafronodi, kwa makusudi mazima, katika mazungumzo ya mdomo na katika maandishi kuwa walikuwa ni nusu watu na nusu wanyama. Kiutu hawakuwa sawa na watu wa mataifa mengine katika dunia ambao wana asili ya Kisanodi na Kiyuronodi. Shabaha ya mafundisho ya fikara na imani zisizo na msingi kama hizo ilikuwa ni kuhalalisha mpango wa 'utumwa' (ukoloni) na ubaguzi wa rangi.

Utumwa huu unaozungumziwa hapa ni tofauti na utumwa wa jadi ulioendeshwa katika kila jamii na wanajamii wenyewe. Utumwa unaojadiliwa katika sura hii ni utumwa ambao ni wa hali ya juu kabisa. Utumwa huu, ingawa fikara za aina hiyo hazikuwepo hapo awali, uliwafanya Waafronodi wote, kama taifa na kwa sababu ya rangi yao nyeusi, kuwa ni watumwa kimwili na kifikara wa mataifa yote ya Kisanodi na Kiyuronodi. Utumwa huu ulikuwa ni mbaya kuliko aina zote za utumwa katika dunia hii.

Kifikara wakoloni walifundisha kuwa Waafronodi hawakuwa

na uwezo wa kufanya jambo lolote la maana pasipo msaada ama wa Msanodi au Myuronodi. Matokeo yake ni kuwa Mwafronodi aligiribika na kusahau kuwa alikuwa amepiga hatua kubwa sana za maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kitamaduni na kitekinologia kwa siku za nyuma bila ya msaada wa Msanodi au Myuronodi. Kwa sababu ya kasumba waliyowapika Waafronodi katika kipindi cha ukoloni, mabeberu wa Kiyuronodi na Kiarabu walifanikiwa sana kumteka Mwafronodi kifikara na kitamaduni. Walimfanya aamini kuwa yeye hakuwa na uwezo kama wao na kwa sababu hiyo asingeweza kujitegemea. Imani hii ni ya hatari sana na kusema kweli haina msingi wo wote wa kiakili. Wasanodi na Wayuronodi walipofika mara ya kwanza Afrika walishuhudia maendeleo ya wanaAfronodi. Wakastajabia na kuvutiwa na utamaduni na tawala za Waafronodi na kutoa heshima ya kiitifaki kwa watemi wake, kama vile, akina Manikongo wa huko Afrika Magharibi. Kwa mfano, Mfalme wa Ureno na Mtemi Manikongo wa Afrika Magharibi waliwekeana mabalozi, wakabadilishana wataalam na utamaduni. Biashara ya halali ya vitu ikaanzishwa na kustawishwa baina ya Wayuronodi, Wasanodi na wananchi. Na zaidi ya yote wakaheshimiana kama watu sawa na kwamba hatua kali zilichukuliwa na watemi wetu kila wageni hao wa Kisanodi na Kiyuronodi walipojaribu kuingilia mambo yao ya ndani. Lakini kwa sababu ya janga hilo la biashara ya watumwa wana-Afronodi wote, kama taifa, wakashushiwa hadhi yao.

Tokeo la tatu ni hatua zilizochukuliwa na mabepari wa Uingereza kuingiza ubeberu na ukoloni-mkongwe katika Bara la Afrika. Ukoloni ulikuwa ni mpango wa mabepari - pamoja na wote wenye fikara na tamaa za kunyonya.

Matajiri na wanyonyaji wa Kiingereza ndio walioanzisha 'Chama cha Upelelezi wa Sehemu za bara la Afrika' mwishoni mwa karne ya kumi na nane. Licha ya kuanzisha chama hicho, mabepari ndio waliokuwa na uwezo na wajibu wa kugharamia misafara yote ya upelelezi. Shabaha ikiwa kutafuta aina mbali mbali za utajiri: madini, mazao ya kilimo, misitu na kadhalika. Ni kweli kuwa shughuli nzima ilikuwa ni mpango rasmi na wala haikuwa tukio la bahati nasibu. Lengo lilikuwa ni kubadilisha utumwa-mkongwe na biashara ya watumwa na mpango rasmi wa uchumi wa jamii uliojulikana kama ukoloni. Na ndio maana suala la upelelezi linaanza wakati mmoja na kampeni za kukomesha biashara ya watumwa. Misafara ya upelelezi ichukuliwe kama ni hatua za awali za ukoloni. Na kusema kweli

shughuli za upelelezi ziliimarishwa sana na mabepari kati ya miaka 1800 na 1870. Mara tu baada ya shughuli za upelelezi kukamilika mabepari wa Ulaya wakaanza kulivamia Bara la Afrika na hatimaye kuligawanya katika kikao rasmi cha 1884, kikao kijulikanacho kama Mkutano wa Belini.

Sura ya 10

UBEPARI NI CHANZO CHA UBEBERU, UKOLONI NA MGAWANYO WA AFRIKA

Ukoloni kama mpango wa uchumi na maisha ya jamii una uhusiano mkubwa sana na ubepari ulioletwa na mapinduzi ya sayansi na viwanda ya huko Ulaya. Ili suala zima la ukoloni lipate kueleweka vema hapana budi kwanza maelezo machache yatolewe kuhusu ubepari, kama mpango mpya wa uchumi wa maisha ya jamii, pamoja na suala la ubeberu. Wakati huo huo itabidi kuzingatia maelezo ya nyuma kuhusu utumwa-mkongwe, ukabaila na ubepari wenyewe; na kisha kutoa maelezo juu ya juhudi za kukomesha biashara ya watumwa zilizofanywa na mabepari wa mataifa ya kibepari ya Kiyuronodi.

Kuanzia nusu ya pili ya karne ya kumi na nane mpaka mnamo 1850 Uingereza, miongoni mwa mataifa machache ya Ulaya, ilikuwa imepiga hatua kubwa sana ya maendeleo ya kisayansi na kitekinologia. Maarifa ya kisayansi na kitekinologia yaliiwezesha Uingereza kukuza viwanda, kwa maana halisi ya neno, kwa mara ya kwanza kabisa katika historia ya mtu katika dunia hii. Maendeleo ya viwanda, ingawa yameitwa mapinduzi, hayakuja siku moja au katika mwaka moja; na wala hayakupangiwa na mtu. Neno mapinduzi limetumika katika maana kuwa kwa mara ya kwanza kabisa mtu amegundua njia ya kuzalisha mali kwa kutumia mashine katika kilimo na viwandani badala ya mikono na nguvu ya mtu. Na kwamba baada ya kufikia hatua hii mtu amejikomboa kiasi kikubwa sana kutoka katika unyonge wa asili japokuwa siyo kimfumo.

Viwanda viliweza, licha ya kurahisisha kazi ya mtu, kuzalisha mali kwa wingi na kwa muda mfupi zaidi. Kabla ya kukuzwa kwa viwanda bidhaa zote zilitengenezwa na mafundi wachache kama watu binafsi. Kazi ilikuwa ngumu na ya pole pole sana. Pamoja na kutumia muda mwingi bidhaa zilizozalishwa na mafundi binafsi zilikuwa adimu sana; nazo zilikuwa ni anasa. Ni matajiri tu walikuwa na uwezo wa kuzinunua.

Vile vile ikumbukwe kuwa katika kipindi hicho ukabaila ulikuwa umefikia kiwango cha juu sana cha ukomavu. Umma wa sehemu kubwa ya watu ulifanywa watwana na makabaila wachache. Watwana chini ya makabaila walifanyizwa kazi mbali mbali za kuzalisha mali kwa ujira kidogo sana na hasa kugawiwa sehemu ndogo sana ya chakula muhimu kwa kuendeleza uhai wao pasipo kustawisha hali yao ya maisha. Walipoishiwa na chakula, jambo ambalo lilitokea katika sehemu nyingi za dunia, watwana hao walilazimika kukopa posho kutoka kwa makabaila na waliposhindwa kulipa walilazimika wao na watoto wao kuishi katika ngome ya makabaila na kuwafanyia kazi maisha yao yote kama watumwa. Hali hii ilitokea zaidi huko Uchina na sehemu nyingine. Watumwa waliweza tu kuendeleza maisha yao kwa kugombania makombo ya kabaila. Uhai wao haukuthaminiwa. Na kwa sababu ya unyonge wao uliotokana na kunyonywa vizazi kwa vizazi watumwa na watwana, kama matabaka, walikuwa wamejawa na kasumba ya kuona kuwa utu wao wenyewe haukuwa na thamani sawa na utu wa mabwana na makabaila wao. Hayo yalikuwa ni matokeo ya kukata tamaa na kufa moyo kwa upande wa umma japokuwa wazo la ukombozi lilidumu akilini mwao; na kwamba mapambano baridi yalikuwa yakiendelea.

Makabaila waliwaajiri mafundi wa taaluma mbali mbali. Hao pia walifanyizwa kazi kwa ujira kidogo sana kuwawezesha kununua posho kiasi tu kuwawezesha kuendeleza uhai wao. Kwa hiyo, matokeo ya yote hayo au mpango mzima wa ukabaila kuwafanya watwana na watumwa wasiweze kuwa na fedha; na kwa hiyo kukosa uwezo wa kununua bidhaa za aina yo yote ambazo zimezalishwa na wataalam hao mbali mbali ambao wengi wao walifanya kazi za kabaila. Hali hiyo ya watumwa hasa, watwana, maana utumwa ulianza kufa, ya kutokuwa na fedha na mali ya kutosha ilikubaliana sana na mpango huu wa kikabaila.

Mapinduzi ya viwanda yalileta mabadiliko makubwa katika maisha ya jamii. Watumwa na watwana wengi waliwaacha makabaila wao ili kutafuta kazi katika viwanda. Mabepari ambao walimiliki viwanda hivyo 'waliwamiliki' pia, japokuwa siyo kisheria, wafanyakazi wa viwanda vyao. Kama wafanyakazi, waliondokana na unyonge wa kitumwa na kitwana lakini walikuwa wameingizwa katika aina mpya ya utumwa na unyonge. Unyonge huu mpya ambao ni wa kibepari ulikuwa utumwa wa hali ya juu sana na ndio bado unatupa taabu sana leo sisi wafanyakazi kama watu binafsi au kama taifa katika 'Dunia

ya Tatu'.

Kwa sababu ya kutumia viwanda mabepari, kama tabaka, walikuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuzalisha mali za aina nyingi na kwa wingi zaidi. Na kwa hiyo, walilazimika kubuni mpango mpya wa uchumi. Mpango huu mpya wa uchumi ni kuwagiribu wafanyakazi kutoa tamko kuwa wafanyakazi walikuwa watu huru. Vile vile mabepari waliendeleza falsafa hiyo ya uhuru kwa kubuni mpango wa kuwaajiri watu kwa ujira.

Watu walioajiriwa walikuwa ni wanyonge wasio na chochote isipokuwa uhai wao. Ili waweze kuendeleza uhai wao wanyonge maskini hao hawakuwa na njia nyingine isipokuwa kuuza nguvu zao kwa mabepari. Ingawa mabepari walifurahia hali hii ya umaskini na unyonge wa wafanyakazi wao walilazimika kutoa ujira wa udanganyifu kwa sababu kadhaa.

Kwanza, mabepari walitaka kuona kuwa wafanyakazi watakuwa si wazalishaji tu wa mali bali ni soko pia la wanunuzi na walaji wa mali walizozalisha. Vile vile mabepari walitaka kuendeleza biashara kati yao na makabaila kwa kubadilishana bidhaa. Kabaila na watwana wake alizalisha chakula ambacho mabepari walikinunua na kuwauzia wafanyakazi. Kwa upande mwingine, makabaila walihitaji mashine, kwa mfano, trekta na mbolea za aina mbali mbali za chumvi kutoka viwandani, pamoja na bidhaa nyingine nyingi. Na kwa kuwa mabepari walikuza viwanda vya aina tofauti ilibidi pia waendeshe biashara baina yao wenyewe. Hivyo, suala la mtaji, yaani, fedha, kama chombo cha kukadiria thamani ya bidhaa, likawa muhimu sana. Kwa maneno mengine, bidhaa na nguvu za wazalishaji, pamoja na utu wa wafanyakazi vilikadiriwa kwa fedha.

Kwa jinsi ubepari ulivyozidi kuendelea huko Ulaya Magharibi mabepari walilazimika kubuni mpango mwingine ambao ungewezesha kudumisha na kuendeleza ubepari. Mpango uliobuniwa na kuratibiwa ulikuwa ni ukoloni. Mabepari walihitaji masoko zaidi nje ya nchi zao si kwa sababu ya kuuza ziada tu ya bidhaa zao bali kwa sababu ya kupata bei nzuri na faida kubwa ya bidhaa zao katika masoko ya nje. Kwa njia hii mabepari walikuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuinua hali ya maisha ya wafanyakazi wao huko Ulaya ambao, kama tabaka, walijiunga katika vyama vya wafanyakazi na kupigania maslahi yao. Papo hapo, mabepari walilazimika kuhakikisha kuwa wao wenyewe wanabakiwa na sehemu kubwa sana ya faida. Sehemu ya faida iliyotumika kulipa ujira wa wafanyakazi ilikadiriwa kwa namna kwamba wafanyakazi hawawezi kuondokana na umaskini na

unyonge kwa kulimbikiza mali. Mabepari walijali zaidi, mpaka leo, maendeleo ya vitu badala ya maendeleo ya watu kwa manufaa ya wachache wenye uwezo wa kiuchumi. Hii ina maana kuwa maendeleo ya watu ni kuua ubepari na aina zote za unyonyaji na mabepari hawako tayari kujitoa sadaka ya aina hiyo.

Wafanyakazi katika viwanda huko Ulaya, kwa namna fulani, walikuwa watumwa wa mabepari. Ili kuwaridhisha kidogo wafanyakazi hao wa Ulaya mabepari walilazimika kuwapata vibarua ambao ni wafanyakazi wa gharama ya chini zaidi nje ya mipaka ya nchi zao. Hao ni watu katika makoloni ambao walinyonywa mno na kufanywa wanyonge zaidi.

Ukoloni kama ilivyoelezwa hapo awali ni mpango rasmi wa mabeberu ambao ni mabepari katika kiwango cha juu cha upevu wa ubepari. Mabeberu katika karne ya tisa walitoka nje ya mipaka ya nchi zao ili kujipatia masoko. Ili masoko hayo yaweze kuwa na manufaa zaidi mpango wa makoloni (ukoloni-mkongwe) ulikuwa muhimu sana. Hii ilikuwa na maana kuwa kila taifa la kibepari lililazimika kujipatia makoloni yake ambayo lingeweza kuyanyonya kwa kikamilifu zaidi pasipo bughudhi ya aina yo yote.

Kitendo cha mabepari kutoka nje ili kujipatia makoloni ndicho tutakachokiita ubeberu. Ubeberu daima ni uadui. Vitendo vya mabeberu haviwezi kamwe kuwa vya kiutu. Mabeberu hunyemelea, huiba, huvamia, huwateka watu wa nchi nyingine, huwanyang'anya haki zao za kiutu pamoja na uhuru wao. Mabeberu huwaingiza watu ambao wakati mmoja ni huru katika 'utumwa wa kibepari' ambao ni ukoloni. Ukoloni ni mbaya zaidi kuliko ubepari wenyewe kwa vile unyonyaji wa kikoloni ni wa hali ya juu zaidi; na kwamba wakoloni huwanyonya wenyeji wa koloni kwa manufaa yao wenyewe na ya jamii za nchi wanakotoka.

Mabeberu walihitaji makoloni kwa sababu moja muhimu kama ilivyoelezwa hapo mwanzoni. Kudumisha na kuendeleza ubepari. Kwa hiyo, ubeberu ulilazimika kutekeleza masharti kadhaa muhimu. Miongoni mwa masharti hayo ni kuhakikisha kuwa watu wote katika koloni wanafanywa wanyonge zaidi ya wanyonge wa kwao ili kurahisisha zaidi gharama ya uzalishaji wa mali. Mali hiyo tutaiita 'bidhaa-asili'. Bidhaa-asili ni mali iliyotakiwa kulisha viwanda kwa madhumuni ya kuzalisha 'bidhaa-mbivu' iliyo tayari kwa kuliwa au kutumiwa. Kwa kurahisisha gharama za kuzalisha bidhaa-asili, kwa mpango wa

ukoloni, mabepari na mabeberu walimudu pia kurahisisha gharama za uzalishaji wa bidhaa-mbivu katika viwanda vyao huko Ulaya.

Ili kufanikisha zaidi mpango wa ukoloni mabeberu walijenga tawala zao za kidhalimu juu ya watu waliowateka. Shabaha ya kuingiza utawala wa kikoloni ni kuhakikisha kuwa wananchi wananyonywa kikweli kweli. Serikali za kikoloni zilitunga sheria za kuwakandamiza wananchi wote kwa ujumla. Na katika kutekeleza sheria hizo za kikatili wakoloni waliunda majeshi ya kuzisimamia na kuzilinda.

Licha ya kuunda majeshi wakoloni walijenga magereza, kitu ambacho katika historia ya Waafronodi hakikufahamika. Mahakama zikajengwa siyo kwa ajili ya kusimamia haki sawa za watu bali kwa ajili ya kuwadhulumu wanyonge na kulinda maslahi ya wakubwa. Haki ilikuwa kwa wakubwa, watawala na matajiri; na ambao kwa bahati mbaya wote walikuwa Wayuronodi. Jela na adhabu nyingine za uonevu zilitolewa kwa wanyonge maskini ambao ni Waafronodi.

Katika kuzidi kurahisisha suala la unyonyaji na udhalimu wa aina mbali mbali wakoloni waliwakandamiza na kuwanyanyasa wananchi. Na kwa sababu ya kukandamizwa vikali ilikuwa vigumu sana kwa wananchi hao wanyonge kujimudu na kujitetea kwa namna yo yote ile. Mara nyingi wakoloni waliendesha utawala wao kwa kupitia 'mlango wa nyuma'. Wakaunda tabaka la watu waliowaita 'machifu'. Siasa ya utawala wa mlango wa nyuma ilipendelewa sana na Waingereza nayo ilisaidia sana kurahisisha utawala wao wa kidhalimu. Machifu si watemi ingawa baadhi yao, walikuwa ni tabaka la vibaraka ambao waliteuliwa na wakoloni, na ambao baada ya kuwavua mamlaka na madaraka ya jadi na ya dhati, wakawavika madaraka ya bandia.

Kazi yao muhimu ilikuwa kusimamia na kuhakikisha kuwa sheria mbali mbali za uchumi za wakoloni zilitekelezwa.Machifu walipewa matarishi, mabwana-shamba, mabwana-afya, mabwana-nyama na mabwana-mifugo na kadhalika. Watu hao ambao walitambulikana kwa kutembea bila viatu (kupekua), kuvaa tunga ndefu, vimao na sketi pana walipikwa kasumba kubwa sana. Kasumba ya kikoloni iliwapumbaza sana wananchi hao kiasi kwamba waliweza kuthubutu kuukana si Uafronodi tu bali hata Uafrika wao. Tatizo kubwa! Kwa sababu ya kuukana Uafronodi wao wananchi hao wakageuka kuwa chombo kikubwa cha kutekelezea sheria na mpango mzima wa kidhalimu na

kinyonyaji wa ukoloni. Wakoloni na vibaraka wao waliwanyanyasa wananchi, wakawadharau na kuwapuuza, wakawatesa, wakawadhulumu haki na mali zao na matokeo yake ni kuwaingiza wananchi wote kwa ujumla, katika umaskini, unyonge na wasiwasi.

Tabaka hili la wateule ambalo lenyewe lilipumbazwa lilisaidia pia kuwapumbaza wananchi zaidi na zaidi. Mara nyingi lilijaribu kujitambulisha na tabaka la wanyonyaji na watawala kiasi cha kukiuka na kujiita 'Wazungu-weusi'. Uafronodi na rangi nyeusi ya ngozi yao yalikuwa ni mambo waliyoyasikitikia katika maisha yao. Wangependa, kama wangekuwa na uwezo, hata kujichuna ngozi ili wapate kufananafanana na mabwana zao, yaani, Wayuronodi na Wasanodi wa Kiarabu. Maumbile na mijengo yao ikawa ni kashfa kwao na huzuni kwa maisha yao yote! Suala la ukombozi kwa tabaka hili lilikomea katika dai la kutaka kutambuliwa na kukubaliwa na wakoloni na wala si kupambana nao kwa madhumuni ya kuutokomeza ukoloni na kurudisha uhuru na hadhi ya wananchi. Mzinduko wa kisiasa kwa walio wengi haukuja upesi. Walihitaji, wengi wao, nguvu ya pekee ya msukumo kutoka nje; yaani, kutokana na watu waliokandamizwa.

Mabeberu ni watu werevu, wajanja na wenye njama nyingi. Kila wanapotaka kutekeleza maazimio yao huanza na mipango kamili iliyoratibiwa kitaalam. Utekelezaji wa mipango hiyo hufanywa na kuendeshwa kwa utaratibu na kimaarifa sana. Hutumia kila aina ya mbinu na njama; kunyemelea, kuvamia, kula njama na tabaka la kidhalimu la wananchi, kutumia ujinga wa tabaka hilo na kadhalika.

Mpango wa mabeberu, kama ilivyoelezwa, ulikuwa kujipatia makoloni katika Afrika na sehemu nyingine za dunia. Katika Afrika, wakoloni walipitia hatua maalum za kujipatia makoloni. Walilazimika, kwa nafasi ya kwanza, kuielewa Afrika kuhusu mazingara, utajiri na watu wake. Mabepari wa Kiingereza walikuwa katika mstari wa mbele kuhusu mapinduzi ya viwanda na kwa jinsi hiyo walikuwa wa kwanza katika kuunda vyama vya upelelezi. Vyama hivyo vilituma wajumbe maalum wa kulipeleleza Bara hili na kugharamia shughuli nzima. Kampuni za propaganda zikaanzishwa. Watu wengi, kwa sababu mbali mbali, wakajitokeza kuja Afrika. Miongoni mwao ni akina Mungo Paka aliyeendesha upelelezi wake huko Afrika ya kaskazini kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na nane.

Ingawa mabepari na mabeberu walikuwa kiini na chanzo cha

ukoloni wamisionari waliwekwa katika mstari wa mbele kabisa katika utekelezaji. Wamisionari kama viongozi wa dini, kwa kipindi tunachoongelea, waliheshimiwa na kukubalika sana na waumini wa Ulaya. Na miongoni mwa waumini kulikuwa na mabepari na wanyonge. Ni watoto wa wenye uwezo wa kiuchumi tu walioweza kupata elimu katika kipindi hicho maana elimu haikufikiriwa kuwa ni haki ya kila mtu. Kwa hiyo, ni dhahiri, pengine, kuwa idadi kubwa ya viongozi wa dini walitokana na jamaa za kinyonyaji. Na hii ina maana kuwa mabepari, mabeberu na viongozi wa dini walikuwa na uhusiano mkubwa sana. Wote walikuwa wanyonyaji. Lakini, kwa sababu ya kukubalika zaidi viongozi hao wa dini walijitokeza katika mstari wa mbele zaidi katika mapambano ya kueneza na kudumisha ukoloni. Wengi wao, kwa kutumia imani ya dini, walikuja Afrika kwa shughuli za upelelezi wa kijografia ili kuwafungulia njia mabeberu na wakoloni. Miongoni mwao ni akina Daktari Daudi Livingistoni, Rebumani, na Krafu na kadhalika. Suala la wamisionari kushiriki katika kueneza, kuhudumia na kudumisha ukoloni limejadiliwa zaidi katika sura ya kumi na mbili.

Baada ya shughuli za upelelezi kumalizika katika miaka ya 1870 mabeberu wakaingia katika hatua ya pili. Hatua ya pili ilikuwa kuligawanya Bara la Afrika katika makoloni miongoni mwa mataifa ya kibepari ya Ulaya. Hatua hii iliingiwa baada ya wapelelezi kutoa taarifa kamili ya mambo waliyoyaona katika Afrika. Waligundua, kwa mfano, kuwa Afrika ina utajiri wa aina nyingi. Ina madini mbali mbali na kwa wingi sana. Ardhi bora kwa kuotesha mazao muhimu ya bidhaa; na watu wengi wenye nguvu na maarifa ambao wangeweza kuwatumia katika shughuli mbali mbali za kuzalisha mali. Maarifa hayo yalikuwa kinyume cha imani ya miaka mingi ya mabeberu wa Ulaya kwamba Afrika ilikuwa maskini; kwa jinsi hiyo haikuwa na mchango isipokuwa kutoa uhai wa watu wake kama watumwa wa kutumikishwa ugenini.

Kila taifa la kibepari likaanza kutoa madai yake kuhusu sehemu maalum. Mara nyingi taifa lilidai sehemu ambazo zilifanyiwa upelelezi na watu wa taifa hilo au waliokuwa katika utumishi wa taifa hilo kama ni taadhira zao. Kwa kuwa sehemu kubwa ya upelelezi ilifanywa na wamisionari ambao pia walianzisha maskani katika Afrika taifa lililohusika liliweza pia kutoa madai yake kuhusu sehemu hiyo.

Kitendo hicho cha kila taifa kutoa madai kilianza kuleta

mvurugano na milipuko miongoni mwa mataifa mbali mbali ya kibepari ya huko Ulaya. Kwa sababu baadhi ya mataifa yalimiliki sehemu kubwa ya Afrika na mengine ambayo yalichelewa kukuza ubepari na kuunda umoja wa kitaifa huko makwao yalikuwa pia na haja ya kujipatia makoloni. Hivyo, basi, ilibidi utaratibu ufanyike ili kuzuia lipuko au sokomoko. Kwa sababu hiyo, pamoja na sababu nyingine, mabeberu wakaamua kukutana huko Belini, Makao Makuu ya Ujerumani, ili kujadili juu ya utaratibu wa kuligawanya Bara la Afrika pasipo kuleta mgongano baina yao.

Mkutano wa Belini ni tukio kubwa sana ambalo wanaAfrika, hasa Waafronodi, wapaswa kulijua na kulitafakari. Mkutano huo ingawa ulifanyika Ulaya ulikuwa juu ya Afrika. Mabepari kwa mara ya kwanza katika historia yao wakakutana ili kuhalalisha suala la ubeberu na ukoloni kama mpango rasmi wa unyonyaji. Vile vile mkutano huo ulikuwa kiini cha muungano wa umoja wa mabepari na mabeberu kama tabaka na wala si mabepari wa Ulaya tu bali wa dunia nzima. Moja ya maazimio yake ilikuwa kuligawanya Bara hili katika makoloni miongoni mwa mataifa mbali mbali ya kibepari ya Ulaya. Wakatwaa ramani ya Afrika na wino mwekundu kisha wakachorachora mistari, yaani, mipaka. Sehemu kubwa ya mipaka hiyo ya 1884/1885 iko mpaka leo. Kitendo hicho kilikuwa cha udhalimu na uhasama. Mabeberu hawakujali kama waliwagawa watu wa asili moja ya kitawala na kiutamaduni na kadhalika; na kwamba kwa vyovyote vile hawakuwa na haki ya kuvamia na kugawanya Afrika.

Maazimio ya Mkutano wa Belini yalihusu njama na mbinu za utekelezaji wa mpango wa ukoloni. Mabeberu waliligawanya bara hili kirahisi sana kwa kuchora mipaka katika ramani wakiwa Belini. Jambo la kukumbuka ni kuwa mabeberu hawakuwa wameyamiliki makoloni hayo ambayo yalieleweka kiramani na kimaandishi tu. Kazi kubwa iliyofuata ni kuzivamia na kuziteka nchi hizo na kuzifanya makoloni halisi, yaani, kuzimiliki. Katika mkutano wa Belini wanaAfrika hawakushirikishwa lakini katika kutekeleza uamzi wananchi walilazimika kujiingiza kwa namna moja au nyingine; na mabeberu walifahamu kabisa jambo hilo na ndiyo maana walikula njama na kubuni mbinu za jinsi ya kutekeleza.

Kutekeleza njama zao mabepari walitumia mbinu nyingi

kuziteka jamii na tawala za Kiafrika. Baadhi yao walitayarisha mikataba ya udanganyifu ambayo waliwaomba watemi wetu kutia sahihi zao.* Ufuatao ni mmoja ya mikataba mingi ya udanganyifu ambao ulifanywa kati ya Mtemi Mangungo na Kalo Petro.

"Mangungo, mtemi wa Msovero katika Usagara, na Daktari Kalo Petro. Mangungo kwa niaba ya watu wake wote na Daktari Petro kwa niaba ya wenzake wote aliofuatana nao na washiriki wa baadaye wanawekeana mkataba wa urafiki wa milele.

Mangungo anakubali kuitoa nchi yake na haki zote za kitawala kwa Daktari Kalo Petro akiwakilisha Chama cha kutafuta makoloni cha Kijerumani, kwa matumizi yake na ya dunia kwa madhumuni ya kueneza ukoloni wa Kijerumani.

Daktari Kalo Petro kwa hiari yake na kwa niaba ya chama,. . . . . .anatoa kibali chake kuitwaa nchi ya Mtemi Mangungo na haki zake zote kwa niaba ya Chama cha Makoloni cha Wajerumani pasipo kuingilia uhuru wa Mwenyi Sagara.

Kufuatana na hayo yote, Mtemi Mangungo anaitoa nchi yote ya Msovero, nchi ambayo ameipata kwa urithi au iliyopata kuwa chini ya mamlaka yake kwa nyakati zote, na kumkabidhi Daktari Kalo Petro, akitoa pamoja na haki zake zote za kitawala.

Daktari Petro kwa niaba ya Chama chake . . . . . .anaahidi. . . . . .kuilinda nchi ya Msovero wakati wa kuiteka nchi ya Usagara.

Mkataba huu umetafsiriwa kwa Mtemi Mangungo na mkalimani Ramzan bila makosa na kukubaliwa na pande zote mbili, kuambatana na mila na desturi za Kisagara. Mtemi Mangungo kwa vyo vyote hakuwa chini ya mamlaka ya Sultani wa Zanzibar, na kwamba hakufahamu kama kulikuwa na Sultani wa Zanzibar.

Imetiwa sahihi na
Daktari Petro
Imetiwa sahihi na
Mangungo

* I.N. Kimambo, A.J. Temu, (ed), *A History of Tanzania*, Nairobi, Uk. 99

Mkataba huu umefanyika kisheria na kuhalalishwa kwa muda wote mbele ya mashahidi wengi, tunaahidi:

Kagakinga (Dole gumba), Mwana wa mtemi Mangungo, mtawala wa Gobola (dole gumba) Mwana wa pili wa Mangungo, mtawala wa Draman (dole gumba) Graft Peil August Otto. (Dole gumba la Ramazani na kadhalika)

Daktari Kalo Julke.
Msovero Usagara Novemba 29, 1884.

Watemi wetu hawakuelewa maana ya mikataba hiyo. Mikataba iliandikwa katika lugha za kigeni na wananchi hawakujua kusoma. Wakalimani waliotumiwa wenyewe pia hawakuwa wasomi. Na hii imethibitishwa na mkalimani Ramzan aliyetumiwa na Kalo Petro katika kuwadanganya watawala wetu. Ramzan, kama watemi wetu, alitia sahihi yake kwa kutumia dole gumba. Kuna uwezekano mkubwa kwamba maneno aliyoambiwa Ramzan na Petro ili kuwaeleza watemi yalikuwa tofauti na yale aliyoyaandika katika mikataba yake ambayo wananchi hawakushiriki katika kuitayarisha.

Kwa jinsi hiyo Lobengula wa Zimbabwe, na watemi wengine wengi, alidanganywa na Sesili Rodesi kutoka Afrika Kusini. Ukweli juu ya mabeberu kutumia ujinga wa watemi wetu na wa wananchi kwa ujumla umedhihirishwa na milipuko ya mapambano iliyotokea baadaye baada ya watemi hao kung'amua hila za mabeberu. Kwa mfano, mwaka 1893, Lobengula na watu wake, Wamatabele, waliamua kuutokomeza ukoloni ambao ulianza kuweka mizizi yake katika nchi yake. Alikuwa amechelewa kung'amua baada ya kudanganywa; na matokeo yake alipoteza maisha yake na ya wengi wa watu wake licha ya kupoteza nchi na uhuru wa wana Zimbabwe.

Katika kipindi hiki cha pili cha karne ya kumi na tisa jamii nyingi za Kiafronodi zilikuwa katika hali ya kuendeleza mapinduzi ya kisiasa. Tawala nyingi ziliangushwa kama moja ya matokeo ya biashara ya watumwa na nyingine kubwa na zenye nguvu zaidi zikaundwa badala yake. Lakini jambo la maana ni kuwa wananchi wenyewe, kwa sababu kadhaa zitokanazo na kukua kwa fikara za jamii yoyote yenye kujimudu, walipatwa na fikara ya umoja. Umoja huo ulikuwa na maana kwamba jamii nyingi zinaungana chini ya utawala na uongozi mmoja. Hii ilikuwa na maana pia kwamba baadhi ya watemi ilibidi waziteke tawala nyingine zilizo dhaifu ili kuwaunganisha watu wake. Hali hii ilikuwepo huko Afrika Kusini wakati wa Mfecane; katika

Afrika ya Kati na Mashariki hasa katika Tanzania Bara baada na hata kabla ya kuwasili kwa Zwangendaba na wafuasi wake kutoka nchi ya Uzulu. Huko Afrika Magharibi pia jamii nyingi ziliendelea katika kuendesha mapinduzi ya aina hiyo. Uganda katika Afrika Mashariki ni mfano mwingine ulio mzuri na dhahiri zaidi. Kulikuwa na tawala tatu zenye nguvu katika karne ya kumi na nane na kumi na tisa katika Uganda nazo ni Buganda, Bunyoro na Ankole. Tawala hizi tatu ambazo zilikuwa ni falme zenye nguvu daima ziliishi katika uhasama na uadui mkubwa, hasa katika kipindi kinachoongelewa. Buganda ambayo ilionekana kuwa na nguvu zaidi ilitumiwa sana na Waingereza katika kuteka Bunyoro na Ankole na jamii nyingine ndogo ndogo.

Wakati wakoloni walipoanza kuvamia jamii za Kiafrika katika miaka ya 1880 waliikuta hali hiyo ya mapinduzi ya kisiasa. Nao (wakoloni) wakaitumia hali hiyo kwa manufaa yao. Lengo la mabeberu lilikuwa kuziteka jamii za Kiafrika na kisha kuziingiza katika ukoloni. Kwa upande mwingine, baadhi ya watemi wenye nguvu na wenye fikara za kimapinduzi walikuwa na shabaha ya kuziteka baadhi ya temi dhaifu katika ujirani ili kuwaunganisha wananchi katika utemi moja mkubwa na wenye nguvu na uwezo zaidi wa kujilinda na kujiendeleza. Hakuna mtemi aliyekuwa tayari kuiingiza nchi yake katika ukoloni kama ilivyoelezwa na baadhi ya wanahistoria. Wakoloni walikuwa wajanja na werevu zaidi kuliko watemi wetu. Hii yote ilitokana si kwa sababu wao, wakoloni, walikuwa na uwezo na utu zaidi kuliko Waafronodi. Bali kwa sababu ya historia yao ndefu ya maendeleo katika ulimwengu wa sayansi, tekinologia na, kwa hiyo, wa kifikara pia.

Hivyo, kwa werevu mkubwa wakaanza kufanya urafiki na temi kubwa na zenye nguvu. Watemi hao ambao walitaka kuwaendeleza watu wao na kudumisha uhuru wao hawakuelewa hila za mabeberu. Waligiribika kwa kuwakaribisha mabeberu katika nchi zao na kupokea silaha zao kwa shabaha ya kuziangamiza temi nyingine. Kwa ufupi, watemi hao waliuchukua ushirikiano huu kama ni urafiki wa dhati wa watu walio huru na sawa. Urafiki wa kiitifaki. Mabeberu, kwa upande mwingine, walijua kuwa katika kuwagiribu watemi hao walikuwa wanadhoofisha nguvu ya wananchi kwa kujenga uhasama, chuki, mtengano na uadui miongoni mwa watu wa temi mbali mbali. Baada ya watemi hao kumaliza tu kazi yao ya kuziteka temi nyingine wakoloni wakaanza kuzivamia na kuziteka

kwa urahisi. Mara nyingi jamii ndogo ndogo ambazo hapo awali zilitekwa na temi za kimapinduzi hazikuweza kushiriki kikamilifu katika kutetea uhuru wao. Wakoloni walipendezewa sana na hali hii ya ujinga wa wananchi ya kutokutambua mapema umuhimu wa kuungana mbele ya adui wa wote, yaani, ukoloni.

Baadhi ya tawala zilizotumiwa kijanja na wakoloni zilitekwa kwa kudanganywa. Mabeberu waliwapumbaza watemi na wafalme wa tawala hizo kwa kuwadanganya kuwa tawala zao zilikuwa huru chini ya ulinzi mathubuti wa serikali za mabeberu. Ulinzi huo ulikuwa juu ya nini na kwa maslahi ya nani? Askari wa ulinzi walikuwa ni watu gani? Ni vigumu pia kujua kwa jinsi na kiasi gani tawala hizo zilikuwa huru! Ukweli ni kuwa hizo zilikuwa ni mbinu tu za mabeberu. Tawala hizo ingawa ziliachiliwa kuunda serikali zake, kusema kweli, serikali hizo zilikuwa za bandia; na kwamba watemi na watu wote wa tawala hizo walikuwa chini ya mamlaka ya serikali ya kikoloni. Hawakuwa huru; na wala hawakuwa na uhuru wa kuamua mambo yao kwa shabaha ya maendeleo ya jamii zao. Walikuwa mateka kama vile nchi nyingine zilizotekwa kwa kuvamiwa. Hata hivyo, jambo muhimu la kukumbuka ni kuwa uhuru huo ulikuwa ni njia bora ya kurahisisha suala zima la utawala na unyonyaji wa kikoloni. Kama kielelezo, Waingereza walitumia sana utawala wa Kabaka wa Buganda katika kuteka, kukandamiza na kunyonya tawala za Bunyoro na Ankole katika Uganda.

Jamii ambazo ziling'amua mapema hila na njama za mabeberu hazikukubali kudanganywa, kupumbazwa wala kutumiwa kama vibaraka. Zilisimama imara. Mabeberu nao kwa upande wao waliweza kutambua msimamo na nguvu za tawala hizo za wananchi. Hivyo, hapakuwa na ujanja au njia nyingine kwa upande wa mabeberu. Hapakuwa na uchaguzi isipokuwa kuzivamia nchi hizo kwa vita vya ana kwa ana. Baadhi ya jamii zilizosimama imara katika kupinga ubeberu na ukoloni ni Wahehe, Wayao, Wanyamwezi, na Wangoni*katika Tanzania. Katika sehemu nyingine za Afrika pia kulikuwa na jamii zilizopinga kuingia kwa ukoloni, kwa mfano: Wazulu, Wasutu, Wamatabele, Wamashona, Walundo, Waashanti na kadhalika.

Katika mapambano hayo ya vita vya ana kwa ana wakoloni ndio walioanza kushambulia. Wananchi walipigana katika kutetea uhuru wao. Lakini baada ya mapambano makali na ya muda mrefu wananchi walielemewa na kushindwa isipokuwa

* Wangoni–hawakupigana na Wajerumani kwa sababu Wajerumani kwa hila yao waliwahi kuwavizia watemi wote wa Songea na kuwakamata kabla ya mapambano.

Wahabeshi na Wasutu. Wasutu baada ya kuvamiwa na kuwashinda Makaburu na mabeberu wa Kiingereza wa huko Afrika Kusini wakaonelea afadhali kujiweka chini ya 'ulinzi' wa ufalme wa Uingereza. Uchaguzi huu haukuwa wa hiari bali walilazimika kufanya vile. Afrika nzima ilikuwa imeelemewa na mabeberu na kwamba tawala hizo zilijua kuwa punde nazo zingeelemewa na kutekwa. Ulinzi huo waliouomba haukuwa ulinzi wa dhati bali ilikuwa ni kujitumbukiza katika ukoloni; na papo hapo ilikuwa kukiri udhaifu wao uliotokana na uhafifu wa silaha zao na, hasa, utovu wa umoja. Hali hiyo ilisababishwa na tofauti ya mendeleo ya kisayansi na kitekinologia kati ya mabeberu na wananchi.

'Mmisionari na biblia yake atamtangulia askari na bunduki yake'. Hayo yalitamkwa na mfalme mmoja wa mataifa ya kibeberu ya huko Ulaya Magharibi katika karne ya kumi na tisa. Matamshi hayo ni ushahidi na uthibitisho wa ukweli wa mambo yaliyopata kutokea katika Afrika. Wamisionari waliwatangulia askari na wakoloni katika suala la kuzivamia tawala za Kiafrika ili kuziingiza katika ukoloni.

Katika kuzungumza suala la wamisionari na ukoloni itabidi mambo kadhaa yazingatiwe. Kwanza kabisa, kuna suala la 'imani' yenyewe. Imani yoyote ya dini ni safi na wala haina dosari. Imani ya dini inasisitiza juu ya maisha bora ya jamii. Lakini imani hiyo hiyo ina wahubiri na waenezi wake. Waenezi wa imani ya dini katika Afrika walikuwa wamisionari. Wamisionari tuliowapata katika Afrika ni wa aina mbili. Wamisionari wa Kikristo na wa Kiislamu. Wamisionari wa Kikristo ambao habari zao zitaongelewa zaidi katika sura ya kumi na mbili walikuwa ni Wayuronodi. Nao walimiminika katika Afrika kuanzia miaka 1840. Wamisionari wa Kiisilam walikuwa Wasanodi, hasa, Waarabu.

Wamisionari wa Kikristo walijenga makanisa na kuhubiri dini kwa wananchi. Pamoja na kuhubiri habari za Mungu wamisionari hao walitumia imani hiyo kwa kuwaandaa wananchi kwa ajili ya kuupokea ukoloni wa kibeberu. Pole pole wakawapika kasumba wananchi. Waliwafundisha kukashifu na kuukana Uafronodi na kila kitu cha Kiafronodi. Badala yake wananchi wakafundishwa kupenda na kuthamini zaidi utamaduni wa kibeberu ambao ni wa Kiarabu na Kiyuronodi. Na kwa kuwa wamisionari wa Kiyuronodi walitokana na mataifa mbali mbali wananchi pia walifundishwa utamaduni wa mataifa mbali mbali ya Kiyuronodi. Hata hivyo, Waafrika, hasa Waafro-

nodi, walifundishwa kasumba ya kutojiamini na kumtegemea Msanodi au Myuronodi. Matokeo ni kuwa utamaduni wetu ulizoroteshwa. Maendeleo ya aina yote yalikatishwa. Wananchi waliingizwa taratibu katika fikara za kibeberu, kikoloni na ubinafsi. Fedha zikafanywa ndio msingi wa heshima badala ya utu, upendo na kazi. Kwa ufupi, waliwaandaa wananchi kama soko la bidhaa za mabepari wa Ulaya.

Wamisionari, licha ya kuwagawanya watu kifikara na kitamaduni kutegemea mataifa ya kwao, walijenga na kuimarisha uadui, uhasama na fikara za ubaguzi, miongoni mwa wananchi. Waislam walifundishwa kutoshirikiana na wakristo kwa jinsi yo yote. Wakristo nao walifundishwa kuwabagua waislam na watu wengine wasioamini imani yo yote au waumini wa imani zao za jadi. Ubaguzi wa kimadhehebu ulijenga uadui na uhasama mkubwa miongoni mwa watu wa nyumba moja, ukoo mmoja, jamii moja na kadhalika. Hali hii ya fujo iliwafanya wananchi washindwe kushirikiana katika vita vya kupinga ukoloni na baadaye vya ukombozi wa kujitarakisha kutoka ukoloni-mamboleo; na hasa katika mapambano ya kuleta maendeleo ya jamii, kwa ujumla.

Baada ya kuwaandaa wananchi kifikara na kitamaduni wamisionari waliwagiribu wananchi kwa kuwashawishi kuziweka nchi zao chini ya mamlaka ya serikali za kibeberu. Baadhi ya temi zilipinga na kushinda ushawishi wa aina hiyo. Lakini baadhi ya temi zikagiribika. Kwa mfano, Padure mmoja aitwaye Fransisi Kwayadi* ambaye alitokea Uingereza alifaulu kumshawishi mtemi wa Walozi, jamii iliyoko katika jimbo la kusini magharibi la Zambia, kwa jina Lewanika, kuiweka nchi yake chini ya taathira na himaya ya Kiingereza. Barua za maombi zilizopelekwa kwa mfalme wa Uingereza ziliandikwa na Fransisi mwenyewe kupitia kwa Gavana wa Kiingereza katika Boswana. Jamii ya Kilozi ikapoteza uhuru wake na kuingizwa moja kwa moja katika ukoloni. Fransisi hakufanya kitendo hicho kwa bahati mbaya bali kwa kudhamiria akielewa kabisa anafanya nini. Kwa upande mwingine, Mtemi Lewanika alikuwa amedanganywa. Hapo dini ilitumiwa na wamisionari kwa kueneza ubeberu na ukoloni katika Afrika kwa manufaa ya mabepari wa Ulaya. Kadhalika uhusiano baina ya Padure Robati Moffati na Mtemi Msilikazi, baadaye na mwanae Mtemi Lobengula; wamisionari wa Buganda na Kabaka ulikuwa na

* A.J. Wills, Uk. 161 – 2

lengo hilo hilo.

Wamisionari kama akina Livingistoni mara nyingi walihutubia mikutano huko kwao wakiwaalika mabepari na makabaila kuja kuchukua ardhi ya wananchi. Mbali ya hotuba wamisionari hao walikuwa wanawaalika jamaa zao kwa njia ya maandishi wakisifia utajiri wa Afrika ingawa baadaye waliwagiribu wananchi kuwa Afrika ilikuwa haiendelei kwa sababu eti ilikuwa maskini. Ukweli wenyewe ni kuwa Afrika si maskini ingawa watu wake ni maskini. Umaskini huo wa wananchi unatokana na kutawaliwa, kukandamizwa na kunyonywa kwa muda mrefu na wakoloni. Leo umaskini wa wanaAfrika unaendelezwa na kasumba za kikoloni pamoja na ukoloni-mambo-leo.

Mabepari waliitika wito wa wamisionari, nao wakaja hima. Wakanyakua sehemu kubwa ya ardhi ya wananchi. Sehemu walizozinyakua ni zile ambazo zilikuwa tajiri kwa madini; na zenye rutuba kwa kuotesha na kustawisha mazao mbali mbali ya bidhaa yaliyohitajika kwa kuendeshea viwanda vyao vya huko Ulaya. Haukupita muda mrefu, wamisionari pamoja na walowezi wakaanzisha kampeni za kuziingiza sehemu hizo katika ukoloni. Wakaziandikia serikali zao za huko Ulaya kuwa Waafrika, hasa Waafronodi, walikuwa washenzi, wakatili, na wauaji. Na kwamba maisha ya wamisionari na walowezi yalikuwa wakati wote katika hatari. Ili kuhakikisha usalama wao na wa mali zao waliziomba serikali zao kuja kujenga utawala wa kikoloni juu ya wananchi. Hii ilikuwa na maana kwamba serikali za wakoloni zije kujenga serikali zao pamoja na kuunda majeshi na taasisi nyingine muhimu za kuwakandamizia wananchi kwa shabaha ya kurahisisha shughuli za unyonyaji ambazo ziliendeshwa na walowezi pamoja na wamisionari wenyewe katika sehemu mbali mbali za Afrika.

Jambo la maana linalopaswa kukumbukwa ni kuwa imani ya dini yoyote ina nguvu kubwa sana. Inaweza kuharibu fikara za mtu na jamii nzima. Kwa sababu ya nguvu hiyo hiyo imani ya dini ilitumiwa na wamisionari katika kuandalia ukoloni. Na kwamba wamisionari wenyewe kwa ajili ya vitendo vyao, fikara zao, na mwenendo wao walikuwa mabeberu, mabepari na wakoloni wa mstari wa mbele kabisa.

Kwa kumaliza, ingawa wakoloni waliligawanya bara hili kirahisi katika makoloni katika mkutano wa Belini utekelezaji wake ulikuwa mgumu sana. Iliwachukua wakoloni kiasi cha miaka kumi na sita au zaidi kuiteka Afrika na kuzimiliki sehemu mbali mbali kama makoloni. Wananchi walikuja juu. Lakini kwa

sababu ya kukosa umoja na silaha za kulingana na wakati wananchi walishindwa katika mapambano yao ya awali ya kupinga ukoloni. Hata hivyo, wananchi hawakukata tamaa bali waliendeleza mapambano yao kwa njia na mbinu tofauti kama itakavyoelezwa katika sura ya kumi na mbili.

Sura ya 11

UTAWALA NA SIASA YA KIKOLONI

Mnamo 1900 Afrika ilikuwa imetekwa na kugawanywa katika makoloni isipokuwa Ethiopia. Wananchi walipoteza uhuru wao. Wakawekwa chini ya serikali za mataifa ya kibeberu ya Ulaya tayari kutawaliwa, kukandamizwa na kupuuzwa kwa shabaha moja kubwa; nayo ni kuwanyonya wanaAfrika. Kwa upande mmoja wakoloni walitumia siasa na mbinu mbali mbali ikiwa ni juhudi ya kufanikisha shughuli nzima ya unyonyaji.

Kwa upande mwingine, Wajerumani hawakuwa na ufundi sana wa kuendesha makoloni. Wao walitawala kwa njia ya mabavu. Badala ya kuwatumia watemi kama 'machifu'. yaani, vibaraka, Wajerumani waliwaondoa watemi hao, wakawakashifu, wakawadharau na kuwaaibisha mbele ya raia wao. Wananchi hawakufurahishwa na vitendo hivyo vya Wajerumani maana walikuwa na imani, upendo na heshima kubwa kwa watemi wao.

Siasa ya mabavu iliwaletea taabu sana Wajerumani. Wananchi popote katika makoloni ya Wajerumani waliweza kuona dhuluma za wakoloni moja kwa moja; maana Wajerumani na vibaraka wao, kama vile maakida na maliwali, wote walikuwa wageni; na kwamba mara nyingi walitokana na jamii za Kisanodi hasa katika Tanzania. Kwa jinsi hii wananchi waliwatambua upesi maadui wao, yaani, Wajerumani na vibaraka wao. Hivyo, bila ya kusita wananchi wakaanza kujiandaa kwa vita vya ukombozi. Katika Tanzania Bara, wananchi wakaanza kuwashambulia Wajerumani katika mapambano makali ya Vita vya Maji Maji vilivyopigwa kati ya miaka 1905 na 1907. Vita hivyo, vikiwa ni moja ya vita chache vya kwanza katika historia ya mapambano ya Waafronodi na ukoloni vilipigwa karibu na wananchi wote kusini ya Reli ya Uhuru. Wananchi waliunganika chini ya imani ya maji ambayo Nabii wake Mkuu alikuwa Kinjikitile. Kinjikitile ambaye hakuwa mmoja wa watemi alikuwa kiongozi

aliyehitajiwa na wananchi kwa wakati huo kuendesha mapinduzi.

Ni jambo la kustaajabia kuona kuwa katika kipindi hiki si wanachi wa Tanzania tu walioamua kupambana na ukoloni na ubeberu wa Kijerumani. Wananchi katika makoloni ya Wajerumani ya Togo na Kameruni katika Afrika Magharibi nao walishika silaha na kuendesha mapambano ya vita vya ana kwa ana na Wajerumani kwa shabaha ya kujikomboa. Kadhalika wananchi wa Namibia hasa wa jamii ya Waherero nao waliamua kupigana na Wajerumani mnamo 1904. Baadaye vita hivyo viliendelezwa chini ya uongozi wa Samueli Maherero mwana wa Mtemi Maherero. Baada ya Waherero kupigwa Wanama nao wakaanza kuwashambulia Wajerumani chini ya uongozi wa Mtemi wao Hendriki Witiboi.

Ijapokuwa wananchi walipata ushindi katika mapambano mengi, wananchi hatimaye walishindwa kuubwaga ukoloni wa Kijerumani. Sababu kubwa ya kushindwa kwao ni utovu wa umoja na uongozi wa pamoja. Wananchi walipambana kivikundi na kiukoo ingawa lengo ni moja: uhuru!. Hivyo, ilikuwa rahisi sana kwa Wajerumani kupiga kikundi kimoja baada ya kingine. Kwa mfano, katika Namibia Wanama hawakuungana nguvu na Waherero mpaka tu Waherero waliposhindwa na kuteketezwa na Wajerumani ndipo nao wakatangaza vita. Njaa ambayo ilisababishwa na vitendo vya kinyama vya Wajerumani kuchoma moto mashamba na ghala za chakula viliwafanya wananchi wafe kwa wingi zaidi kuliko idadi ya watu waliokufa katika vita yenyewe. Jambo la tatu lililosababisha kushindwa kwa wananchi ni uhafifu wa silaha zao; na kutokubadili mbinu zao za vita. Wajerumani walikuwa na silaha bora zaidi kuliko wananchi. Lakini suala la silaha katika mapambano hayo ya awali halikuwa sababu ya kwanza ya ushindi wa Wajerumani. Wajerumani walielemewa sana na ndiyo maana wakaomba msaada wa kijeshi kutoka kwa Waingereza na kuwaagiza wengine kutoka Ujerumani na Afrika Kusini.

Leo nchi huru za Afrika, licha ya kujenga fikara na mfungamano wa kitaifa na wa kizalendo miongoni mwa wananchi, haziwezi kupuuza suala la umuhimu wa silaha za kisasa na mafunzo ya miondoko na mbinu mpya ili kuweza kupambana kiume na ubeberu na ukoloni-mambo-leo. Hii haina maana kuwa mataifa huru ya Kiafrika yategemee tu kununua silaha kutoka kwa mataifa makubwa ambayo yenyewe ni mabeberu. Silaha watakazotoa mabeberu ni silaha hafifu. Mafunzo watakayotoa

kwa wanajeshi wetu ni kwa shabaha ya kuangusha serikali halali za kimapinduzi na kurudisha nyuma maendeleo yote ya Afrika. Jambo la kwanza ni kuyafunza majeshi yetu mbinu za Kiafrika ambazo hazina budi kubuniwa na kukuzwa na wanajeshi wa Kiafrika wenyewe. Mipango yetu ya maendeleo itilie mkazo juu ya suala la elimu ya utaalam, sayansi, tekinologia na ufundi ili kuwezesha kugundua na kuunda aina mpya za silaha; au kuendeleza silaha za mataifa makubwa na kuzifanya bora zaidi na zaidi. Kwa hiyo, suala la kujenga viwanda vya zana katika kila nchi ni muhimu sana.

Pamoja na kushindwa kwa wananchi kuna haja ya kujadili suala zima la sababu ya vita hivyo kupigwa katika wakati huo; tena kwa wakati mmoja katika makoloni ambayo yalitengana kwa mamia na maelfu ya maili. Wanahistoria wengi wameshikilia fikara ya kuwa vita hivyo vilikuwa ni maasi ya wananchi kwa serikali; na kwamba vita hivyo vilisababishwa na vitendo vya kikatili vya wakoloni kama watu binafsi badala ya ukoloni kama mpango wa kisiasa na kiuchumi wa jamii. Maelezo haya husikika kana kwamba yana ukweli ndani yake. Lakini maelezo ya kuridhisha na ya kiakili yangeweza kutolewa na wanahistoria wenye msimamo na fikara za kimapinduzi. Hii ina maana kuwa wanahistoria wa kimapinduzi sharti watazame na kuchunguza vipya, tena kwa utafiti mkubwa, shabaha na misimamo ya wanahistoria ambao walitaalamika juu ya historia ya Afrika katika wakati wa ukoloni; pamoja na lengo la kuandika na kufundisha somo la historia.

Ukweli wa mambo ni kuwa vita hivyo vilivyopigwa na wananchi baada ya ukoloni kuingia havikuwa maasi. Vilikuwa vita halisi vya ukombozi kutokana na minyororo ya ukoloni. Mbali ya kuwa na lengo wananchi waliohusika na vita hivyo walikuwa na mipango halisi kuhusu vita, mbinu na utaratibu wa kupigana. Kwa maneno mengine, vita havikupigwa holela. Imani ya maji, kwa mfano, ilikuwa na makusudio mawili; kuwaunganisha wananchi kuwa wamoja na wenye shabaha moja. Pili, kuwapa wananchi msisimko wa siasa wa kizalendo na papo hapo kuwafanya washupavu katika mapambano. Tatu, maji yalikusudiwa, na yakasaidia sana, kukuza nidhamu ya kijeshi miongoni mwa wananchi. Wananchi wengi walikusanyika pamoja kwa siri katika kipindi cha maandalio. Hapo ndipo walijifunza jinsi ya kuendesha vita; na jinsi ya kupigana.

Vita hivyo havikuwa maasi kwa sababu serikali za kikoloni ambazo wananchi walikusudia kuzing'oa na kuzitokomeza

hazikuwa serikali halali. Utawala wa kikoloni siku zote ni utawala wa kidhalimu na kwa hiyo ni haramu. Utawala wa kikoloni haukukubaliwa na wananchi. Wananchi walilazimishwa na wakoloni kuutambua utawala wao japokuwa kwa shingo upande. Na hii ni dhahiri kuwa wakoloni, iwapo walikuwa ni watu wa kutazama mbali na mbele zaidi, kusema kweli hivyo ndivyo walivyokuwa, walitambua na walitazamia kuwa wakati wowote ule wananchi wangeamua kupambana nao kwa shabaha ya kurudisha uhuru na hadhi ya utu wao na wa Waafrika wote. Shabaha ya wananchi hao ni ile ile ambayo wanasiasa na wapigania uhuru wa kitaifa katika nusu ya pili ya karne ya ishirini walikuwa nayo.

Swali linalopaswa kujibiwa ni kuhusu wakati ambapo uamuzi huo ulitolewa; na sababu zilizowafanya wananchi katika makoloni ya Kijerumani kuwa katika mstari wa mbele zaidi katika kuamua na kutangaza vita hivyo vya ukombozi. Ni wazi kwamba hapakupita muda mrefu sana tangu wakoloni wamalize kazi ya kuziteka jamii hizo za Kiafrika. Hatua hizo za mapambano ya ukombozi zilizochukuliwa na wananchi ziliharakishwa na vitendo vibaya na vya kikatili vya Wajerumani kama watu binafsi na pia kama watawala kwa sababu ya sheria na siasa yao mbaya ya kuendesha makoloni. Hii haina maana kwamba shabaha ya vita hivyo ni kukomesha tu vitendo vibaya na dhuluma ya mabeberu. Vinginevyo vita hivyo vingewahusu watu wale tu ambao walipata kusumbuliwa zaidi na dhuluma hizo pasipo kuungwa mkono na jamii nyingine. Tena wananchi kila walipo wangekuwa wanawashambulia wakoloni wa sehemu yao tu kama walivyofanya wananchi wa miaka ya 1930 na 1940 na vyama vyao vya maslahi.

Katika makoloni ya Kiingereza, juhudi za awali za kujikomboa zilicheleweshwa kwa sababu ya mbinu za kijanja zaidi za Waingereza. Waingereza walikuwa wepesi kujifunza kutokana na makosa ya wengine kama vile Wajerumani. Ndipo wakabuni utaratibu wa 'utawala wa mlango wa nyuma' ambao pia ulikuwa ni wa kikatili na kidhalimu sawa na ule wa Wajerumani na kusema kweli wao ulikuwa mbaya zaidi. Lakini Waingereza hawakuyumbishwa kwa sababu walikuwa sawa na chui katika ngozi ya kondoo. Wao walizidi ujanja. Ukatili wao ulionekana katika vibaraka ambao ni wananchi. Hivi, ilikuwa vigumu zaidi katika kipindi hiki kwa wananchi, na kusema kweli ilichukua muda mrefu sana, kung'amua kuwa ukoloni ulikuwa hasa ndio msingi wa mateso na dhuluma walizofanyiwa; japokuwa ukoloni

wenyewe umechukiwa na kupingwa muda wote.

Siasa ya Wareno ilijulikana sana kama siasa ya asimilado. Siasa ya asimilado ilikuwa na maana kuwa walowezi wa Kireno ambao ni mabeberu walihimizwa kuishi, kuchanganyikana, kushirikiana na kuoleana na wananchi ambao ni Waafronodi. Siasa hii ya Wareno ambayo ilifanikiwa kuyahadaa mataifa katika dunia na kupewa sifa sana na wanahistoria wa wakati wa ukoloni ilikuwa ni ya udanganyifu mkubwa.

Wareno kama wakoloni hawakuweza kuchanganyika wala kuoleana wala kuishi au kushirikiana na wananchi kwa maana halisi ya madai yao. Bali waliishi pamoja kwa mpango wa ukoloni, yaani, wananchi wakiwa ni tabaka la wanyonge. Walowezi wa Kireno wakiwa ni 'mabwanamkubwa', yaani, tabaka la wanyonyaji hawakuoleana na wananchi wenye asili ya Kiafronodi. Bali kama kawaida yao walifanya mapenzi na wasichana wa Kiafronodi na kuwazalisha Machotara. Kitendo hicho kilihimiza na kuendeleza tabia mbaya ya umalaya tabia ambayo ni kinyume cha utamaduni wa Kiafronodi. Kielelezo kifuatacho ni ushahidi mkubwa kukanusha na kupinga madai yasiyo na msingi ya siasa ya 'asimilado' ya Wareno; siasa ambayo ilikuwa ni mbinu za kuhalalisha na kuendeleza unyonyaji wa Kireno chini ya mpango wa ukoloni-mkongwe. Hii yote inatokana na umaskini; na pia na utovu wa maendeleo ya aina zote katika Ureno kulinganisha na mataifa mengine ya kibeberu. Na kwa sababu hii Wareno huendelea kung'ang'ania makoloni yao kama makupe hadi leo wakati mabeberu wengine wamebadili mpango wao wa ukoloni.

Kielelezo* hiki ambacho kinahusu suala la kuchanganyikana na kuoleana katika Angola ni kithibitisho mahususi cha kuonyesha kwamba madai ya Wareno kuhusu siasa yao ya asimilado si ya kweli. Mwaka 1954 jumla ya wanaume 158 walifunga ndoa za kiserikali. Kati yao kulikuwa na Wayuronodi 131, Machotara 17 na Waafronodi 10.

Wanaume	**Wanawake**	**Idadi.**
Wayuronodi	Waafronodi	—
Wayuronodi	Machotara	18
Wayuronodi	Wayuronodi	113
Machotara	Waafronodi	1
Machotara	Wayuronodi	1

* Institute of Race Relations, *Angola: A Symposium (view of Revolt)*, London, Uk. 60

Machotara	Machotara	15
Waafronodi	Wayuronodi	—
Waafronodi	Machotara	2
Waafronodi	Waafronodi	8

Kutokana na kielelezo hiki ni wazi kuwa Wayuronodi walioana wao kwa wao, kadhalika Machotara na Waafronodi. Lakini kwa kuwa kulikuwa na Machotara 26,335 mnamo 1950 katika Angola ni dhahiri pia kuwa Wareno waliwaingilia sana mabinti wa Kiafronodi; uhusiano ulikuwa wa mkondo moja tu.

Wafaransa na Wabelgiji katika Afrika walifuata siasa ya aina moja katika kuendesha makoloni yao. Siasa yenyewe ni kuwazaa 'Wafaransa wa Kiafronodi'. Wayuronodi na Wasanodi ndio waliosadikiwa kuwa ni watu halisi na bora. Waafronodi walifanywa nusu watu. Baadhi ya Waafronodi katika mikondo ya elimu wakapewa gredi ama hadhi ya kuitwa Wafaransa au Wabelgiji, maana yake, ni kuwa sawa na Wayuronodi au Wasanodi ambao ndio peke yao walisadikiwa wamefikia hali ya utu kamili. Waafronodi hao wachache nao wakafanywa kuwa ni watu sawa na bora, ingawa kwa maslahi yao wenyewe, yaani, wakoloni.

Waafronodi hao, kwa sababu ya kasumba na unyonge wao, walifurahia sana kitendo hicho cha wakoloni cha kuwafanya wao watu zaidi kuliko wananchi wengine. Bila ya kuzinduka na kutambua hila ya wakoloni wakausifu na kuuonea fahari kubwa mpango huu. Je, hao walikuwa akina nani? Hawakuwa wengine bali vibaraka hodari na mateka wa wakoloni. Wengi wao walilowea huko Ufaransa na Ubelgiji. Wachache wao wakateuliwa, ikiwa ni mbinu ya kucheleweshe mwamko wa siasa ya kitaifa, kama wabunge katika mabaraza ya kutunga sheria ya huko Parisi na Bruseli. Sheria hizo ziliwahusu na zilikuwa na shabaha ya kuwakandamiza wananchi katika makoloni.

Shabaha ya wakoloni katika kuwateka Waafronodi hao ilikuwa ni kutekeleza siasa yao kuu ya "uwagawanye upate kuwatawala". Waafronodi waliopandishwa hadhi kufikia, kwa lugha yao wenyewe, kiwango cha "utu kamili" hawakujua wafanyalo, kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine, wakoloni hawakuweza kuwatambua Waafronodi hao katika mienendo yao ya maisha kama ni watu wenye utu kamili kama wao, yaani, kulingana na Wasanodi na Wayuronodi, kuweza kustahili heshima na maslahi sawa na raia wengine wa asili ya Kisanodi

na Kiyuronodi. Uraia wao ulikuwa kilemba cha ukoka. Hata hivyo, wakoloni: Wafaransa na Wabelgiji, walifanikiwa sana kwa siasa hii. Matokeo ni kwamba baadhi ya viongozi wa siasa wa Kiafronodi katika nchi zilizotawaliwa na mataifa hayo, yasemekana, walidiriki hata kukataa uhuru wa kujitawala na kupendekeza kuwa nchi zao zingebaki kuwa majimbo tu ya Ufaransa au Italia na kadhalika. Hicho ni kitendo cha usaliti ambacho asili yake ni ujinga, kutojiamini na unyonge. Hata hivyo, Wafaransa kwa sababu ya kukwepa lawama kutokana na ukoloni-mkongwe na kwa sababu ya kupendelea ukoloni-mamboleo ilibidi watoe uhuru kwa nchi hizo kwa nguvu ikiwa kinyume cha matakwa ya viongozi wa siasa wa nchi hizo dhidi ya matakwa ya wananchi. Viongozi hao hulia na kusononeka zaidi kushinda hata wana-ndugu wakati mmoja wa mabwana zao anakufa; na wakati huo huo kuonyesha utovu wa huzuni wakati maafa na misukosuko inapowapata viongozi na wana-mapinduzi katika nchi huru za Kiafrika; au katika nchi zinazopigania uhuru wa nchi zao.

Wakoloni wote kwa ujumla waliendesha siasa ya aina moja. Kuwagawanya wananchi ili kuwatawala. Waingereza, Wafaransa, Wareno, Wabelgiji na kadhalika, wote waliendesha siasa hiyo. Sheria zote zilizotumika katika makoloni zilisawadiwa na kupitishwa na mabunge ya wakoloni makwao. Kwa mfano, sheria nyingi zilizotumika katika makoloni ya Kiingereza zilikuwa na msingi wake wa utamaduni: mila na desturi za Waingereza wenyewe.

Wakoloni wote kwa ujumla walitumia na kuzingatia sana kasumba ya kihamati, yaani, kumfanya Myuronodi na Msanodi aonekane mtu bora zaidi kuliko Mwafronodi na huu umekuwa ndio msingi mkuu wa ubaguzi wa rangi. Wote waliendesha siasa ya kuuma na kupulizia[2]. Hii ina maana ya kuwafanya Waafronodi kuwatambua, kuwatii, kuwatukuza na kuwategemea Wayuronodi kama wafadhili na wazazi wao. Hilo walitekeleza kwa mafanikio makubwa sana kwa kutoa vizawadi na bakishishi angalao mara moja kwa mwaka hasa wakati mabeberu walipokuwa wameburudika au wamefurahia maisha. Na mara nyingi hayo yalifanyika nyakati za Sikukuu za Iddi, Pasaka, Noeli, Dola, n.k. Shabaha ni kuwanunua na kuwapumbaza Waafronodi kwa

1. Makala ya Mwalimu Mbakileki kuhusu siasa ya mahakama katika Tanzania aliyoitoa katika semina ya walimu wa Chuo cha Kivukoni, 1973
2. Kuuma na kupulizia — wakoloni walijifanya wazazi wa wananchi ili kujaribu kuficha ubaya wao.

jinsi wajione kuwa wakoloni ni wema na wenye huruma.

Licha ya kunyang'anya ardhi wakoloni waliwalazimisha wananchi kulima mazao yale tu ambayo wao wenyewe waliyahitaji kwa kuendeshea viwanda vyao kama bidhaa-asili. Bei walizopewa wananchi kwa mazao yao zilikuwa za chini sana; na kwamba wakoloni hawakujishughulisha wala kuchukua hatua zo zote kuhakikisha hali njema ya wananchi. Huduma kama vituo vya afya na utabibu, elimu, maji na kadhalika, zilikuwa chache sana na mara nyingi huduma hizo zilitolewa karibu na sehemu walizoishi wakoloni wenyewe.

Wakoloni waliua moyo wa utafiti na kujiendeleza wa Waafronodi katika mambo mbali mbali. Ngoma, michezo na nyimbo za Waafronodi zilikashifiwa. Badala yake ngoma, michezo, nyimbo, tabia, mienendo, n.k. ya kikoloni ikahimizwa. Yasemekana kuwa Mwafronodi ambaye alithubutu kuonyesha maarifa fulani ya ufundi, kwa mfano, kutengeneza zana kama bunduki, baiskeli n.k. mara nyingi alikabiliwa na adhabu kali ya kukatwa sehemu ya viungo vyake. Viungo hivyo mara nyingi vilikuwa ni mikono. Kwa njia hii Waafronodi walitiwa hofu na hatimaye kuacha kujishughulisha na elimu ya ufundi na utafiti wa aina zote. Vile vile utaalam wa kiufundi ulikufa kwa sababu vyombo ambavyo Waafronodi walivihitaji; kwa mfano: majembe, mashoka, mapanga, visu na kadhalika viliweza kutengenezwa na wakoloni kwa wingi katika viwanda vyao na kuwauzia Waafronodi.

Wakoloni hawakuwa na haja ya kuendeleza maisha ya wananchi. Mabarabara mazuri yalijengwa mijini kwa sababu ya kuwapatia raha wakoloni wenyewe. Sehemu za wananchi na mashambani njia za uchukuzi zilikuwa chache na mbaya sana. Mara nyingi zilielekezwa katika sehemu ambako bidhaa-asili zilipatikana. Wananchi walilazimika kutembea mwendo mrefu sana na mizigo kichwani ili kufikia vituo vya njia za uchukuzi na mawasiliano . Mara nyingi wananchi walishindwa kuendeleza kilimo . sababu mazao yao hayakuweza kufikishwa kwenye masoko amb· yo yalikuwa machache na mbali.

Sheria za wakoloni popote katika makoloni yao zilikuwa za kikatili na za kukandamiza. Wananchi hawakuelezwa, kwa mfano, kwa nini walilazimishwa kuchimba vyoo. Maarifa kuhusu kilimo bora, chakula bora, afya bora na utamaduni wa kazi hayakutolewa.

Kisiasa wananchi walinyimwa kila nafasi ya kushiriki na kujiendeleza. Wakaanzisha 'Utawala wa Mamlaka ya Wananchi,' yaani, utawala wa mlango wa nyuma ili kuhakikisha kuwa

mapambano yote ya kisiasa ya Waafronodi yanakomea huko. Na kwa njia hii waliweza kuwazuia Waafronodi kushiriki katika serikali ya 'mamlaka ya kati'. Wakoloni, wote kwa ujumla, walikuwa wabaguzi wa rangi japokuwa tabia hiyo haikuonyeshwa waziwazi na kwa uzito mmoja. Baadhi yao walionyesha waziwazi ubaguzi wao, wengine waliendesha ubaguzi huo kisirisiri. Elimu na madhehebu ya dini vilikuwa vyombo muhimu sana vya kuendeleza ubaguzi na mtengano wa wananchi. Pia elimu na vituo vya matibabu ambavyo mara nyingi viliendeshwa na mashirika ya Kikristo vilikuwa vyombo vya kununulia roho za Waafronodi. Kwa hiyo, wananchi ambao walionyesha msimamo thabiti kuhusu imani zao, kama waislam au waumini wa dini zao za jadi, walizikosa au walizipata kwa taabu sana huduma hizo. Matokeo yake ni tofauti kubwa ya maendeleo baina ya Waafronodi waliozingatia msimamo wa madhehebu yao na wale ambao waliamua, kwa sababu moja au nyingine, kujiunga na mashirika ya Kikristo na kunufaika na huduma zake.

Sura ya 12

WAMISIONARI NA UKOLONI: VIONGOZI WA DINI WANANCHI NA UJENZI WA MATAIFA YAO

Madhumuni ya sura hii ni kujaribu kutoa maelezo ya msingi kuhusu mwenendo, matendo, na siasa ya wamisionari wa madhehebu mbali mbali katika kipindi cha ubeberu na ukoloni. Ni makusudio ya mwandishi pia kujaribu kuonyesha uhusiano baina ya watawala, wamisionari na walowezi (mabepari na makabaila) wa kikoloni, kwa upande mmoja; na wananchi, kwa upande wa pili. Kwa kufanya vile mwandishi hana shabaha ya kuunda chuki na uhasama kati ya viongozi wa dini na waumini wao kwa maana kazi ya wamisionari karibu imekwisha.

Lawama zitakazotolewa katika sura hii zichukuliwe kwa moyo mkunjufu kama ni makosa ya kihistoria ambayo yalipata kutokea; na kwamba kutokana na makosa hayo tunaweza kujifunza jinsi ya kurekebisha mambo. Kwa hiyo, lengo kubwa ni kujaribu kuwasaidia viongozi wa madhehebu kutambua makosa hayo ya kihistoria ili kuchukua hatua muhimu na zifaazo kuzijenga imani hizo upya katika misingi ya kitaifa. Na kwamba haina budi kufahamika kuwa kama kuna dosari, basi, dosari hizo hazitahusu imani bali waenezi wa imani hizo kama watu. Wamisionari na wakoloni, kwa ujumla, walitumia imani kwa ajili ya manufaa yao wenyewe kama watu, hasa kiuchumi na kisiasa. Dini ambazo ni vyombo vya kumwezesha mtu kufika peponi zilithaminiwa zaidi kuliko utu wa Mwafronodi mwenyewe ambaye ndiye aliyekuwa na haja ya kusaidiwa na vyombo hivyo, yaani, dini. Pamoja na mashtaka yatakayotolewa wamisionari hawana budi kutambuliwa kwa huduma zao nyingi, japokuwa misingi na shabaha za huduma hizo hazikuwa za kumwendeleza Mwafronodi.

Silaha kubwa ya wakoloni ni siasa yao ya kuwagawanya watu katika matabaka, makundi na vikundi vya kihasama. Waliofanikisha sana utekelezaji wa siasa hiyo ya mgawanyo na ubaguzi miongoni mwa jamii za Kiafronodi ni wamisionari wa dini za

imani zote: Wahubiri Kurani na Wahubiri Enjili. Wamisionari hao wa aina zote mbili wanaweza kushtakiwa kwa uhalali kabisa kwa kosa la kuandalia, kuhudumia na kuendeleza ukoloni katika Bara la Afrika.

Katika Afrika wamisionari hawakuwa tofauti na walowezi wengine wa Kiyuronodi au Kisanodi na watawala wa kikoloni. Kusema kweli wote walikuwa wakoloni na wanyonyaji. Hata hivyo, wamisionari walikuwa katika mstari wa mbele zaidi katika kuandalia njia ya ukoloni na kuhakikisha kuwa Waafronodi wanatawalika na wanayonyeka vema. Na wao wenyewe, yaani, wamisionari, walishiriki katika shughuli nzima ya kunyonya.

Huko Afrika Magharibi wanahistoria wanatuambia kuwa baadhi ya wamisionari walijiingiza katika shughuli ya biashara ya watumwa*. Waliwatumia watumwa japokuwa kwa kisingizio kuwa watumwa hao walikuwa watu huru. Ni vigumu kuelewa maana ya uhuru wao. Labda uhuru katika maana kwamba wananchi hao hawakuuzwa kwa wanyonyaji wa Ulaya, Marekani na sehemu nyingine za dunia.

Vile vile wamisionari walimiliki sehemu kubwa ya ardhi walizozinyang'anya kutoka kwa wananchi aidha kwa hila au kwa kugawiwa na serikali dhalimu za kikoloni. Ardhi walizochukua mara nyingi zilikuwa ni ardhi zenye rutuba na ambazo zingeweza kustawisha siyo mazao tu ya chakula bali hata mazao ya biashara. Maana wamisionari hao hawakuwa wajinga. Walitaalamika sana; na hasa kwa kuwa wengi wao walifika Afrika ya Waafronodi katika kipindi ambapo ubepari ulikuwa umeanza au umekwisha kukomaa. Hao walikuwa wamisionari wa madhehebu ya Kikristo. Wamisionari waliwatoza kodi wananchi wote walioishi katika maeneo yao ambayo waliyaita ni nchi huru. Hata hivyo, mara nyingi siasa ya wamisionari ilikuwa ni kujitenga na umma wa waumini wao ambao muda wote waliachwa wakikabiliwa na unyonge: umaskini, maradhi na ujinga. Na wakati wowote walipoonelea, kwa sababu fulani hawakukubaliana na wananchi katika eneo lao hata kama kutokubaliana huko kulikuwa katika msingi wa kiroho au kimsimamo, waliweza kuwafukuza wananchi hap pasipo hata kuwapa nafasi ya kujitetea wala kulipwa fidia kwa mali zao. Walikuwa na malori ya uchukuzi, maduka ya biashara na viwanda vya taaluma mbali mbali. Mara nyingi wazalishaji mali katika viwanda hivyo hawa-

* J. Duffy, *Portuguese Africa*, Cambridge (Massachusetts)

kulipwa ujira wa haki. Na mara nyingi wataalam wa viwanda vyenyewe walikuwa ni wananchi wenyewe kama mafundi waliolipwa ujira wa chini au kama wanafunzi wasiolipwa; na ambao (wanafunzi) walijilisha wenyewe kwa kukuza mifugo na kulima mashamba makubwa ya wamisionari hao.

Pasipo wamisionari, hasa wa madhehebu ya Kikristo, mpango mzima wa ukoloni usingekuwa na mafanikio makubwa. Wamisionari walitumia imani ya dini kwa kuwapika kasumba au kwa maneno mengine, kuwapumbaza wananchi kusudi wapate kutawalika na kunyonyeka kirahisi. Waliwawekea miiko ya vitisho ambayo matokeo yake ni kumlaza Mwanaafronodi. Kwa mfano, waliwafundisha wananchi kuwa utajiri, yaani, mali, ni dhambi, na kwamba ili mtu afike peponi sharti anyenyekee, awe fukara na mnyonge. Mfano wa tajiri na Lazaro, ngamia na tundu la sindano, n.k.; ilikuwa ndiyo vielelezo vikubwa vya kupikia kasumba. Wananchi waliogopa kujenga nyumba nzuri na kuvaa vizuri maana maisha bora yalielezwa kuwa ni maisha ya anasa na ufahari. Japokuwa woga huu wa Waafronodi ulisababishwa pia na imani ya kichawi ambayo asili yake ni ujinga. Na kinyume cha mahubiri yao wakanyonya mali-asili, nguvu na jasho la wananchi kwa kuwatumikisha pasipo ujira au kwa ujira kidogo zaidi mno kuliko hata ujira uliotolewa na serikali, watawala, makampuni ya mabepari na makabaila. Watumishi wao mara nyingi walikufa kifo cha punda. Hawakuwa na hifadhi ya maisha. Na kwamba mara nyingi watu waliowafanyia kazi waliishi maisha ya kitumwa zaidi. Wamisionari waligeuka (kwa kujifanya) kuwa baba na mama, walinzi na wafariji wa wananchi wanyonge. Na hii ilifanyika wakati ule tu watumishi hao wa Kiafronodi walipoonekana na afya bora. Na hii inaeleweka! Mara nyingi Waafronodi walitwikwa dhambi ambazo hazikuwa dhambi ili tu mradi wawatishie kuwa dhambi zao zisingeondolewa kwa kuwazuia sakramenti ya kutubu mpaka wamefanya 'malipizi ya wazi'. Malipizi ya wazi maana yake 'wakosefu hao', hata kama walitoka maili arobaini, walilazimika kufanya kazi ya kujenga maboma ya wamisionari, maboma ya wanyama wao pamoja na makanisa kwa kipindi walichokikadiria wao. Lakini kabla ya kazi ilibidi kuhudhuria misa (ibada) kuanzia mnamo saa kumi na mbili mpaka saa moja alfajiri; na mumo humo kanisani walipikwa kasumba kali sana. Adhabu hizo walizopewa wananchi zilikuwa na shabaha ya kuwafedhehesha, kuwashushia hadhi yao na juu ya yote kuonyesha nguvu ya ukoloni na kuwanyonya kijanja.

Wamisionari kama wakoloni wengine, walikuwa watawala na mahakimu wakubwa. Waliweza kuwachapa viboko na makofi wananchi wa umri na rika yoyote bila aibu. Katika sehemu za mashambani walichukua jukumu, mamlaka na madaraka ya serikali ya kikoloni. Walipelekewa wahalifu nao waliweza kuwapelekea wahalifu hao barua za 'kuitwa shaurini'. Wananchi walilazimika kutii. Waliweza kupitisha hukumu kadiri walivyopendezewa isipokuwa kifungo cha jela, faini au kunyonga. Kama shauri lilikuwa kubwa basi waliweza kuyalazimisha mamlaka ya wananchi kumpiga au kumsafirisha hadi bomani kwa D.C. ambako aliweza, kutokana na ushauri wao, kufungwa au kupata adhabu nyingine iliyolingana na hiyo.

Ilikuwa ni jambo la kawaida kwa wamisionari kuwalazimisha au kuwatazamia wananchi, kinyume cha mahubiri yao, kuwabeba wavukapo mito; na kuwabeba katika machela wanapokwenda katika safari za mbali. Waliwakataza Waafronodi kuvaa viatu maana viatu vilihesabiwa kama umaridadi na ufahari wakati wao wenyewe wakivaa viatu safi vilivyoshonwa na kung'arishwa na watumishi wa Kiafronodi. Wamisionari hawakuwa na aibu. Ijapokuwa walifundisha kuwa amri kuu ya Mungu ni mapendo, yaani, 'umpende mwenzio kama unavyojipenda mwenyewe'. Wao walikuwa ndio wavunjaji wakubwa wa amri hiyo. Wakati wananchi ambao ni watumishi wao wanateseka na kufa kwa njaa wao wanacho chakula kutosha na kuzidi kilichozalishwa na hao wananchi wanyonge. Masalia ya chakula hutupwa au kuwapatia mbwa na nguruwe. Mbwa walilishwa katika sahani safi. Nguruwe na ng'ombe walijengewa nyumba safi, kubwa, zenye madirisha na hewa ya kutosha wakati watumishi wao wanawalaza katika vibanda visivyo na madirisha wala hewa. Mapendo yalikuwa na maana kuwa Mwafronodi ambaye ni maskini atoe hata kile kidogo alicho nacho awaongezee matajiri ambao ni Wasanodi na Wayurunodi. 'Mpeni Kaizari kilicho chake na Mungu kilicho chake' — kodi na utumishi wa kunyonywa vilihesabika kuwa ndiyo mali ya Kaizari. Kidogo hicho ni matunda, mayai, mahindi, fedha, jasho na nguvu. Tabia hii imejenga katika mioyo na fikara za waumini wengi ambao kusema kweli mara nyingi ni watu walio maskini na wanyonge. Matumaini yao ni maisha ya 'baadaye' yaani, peponi, na katika wingi wa watoto pasipo hata kujali hali, afya na huduma za watoto wenyewe. Mara nyingi utasikia: "Mungu akupe nini. Amekujalia watoto". Watoto walikuwa, mpaka sasa, ndiyo hazina, yaani, kitulizo na faraja ya

Waafronodi ambao ni wanyonge. Tegemeo la wanyonge hao ni maisha bora baada ya kufa, yaani, faraja ya milele huko mbinguni. Imani hii ni mbaya sana nayo ni chanzo cha unyonge na maisha duni ya wananchi kwa sababu inaimarisha uvivu wa kazi na kufikiri mipango halisi ya kupambana na matatizo. Badala ya kufundisha watu njia bora za kuzalisha mali ili kustawisha uhai na afya zao wamisionari na mashehe waliwafundisha wananchi kutumia muda mrefu katika sala, kutubu dhambi, kujikomba kwa wakubwa wao, kupigiana majungu na hata kupigania makombo. Hawakuwahi hata mara moja kuwaeleza wananchi kuwa heshima ya binadamu ni kazi na kujitegemea. Badala ya kujenga majengo makubwa kwa ajili yao (wamisionari wa Kikristo) ambayo leo hayana faida wangeweza kabisa kuwasaidia watumishi wao hata kwa njia ya mikopo kujenga vijumba vya kisasa. Na kwa jinsi hii wangeweza kupata shukrani na upendo wa dhati kutoka kwa waumini wao.

Wamisionari walifanikiwa sana katika mpango wao wa kuhudumia na kuulinda utawala wa kinyonyaji na kidhalimu wa kikoloni kwa sababu moja kubwa. Nayo ni utii wa woga walioujenga taratibu katika mioyo ya wananchi. Kwanza kabisa, waliwafundisha wananchi kuwa kumtukana, kumpuuza, kumdharau, kumbishia au kumpiga mmisionari au mtawa yeyote; Padure, Bruda na Mama na Shehe, ilikuwa ni dhambi ya mauti kwa maana, ilielezwa ilikuwa sawa na kumtukana au kumpiga Mungu mwenyewe. Kwa sababu watawa na mashehe walisadikiwa kuwa ni 'watoto wa Mungu'. Kitu kingine kilichowafanya wananchi wawaogope Mapadure na Mashehe ni imani kuwa watu hao walikuwa na uwezo wa kuwadhuru watu kwa sala na majini. Mafundisho hayo yalikuwa na shabaha ya kuwalinda na kuongeza hadhi na heshima ya wamisionari wenyewe; na pia kuwafanya waonekane machoni mwa wananchi kama vimiungu vidogo vidogo. Mavazi yao, miondoko au miendo yao, zungumza na lafudhi yao yote ilielekezwa kwenye lengo hilo. Na kwamba yote yalikuwa na shabaha ya kujilinganisha na makabaila wa Ulaya na Uarabuni. Wananchi wote kwa ujumla wakageuzwa kuwa duni, watoto wadogo na wachanga wanaomtegemea mzazi. Kutokana na nidhamu hii ya juu, wamisionari waliweza kusikika na kupata heshima kubwa zaidi kuliko walivyostahili; na pia walipewa heshima kubwa zaidi kuliko waliyopata wakoloni wengine. Baada ya kujenga nidhamu hiyo waliendelea kuwafundisha wananchi kuwa ilikuwa ni dhambi kupenda raha, furaha, mali, cheo na heshima. Kwa

maneno mengine, Waafronodi walifundishwa kuukana unafsi wao; na kuwafanya waamini kuwa heshima, furaha, cheo, na mali vyote vilikuwa haki ya pekee ya Wasanodi na Wayurunodi. Imani hii ya kuridhika na kungojea tuzo na faraja huko peponi ndiyo msingi mkubwa wa unyonge wa Mwafronodi katika kipindi hiki cha ukoloni, na hilo limebaki tatizo hata baada ya kujitawala. Imani hii inazuia na kupinga hatua zote za maendeleo ya kimapinduzi hata katika nchi huru. Wananchi wanahitaji kukombolewa kwa upande huu. Ukombozi huo hauna maana ya kukana dini bali ina maana kuwa madhehebu yenyewe yaanze kuchukua hatua muhimu za kujikomboa kwa kuanza kuondoa na kufuta pole pole fikara hizo za kumlaza Mwafronodi na kumfanya amtegemee Myuronodi na Msanodi. Wamisionari wangeweza kupongezwa sana kama wangeweza kujenga imani zao juu ya msingi wa maisha ya uyakinifu[1] badala ya kusisitiza juu ya maisha ya udhanifu[2] ambayo yanaweza kuwepo au yasiwepo. Hata kama yapo Mungu aliwaumba watu na akawakabidhi dunia kuitawala. Mwili wenye afya huhifadhi roho yenye afya. Mwili mnyoofu huhifadhi roho nyonge pia. Hayo ndiyo maoni ya mwandishi.

Kanisa, wala Bakwata, halitaweza kuchukua hatua muhimu za kujikomboa mpaka kwanza limetatua tatizo la kutegemea misaada ya Roma, Marekani, Kantebari[3] na Maka. Kujitegemea kwa kanisa au Bakwata siyo kukana imani tulizoletewa na wageni; na wala siyo kuanzisha imani mpya na wala siyo kukana misaada. Kujitegemea kuna maana ya kutambua, kwa nafasi ya kwanza, kuwa kazi ndio msingi wa maisha na maendeleo ya jamii. Vile vile kutambua kuwa imani ni kwa ajili ya kuokoa 'roho' za watu. Ili kuweza kupata waumini wa dhati hapana budi kwanza kuhakikisha kuwa waumini wenyewe ni watu wenye akili safi na timamu. Watu hawawezi kuwa na akili safi mpaka wamekuwa na afya bora. Na afya bora ni matokeo ya utabibu, neema na ubora wa chakula, malazi bora, mavazi bora na safi; na hayo yote huletwa na kitu kazi. Uchaji wa watu maskini siyo wa dhati sana maana unatokana na unyonge na kukata tamaa ya maisha kwa sababu ya kushindwa kutatua matitizo ya kimwili,

---

1. Maisha ya uyakinifu – Maisha halisi na ya kweli ambayo mtu anaishi hapa duniani.

2. Maisha ya udhanifu — Maisha ya baadaye ambayo mtu hana uhakika nayo bali hutegemea mafundisho ya imani ya dini yake.

3. Kantebari — Ni makao makuu ya Kanisa la Kiangalikani huko Uingereza.

kijamii na kiuchumi. Kwa hiyo, basi, mwili dhaifu na mnyonge husababisha udhaifu wa akili na roho, maana mtu hawezi kuwa na nguvu au afya bora kuweza kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa jinsi, kwa mfano, malaika wa mbinguni ambao hawana dhiki wala matatizo wanavyoweza kumtukuza kwa maisha yao yote.

Mungu anapenda kuziona roho zenye afya njema na ambazo zimejawa na furaha. Na hii inawezekana tu iwapo mwili ambamo roho inaishi una afya. Mungu mwenyewe alimwagiza Adam, "utaishi kwa jasho lako"; maana yake: utaishi kwa kutumia akili na jitihada yako. Kwa ufupi, Adam aliambiwa angeishi kwa kazi. Lakini kwa bahati mbaya maelezo hayo yaliambatanishwa na kosa lake Adam lijulikanalo kama 'dhambi ya asili'. Kwa jinsi hiyo maana ya kazi imepotoshwa. Kwa Adam, kazi, japokuwa ilikuwa ndiyo msingi wa maendeleo yake na ya vizazi vyake, ilikuwa pia ni laana.

Wamisionari wa Kikristo walikuwa viongozi wa dini lakini papo hapo walikuwa raia wa nchi za kibepari na kibeberu. Na kwa sababu hiyo kuhudumia na kupigania kudumu na kuendelezwa kwa mfumo wa ubepari na mpango wa ukoloni kulikuwa ni sahihi kwa upande wao; na kwamba walikuwa katika mstari wa kunyooka kama watu japokuwa kiimani walipotoka.

Leo nchi nyingi zimejitawala katika Afrika. Sehemu kubwa ya nafasi, pamoja na uongozi wa juu, za wamisionari wa imani zote zimejazwa na wananchi. Hao wanaongoza makundi makubwa sana ya wananchi kiroho. Ni viongozi. Makasisi na Mashehe ni raia wa nchi huru za Kiafronodi. Wana na ndugu wa Waafronodi. Wamelelewa na kukulia katika mazingara ya Kiafronodi. Watu wanaowaongoza ni Waafronodi ambao wana utamaduni wao wa asili; wana mila, desturi na thamani za maisha za Kiafronodi.

Lakini wahubiri hao kwa sababu ya elimu waliyopewa chini ya ukoloni wamejawa, kama viongozi wengine, na kasumba za kimisionari ambazo, kusema kweli, ni kasumba za kikoloni. Hawana uchaguzi bali kukiri kuwa wao ni Waafronodi, pia ni viongozi; na kwamba ni raia wa nchi huru za Kiafrika. Baada ya hapo hawana budi kukiri na kuchukua jukumu la kutetea siasa za nchi zao ambazo zina shabaha na madhumuni ya kuwatoa wananchi katika unyonge ili kustawisha maisha yao; kuwapatia faraja na kitulizo. Faraja hupatikana tu iwapo kuna shibe, afya bora kutokana na chakula bora na huduma za utabibu, na pia

kutokana na elimu kwa watu na taifa zima. Mambo hayo yanaweza tu kufikika iwapo viongozi wa imani za madhehebu mbali mbali wataungana na viongozi wa vyama vya siasa na serikali za kimapinduzi za nchi zao. Shabaha ya kufanya vile ni kuleta maendeleo ya walio wengi, yaani, maendeleo ya watu kwa ujumla na wala si kwa manufaa ya wachache au vikundi.

Katika Afrika, Asia na Latini Marekani siasa ya pekee ya kuleta mapinduzi ya watu ni siasa ya Ujamaa. Siasa ya kibepari iliwalaza Waafronodi, ikawafanya wasijiamini, ikawaondolea uwezo, heshima ya kiutu, ikawaingiza katika umaskini, ikaendeleza ujinga wa Waafronodi na matokeo ya yote hayo yakawa ndiyo unyonge wa Mwafronodi.

Makasisi ambao walipata makombo ya kutosha ya wamisionari katika mfumo wa kibepari chini ya mpango wa ukoloni hawana budi kutambua kuwa wao wenyewe, yaani, makasisi na mashehe, kama wasomi wengine, waliandaliwa kuendeleza mfumo wa kitabaka wa kibepari na mpango wa ukoloni-mambo-leo. Mpango huo ambao mabeberu waliubuni katika karne ya kumi na tisa una uwezo mkubwa sana wa kunyonya; na zaidi sana unashinda mara dufu unyonyaji pamoja na fedheha iliyopata kuletwa na mpango wa ukoloni-mkongwe.

Karibu madhehebu ya imani zote makao yake makuu yako katika nchi za kibepari. Nchi hizo ndizo zinazoimarisha ubeberu. Ubeberu hauna huruma wala utu. Ubeberu ni adui wa maslahi ya walio wengi. Unapinga kabisa siasa ya kujitegemea ambayo ni msingi wa maendeleo ya wanyonge. Mashirika mbali mbali hutoa, baada ya kuombwa na kubembelezwa kwa unyenyekevu na unyonge, misaada si kwa ajili ya kuendeleza imani za madhehebu bali uhai na maisha bora ya wale waliowaandaa kuendeleza mfumo wao. Misaada hiyo ambayo hutegemewa sana, na kusema kweli huishi kwa hiyo tu, na viongozi wa madhehebu fulani fulani hasa ya Kikristo ina hatari nyingi.

Kwa hiyo, kujikomboa kwa madhehebu ni kuanza kuendeleza fikara na mipango ya kujitegemea badala ya kutegemea misaada. Hata hivyo, hapana budi kufahamika misaada ya aina moja au nyingine – yaani, kubadilishana misaada kati ya watu au mataifa yanayojitegemea - si jambo baya. Lakini iwapo taifa au jamii itaishi kwa kutegemea zaidi misaada ya wakubwa ni dhahiri kuwa taifa au jamii hiyo itakuwa imetekwa na kuingizwa katika unyonge. Viongozi wa madhehebu mbali mbali katika Afrika wamesahau jambo hilo maana mpaka sasa hawajaazimia kuanzisha mipango ya kimapinduzi ya kiuchumi, kifikara na ya

ustawi wa jamii kwa ujumla. Wametanguliwa na wanasiasa katika kufikiria maisha bora ya watu. Hata hivyo, wanayo nafasi kubwa ya kuchukua jukumu la kupanga mipango ya maendeleo ya watu ili kuwatoa Wanaafronodi katika unyonge. Kimwili Waafronodi hudharauliwa na kubaguliwa na mabeberu. Kiroho pia hubaguliwa na ndiyo maana kuna sehemu na saa tofauti za kuabudu kwa Waafronodi na kwa Wasanodi au Wayurunodi japokuwa hali hii huvumiliwa siku hizi katika sehemu nyingi. Hali na tabia hii ya ubaguzi msingi wake ni tofauti na ubora wa maisha kati ya jamii zilizoendelea kiuchumi ambazo ni za Kiyuronodi na jamii za Kiafronodi ambazo bado zinaishi katika umaskini na unyonge. Njia ya pekee ya kuwaunganisha watu wa jamii hizi mbili kiroho ni kuweza kuondoa tofauti za maisha ya kimwili baina ya jamii hizo. Na hii inahitaji kazi kwa vitendo na wala siyo maneno. Wakati wa maneno umepita.

Katika Afrika kazi ya kueneza Kurani au Uislam ilifanywa, kwa mara ya kwanza na katika sehemu kubwa ya bara hili, na Wasanodi. Wasanodi hao, tofauti na wamisionari wa Kikristo, walikuja Afrika kama wachumi, yaani, kama wafanya biashara. Katika sehemu nyingine Uislam ulienezwa na wafanya biashara wa Kiafronodi ambao walipata kuzitembelea sehemu za Asia kwa minajiri ya biashara.

Tangu mwanzo waenezi wa imani ya Kislam waliruhusu na kuhimiza ubaguzi wa rangi. Misikiti tofauti ya ibada ilijengwa kwa ajili ya jamii za Kihindi, za Kiarabu na za Kiafronodi. Japokuwa mtengano huu ulikuwa katika misingi ya tofauti za imani ya madhehebu ya Kiislam ya Wahindi na ya baadhi ya Waarabu hayakuacha mlango wazi kwa Waafronodi kujiunga nao.

Kama wamisionari wa Kiyuronodi, hasa wa madhehebu ya Kikatoliki walivyozingatia Kilatini kama lugha ya Mungu, Waarabu walitumia lugha ya Kiarabu kuwatenga wahubiri wa Kiafronodi na waumini wao ambao pia ni Waafronodi kwa shabaha ya kuwalaza na kutukuza utamaduni wa Kiarabu. Mashehe na walimu wa Kiislam, kwa sababu ya kukariri misahafu na lugha ya Kiarabu walijifanya na kuonekana watu bora kuliko waumini wao. Viongozi hao waliifurahia sana hali hiyo ambayo, kusema kweli, ilikuwa ni kasumba. Mbele yao waumini walijisikia wanyonge na wajinga. Hivyo, ni dhahiri kuwa jumuiya ya Waislam iligawanywa katika tabaka la viongozi waliostahiwa na waumini ambao walionekana wanyonge mbele ya viongozi wao.

Kulikuwa na mambo mengine kadhaa yaliyowatenganisha viongozi wa Kiislam, na waumini wao. Kwanza kabisa viongozi wa Kiislamu, hasa mashehe na wengine, walijenga nidhamu ya woga miongoni mwa waumini wao na wananchi wengine kwa ujumla. Mara nyingi mashehe walisadikiwa kuwa wana uwezo wa kuagua na kutibu maradhi ambayo yalisadikiwa kuwa yalitokana na ulozi. Juu ya yote iliaminiwa kuwa mashehe walikuwa wanafuga majini na kuyatumia katika kuwadhuru wananchi ambao waliweza kushtakiwa mbele yao kama waovu. Wakati mwingine mashehe walitumia Kurani kwa kuwadhuru watu; na kitendo hicho hujulikana kama somo la albadiri nacho hulipiwa. Hicho ni kitendo cha uchawi na ushirikina, kwa lugha ya kawaida. Kitendo hicho kiliwatisha sana wananchi, na papo hapo kikakuza utii wa woga kwa viongozi hao; na kwa hiyo, kuongeza heshima ya viongozi mara dufu.

Misikiti ya Kiislam haikuwa mali ya madhehebu bali mali ya shehe au kiongozi wa imani. Kiongozi aliweza kujenga msikiti kwa sababu ya ubora wa hali yake ya uchumi. Hali hiyo bora ni utajiri.

Uwezo huu wa kiongozi kujenga msikiti ulisaidia sana kuongeza heshima na ufahari wa kiongozi. Kama mapadure wa Kikatoliki walivyojitambulisha kwa kuvaa mavazi ya mtindo wa makabaila wa Ulaya, na kutumia lugha yao, mashehe na viongozi wengine wa Kiislam pia walijitambulisha kwa kuvaa mavazi ya mtindo wa makabaila wa Kiarabu wa huko Uarabuni. Utamaduni huo wa kigeni, licha ya kuwapa ufahari, uliwatenga viongozi hao na waumini wao; hata na wananchi wengine.

Kiuchumi viongozi wa Kiislam walikuwa wanyonyaji japo-kuwa unyonyaji wao haukuwa wa hali ya juu sana kuweza kuli-nga-nishwa na unyonyaji wa wamisionari wa Kikristo. Pili licha ya kuwa na msikiti ambao ulikuza sifa na ufahari wao, mashehe, kama walimu, waliendesha madarasa. Vijana wa Kiislam waliokuwa wamejiandikisha katika madrasa walitumiki-shwa na mwalimu wao au shehe kwa jinsi nyingi. Walilazimika kulima mashamba ya mashehe, kuwapasulia kuni wake wa mashehe, kusafisha mazingara ya nyumba za mashehe, kuchunga mifugo ya mashehe na kuwavunia mazao ya mashambani. Kazi ya mikono kwa mashehe ilikuwa ni mwiko na fedheha.

Wakati wa Idd'El-Fitri waislam hutoa sadaka au zaka kwa njia ya mazao au fedha ambayo hukabidhiwa shehe au mwalimu. Fedha hiyo ikiwa ni sadaka, inatakiwa itumike kwa ajili ya watu maskini ambao hawajiwezi. Lakini kinyume chake mashehe

hutumia fedha hizo za zaka kwa manufaa yao wenyewe. Vile vile kwa kuendeleza utamaduni wa Kiarabu mashehe walihimiza kisomo maalum cha mazishi. Kisomo maalum hulipiwa na ndugu wa wanaohusika; nacho hufanana sana na misa ya wafu ambayo mapadure humsomea marehemu, na kulipiwa na ndugu wa marehemu. Japokuwa kunaweza kutolewa mjadala kuhalalisha tabia hii ukweli utabaki kuwa hiyo ni moja ya njia za kumpatia ridhiki yule anayeongoza kisomo au ibada hiyo. Na kwa jinsi hiyo ibada hiyo hugeuka kuwa biashara.

Tabia ya kutoa matanga ambayo hufanyiwa hitima kubwa na Waislam hurudisha nyuma maendeleo ya wananchi. Vyakula vingi hupikwa kwa wingi na kwa fujo, na mara nyingi ndugu wa marehemu hulazimika kuingia katika madeni makubwa ili kutekeleza wajibu huo wa kutoa matanga. Hivyo, basi, ni wazi kuwa kiuchumi na kimaisha mashehe walikuwa na hali nzuri zaidi kuliko waislam wa kawaida. Kutokana na njia hizo zote za kupatia fedha mashehe waliweza kulimbikiza mali na kisha kujijengea majumba ya kupangisha katika sehemu za miji na kuendelea kunyonya.

Suala la hija haliwezi kupita bila kuongelewa. Hija na ziara zote zinazofanywa na Waislam huko Maka na Madina zinaweza kuelezwa kwa njia mbili. Kwanza kabisa ziara hizo zinafanywa na watu ambao wana uwezo tu. Na baada ya kurudi Afrika wahiji hao hujulikana kama Al haji. Licha ya kuwapa wahiji uchaji, kitendo hicho ni cha ufahari. Badala ya mtu mmoja tajiri kwenda safari nyingi za hija wangeweza kabisa kutoa pesa kwa watu wasio na uwezo wa kiuchumi bali ni wacha Mungu kuwawezesha nao kufika sehemu hizo zinazosadikiwa kuwa ni sehemu takatifu ili kuongeza ucha Mungu wao.

Tatu ni jambo la msingi kwa Waislam wa Afrika kuanza kutafakari juu ya shughuli nzima ya hija. Kila mwaka maelfu na maelfu ya Waafrika huenda Maka, wengi wao hupoteza maisha yao huko huko. Kiuchumi Serikali na wananchi wa Uarabuni hunufaika sana na ziara hizo za hija kwa kujipatia fedha ya kigeni kutoka mataifa mbali mbali ya Kiafrika.

Wamisionari wa Kikristo na wakoloni nao pia walitengana na watu waliowaongoza kwa sababu hali yao ya maisha ya kimwili ilikuwa tofauti. Wao walikuwa na mtaji ambao uliwawezesha kununua nguvu ya Waafronodi walio wanyonge kuwazalishia mali au vitu walivyohitaji kwa maisha yao ya kila siku. Fedha pia iliwapa uwezo wa kununua vitu ambavyo, kwa mfano, jamii ya leo inaviona ni muhimu sana. Vitu hivyo ni kitanda, godoro,

mablanketi, shuka za kitandani, na mavazi safi. Ili vitu hivyo visiweze kusababisha mwili kunuka mtu anahitaji sabuni ya kufulia na kuogea pamoja na marashi. Hata kama kuna uwezekano wa kuyapata yote hayo kuna haja ya kuwa na maji safi na ya kutosha, chakula bora na vyombo bora vya kulia. Hata hivyo, iko haja ya kuwa na nyumba ya kisasa ambamo vitu hivyo vyote vinaweza kuhifadhiwa. Mwafronodi hakuweza, bado ni tatizo kwake mpaka leo, kuvipata vyote hivyo kwa sababu ya umaskini na unyonge wake. Mbele ya Msanodi na Myurunodi, kwa sababu ilimlazimu pia kulala katika nyumba moja na wanyama kama kuku, ndama na mbuzi - Mwafronodi alitoa harufu ya kinyama, akakimbiwa na kubaguliwa kama vile Waafronodi waliosoma wanavyowabagua baadhi ya wananchi ambao wanaishi katika hali kama hiyo ya kinyonge.

Viongozi wa madhehebu ambao ni wananchi hawana budi kutambua hayo. Badala ya kuendelea kuishi mbali na wananchi na kufanyiwa kazi wanapaswa kuchukua hatua za kimapinduzi kama Waafronodi halisi kuwafuata watu waliko; kuishi maisha ya kawaida ingawaje mwandishi anatambua tatizo na ugumu wa utekelezaji wa fikara hizo. Lakini jambo la kusisitiza ni kuwa hakuna uhalali wowote kwa viongozi wetu wa dini kung'ang'ania kuishi mbali na watu, kuishi maisha ya kibepari ambayo hata misahafu mitakatifu imelaani. Kuongoza si kutawala bali kuwaelekeza watu kufikia lengo; na papo hapo wawe tayari kujifunza kutokana na wale wanaowaongoza ili pia kuongeza ujuzi, uwezo na fadhila za uongozi. Kuongoza kwa kutengana na watu ni sawa na kutawala; na kutawala ni uhasama na kwamba hakusukumi 'maendeleo'.

Tatizo la viongozi wa madhehebu, hasa yale yaliyo chini ya Vatikani, ni kuwa kama wataondokana na misaada ya Vatikani, ya mabeberu wa Ulaya na Marekani, kutakuwa ndio mwisho wa uhai wao. Na hii si kweli. Hofu hii isiyo na msingi inatokana na kasumba tu; hasa ikifahamika kuwa wazazi, ndugu na jamaa wa viongozi hao huishi maisha ya kawaida na wanaweza kujipatia mahitaji yao ya maisha. Kasumba nyingine ni kuwa kuishi na wananchi kutabomoa misingi ya taasisi yao, hofu ambayo ni ya kweli. "Utaishi kwa altare" maana yake pale pale unapoishi na kutoa huduma utapata ridhiki, hata heshima yako. Na hii haitakiwi kutengana na watu. Huko walikotoka wamisionari, viongozi wa dini waliishi siyo tu karibu ya watu bali pamoja nao ingawa kama tabaka la wanyonyaji. Walikuwa makabaila, vibepari na walitumia - sehemu kubwa bado inaendeleza mpango

huo - nguvu ya wanyonge kuwazalishia mali. Viongozi wetu nao wameonja na kurithi uhondo huo. Hivyo, si rahisi kuamua kuondokana na mpango ambao ndio msingi wa maslahi na heshima yao. Inahitaji mzinduko wa juu na moyo wa kujitoa mhanga.

Ili kuleta maendeleo ya haraka ya watu siasa ya ujamaa ndiyo njia ya pekee. Ujamaa siyo 'lipenenga'[1] au 'lelemama'[2] bali ni vita. Ujamaa unadai sadaka kubwa sana kutoka kwa viongozi, matajiri na waheshimiwa. Sadaka yenyewe ni kukubali kwanza kuwa sawa na watu wengine wote kiutu. Kuheshimiana, kupendana kidhati, kushiriki katika kupanga mipango ya maendeleo na katika utekelezaji wake. Tabia za ubwana, umwinyi, ubwanyenye na ubinafsi ni sharti kuondokana nazo. Ujamaa unataka kujenga mataifa tajiri, yenye watu wenye afya bora, nguvu, akili safi, tabia njema na yanayojitosheleza kwa kila hali. Na hayo yote yamo katika msingi wa misahafu ya madhehebu yote. Hayapingani na wala hayagongani.

Ujamaa ndiyo siasa ya pekee inayoziwezesha jamii kuishi pamoja na kushrikiana katika shughuli zote za kuzalisha mali kwa faida ya wote. Kwa hiyo, hauna budi kuungwa mkono na kubarikiwa na madhehebu yote. Ujamaa siyo dini. Kinyume chake itikadi ya ujamaa inazifanya dini - ambazo ni taasisi zilizoundwa kwa madhumuni ya kumsaidia mtu kufika peponi baada ya maisha ya hapa duniani - kuwa yakinifu zaidi. Viongozi wa dini, ambao hawana budi kutokana na watu wenyewe, ujamaa unawawezesha kuishi pamoja kidugu na watu wanaowaongoza, kushirikiana nao zaidi; na kwa njia hii hata mahubiri yao yataonekana yakinifu, yaani, yenye ukweli unaoweza kueleweka na kukubalika kirahisi.

Haifai tena kurudia kosa la kihistoria la kujenga maboma na makanisa makubwa kwa ajili ya sifa na ufahari wa viongozi. Ni dhahiri kwamba wamisionari hawakuona mbali sana wakati, kwa mfano, wakijenga makanisa kama ya Peramiho na Lituhi katika mkoa wa Ruvuma katika Jamhuri ya Tanzania. Makanisa hayo yakijazwa na maelfu ya wananchi kutoka maili nyingi. Dunia ya leo imeendelea; na ukweli ni kuwa ni vigumu sana, kuwategemea wananchi kusafiri maili nyingi kufuata huduma za kiroho. Hivyo, makanisa hayo makubwa kama milima hubaki au yatabaki kama magofu. Maboma ya kuishi wamisionari, (mmoja

1. Lipenenga — aina ya ngoma ichezwayo na baadhi ya jamii za Tanzania.
2. Lelemama — Aina ya ngoma ya Kizaramo katika Tanzania.

au wanne) yalikuwa makubwa hata huwatosheleza watu wote waishio katika wilaya moja ndogo ya Tanzania. Siyo kwamba kulikuwa kukufuru tu bali maboma hayo leo huwa ni vigumu sana kuyatunza, na hasa wakati watu wanapotaka kupelekewa huduma huko waliko.

Ni kweli kuwa baadhi ya viongozi walikuwa na uwezo mkubwa sana wa kiuchumi. Mali hii ilitokana na waumini wa kwao kwa ajili ya kuwasaidia maskini wa Afrika. Wamisionari walilimbikiza mali hiyo na kuiongeza mara dufu kwa kuanzisha shughuli mbali mbali za kiuchumi katika sehemu zao. Mali hiyo iŋgeweza kabisa kutumika zaidi kwa kutoa huduma za kusukuma maendeleo ya wananchi kwa ujumla. Lakini furaha ya wamisionari ilikuwa kuhakikisha kuwa wanazungukwa na wananchi walio maskini na wanyonge ili waweze kuwatawala vema. Leo viongozi wetu wa dini ni wananchi. Nao wamerithi uwezo huo mkubwa wa kiuchumi. Kwa hiyo, badala ya kuutumia uwezo huo wa kiuchumi kwa kuonyesha ufahari wao mbele ya waumini wanyonge wanashauriwa kuutumia uwezo huo wa kiuchumi katika mipango ambayo itasaidia kuwaendeleza wananchi na hatimaye kuwaondoa katika unyonge. Mipango hiyo inaweza kuwa ya kutoa aina mbali mbali za huduma kama vile mashule, hospitali, zahanati, vituo vya afya, karakana, bohari za kuhifadhia mazao; kununulia zana za kilimo; na kadhalika.

Pamoja na yote hayo viongozi wa madhehebu yote, hawana budi kuondokana na fikara za kibepari. Pamoja na kuhubiri dini wanapaswa pia kuhubiri itikadi ya ujamaa ambayo, hasa kwa wanaAfronodi, inaeleweka vema na kirahisi zaidi. Kupinga ujamaa ni sawa na kupinga mapambano ya ukombozi wa jamii kutokana na minyororo ya ukoloni. Iwapo dini za madhehebu yote leo zinaunga mkono fikara na juhudi za jamii kujikomboa kutoka utumwa na ukoloni ni dhahiri kwamba viongozi wa madhehebu wataona kuwa ni halali zaidi kujiingiza, na ikiwezekana hata kuchukua nafasi ya mbele, katika suala la ujenzi wa ujamaa. Ujamaa ndiyo njia pekee ya kusukuma maendeleo ya watu na kukamilisha uhuru wa jamii zilizopata kukabiliwa na utumwa na ukoloni kwa kupambana na mazingara.

Badala ya kuhubiri 'usipende mali, heshima, furaha wala cheo', wananchi wahimizwe kushirikiana kutumia maarifa na juhudi katika kupambana na mazingara kwa shabaha ya kuzalisha mali kwa wingi ili kulifanya taifa na watu wake tajiri, lenye afya, furaha, akili safi, nguvu na heshima. Watu waelewe ukweli kuhusu cheo. Cheo si kibaya na wala si haramu. Baadhi ya watu

lazima wawe katika cheo. Lakini cheo kinakuwa kibaya wakati watu wachache, kama vile wakoloni, au tabaka la wanyonyaji, wanapokichukulia kama ni haki yao ya pekee. Huo ni uhasama. Katika jamii ya kijamaa kila mtu anastahili kushika nafasi ya madaraka au uongozi kulingana na uwezo na juhudi yake. Cheo, hasa kikieleweka kuwa ni dhamana, ni kitu halali na kilichotakatifuzwa. Kulaani kupenda cheo au madaraka ni kuua juhudi ya wananchi. Wakati wa ukoloni cheo kilikuwa dhambi kwa Mwafronodi; papo hapo kilifanywa halali kwa Wasanodi hasa kwa Wayuronodi ambao ni wakoloni. Kwa hiyo, mahubiri yetu sasa yawe kuwahimiza wananchi kuongeza juhudi ili kuonyesha uwezo hata wa kukabidhiwa madaraka. Waafronodi wengi kwa sababu ya kasumba hiyo wanaogopa na kugoma kupokea madaraka hata kama wanao uwezo. Woga wao unatokana na kutojiamini kwa sababu cheo ni moja ya mambo aliyofundishwa kuyachukia na kuyakana.

Viongozi wa dini za madhehebu yote hawana budi kukiri pia kuwa viongozi wa siasa wamewatangulia sana katika kufafanua, kuendeleza na kutetea haki za watu, kazi ambayo pia imo katika jukumu lao, yaani, wahubiri wa imani mbali mbali za dini. Hata hivyo, hawajachelewa sana. Kama wanamapinduzi, hawatasita kushirikiana bega kwa bega na viongozi wa siasa na serikali katika kuleta maendeleo ya watu. Kwa vile ujamaa na kujitegemea ndiyo njia ya pekee ya kumkomboa Mwafronodi na tabaka la wanyonge wanaonyonywa na kukandamizwa na mabepari popote katika dunia, wito ni kwamba viongozi wa madhehebu wachukue nafasi ya mstari wa mbele kujifunza na kuelewa barabara siasa ya ujamaa na kujitegemea. Kisha kuifundisha siasa hiyo pasipo kupotosha.

Lakini ili waweze kutekeleza yote hayo hawana budi kwanza wao wenyewe kuondokana na kasumba za kikoloni; fikara za ubwana, umwinyi, ubwanyenye na ubaba; kuacha kuvaa kifahali, kuzungumza na lafudhi ya kibwana mkubwa na kujiona kuwa wao ni tofauti na wananchi wengine. Baada ya hapo, ndipo wote tuongoze sasa safari ya vijijini na viwandani ili kuungana na wananchi wenzetu katika kuzalisha mali, katika shughuli za kitamaduni, kuelekezana kifikara pamoja na kupeana maarifa ya kiufundi, kiuchumi, kitaalam na ya kiroho. Ujamaa ni itikadi ambayo nchi za Dunia ya Tatu zimeipokea na kuonekana kuwa ina nguvu kubwa sana ya kusukuma na kuharakisha maendeleo ya watu. Na kwa kuwa inakwenda sambamba na imani ya dini basi ni wajibu wa viongozi wote wa siasa, serikali na dini kuchukua

hatua ya haraka kuwafuata watu na hasa kuanzisha vijiji vya ujamaa pamoja na kuwashawishi wanyonge kuhamia huko.

Sura ya 13

UAFRONODI NA JUHUDI ZA WAAFRIKA KUJIKOMBOA KITAIFA

Kurudi nyuma miaka 75 Afrika nzima, isipokuwa 'Ethiopia' ambayo ilitawaliwa na Wataliano kwa muda mfupi tu, ilikuwa imegawanywa na kufanywa makoloni ya mabeberu. Lakini kabla ya Afrika kuingizwa katika ukoloni-mkongwe mabeberu wa Ulaya na Uarabu waliwauza Waafrika katika utumwa huko Asia, Ulaya na hasa katika bara la Marekani na Visiwa vya Karibiani. Waafrika hao waliouzwa utumwani walikuwa wa asili ya Kiafronodi.

Juhudi nyingi za kujikomboa zilifanywa na jamii zenye asili ya Kiafronodi katika nchi za ugenini tangu karne ya kumi na nane,* yaani, kabla hata ya ukoloni-mkongwe kuingia katika Afrika. Hata hivyo, juhudi hizo za watu wenye asili ya Kiafronodi hazikuwa za mafanikio sana huko ugenini. Waafronodi walie-ndelea kunyimwa haki zao za kiutu. Walidharauliwa, waliba-guliwa, walikandamizwa na kunyonywa; na kwa walio wengi, hali hiyo bado inaendelea mpaka leo.

Fikara, yaani, fikara za umoja wa watu wenye asili ya Kiafronodi zilianzishwa na wanyonge wa Kiafronoddi huko Marekani na visiwa vya Karibiani. Kwao umoja wa aina hiyo ulikuwa wa maana sana katika mapambano yao na mabepari na mabeberu. Ni kweli pia kuwa baadhi ya wananchi wa Afrika kama akina Kinjikitile na wengine walikuza fikara za uafrika kwa maana ya uafronodi, yaani, umoja wa Waafrika wenye asili ya Kiafronodi.

Umoja uliozungumziwa na jamii za watu wenye asili ya Kiafrika ulikuwa na maana tatu. Kwanza, ulikuwa na maana ya kuwaunganisha watu wote wenye asili ya Kiafronodi katika nchi za ugenini katika mapambano yao na mabeberu; pia katika

---

* J.C. Anene, G. Brown (ed), *Africa in the 19th and 20th Centuries*, Ibadan, Uk. 528 – 38

kupambana na serikali za kidhalimu na ubaguzi zilizoundwa huko ugenini na watu wenye asili ya Kiyuronodi. Papo hapo umoja huo ulikiuka mipaka na maana yake kupanuliwa. Wananchi hao wa nchi za ugenini wakaanza kujitambulisha na ndugu zao wa Bara la Afrika ambako ndiko mababu zao waling'olewa. Hao waliojitambulisha nao walikuwa Waafrika wa asili ya Kiafronodi. Kwa hiyo, fikara hizo za watu wenye asili ya Kiafronodi katika ugenini zilikuwa na maana halisi ya uafronodi na wala si uafrika kwa maana ya matumizi yetu ya msamiati. Na kwa sababu hiyo hiyo wakati wananchi hao walipoanzisha vyama vyao vya siasa na kupigania kurudi kwenye nchi yao ya asili ilikuwa ni kurudi katika Afrika ya Waafronodi, yaani, kusini ya Sahara.

Marekani na Visiwa vya Karibiani vimejengwa na kuendelezwa, angalau misingi yake, kwa jasho na damu ya watumwa wa Kiafronodi na vilembwekezi wao ambao bado hukandamizwa mpaka leo. Uamuzi wa watu wa asili ya Kiafronodi kurudi Afrika na kuungana na ndugu zao si wa busara. Vile vile uamuzi wa aina hiyo ni dalili dhahiri ya kutangaza kushindwa kwao katika mapambano ya ukombozi. Wananchi, kwa mfano, wa huko Marekani ambao wana asili ya Kiyuronodi hawana haki zaidi ya 'uananchi' na uraia kuliko watu wa asili ya Kiafronodi. Wote walifika Marekani karibu wakati moja. Wote wana asili ya mabara mengine kuondoa Wamarinodi ambao ndio peke yao ni watu wa asili ya Bara la Marekani. Marekani ni taifa lililoundwa na wageni. Wageni hao, kwa sababu ya kuishi huko vizazi vingi, wameweza kujenga fikara, utamaduni, thamani ya maisha na misingi mingine ambayo ni ya Kimarekani. Kwa msingi huo watu wa asili ya Kiafronodi huko Marekani hawana uhalali wo wote kutokujiita Marekani kama Marekani wengine wenye asili ya Kiyuronodi na Kimarinodi na kudai haki sawa za Kimarekani kama raia.

Lakini, maadam wao, Waafronodi wa huko ugenini, wamepitia hatua sawa za kukandamizwa, kubaguliwa, kunyanyaswa, kuteswa na kunyonywa wanao wajibu wa kujitambulisha na Waafronodi wa Afrika siyo katika kuhakikisha tu ukombozi wa watu wenye asili ya Kiafronodi bali pia ukombozi wa watu wote wa Afrika; papo hapo wakiunganika na wanyonge wengine kokote duniani katika juhudi za kuutokomeza ukoloni, ubeberu na unyonyaji.

Fikara za Uafronodi, yaani, umoja wa watu wenye asili ya Kiafronodi duniani zilienezwa katika Afrika kuanzia karne ya

kumi na tisa hadi karne ya ishirini. Watu wa kwanza, inasemekana, kueneza fikara za uafronodi katika Afrika walikuwa ni viongozi wa dini wa Kimarekani wenye asili ya Kiafronodi ambao waliendesha shughuli zao katika Afrika huko Liberia. Miongoni mwao wakiwa Askofu Alexander Walter wa madhehebu ya African Methodist Episcopal Zion Church, na Daktari Edward W. Blyden,[1]. Vile vile kulikuwa na baadhi ya Waafrika wenye asili ya Kiafronodi ambao waliwahi kupelekwa Marekani kwa ajili ya elimu. Miongoni mwao wakiwa hayati Mchungaji Yohana Chilembwe[2] wa huko Malawi. Chilembwe alikwenda Marekani (U.S.) mwaka wa 1897.

Jambo la kukumbuka ni kuwa fikara hizo za mwanzo za umoja wa Kiafronodi pengine hazikuwa za kiitikadi. Watu kama Askofu Walter walihimiza na kukuza moyo wa Kiafronodi kwa ajili ya kuwawezesha Waafronodi kushiriki na kupata maslahi sawa na watu wa asili nyingine chini ya mpango wa ukoloni; au chini ya serikali ya wachache. Na hii huonekana kama siasa ya mseto ambayo huhimiza na kuimarisha utaifa kufuatana na rangi au asili ya watu.

Kwa upande mwingine fikara za akina Chilembwe ingawa hapo mwanzoni zilikuwa za kupigania maslahi sawa na walowezi wa Kiyuronodi zilisaidia sana kukuza na kutukuza utu wa Waafronodi na kwa jinsi hiyo kuwaunganisha wananchi. Muungano au umoja wa wananchi ulikuwa nï msingi muhimu sana wa mapambano ya kiitikadi na ukombozi wa kitaifa. Mnamo 1895 Chilembwe alimwandikia Mkurugenzi wa misioni ya Kiingereza kwa lugha ifuatayo:

'Lakini nimefurahishwa sana na kijitabu ulichoniletea . . . nikisoma kitabu hicho kwa sauti . . . ninasikia baadhi ya maneno . . . . . kuhusu Ham na wanawe . . . . . "Wacha Ham alaaniwe pamoja na wanae, Kanani, kwa maisha yote bila mwisho.

Watumwa wa watumwa watakuwa; watumwa kwa Shem na kwa Jafeti!" Ndiyo, hayo yote yangekuwa hivyo, kama ingekuwa zama hizo, lakini kwa sasa hayawezi kuwa vile, mmoja wa wana wa Ham anena. Sasa wana wa Ham watakuwa watumishi si kwao tena, wapenzi ndugu na dada wa Kisanodi na Kiyuronodi[4].

Maneno hayo ya Chilembwe yanaonyesha fikara za usawa wa

---

1. J.C. Anene, G. Brown (ed) Uk. 529
2. R.I. Rotberg, *The Rise of Nationalism in Central Africa*, London, Uk. 61 – 4
3. Ibid., Uk. 62

watu ambazo Waafronodi walikuwa nazo. Ni jambo la maana kukumbuka kuwa ijapokuwa fikara hizo mwanzoni hazikuwa za kiitikadi zilikuwa ni msingi mzuri wa kuwaunganisha watu kiitikadi kwa miaka iliyofuata. Mnamo 1915 Chilembwe alizendeleza fikara zake kiasi hata kuwaunganisha wananchi na kuanza juhudi za kuwabwaga wakoloni katika mapambano ya ukombozi ambayo wakoloni wameyaita, kama kawaida yao, maasi ya Chilembwe. Chilembwe aliwahi kuishi na jamaa ya Yosefu Buti mmisionari, wa asili ya Kiyuronodi, ambaye anasadikiwa kuwa ni mmoja aliyeonyesha juhudi za kutetea maslahi na haki sawa za Waafronodi huko Afrika ya Kati. Pia Chilembwe aliwahi kwenda kusomea Marekani. Lakini Kinjikitile na Wamatumbi wenzake hawakuishi na Wayuronodi au Wasanodi na wala hawakutoka nje ya nchi zao na wala hawakusoma. Walizungumza juu ya umoja wa watu wa Afrika wakiamini kuwa bara zima lilikaliwa na Waafronodi. Kwa maneno mengine, Kinjikitile alitaraji kujenga umoja wa kiitikadi katika msingi wa Uafronodi. "Sisi sote ni Waafrika", akiwa na maana ya kuwa 'sisi wote ni Waafronodi; na kwamba wote tu wamoja'.

Hii inamaanisha kuwa fikara za umoja wa watu wenye asili ya Kiafronodi zilikuzwa pia na baadhi ya viongozi wa kimapinduzi wa humu Afrika. Hata hivyo, fikara zao za umoja wa watu wenye asili ya Kiafronodi ziliwahusu Waafronodi wa Afrika tu. Watu wenye asili ya Kiafronodi katika dunia mpya hawakufikiriwa kwa sababu ya utovu wa maarifa ya kijografia; na pengine kwa kufahamu kuwa uwezekano wa watu hao kurudi Afrika na kuungana na ndugu zao katika kupambana na ukoloni haukuwepo kwa sababu ya umbali.

Kwa upande mwingine, watu wa asili ya Kiafronodi katika sehemu nyingine za dunia hawakuwa pia na maarifa ya kutosha kuhusu jiografia ya Afrika; wala mpango na siasa ya kikoloni katika Afrika. Kama wangejua, wangetambua ugumu wa kuwaunganisha Waafronodi wote wa Afrika na watu wa asili ya Kiafronodi kutoka nchi za ugenini kwa sababu ya ukubwa wa bara hili, kasumba za siasa na mbinu tofauti za wakoloni.

Mkutano wa Umoja wa watu wenye asili ya Kiafronodi uliitishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1900. Uliitishwa na mwanasheria mmoja wa Kitrinidadi, kwa jina H. Sylvester Williams;* nao ulifanyika mjini Londoni. Wajumbe walitoka Marekani, Visiwa vya West Indies; na wachache kutoka Bara la

* I.C. Anene, G. Brown (ed) Uk. 529

Afrika. Umoja huo ulifanya mikutano mingi sana kati ya 1900 na 1927 chini ya uongozi wa Dk. William E.B. Dubois kabla ya kuvunjika.

Baadaye Markusi Garvei akajitokeza na fikara za kuwataka watu wote katika Marekani na sehemu nyingine katika dunia ya ugenini ambao walikuwa na asili ya Kiafronodi kuja kuishi Afrika. Fikara za Garvei zinadhihirisha wazi kuwa Uafrika ulioongelewa ulikuwa ni Uafronodi. Hata hivyo, fikara hizo za Garvei zilikuwa za kibaguzi wa rangi, fikara ambazo zinakubaliana na siasa ya Wamarekani wenye asili ya Kiyuronodi ambao huwabagua Wamarekani wenzao wenye asili ya Kiafronodi kwa msingi wa rangi. Pia fikara hizo zilikuwa za kukatisha tamaa na kukwepa mapambano halisi ya kuwapatia haki sawa Wamarekani wenye asili ya Kiafronodi huko huko Marekani; japokuwa mtungaji anatambua hali na ugumu wa Wamarekani wa kujikomboa huko huko Marekani.

Kwa hiyo, fikara hizo za Garvei hazikuwa na msingi wa kimapinduzi. Kurudi kwa mamilioni ya Waafronodi walioko nje ya Afrika pia kungesababisha matatizo kadhaa katika Afrika. Kwa sababu ya tofauti za kitamaduni, kifikara, kisayansi na kitekinologia kati ya Waafronodi wa Afrika na watu wa asili ya Kiafronodi wa nje ya Afrika (Liberia ikiwa mfano mzuri wa kuelezea) migongano kadhaaa ingeweza kutokea. Hali hii ni dhihirifu na wala si ya kubuni. Wamarekani na watu wa sehemu nyingine wenye asili ya Kiafronodi ambao leo, kwa sababu mbali mbali, huishi katika nchi huru za Kiafrika hujibagua na kubaguliwa kwa namna nyingi sana. Hawapendi sana, isipokuwa kitaalam na kisiasa, kujitambulisha na kushirikiana na wananchi (Waafronodi) kimaisha ingawa ubaguzi wa aina hii upo pia kati ya Waafronodi wa nchi huru za Kiafrika.Ni jambo la kawaida kwa watu wa taifa au nchi moja kujitambulisha; na hii ina maana ya kuwa jamii inajitofautisha yenyewe na watu wa jamii au taifa jingine. Kusema kweli huu si ubaguzi. Lakini inapotokea watu wa jamii au taifa moja huishi kwa uhasama na watu wa jamii au taifa jingine kwa sababu ya rangi na asili zao au maendeleo yao ni tofauti huwa ni ubaguzi.

Kwa upande mwingine, fikara za watu wa asili ya Kiafronodi kupigania ukombozi na haki zao katika nchi na katika mataifa yao huko ugenini, kama ilivyoimarishwa na kusisitizwa na akina Du Bois na George Padmore, zilikuwa za kimsingi kabisa. Fikara za Uafronodi zingeweza tu kuonekana za kimapinduzi katika maana ya umoja wa kushirikiana katika kupeana misaada ya

kitekinologia, kisayansi, kifikara, kielimu na kitaalam. Hasa ikikumbukwa kwamba watu wa asili wa Kiafronodi katika nchi za kigeni walikuwa wameendelea zaidi katika taaluma mbali mbali. Umoja na ushirikiano wa aina hii; na kwa namna hii tu, ungeweza kuwa wa dhati na wa maana kwa watu wenye asili ya Kiafronodi katika Afrika na nje ya Afrika.

Kadiri fikara hizo zilivyoendelezwa na hasa baada ya vita kuu ya pili, Uafronodi ulianza kupewa tafasiri tofauti. Mabadiliko hayo yalisababishwa na kuongezeka kwa maarifa ya kijografia juu ya Afrika na dunia kwa jumla. Vile vile mabadiliko yalisababishwa na maarifa ya kutosha kuhusu mateso na unyonyaji wa mabeberu chini ya mpango wa ukoloni. Afrika yote ilikuwa imegawanywa na mabeberu wa Ulaya katika makoloni. Watu wote wa Afrika, yaani, wenye asili ya Kisanodi na Kiafronodi, waliingizwa katika janga la kutawaliwa, kukandamizwa, kudharauliwa, kupuuzwa, kuteswa na kunyonywa.

Baada ya kutambua hayo yote watu wa asili hizo zote mbili wakaanza kujiona kwa kiasi fulani, kama wamoja. Wote walikabiliwa na adui wa aina moja - ukoloni. Kwa hiyo wakajitambulisha—hasa viongozi wanamapinduzi—kisiasa, kifikara kama Waafrika. Na baada ya hapo tu fikara za Uafronodi zikaanza kuonekana zimefikia kiwango cha juu. Uafronodi, kwa uhalali wote, sasa unaweza kuongelewa kama Uafrika.

Mkutano wa tano wa umoja wa watu wenye asili ya Kiafrika ulifanyika mjini Manchesta mnamo 1945, yaani, baada ya Vita Kuu ya pili. Washiriki wa Mkutano huo walikuwa wanafunzi wa vyuo vikuu; na kwa mara ya kwanza, Waafrika kutoka Afrika waliongoza mkutano huo. Miongoni mwa Waafrika walioshiriki katika mkutano huo wa Manchesta ni Mzee Jomo Kenyatta, Daktari Hestingi Kamuzu Banda na hayati Daktari Kwame Nkurumah. Joji Padmoa wa Trinidadi alikuwa kiungo kikubwa sana katika mkutano huo kati ya Waafronodi wa Afrika na watu wenye asili ya Kiafronodi nje ya Afrika. Mkutano wa Manchesta ulikuwa wa maana sana. Mkutano ulisisitiza juu ya umuhimu wa watu wenye asili ya Kiafrika, katika Afrika na nje ya Afrika, kuungana kwa madhumuni ya kupambana na kuutokomeza ubeberu, ukoloni na unyonyaji wa kila aina kokote duniani.

Mkutano wa Manchesta ulifuatiwa na mkutano wa Akra* wa mwaka 1958. Huu ulikuwa ni mkutano wa kwanza wa nchi huru

---

* Akra — mji mkuu wa Ghana

za Kiafrika; nao ulihudhuriwa na wajumbe kutoka nchi nane: Ethiopia, Ghana, Liberia, Libya, Misri, Moroko, Sudani na Tunisia.

Mkutano huu ni muhimu sana kwa sababu mbili kubwa. Kwanza, kwa kuwa ulihudhuriwa na Waafrika wa asili ya Kiafronodi na Kisanodi ni dhahiri kuwa fikara za Waafrika kama watu wamoja zilivuka upeo na mipaka ya Uafronodi na Usanodi. Pili ulikuwa ndiyo msingi hasa wa Uafrika, yaani, umoja wa watu wa Afrika katika maana yake halisi.

Mkutano wa Akra ulifuatiwa na mkutano wa Addis Ababa wa mwaka 1960. Mkutano huu ulihudhuriwa na wajumbe kutoka nchi huru kumi na tano za Kiafrika. Ndoto za fikara za Uafrika, yaani, umoja wa watu wa Afrika, pasipo kujali asili ya watu au utamaduni wao — hasa dini, zilidhihirika mnamo 1963 wakati nchi huru thelathini na mbili zilipokutana katika mkutano wa pili mjini Addis Ababa, Ethiopia, na kuunda Chama cha Umoja wa Nchi huru za Afrika (OAU). Nchi ambazo zilishiriki katika mkutano huo na kuunda katiba ya Umoja huo ni kama zifuatazo:

1. Algeria	2. Apa Volta
3. Burundi	4. Chadi
5. Dahome	6. Ethiopia
7. Gaboni	8. Ghana
9. Gine	10. Ivori Kosti
11. Jamhuri ya Afrika ya Kati	12. Jamhuri ya Muungano ya Waarabu (Misri)
13. Kameruni	14. Kongo
15. Liberia	16. Libya
17. Malagasi	18. Mali
19. Moritania	20. Moroko
21. Nigeria	22. Nigeri
23. Rwanda	24. Senegali
25. Sierra Leone	26. Somalia
27. Sudani	28. Tanzania Bara
29. Togo	30. Tunisia
31. Uganda	32. Zaire

Shabaha na madhumuni ya Umoja huo ni pamoja na kuendeleza juhudi za kujenga umoja mathubuti wa watu wote wa Afrika, kuendeleza juhudi za ukombozi wa Afrika, kupambana na ukoloni-mambo-leo, kulinda uhuru wa nchi za Afrika, kuendeleza hali za maisha ya watu wa Afrika kiuchumi, kitamaduni, kielimu na kadhalika.

Msimamo wa Umoja wa Nchi huru za Afrika ni kuwa Umoja huo utaheshimu serikali huru za wanachama wake; na kwamba Afrika ikiwa ni moja serikali huru zinazounda umoja huo zitakuwa na msimamo moja na kushirikiana katika kutatua matatizo yanayoikabili Afrika kwa ujumla au yanayozikabili baadhi ya nchi za Afrika ambazo ni wanachama wake.

Fikara za umoja wa watu wa Afrika tangu mwanzo zilikuwa na shabaha ya kuunda chombo ambacho kingesaidia kulikomboa Bara zima la Afrika; na papo hapo kujenga taifa moja la Kiafrika ambalo ni huru. Kwa jinsi hiyo ni wazi kuwa fikara hizo zilikuwa za kimaendeleo na kimapinduzi. Lakini kwa sababu ya mazingara ya Afrika: ukubwa wa nchi, tawala na siasa mbali mbali za kikoloni, tofauti ya mwamko wa kisiasa na kadhalika; suala la kuunda chombo kimoja cha ukombozi au, kwa maneno mengine, kuunda taifa moja la Waafrika wote lilionekana kuwa gumu sana. Uamuzi wa busara ni kuwa kila watu katika makoloni yao walilazimika kupigania uhuru wao kama taifa. Uamuzi huu haukuwa na maana ya kuua fikara za umoja bali ulichukuliwa kwa shabaha ya kuharakisha kuundwa kwa umoja wenyewe. Baada ya nchi nyingi za Kiafrika kujikomboa kitaifa pendekezo lililotolewa na Umoja huo ni kuunda serikali za muungano kutegemea mazingara ya kiuchumi na hasa ya kijografia. Shabaha ya kufanya vile ni kufikia umoja kamili wa Afrika nzima.

Lakini kwa hali ilivyo hivi sasa ni hatari kuwa nchi nyingi za Kiafrika, hasa zile za kaskazini ya Sahara, huondokana na fikara za Uafrika na kuanza kukuza fikara za Usanodi. Hilo ni kosa kubwa la kihistoria. Mafanikio makubwa ya wakoloni katika Afrika yalitokana na siasa yao ya kuwatenga watu katika makundi ya kihasama, ingawa mahali pengine walikuta hali hiyo ya mgawanyiko na wao wakaitumia kwa faida yao. Mabeberu wa Kiyuronodi wanashangilia sana kitendo cha Afrika kujigawanya tena, hasa katika kuunda serikali za muungano, katika misingi ya asili ya watu au dini.

Ni kweli kuwa kidini Afrika imegawanyika katika ulimwengu wa Kiislam na ulimwengu wa Kikristo. Dini kwa vyo vyote vile haziwezi kuwa msingi imara wa watu kuungana. Dini hazileti maendeleo au hali bora ya maisha ya watu; na wala haziwezi kupewa maelezo ya kiakili. Dini ni imani ambayo inaweza ikazingatiwa na watu wa mataifa mbali mbali hata kama mataifa hayo yanaishi katika hali ya udugu au uhasama. Mapambano ya Afrika hayawezi kuendeshwa kwa msingi wa imani za dini bali

kwa msingi wa makabiliano na hali halisi ya maisha.

Tangu mwanzo fikara za Uafrika zilionekana kuwa za kimapinduzi kwa sababu zilikuwa na shabaha ya kuwaunganisha watu wote wenye asili ya Kiafrika nje na ndani ya Afrika. Ingekuwa kosa kubwa leo kama juhudi za umoja wa Nchi huru za Afrika zingekomea katika Afrika tu. Juhudi za Umoja wa watu wa Afrika hazina budi kuunganika na juhudi za watu wengine wanaokandamizwa duniani ili kupambana na ubeberu, ukoloni-mambo-leo, serikali za kidhalimu na kibaguzi za wachache; uonevu na unyonyaji unaoendeshwa na mataifa makubwa kwa mataifa madogo katika dunia. Kwa jinsi hii fikara za uafrika zitakuwa zimevuka upeo wa uafrika na kufikia upeo wa muungano na ushirikiano wa mataifa yanayoonewa na kudhulumiwa; pia utakuwa ni muungano wa Waafrika na tabaka la wanyonge kokote ulimwenguni kwa sababu ya kuendeleza mapambano ya kuleta usawa wa jamii.

> Uhuru na Uafrika! Uhuru na kujenga ushirikiano mwema ili kuleta haki sawa na maendeleo ya watu wote wanaodhulumiwa na kugandamizwa; na hatimaye kukabiliwa nà unyonge ambao husababishwa na baadhi ya watu au jamii.

Baada ya kuangalia maendeleo ya fikara za umoja wa watu wenye asili ya Kiafronodi duniani hadi kufikia muungano wa watu wa nchi huru za Afrika mnamo 1963 hapana budi kutolewa maelezo kuhusu mapambano yenyewe ya uhuru wa kitaifa. Mapambano hayo ya ukombozi yatatazamwa katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza itahusika na mapambano ya kujipatia uhuru wa bendera, yaani, uhuru wa kutokana na ukoloni-mkongwe. Sehemu ya pili itahusu mapambano ya kujitakasa kutokana na makovu ya kasumba za kikoloni;* mapambano na ukoloni-mambo-leo, ujinga, umaskini na maradhi. Kwa kuwa sehemu hii ya pili ya mapambano ya ukombozi kwa shabaha ya kuimarisha uhuru imeelezwa zaidi katika sura ya kumi na tatu, sura hii itaelezea mapambano ya aina ya kwanza.

Kabla ya mapambano yenyewe kuanza kulibidi mambo fulani yawepo na yafahamike. Waafronodi na Waafrika wote, kwa ujumla, tangu mwanzo walitambua ubaya wa ukoloni na ubeberu na ndiyo maana waliamua kuupinga tangu siku za mwanzo za kuingia kwa mpango huu. Lakini kama ilivyoelezwa katika sura

---

* Rejea tena sura ya tatu kwa maelezo zaidi.

ya kumi kwa kutumia njama na mbinu mbali mbali wakoloni waliiteka Afrika. Haukupita muda mrefu wananchi katika sehemu nyingi za Afrika ya Waafronodi waliamua kuchukua silaha na kupambana na ukoloni. Mapambano hayo yanajumuika katika mapambano ya Vita vya Maji Maji katika Tanzania Bara ya 1905 - 1907 na mapambano ya Waherero ya kipindi hicho yaliyoendeshwa katika Namibia. Hiyo, ni mifano tu ya mapambano yaliyoendeshwa na Waafronodi kwa madhumuni ya kurudisha uhuru na heshima yao. Kwa wakoloni vita hivyo vilikuwa ni maasi.

Kipindi kati ya Vita Kuu ya Kwanza na Vita Kuu ya Pili ni cha kutatanisha hasa kama kisipofanyiwa utafiti wa kutosha. Wakoloni wengi wamekieleza kipindi hiki kama kipindi cha kujiendeleza na kutofautisha"*. Dai hilo si la kweli; nalo lina maana kuwa wananchi hawakujua la kufanya ili kujifunza mbinu kutoka kwa wakoloni. Ukweli ni kuwa muda wote huo wananchi walikuwa katika shughuli za kuendeleza mapambano ya tangu kuingia kwa ukoloni katika Bara hili. Wananchi walirekebisha mbinu zao za mapambano kufuatana na mazingara ya siasa ya wakoloni katika kipindi hiki. Ni dhahiri kuwa vita kama mbinu ya mapambano isingeweza kuwaletea wananchi ushindi na badala yake ingewakatisha tamaa zaidi kwa vile ukoloni ulikwisha jiimarisha katika bara zima. Na hil ni sababu mojawapo ya umoja wa watu wenye asili ya Kiafrika kupitisha uamuzi wa watu kujikomboa kitaifa katika makoloni yao badala ya kupigania uhuru wa bara zima kama taifa moja; jambo ambalo lilionekana kuwa si gumu tu bali lisilowezekana; hasa kwa wakati ule.

Katika kipindi cha kuimarisha utawala wao wa kidhalimu wakoloni hawakuruhusu vyama vya siasa ambavyo ndiyo silaha ya pekee wananchi walibakiwa nayo. Silaha hii ilitokana na kutazama hali halisi ya siasa ya wakoloni na kwa upande ilitokana na elimu ya wakoloni wenyewe. Lakini kitu ambacho wakoloni walivumilia, na wengine waliruhusu, ni kuwepo kwa vyama vya starehe na vya kupigania maslahi sawa ya kiuchumi na walowezi wa Kiyuronodi. Vyama vya wakulima viliundwa ili kupigania bei bora za mazao yao; wafanyakazi viwandani na katika mashamba ya mabepari nao waliunda vyama vyao kwa shabaha ya kupigania mishahara bora na hali njema ya maisha.

Vyama hivyo vya wananchi vilikuwa muhimu sana katika

* J. Illife, *Tanganyika under the German Rule*, Nairobi, Uk. 166 – 200

kuendeleza mapambano ya ukombozi wa kitaifa. Wanahistoria wengi wameshindwa kutambua umuhimu na nguvu ya vyama hivi katika harakati ya mapambano ya uhuru. Hatua hii ni muhimu sana. Vyama hivi viliwafunza wananchi mbinu mbali mbali za kuukabili ukoloni pasipo wakoloni wenyewe kutambua kama wanapigwa vita vya kung'olewa japo si kwa njia ya mkato na ya haraka. Vyama hivi pia vilikuwa muhimu kwa sababu viliwezesha uongozi mpya kujifunza mbinu na njama za ukoloni; na kwa jinsi hii kujifunza mbinu na mkabala mpya wa mapambano.

Jambo jingine ambalo wanahistoria wameshindwa kuliona katika vyama hivyo vya wananchi wanyonge ni kuwa wananchi hao walikuwa hasa katika uwanja wa mapambano na ukoloni kama mpango. Moja ya mbinu za wakoloni ilikuwa ni siasa ya wagawanye upate kuwatawala". Vyama hivi vya wananchi bila ya kujitangaza kuwa vilikuwa katika harakati ya mapambano ya uhuru vilikuwa vinavunja msingi wa siasa hiyo ya wakoloni. Vilikuwa vinavunja misingi ya ubaguzi na mtengano wa kihasama miongoni mwa wananchi kwa kuwashirikisha wananchi wa madhehebu mbali mbali, jamii mbali mbali, wakulima, wafanyabiashara, wafanyakazi, wasomi na wasiosoma. Msingi wa siasa hii ya wakoloni ulikuwa ni matokeo ya ushauri wa Tume ya Elimu kwa Waafronodi ya mtaalam mmoja ajulikanaye kwa jina la Felipo Stoku. Na moja ya kazi kubwa ya maandalio kwa kipindi cha mapambano ya hali ya juu iliyofanywa na vyama vya wananchi wa Kiafronodi katika kipindi hiki ni kupigania elimu bora kwa wananchi wa Kiafronodi ambao Tume ya Felipo ilipendekeza kuwanyima na hatimaye wakanyimwa kweli.

Vita Kuu ya Pili ya mabeberu, bila ya matakwa ya mabeberu wenyewe, ilisaidia sana kuendeleza juhudi na harakati za mapambano ya uhuru wa Waafronodi. Moja ya mbinu zao ikiwa ni kutumia 'siasa ya kutawisha', yaani, kutowaruhusu watu wa koloni moja kutembelea makoloni mengine, hasa kama makoloni hayo yaliendeshwa na mabeberu wa mataifa tofauti. Sababu ya kufanya vile ilikuwa kuwazuia wananchi wa koloni moja kujifunza kutoka kwa wananchi wa makoloni mengine au kulinganisha hali ya maisha ya wananchi katika makoloni mbali mbali. Kitendo hicho na siasa nzima ya kutawisha*, kilikuwa na

---

* 'Siasa ya kutawisha' – hii ilikuwa siasa ya wakoloni ya kuwazuia watu kutoka nje ya makoloni yao; shabaha ikiwa kuzuia mwamko wa siasa ya kitaifa. Wabelgiji waliitumia sana siasa hiyo.

shabaha ya kuwazuia wananchi kupata mzinduko wa kisiasa wa kitaifa. Kwa ufupi, kilikuwa na shabaha ya kuwalaza wananchi kisiasa kwa kuwafanya waridhike na makombo ya wakoloni katika makoloni yao. Kifaranga cha kuku ni kuku na kifaranga cha kwale ni kwale. Kifaranga cha kuku hufugika wakati kifaranga cha kwale hakifugiki. Wananchi hawakuweza kuridhishwa kirahisi hivyo. Muda wote walitambua kuwa wao, Waafronodi, ndio waliokuwa na haki ya kutawala nchi zao.

Wakati wa Vita Kuu ya Pili mabeberu kwa kuogopa kupoteza uhuru wa nchi zao na idadi kubwa ya watu wao walilazimika kuwachukua Waafronodi na kuwapeleka katika sehemu za mapambano au mipakani kama askari. Maana kwao, wakoloni, maisha ya mwanaAfronodi hayakuwa na thamani zaidi ya kuwa chombo muhimu cha kuzalishia mali anapokuwa hai na kutokumhudhunikia anapopoteza uhai wake. Hivyo, wananchi wengi wa Kiafronodi walipelekwa India na Burma ambako vuguvugu na mikikimikiki ya mapambano ya kujikomboa kitaifa ilikuwa moto moto. Pia wananchi walipata fursa ya kuwaelewa kinaganaga na kindani zaidi Wasanodi na hasa Wayuronodi; mbinu, hila na njama zao. Wakati huo huo wakijiuliza kwa nini walikuwa huko mipakani. Hali hiyo ilikuwa mbaya zaidi baada ya askari hao kuruhusiwa kurudi makwao baada ya vita. Kulikuwa na kuonewa na kubaguliwa; na yote hayo yaliendeshwa na wakoloni ambao pia walitokea vitani. Kutokuridhika kulizidi kuongezeka; na katika makoloni mengine askari hao waliungana na wananchi wenye msisimko mkubwa wa kisiasa katika kuunda na kuongoza vyama vilivyoundwa kwa madhumuni hasa ya ukombozi wa wanaAfronodi kutoka minyororo ya ukoloni ili kurudisha hadhi na heshima yao.

Hivyo, kazi ya kwanza ya vyama vya siasa ilikuwa kuvunja miiko na vikwazo mbali mbali vilivyowekwa na wakoloni. Miiko hiyo ilikusudiwa kujenga uadui na uhasama miongoni mwa wanaAfronodi katika koloni moja; pia kujenga uadui kati ya wananchi wa koloni moja na mengine. Viongozi wa mapambano ya uhuru wakitambua yote hayo wakaanza kuzingatia suala la umoja wa kitaifa katika makoloni yao kwa kuwapa wananchi mzinduko na msisimko wa kisiasa wa kitaifa; na papo hapo wakizidi kukuza ushirikiano na uhusiano baina ya vyama mbali mbali vya ukombozi - ambavyo katiba zake zilionekana za kimapinduzi zaidi - katika makoloni mbali mbali.

Kuundwa kwa Umoja wa Mataifa kukiwa ni moja ya matokeo ya Vita Kuu ya Pili kulisaidia kuleta nuru na matumaini mema

kwa wanaAfronodi na wananchi wote wa Dunia ya Tatu.

Katiba ya Umoja huo iliongea juu ya haki za asili za mtu na jamii. Moja ya haki hizo za mtu na jamii ni uhuru wa kujitawala na kujiamulia mambo yao, kitendo ambacho Mwongozo wa TANU umekiita "kitendo cha maendeleo hata kama hakiwaletei shibe au afya."*

Vita Kuu ya Pili ilifanya Jamhuri ya Urusi ijulikane na kuogopwa sana na mabeberu. Urusi iliogopwa kwa sababu mbili. Kwanza kisayansi na kitekinologia, hasa katika kuendeleza suala la zana za vita za kisasa. Urusi ndiyo nchi pekee iliyolingana na Marekani katika maarifa na nguvu za kivita. Marekani ni nchi ya kibeberu na kwa jinsi hiyo ikaanza kutegemewa, na bado inategemewa na dunia yote ya mabeberu, kuendeleza na kudumisha ubeberu. Lakini Urusi, kwa upande mwingine, ilikuwa ni nchi pekee yenye nguvu na uwezo mkubwa wa kujitegemea kwa hali zote za maisha kama nchi ya kijamaa. Siasa na itikadi ya ujamaa ni rahisi sana kueleweka na kupokewa na watu wa Dunia ya Tatu. Urusi ikiwa na sauti kubwa katika Umoja wa Mataifa iliweza kutumia uwezo wake kupigania haki za wanyonge wanaodhulumiwa na kukandamizwa na wanyonyaji katika nchi zao; pia iliweza kupigania utekelezaji wa vifungu vya katiba ya Umoja huo kuhusu suala la watu wa makoloni kujipatia uhuru wao.

Urusi pia iliogopwa na mabeberu ikiwa ni nchi ya kwanza ya kijamaa, kwa siasa na uhusiano wake na nchi za Dunia ya Tatu. Kwa mfano, Urusi iliweza kujiingiza katika na kusaidia mapambano ya Kyuba, Uchina na Korea na kadhalika. Vitendo, siasa na msimamo wa Warusi kuhusu nchi za Dunia ya Tatu, uliwafanya mabeberu waanze kubadili fikara na siasa zao kuhusu makoloni. Hivyo, badala ya kuzingatia mpango wa ukoloni-mkongwe mabeberu wakaanza kuchukua hatua ya kuwaandaa vibaraka wananchi wa kuchukua madaraka ya utawala wa nchi zao chini ya mpango ambao walilazimika kuubuni - nao ni 'ukoloni-mambo-leo'.

Hata hivyo, juhudi za wananchi za kujikomboa kitaifa zilisukumwa na kuimarishwa sana na uhuru wa India na Pakistani mnamo 1948, pia uhuru wa Ghana wa 1957; Ghana ikiwa ni nchi ya kwanza ya Kiafronodi kupata uhuru. Kwa ufupi, mapambano ya kujikomboa kisiasa yaliendeshwa katika makoloni mbali mbali, hasa kati ya miaka 1950 na 1960. Mbinu

---

* TANU, *Mwongozo wa TANU*, Dar es Salaam, Ibara ya 28.

mbali mbali zilitumika katika harakati za mapambano ya ukombozi. Mbinu kubwa na ya kwanza kutumika katika makoloni yote ilikuwa ni kupigania uhuru kwa njia ya vyama vya siasa ambavyo viliendesha mapambano ya kikatiba. Katika makoloni ya Kireno wananchi walinyimwa haki hii ya kuwa na vyama vya siasa, kadhalika wananchi wa Afrika ya Kusini na Zimbabwe ambako viongozi wengi wa siasa wametiwa ndani kama wafungwa wa siasa. Matokeo ya dhuluma hizo zote za ukoloni wa Kireno na wa tawala za walowezi wachache katika Afrika ya Kusini na Zimbabwe ni kuundwa kwa vyama vya wapigania uhuru; ambavyo huendesha mapambano ya vita vya silaha.

Sehemu kubwa ya Afrika sasa imejikomboa kutoka ukoloni — mkongwe. Nchi hizo zote, Tanzania ikiwa ni mojawapo, ziliahidi, tangu wakati wa kupata uhuru na hata kabla kuwa zitapigana na ubeberu na ukoloni mpaka bara zima la Afrika limekombolewa. Hii ilikuwa na maana ya kung'oa serikali za kidhalimu za kikoloni na za walowezi wachache ili kujenga serikali halali za kidemokrasi za walio wengi ambao ni Waafronodi. Ni dhahiri kuwa sehemu kubwa inayokabiliwa na ukoloni-mkongwe kwa hivi sasa katika Afrika ni sehemu ya Afrika ya Waafronodi. Lakini pasipo ubaguzi, Waafrika walishirikiana na kuungana kwa nia njema sana katika kutoa tamko rasmi hilo na kulitilia mkazo nyakati zote, hasa, katika mikutano ya Umoja wa Nchi huru za Afrika.

Umoja huo wa Nchi za Afrika umetoa maazimio mengi mengine ya muhimu tangu kuanzishwa kwake. Hatua hizo zimekuwa za kusisimua sana kwa wanaAfrika wote kila zinapotangazwa. Lakini zimekuwa za kukatisha tamaa kwa wananchi wa mataifa yote ya Afrika na kwa wapigania uhuru kila ilipotakiwa kuchukuliwa hatua za utekelezaji. Serikali za nchi nyingi zimelegalega. Kwa jinsi hiyo zimezitia nchi nyingine, ambazo ni wanachama wa umoja huo, wasiwasi; na kwa hali hii kudhoofisha juhudi za kuimarisha umoja, juhudi za kujenga uhusiano wenye nguvu, na uelewano mwema.

Mnamo 1966, kwa mfano, Umoja wa Nchi huru za Kiafrika uliazimia kuvunja uhusiano wa kisiasa na Uingereza kwa sababu ya kitendo cha Smisi na walowezi wenzake cha mwaka 1965 cha kujitangazia 'uhuru' wa nguvu huko Zimbabwe. Tanzania na nchi chache nyingine ziliweza kutekeleza azimio hilo na kukubali kukabili matatizo yote yatokanayo na uamuzi wao; hasa kwa upande wa Tanzania.

Mwaka 1974 uliazimiwa na chama cha TANU kuwa ni mwaka wa ukombozi wa Bara zima la Afrika ikiwa ni moja ya hatua muhimu za kutekeleza ahadi za Umoja huo. Ukombozi huo hauwezi tu kupatikana kwa misaada ya fedha bali kwa mchango wa watu (askari) na zana za vita. Na hii ni hatua inayongojewa na wananchi wote wa Afrika kuchukuliwa na vyama vya siasa na serikali huru za nchi zao. Kwa kweli nchi huru za Kiafrika zingeungana kwa dhati Afrika yote leo ingekuwa huru kutokana na minyororo ya ukoloni-mkongwe, ukoloni-mamboleo na kukandamizwa na serikali za walowezi. Kiuchumi Afrika ingekuwa inajitegemea kadhalika kitamaduni na kiulinzi.

Kuundwa kwa Umoja wa Nchi huru za Kiafrika peke yake kilikuwa kitendo si cha maendeleo tu bali ilikuwa ni silaha kubwa ya kupambana na udhalimu wa kibeberu na ukoloni-mambo-leo. Lakini kwa bahati mbaya mabeberu si watu waliolala. Ni watu wenye akili na wanazitumia akili hizo vema. Hivyo, baada ya kuona watu wa Afrika wanaungana mara moja wakaanza kujifunza mazingara ya Waafrika ambayo ndiyo msingi wa Umoja wao. Mazingara hayo ni hali ya nchi zao, msimamo wao, utamaduni wao, fikara zao kuhusu uafrika wao, hali ya uchumi wa mataifa mbali mbali; na kadhalika.

Kutokana na utafiti wao mabeberu waliweza kugundua udhaifu na ubovu mwingi kuhusu Umoja huu. Kwanza kabisa kuna watu au mataifa kwa kipindi fulani japokuwa walijiunga na Umoja huo waliukana kabisa Uafrika na wakadiriki kudai kuwa Umoja huo uitwe Umoja wa Nchi huru za Afrika na Malagasi, kwa mfano. Hayo ni makosa. Kusema kweli, katika fikara zao, walichokuwa wakikikana siyo Uafrika bali ni Uafronodi; na kumbe Umoja huo haukuwa wa Waafronodi bali wa Waafrika. Msingi wa watu hao kuukana Uafrika ni matokeo ya kasumba ya Kihamiti. Wao wakijiona kuwa sehemu kubwa ya watu wao wana asili ya Kisanodi au Kiyuronodi na kuwa watu wa jamii hizi tu, ilifundishwa, walikuwa watu bora zaidi kuliko Waafronodi, hivyo ilikuwa ni fedheha kwa upande wao kujiunga katika Umoja wa Nchi huru za Kiafrika bila ya kuongeza neno Malagasi. Watu wa Afrika wote ni wanaAfrika kadhalika watu wa visiwa vya Ngazija, Maurisiusi, Madagaska; na kadhalika, ni wanaAfrika.

Kuna wakati ambapo nchi za kaskazini ya Sahara, kama vile Misri na nchi za Magrebu, zimeonyesha fikara za kimapinduzi sana na hata kuchukua nafasi ya mstari wa mbele kabisa katika kuunda na kuimarisha Umoja wa Nchi huru za Kiafrika. Nchi au

taifa huundwa na watu. Lakini fikara za kuongoza taifa mara nyingi hutokana na wachache ambao mara nyingi ni viongozi. Fikara hizo huwa ni za watu wakati watu wenyewe wanapoziunga mkono kwa dhati. Wakati mwingine wananchi hulazimishwa kwa sababu ya hali halisi, kwa mfano, jeshi linapojitwalia madaraka kwa nguvu, kuziunga mkono na kuzihalalisha fikara za wachache japokuwa kwa shingo upande. Kwa sababu ya mabadiliko ya kiserikali mara nyingi nchi zilizokuwa katika mstari wa mbele katika Umoja wa Nchi huru za Kiafrika zimekuwa na fikara na msimamo tofauti.

Badala ya kuzingatia na kukuza fikara za Uafrika baadhi ya nchi au serikali katika vipindi mbali mbali zimeanza kukuza fikara na tabia za Kiafronodi na Kisanodi. Kwa jinsi hii Waafrika hujigawa na kujibagua katika msingi wa Uafronodi na Usanodi. Hali hii ni ya kufurahisha sana kwa mabeberu ambao huitumia na kuiimarisha; maana kihistoria siasa ya wakoloni imekuwa 'wagawanye upate kuwatawala'.

Wakoloni pia wamegundua kuwa Waafrika na viongozi wa serikali za nchi huru za Kiafrika ni maskini. Kwa sababu ya umaskini wao mara nyingi wameelekea kuonyesha fikara, tabia na tamaa za kibepari na ubinafsi. Wakoloni hufurahishwa na kuitumia sana hali ya aina hiyo. Huwateka viongozi hao na kuwatumia kama vibaraka kwa faida yao; mradi tu wakiwahakikishia kiasi fulani cha makombo. Kwa hiyo, hata kama nchi hizo zimo katika Umoja wa Nchi huru za Kiafrika, viongozi wake hujumuika katika umoja huo siyo kama wazalendo na wanamapinduzi wa Afrika bali kama vibaraka wa mabeberu; na wala hawawezi kutegemewa kutekeleza maazimio ya Umoja huu.

Katika nchi ambayo viongozi wake wana msimamo thabiti wa kimapinduzi wakoloni huwatayarisha baadhi ya wananchi kama vibaraka wao. Vibaraka hao mara nyingi hupatikana kwa urahisi kwa sababu ya unyonge wao na pengine kwa sababu ya kukosa mzinduko wa kutosha wa kisiasa wa kitaifa. Kama ilivyoelezwa, kwa sababu ya umaskini na ujinga wananchi hao maskini nao hukuza tabia, fikara na tamaa za kibinafsi na unyonyaji. Mabeberu nao hutumia mafungu makubwa ya pesa kuwatafuta, kuwaandaa na kuwalinda vibaraka hao; na kuwapa kila msaada ili kuwawezesha kuangusha serikali halali za wananchi. Vitendo vya kuangusha serikali halali vinapotokea huleta mfarakano na uhasama miongoni mwa nchi huru za Kiafrika; na papo hapo hubadili na kupotosha siasa na msimamo wa nchi hizo kuhusu suala la Umoja wa Nchi huru za Kiafrika. Hivyo, ni dhahiri

kabisa kuwa hali kama hii, ambayo imepata kuikabili sehemu kubwa ya Afrika huru, imesaidia sana kudhoofisha juhudi za Umoja huo za kulinda uhuru wa nchi zake, kuendeleza juhudi za kuzikomboa sehemu ambazo bado zinakabiliwa na ukoloni-mkongwe na serikali za kidhalimu za walowezi kwa shabaha ya kustawisha hali ya maisha ya wananchi.

Udhaifu mwingine wa Umoja huu unatokana na tofauti ya itikadi na dini ambayo ni sehemu muhimu sana ya utamaduni. Nchi za Kiafrika zilitawaliwa na mabeberu ambao ni mabepari. Hivyo, wananchi wanapokabidhiwa madaraka ya kujitawala hurithi si umbile tu la serikali za kikoloni bali hata siasa yao ambayo ni ya kibepari. Siasa ya kibepari huimarisha unyonyaji, ubinafsi na udhalimu. Baadhi ya nchi hizo baadaye hubadili siasa yao kwa kuchagua itikadi ya ujamaa. Kwa hiyo, katika Afrika leo kuna nchi ambazo zinaongozwa na itikadi ya ubepari na zile zinazoongozwa na itikadi ya ujamaa. Tofauti hii ya itikadi hujenga mazingara ya kuvutia sana kwa mabeberu ambao huyatumia sana kwa kuwagonganisha na kuwafanya watu wa Afrika wafarakane kwa uhasama usio na msingi. Umoja wa Afrika unaweza kabisa kujengeka na kuimarishwa pasipo kujali itikadi. Lakini kwa kuwa nchi zote huru za Kiafrika zimepitia katika tanuru la ukoloni zimejumuika katika nchi za Dunia ya Tatu. Na kama ilivyopata kusisitizwa mara yote kuwa itikadi ya pekee itakayodhamanisha maendeleo na ustawi wa watu wa Dunia ya Tatu ni itikadi ya ujamaa. Kwa hiyo, njia moja ya kuimarisha Umoja wa Nchi huru za Kiafrika na suala la ushirikiano na nchi nyingine katika Dunia ya Tatu nje ya Afrika ni nchi zote za Kiafrika kuamua kujenga ujamaa. Hilo lingekuwa ni pigo kubwa sana kwa wakoloni. Kuamua kujenga ujamaa si rahisi. Ni kujitoa sadaka kwa upande wa viongozi wa aina zote katika taifa pamoja na wote wanaojumuika katika tabaka la wanyonyaji. Ingawa ujamaa ni imani, na kwamba hata maskini wanaweza kuwa wanyonyaji kifikara, ni rahisi sana kwa watu wanaoongozwa, ambao kusema kweli ni wanyonge, kuupokea ujamaa.

Ni jambo la kusikitisha pia kuona tabia za nchi nyingi za Kiafrika, hasa zile ambazo sehemu kubwa ya jamii zake zina asili ya Kisanodi, hujibagua. Nchi hizo hujiita, kwa mfano, Jamhuri ya Muungano ya Waarabu, kwa mfano, Misri hapo mwanzoni; Jamhuri ya Muungano wa Waislam (Libya, Tunisia na kadhalika), muungano ambao umeshindikana au umoja wa jamii za Kiarabu.

Vitendo hivyo vya baadhi ya nchi za Kiafrika vina matokeo yasiyoridhisha kuhusu Umoja wa Nchi za Afrika tena vinadhihirisha fikara za viongzi wa nchi hizo kuthamini zaidi Usanodi kuliko Uafrika. Waarabu wa nchi halisi za Kiarabu (Arabia na Mashariki ya Kati) wangekuwa sahihi kabisa kukuza fikara hizo za Usanodi ambazo zingeweza kuwa msingi bora zaidi wa muungano na ushirikiano baina yao. Kadhalika watu wote wa Afrika hawana budi kukuza fikara za Uafrika wakisahau Uafronodi, Uyuronodi na Usanodi, kwa madhumuni ya kujenga umoja wenye nguvu wa Nchi huru za Kiafrika; papo hapo zikiwatambua na kuwajumlisha Waafrika wote ambao bado wanatawaliwa na kukandamizwa na serikali za kidhalimu za walowezi wachache.

Nchi za Kiafrika, yaani, ukijumlisha nchi zilizo kusini na kaskazini ya Sahara na nchi za Kiarabu, yaani, ukijumlisha nchi zote za Arabia na Mashariki ya Kati zingeweza kujenga uhusiano na umoja wenye nguvu sana kwa misingi ya Uafrika na Usanodi. Na kwa jinsi hii wangeweza kusimama imara sana katika mapambano yao na ukoloni-mkongwe, ukoloni-mamboleo na unyonyaji wa kibeberu. Ushahidi wa ushirikiano mzuri ni uamuzi wa Nchi huru za Kiafrika kuunga mkono hatua zilizochukuliwa na nchi za Kiarabu (pamoja na baadhi ya nchi za Kiafrika) kutumia mafuta kama silaha ya kupambana na mabeberu katika kutatua tatizo la Mashariki ya Kati; ikiwa ni pamoja na kusaidia ukombozi wa Afrika. Hata hivyo, uamuzi huo unaweza kupotosha lengo na shabaha iwapo mafuta yatachukuliwa kwa madhumuni ya kuzinufaisha nchi zinazotoa mafuta kukuza uchumi wake kwa kuzinyonya hata nchi zile zinazounga mkono azimio hilo.

Mbali na itikadi na vikwazo vingine vinavyodhoofisha Umoja wa Nchi huru za Kiafrika kuna suala la viongozi. Viongozi ni Watu. Wana tabia na fikara zinazotofautiana. Tofauti hizo pengine huingilia siyo misimamo yao tu kama watu bali huingilia pia misimamo yao kisiasa kama viongozi wa mataifa yao. Na kwa sababu hiyo hiyo, kila kiongozi hujitahidi sana kuonyesha ukubwa wake, ubingwa wake wa siasa hata kama itabidi kujitambulisha na mabeberu na kudhoofisha juhudi za umoja. Njia moja iliyobaki kwa wanaAfrika ni kujifunza vipengele hivyo vyote vya mazingara; kukamilisha umoja; kusahau Uafronodi na Usanodi (kwa watu wa Afrika wenye asili ya Kiyuronodi na Kisanodi); kukuza na kudumisha fikara za juu zaidi za Uafrika; pamoja na kubuni mbinu mpya za kupambana na mabeberu na njama zao. Umoja mathubuti ndiyo dhamana ya maendeleo ya

wanaAfrika; pia ni fanaka ya juhudi za ukombozi wa wote wana-otawaliwa na kunyonywa katika dunia nzima.

Sura ya 14

UHURU NA MAENDELEO YA MATAIFA 'HURU' YA KIAFRIKA

"Uhuru" na "Maendeleo" siku zote ni matokeo ya mapambano ya mtu au jamii na aina fulani ya mazingara. Uhuru wa kisiasa, ukiwa wenyewe ni sehemu moja ya maendeleo, hutangutia maendeleo ya aina zote nyingine. Kwa hiyo, uhuru huo wa kisiasa hauna budi kulindwa kwa shabaha ya kuendeleza amani na usalama. Pia uhuru ukiwa ni urithi wenye thamani isiyokadirika, unaweza tu kuwa na maana kwa mtu au jamii iwapo uhuru wenyewe utaeleweka kuwa ni 'nguvu' muhimu ya kusukuma na kuharakisha maendeleo ya watu. Kwa msingi huu ni wazi kuwa ingawa leo nchi nyingi zimejikomboa kutokana na minyororo ya ukoloni-mkongwe bado hazijawa kuwa 'huru' kwa sababu moja kubwa – 'uhuru' au 'kujitawala, kwa nchi hizo kisiasa hakujawa kutumiwa kama nguvu ya kusukuma maendeleo ya watu. Na katika nchi nyingi 'uhuru' wa 'kujitawala' au wa kutokana na ukoloni-mkongwe umekuwa ni 'nguvu' ya kurudisha nyuma maendeleo ya watu na ya 'taifa' kwa ujumla.

Msingi huu ni mzuri wa kuanzia mjadala wa somo hili maana unawezesha kutoa tofauti baina ya nchi zilizopata 'uhuru' wa kisiasa kutoka kwa wakoloni kwa njia ya mapambano ya kikatiba kwa upande mmoja na ya kivita kwa upande mwingine; na pia kutofautisha uhuru wa nchi hizo na uhuru wa mataifa ya kibeberu, kwa kawaida ni mataifa ya Kiyuronodi.

Wakati nchi nyingi za Kiafrika na Kisanodi zikiwa bado ni makoloni suala la ulinzi wa kitaifa halikuwa muhimu na wala halikuwahusu wananchi. Mataifa yaliyotawala makoloni hayo yalihusikana na suala la kuhakikisha 'amani na usalama'. Kwa msingi huo wakoloni waliimarisha jeshi la usalama, yaani, polisi pamoja na wapelelezi wa makosa ya jinai. Hata hivyo, iko haja ya kuelezea kwa makini kuhusu maana halisi ya kifungu hicho cha maneno: 'amani na usalama'. Suala la kuwafundisha wananchi kuwa macho halikutiwa maanani.

Kwa mkoloni 'amani na usalama' kulikuwa na maana ya kuwaweka wananchi katika hali ya woga na wasiwasi, hofu na mashaka, kunyenyekea, kutojiamini, kukubali kukandamizwa, kusumbuliwa, kupuuzwa na kutumikishwa. Matokeo ya hayo yote ni hali ya utulivu katika makoloni ambayo iliwawezesha wakoloni kuwatumikisha na kuwanyonya wananchi wake pasipo matatizo, hofu wala wasiwasi. Hii ndiyo maana ya 'amani na usalama' kama ilivyoongelewa na wakoloni; na ndio hasa shabaha ya jeshi la polisi, kwa wakati huo.

Suala la ulinzi wa nchi halikuwa muhimu sana. Wakoloni hata hivyo, waliweka vikundi vidogo vidogo vya majeshi ya ulinzi katika makoloni yao. Shabaha ya vikundi hivyo ni kuhakikisha ulinzi wa dola zao zinapovamiwa na majeshi ya mabeberu wa dola nyingine. Majeshi hayo; kwa maneno mengine, hayakuundwa kwa manufaa ya makoloni. Na ndiyo maana wakati wa Vita Kuu ya Kwanza na ya Pili wananchi wengi kutoka katika makoloni walichukuliwa kwa nguvu kuungana na vikundi hivyo vya kudumu vya wanajeshi na kwenda kupigania uhuru wa dola za wakoloni. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba majeshi yote ya usalama na ulinzi, katika makoloni yalikuwa na shabaha ya kuhakikisha 'amani na usalama na uhuru' wa wakubwa, yaani, wakoloni pamoja na mali' na dola zao. Kwa upande mwingine, majeshi hayo yalikuwa ni vyombo muhimu vya kuwakandamizia wananchi na kuwatia katika hali ya wasiwasi na unyonge.

"Uhuru" katika nchi zilizojikomboa kisiasa hupewa maelezo tofauti. "Uhuru" una maana ya kutoa uwezo kwa wananchi wa kuamua, kupanga na kutekeleza mambo yao wenyewe kama watu au kama taifa. Uwezo wa aina hii ndio peke yake utakaohakikisha na kuharakisha maendeleo ya 'wananchi', na ya taifa kutegemea 'itikadi' ya nchi inayohusika. Hii ina maana kuwa taifa linaweza kukuza sana uchumi wake, lakini, iwapo taifa hilo linaongozwa na kutawaliwa na itikadi ya kibepari, basi, uchumi huo utafaidiwa na wachache tu katika taifa hilo. Walakini kama wananchi wanaamini na kwamba wameamua kuongozwa na itikadi ya 'ujamaa na kujitegemea', basi, uchumi watakaozalisha utakuwa kwa manufaa na maendeleo ya watu wote na kwa taifa zima. Na kusema kweli siasa hii ya ujamaa ndiyo peke yake inayoweza kutoa maana halisi ya uhuru. Kinyume chake ni upotovu wa maana ya uhuru na wajanja wachache kwa manufaa yao.

Kadhalika 'amani na usalama' katika nchi inayojitawala hupewa maelezo tofauti. Ina maana kuwa wananchi waishi

pasipo bugudhi, woga, mashaka, hofu au wasiwasi wa maisha na wa mali zao kama watu binafsi au kama taifa. Amani na usalama iwe ni kinyume cha kunyanyasa, kutisha, kukandamiza na kunyonya. Kwa hiyo, uhuru, amani na usalama havina budi kuwa kwa manufaa ya watu au ya walio wengi.

Ili lengo hili liweze kufikiwa watu wenyewe hawana budi kujijengea nidhamu ya dhati ambayo ni ya kukiuka. Lakini kufikiria kuwa taifa linaweza kukuza nidhamu kubwa kiasi cha kudumisha amani na usalama wa watu, mali zao na nchi kwa ujumla, ni kutumaini mno kupita mipaka ya uwezo wa wananchi. Taifa ni watu. Tabia za watu katika jamii au taifa lolote hutofautiana. Na kadiri taifa linavyozidi kuendelea kiuchumi ndivyo tabia na fikara za watu wake zinavyozidi kutofautiana zaidi na zaidi. Wavivu na wenye juhudi hudhihirika. Watu wenye fikara mbaya nao hujitokeza; kwa kuwa wavivu na wenye tamaa za binafsi nao hupenda maisha bora, basi, tabia na fikara za wavivu na wenye tamaa za ubinafsi hukubaliana kiasi fulani; nao huunda magenge ili kuharibu uhuru, amani na usalama wa watu wanaoelewa na kutafuta maendeleo kwa njia ya mapambano na mazingara. Kikundi cha wavivu na wenye tamaa za ubinafsi hutaalamika zaidi na zaidi katika mbinu za wizi, unyang'anyi, ujahili, ujambazi, na hatimaye kuhalalisha suala la unyonyaji.

Wajibu wa vyama vya siasa na serikali zao umekuwa ni kuhakikisha amani na usalama wa wananchi ili kuwawezesha kuendeleza mapambano yao ya kuleta maendeleo kwa kuzalisha mali kwa wingi zaidi na zaidi pasipo hofu. Kwa nchi inayoamini siasa ya ujamaa na kujitegemea wajibu huo wa vyama vya siasa na serikali zao huvuka mipaka katika shabaha na lengo. Kwa wajamaa, shabaha ya 'amani na usalama' ni kuwaondoa wananchi katika hali ya hofu na wasiwasi ili kuwawezesha kuendeleza mapambano ya kuendeleza, kwa nafasi ya kwanza, maisha yao wenyewe na hatimaye taifa zima. Hata hivyo, bila ya kujali aina ya itikadi vyama vyote vya siasa na serikali katika taifa linalojitawala hulazimika kuweka sheria za kuhakikisha amani na usalama wa taifa; pamoja na kuunda vyombo vya kusimamia utekelezaji wake. Vyombo vya kulinda amani na usalama ni majeshi ya usalama' ambayo mara nyingi ni mapolisi. Katika Afrika, majeshi hayo yaliundwa na wakoloni kwa shabaha ya kulinda maslahi ya mabeberu kwa kuwakandamiza, kuwaghasi na kuwatumikisha wananchi. Kwa mabeberu majeshi yote yalikuwa ni chombo muhimu cha kurahisishia shughuli nzima ya unyonyaji. Kwa jinsi hiyo, muundo, mwenendo, tabia na fikara za majeshi hayo

hubaki kuwa za ukibaraka; na kila mara hujitahidi kujitambulisha na mabwana wao wa zamani (wakoloni) ambao wamekwisha ondoka kimwili. Inayawia vigumu sana majeshi hayo kuchukua hatua za kimapinduzi za kuweza kurekebisha shabaha za huduma zake, muundo wake, mwenendo wake na fikara zake ili kulingana na hali mpya ya taifa 'huru'.

Kwa upande mmoja, majeshi hayo yanaweza kusamehewa kwa kushindwa kuchukua hatua za kimapinduzi kwa sababu kubwa mbili. Sababu ya kwanza wanajeshi hao walioajiriwa na wakoloni mara nyingi walikuwa watu wenye kiwango cha chini sana cha elimu na wengi wao hawakusoma kabisa.

Hivyo upeo wa maarifa yao kuhusu ulimwengu ulikuwa ni mfupi sana. Polisi, kwa sababu ya kufunzwa na wakoloni, kasumba za kikoloni zilikuwa zimewakolea mno; na kwa jinsi kuwawia vigumu sana wanajeshi hao kuweza kuzindukana nazo bila ya kupata msukumo wa watu wengine kutoka nje ya taasisi zao.

Hali hiyo ya majeshi ya usalama ilifanana sana na hali ya majeshi ya 'ulinzi' wa nchi ambayo mataifa 'huru' yaliyarithi kutoka kwa serikali za kikoloni. Badala ya kulinda nchi na watu wake, pamoja na vyama vya ukombozi na serikali, majeshi yalijitenga na wananchi, vyama vya siasa na serikali. Fikara za majeshi kama ilivyopata kudhihirika, zimekuwa kuangusha serikali halali za wananchi na kupiga marufuku vyama vya siasa vya wananchi ambavyo vimepata kufanya kazi kubwa ya kuwaongoza wananchi katika kuendesha mapambano ya ukombozi hadi kuzipatia nchi zao uhuru wa kisiasa. Kuangushwa kwa serikali halali mara nyingi kumesababishwa na tabia za ubinafsi, yaani, uchoyo. Japokuwa tabia, mwenendo na fikara hizo ni za kurithi kutoka kwa wakoloni, majeshi ya wakoloni wenyewe huko makwao hayana tabia hiyo ya kuangusha ovyo serikali za nchi zao kwa sababu yanaelewa na kutambua kuwa tabia hiyo huleta vurugu katika taifa na kwa jinsi hiyo kurudisha nyuma maendeleo ya taifa zima kimizania.

Majeshi ya mabeberu yanatambua wajibu wao wa kulinda siasa na maslahi ya serikali zao ambazo ni za kibepari. Kwa hiyo, ni sahihi kwa majeshi hayo kujimudu kwa jinsi hiyo maana yameundwa kwa madhumuni yayo hayo.

Majeshi ya nchi changa yanatazamiwa kuwa majeshi ya wananchi yakiwa na shabaha na lengo la kulikomboa taifa, kudumisha amani na usalama na kulinda uhuru wa taifa; na siyo kutumikia kikundi cha wanyonyaji wachache katika taifa. Mara

nyingi majeshi yamejaribu kuhalalisha vitendo vya kuangusha serikali halali za wananchi kwa kutumia lugha ya 'mapinduzi'. Lakini utafiti wa ndani umedhihirisha kuwa vitendo hivyo vya majeshi mengi kuangusha serikali halali za watu si vya kimapinduzi hata kidogo. Mapinduzi ya kweli hutokana na watu, huendeshwa na watu wenyewe wakisaidiwa na majeshi iwapo ni lazima. Mfano mzuri wa mapinduzi ya kweli ni kitendo cha wananchi wa Zanzibar cha Januari 12, 1964, cha kupindua serikali ya kidhalimu ya kibaraka Sultani.

Tofauti kati ya mapinduzi na kuangusha serikali ni kubwa sana. Mapinduzi maana yake ni kuangusha serikali ya wadhalimu wachache na kuweka madaraka mikononi mwa umma wa wafanyakazi na wakulima kwa minajiri ya kuharakisha maendeleo ya umma wenyewe kwa kujenga mfumo wa kijamaa. Kuangusha serikali kunatokea wakati kikundi cha wachache kinapotwaa madaraka kwa nguvu ya kijeshi kutoka kwa umma wa wananchi au kutoka kwa kikundi kingine cha wanyonyaji kwa shabaha ya kujinufaisha na kujiendeleza chenyewe kwa kukandamiza umma wa walio wengi nchini. Hata hivyo, hapana budi kukumbuka kuwa katika kuleta mapinduzi siyo lazima kuangusha serikali. Mapinduzi ni vita ambayo inaweza kuendeshwa kifikara, kiitikadi, kiuchumi, kielimu na kadhalika.

Kwa muda mrefu suala la ulinzi wa taifa halikutiliwa maanani sana na viongozi wa siasa na serikali. Hasa katika nchi ambazo zilipata uhuru kwa njia ya katiba, yaani, pasipo kumwaga damu. Mfano mzuri ni nchi ya Tanzania Bara ilivyopata uhuru mnamo 1961. TANU, kama vyama vingine vya kimapinduzi vya ukombozi katika Afrika inayojitawala kisiasa, haikuchukuwa hatua zo zote za kuleta mapinduzi katika jeshi ambalo ilirithi kutoka kwa Waingereza ili kulifanya jeshi hilo kuwa la wananchi na kuwajibika kwao. TANU yenyewe ilizinduliwa na tukio la aibu la maasi ya jeshi hilo la 1964. Ni baada tu ya hapo ndipo TANU ikalazimika kuchukua hatua muhimu za kufafanua vipya shabaha za jeshi, kuliunda vipya, kulipa sura na muundo uliofanana na siasa ya nchi ambayo ni siasa ya TANU. Hata hivyo, hatua muhimu zaidi zilichukuliwa baada ya 'Azimio la Arusha' kwa kutoa elimu ya siasa kwa wanajeshi wa daraja zote na kwa kulishirikisha na wananchi. Elimu ya siasa imesaidia sana kulipa jeshi mwamko mkubwa wa siasa ya kitaifa na moyo wa kizalendo; na kwa hivi sasa moyo wa kijamaa. Kitendo cha watu kutoroka nchini, kuiba ndege, kuiba au kuharibiwa kwa mali ya umma vyote vinadhihirisha kuwa suala la 'kuwa macho' katika ulinzi wa sehemu zote

za maisha ya watu halikutiliwa mkazo uliostahili. Hata hivyo, hatua za ulinzi zilizochukuliwa na TANU baada ya Mwongozo wa 1971 za kupanua zaidi maana ya ulinzi kwa kuwashirikisha wananchi kwa mpango wa 'Ulinzi wa Mgambo', ilikuwa muhimu sana. Ulinzi wa mgambo ni kitu kipya. Ni jambo jipya katika maana ya kuunganisha ulinzi wa majeshi yetu ya kudumu na ulinzi wa wazalendo wa nchi zao. Hii ni mbinu mpya kwa sababu Ulinzi wa Mgambo umeanzishwa kwa mpango wa kisiasa kwa maana kwamba wananchi huandaliwa kwanza kwa njia ya elimu ya siasa. Pia mpango wenyewe ni wa kimapinduzi kwa sababu una shabaha ya kulinda uhuru wa taifa, mali ya taifa, pia kulinda na kuimarisha siasa na uongozi wa TANU: TANU ikiwa ndicho Chama chao cha pekee. Na katika sehemu nyingine za Afrika shabaha ya Ulinzi wa Mgambo ni kama zizo hizo.

Kwa ufupi, majeshi katika nchi huru lazima yawe ya watu na kwa manufaa ya watu wenyewe kama taifa. Matakwa hayo hayatoshi mpaka hatua ya kuyaelimisha majeshi yenyewe kiitikadi (kisiasa) na kuyapa muundo mpya zimechukuliwa. Hayo yote yakitekelezwa kikamilifu, basi, majeshi hayo yatakuwa yanawajibika na ulinzi wa uhuru, amani na usalama' wa wananchi na mali zao. Kwa jinsi hiyo, majeshi yatahakikisha na kuharakisha maendeleo na hali bora za maisha ya wananchi.

Hapo awali ilielezwa kuwa historia ni somo lenye uhai. Kwa hiyo, umaarufu wake hauna budi kuonyeshwa kwa jinsi inavyoweza kusaidia kusukuma maendeleo ya watu. Pia imeelezwa kuwa maendeleo ni matokeo ya kazi na kwamba kazi hii ya maendeleo inayoongelewa siku zote itakuwa ni matokeo ya mapambano ya watu au jamii na mazingara. Lengo la mapambano hayo ni kumwondoa mtu au jamii katika unyonge.

Unyonge ni hali iliyozipata jamii zote duniani tangu mtu wa kwanza. Lakini kutegemea mazingara na hatua za mapambano jamii nyingi duniani zimeondokana kwa sehemu kubwa sana na unyonge. Na hizo ni jamii ambazo zasemekana zimeendelea. Jamii ambazo zimo bado katika hatua za mwanzo za mapambano ya maendeleo zaweza kuitwa jamii zilizo nyuma kimaendeleo na ambazo bado zinakabiliwa, kwa sehemu kubwa, na unyonge. Jamii za Kiafrika hujumuika katika kundi hili.

Unyonge wa Mwafrika umesababishwa na hali tofauti ya mazingara. Afrika ina mazingara tajiri na yenye kuvutia. Lakini watu wake ni maskini na wanyonge. Afrika ina mvua ya kutosha, maji mengi ya mito na maziwa, misitu ya mali,

mabonde na ardhi ya kutosha ya kustawisha mazao ya aina mbali mbali. Pia Afrika ina madini mengi ya thamani pamoja na mafuta ambayo leo ni muhimu sana katika kuzalisha nguvu muhimu kwa maendeleo.

Sababu za Afrika kubaki nyuma na kukabiliwa na unyonge hazina budi kueleweka kwanza kinaganaga kabla ya kuanza kufikiria hatua za kupanga maendeleo. Ni wazi kuwa jamii za Ulaya kati ya karne ya kumi na tano na kumi na tisa zilikuwa zimepiga hatua kubwa zaidi ya maendeleo katika ulimwengu wa sayansi na tekinologia kulinganisha na maendeleo ya jamii nyingi za Kiafrika na za sehemu nyingine za dunia. Sehemu kubwa ya asili ya maendeleo hayo ni Afrika, hasa Afrika ya kaskazini ya wakati wa Waafronodi. Kwa mfano, maarifa ya maandishi, mahesabu na kadhalika yalianzia Afrika. Hata hivyo, maendeleo hayo ya Waafronodi yalikatishwa kuanzia karne ya kumi na sita hadi kumi na tisa na kipengele cha mazingara: 'Biashara ya Watumwa'. Na kuanzia karne ya kumi na tisa mpaka karne ya ishirini maendeleo ya wanaAfrika yamedhoofishwa na kurudishwa nyuma na baa la ubeberu na ukoloni mkongwe; na kwa hivi sasa, hasa kwa nchi zilizojitawala, na ukoloni-mambo-leo. Ukoloni mkongwe na ukoloni-mamboleo wote hufanya kipengele cha mazingara ya Mwafrika.

Biashara ya watumwa ilirudisha nyuma maendeleo ya wa-Afronodi na kuwaingiza katika unyonge zaidi. Kwanza, biashara hii iliwachukua wana-Afronodi wenye nguvu, akili safi, uwezo mkubwa wa kuzaa na kujenga jamii zenye nguvu zaidi za baadaye ili kuwauza na kuwatumikisha katika mapambano ya kuleta maendeleo ya mataifa na hasa ya tabaka la wanyonyaji wa Ulaya katika nchi za kigeni. Kiidadi ilikuwa vigumu sana kwa waAfronodi kuongezeka. Na kwa kuwa watu waliobakizwa nyuma ni wazee na vilema ni dhahiri kuwa watoto waliowazaa katika hali ya unyonge: afya mbaya, maradhi, ujinga na umaskini, na kadhalika — walikuwa wanyonge pia. Kitendo cha wanaAfronodi kuuzwa sokoni kama samaki kiliteremsha hadhi yao, kikawafanya wanyenyekevu kupita kiasi na kutojiamini. Hata hivyo, wana-Afronodi walipambana na hali hii humu humu nchini na huko ugenini walikopelekwa kwa kiasi cha kufanya shughuli nzima ionekane aghali sana kwa vile mara nyingi iligharimu maisha ya wanyonyaji wenyewe na vibaraka wao. Mapambano hayo yalichukuliwa na mabepari kama ni moja ya sababu muhimu za kukomesha biashara ya watumwa na 'utumwa' katika karne ya kumi na tisa japokuwa sababu kubwa ilikuwa kukua kwa ubepari

na ubeberu.

Pili, ukoloni nao ulizuia kuongezeka kwa wanaAfrika kwa kuwakamua hata tone la mwisho la damu yao. Wakoloni wakawafukuzia wananchi katika sehemu kame, wakajitwalia ardhi yenye rutuba huku wananchi wakikabiliwa na njaa. Wakoloni wakawapika wananchi kasumba za aina nyingi. Waliwafanya wasijiamini kuhusu uwezo wao; na badala yake kuwafanya wawategemee Wayuronodi ambao ni mabepari na mabeberu wakubwa wa dunia. Wakoloni waliwafanya wana-Afronodi waamini kuwa kazi ya kuzalisha mali ilikuwa ni laana; nayo ni kwa ajili ya waliolaaniwa.

Elimu ilieleweka kuwa ni njia ya kuondokana na 'kazi' na kufarakana na watu wanaokabiliwa na unyonge; na kwamba elimu ilikuwa ni njia ya kuwanyonyea, kuwanyanyasia na kuwakandamizia wananchi wanyonge. Fikara nyingine yenye kasumba ya kikoloni ni kuwa elimu ilifikiriwa kuwa ni haki ya wachache; na kwamba wachache hao tu ndio wenye uwezo na akili za asili; na kwa hiyo, kazi ambayo wasomi wanastahili kufanya ni kazi ya kukaa maofisini na kuvaa masuti. Ofisi zenyewe hazikufikiriwa kuwa ni mahali tu pa kurahisishia shughuli mbali mbali za manufaa kwa wananchi. Ubinafsi, ni kasumba nyingine ambayo wanaAfronodi walipikwa kwa ukamilifu sana. Na mbaya zaidi kuliko zote ni kasumba ya kuamini kuwa unyonge, yaani, umaskini, ujinga, afya mbaya kutokana na utovu wa chakula bora cha kutosha na kadhalika — ni adhabu ya maisha ya MwanaAfronodi kutokana na laana ya Mungu; na kwamba unyonyaji, udhalimu, maisha bora na hadhi ya juu ni haki ya asili ya mabeberu na vibaraka wao wa ndani. Kwa maneno mengine, wakoloni walifanya wanaAfronodi waamini kuwa huo ulikuwa ni mpango uliohalalishwa na Mwenyezi Mungu.

Ili Mwana-Afronodi aweza kuondokana na unyonge baada ya kuung'oa ukoloni mkongwe; na kisha kutambua kuwepo kwa mbinu za mabeberu katika kuendeleza ukoloni-mambo-leo hapana budi kuchukuliwa hatua zaidi za mapambano ya kuleta maendeleo yakinifu ya watu.

Maendeleo ni kipimo cha kiwango kilichofikiwa na mtu au jamii katika mapambano yake na mazingara. Kwa ufupi, maendeleo ni kipimo cha kiasi cha matokeo ya kazi iliyofanyika. Jamii au taifa hujiendeleza katika njia nyingi. Maendeleo ya mtu huonekana katika umbile lake, fikara zake, utamaduni wake, na katika ulimwengu wa sayansi na tekinologia.

Maarifa ya sayansi na tekinologia ndiyo msingi wa maendeleo

ya aina zote. Mtu au jamii hutumia maarifa hayo, ambayo pia ni matokeo ya kazi ya mapambano, katika kutengeneza zana na vifaa mbali mbali, au kuzalisha nguvu, ambayo pia ni muhimu sana katika shughuli nzima ya uzalishaji mali na ustawi wa jamii.

Mtu kwa mamilioni ya miaka amepambana na mazingara yake kwa taabu akitumia vyombo na zana duni sana. Hivyo, kadiri miaka ilivyopita na ndivyo mtu alivyojiendeleza katika maarifa na ufundi wa aina nyingi. Mpaka leo mtu amefikia hatua ya juu sana ya maendeleo hasa katika ulimwengu wa kisayansi na tekinologia; na zaidi katika kulimbikiza maarifa na ujuzi. Maarifa ya kutengeneza vyombo kama: ndege, meli, garimoshi, motokaa, baiskeli, zana za vita, ujenzi wa majumba ya kisasa, vifaa na vyombo vya nyumbani; na kadhalika ni urithi mkubwa wa mtu; nao ni wa kudumu maisha yote ya mtu. Jamii ambazo hazijapata kulimbikiza maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusu ufundi wa taaluma mbali mbali nazo pia hunufaika na maarifa hayo ya mtu kutoka katika jamii za sehemu mbali mbali. Hivyo, hata jamii zisizopiga hatua ya kutosha hazina haja ya kurudi nyuma na kuanza safari ndefu za kulimbikiza maarifa na ujuzi ili kuzifikia jamii zilizoendelea. Jambo la maana ni kuanzisha mipango ambayo inaweza kuharakisha mapambano na kubadilisha sura ya maisha ya jamii kwa haraka.

Kazi ikiwa ndio msingi wa maendeleo ndicho kitu peke yake kilichompatia mtu ushindi mkubwa kuliko wanyama na vitu vingine vyote vyenye uhai. Kutokana na kitu kazi mtu anaweza kuendeleza kwa mafanikio makubwa kizazi chake po pote katika dunia wakati ambapo wanyama na vitu vingine vingi vyenye uhai vimefifia na kufutika kabisa katika uso wa dunia hii.

Licha ya kudumisha na kuendeleza kizazi chake mtu amefaulu sana kujiendeleza kiidadi katika vipindi mbali mbali vya kihistoria hata kufikia wakati wa kuamua kupanga uzazi wa majira. Kupanga uzazi wa majira nayo ni maendeleo ya aina ya pekee ya mtu. Kuongezeka kwa idadi ya watu katika jamii kunategemea sana maendeleo ya jamii yenyewe na ya watu binafsi katika jamii hiyo. Ni vigumu sana kwa jamii zinazokabiliwa na umaskini, ujinga, chirwa na maradhi mengine kutokana na njaa ikiwa pamoja na kukosa chakula bora kujiendeleza kiidadi. Watu wenye afya bora kutokana na shibe, huduma za kitabibu na malazi bora ndio wenye uwezo mkubwa wa kuzaa watoto kwa wingi, wenye afya na akili safi. Watoto wanaozaliwa na kukua katika unyonge mara nyingi afya na akili zao huwa duni. Na wengi wao hufa wakiwa wadogo. Hivyo, idadi ya jamii hubaki

vile vile au hudidimia mwaka hata mwaka ingawa haiwezi kumalizika kabisa kwa sababu ya uwezo wa pekee aliojaliwa mtu wa kupambana na kuyatawala mazingara yake.

'Mtu — mkusanyaji na mwindaji' hakujali kula cho chote kilichoweza kulika na kumezeka ili kudumisha uhai wake. Mtu wa karne ya leo, mbali ya kudumisha uhai wake, anakabiliwa na suala la kustawisha maisha na uhai. Hayo yote yanawezekana tu kwa kuyatawala mazingara yote kwa ukamilifu. Hivyo, tatizo la leo la mtu ni chakula bora, nyama bora, samaki bora, matunda bora, huduma bora za utabibu, maarifa bora, na yenye manufaa na kadhalika.

Ni dhahiri kuwa kadiri jamii inavyojiendeleza kiuchumi, kwa kuzidisha kiwango cha uzalishaji mali, na ndivyo matatizo katika jamii yanavyozidi kuongezeka. Wezi, majahili, majambazi majasusi, wasaliti, wala rushwa, walaghai, mabepari, makabaila na mabwanyenye; askari wa kukodishwa (wauzaji wa maisha) na malaya (wauzaji wa miili yao), nao hujitokeza na kujiendeleza kwa mbinu za hali ya juu sana. Ili kusawazisha hali ya maisha ya watu jamii yenyewe huchukua, licha ya kupambana na mazingara, hatua zote za kupambana na matatizo yatokanayo na tabia zisizoridhisha za baadhi ya wanajamii waliojumulishwa hapo juu.

Kisiasa jamii hujiendeleza kwa kuanzisha taasisi ya kitawala ambayo ni serikali. Kazi ya serikali ni kuhakikisha usalama wa jamii na wa watu binafsi na mali zao. Vile vile serikali ina wajibu wa kupanga maendeleo ya nchi pasipo kujali itikadi na mfumo wa jamii kwa sababu maendeleo ya vitu, katika maana ya kuzalisha na kukuza vitu vya aina nyingi, yaweza kupatikana katika itikadi yo yote ile. Lakini serikali inayojali watu hupanga maendeleo ya watu kwa kujenga mfumo unaoongozwa na itikadi ya ujamaa.

Kitamaduni maendeleo ya jamii huonekana katika lugha, taasisi za kijamii kama dini, ubora wa nyimbo, ngoma na kadhalika. Kwa kadiri jamii itakavyojiendeleza kiuchumi, kifikara, kisayansi na kitekinologia ndivyo itakavyojiendeleza kitamaduni. Vitu vitakavyozalishwa vitakuwa vingi kwa kiasi na kiaina. Na hivyo vyote husaidia kukuza, kwa mfano, msamiati wa jamii. Na kwa sababu jamii iliyoendelea huondokana na unyonge hata msamiati na lugha kwa ujumla itazidi kuchukua sura ya kitaalam na kizito. Taasisi za jamii, kama vile dini, imani, miiko, mila na desturi, n.k. hujengewa madhehebu mazito. Ndoa hufanyiwa maadhimisho makubwa na mazishi nayo hufanyiwa matanga ya ajabu.

Hata hivyo, madhehebu hayo yanaweza kusaidia kusukuma maendeleo au kurudisha maendeleo. Jambo la kuzingatia ni kuwa jamii hujiendeleza kiutamaduni na kifikara katika vipindi mbali mbali kutegemea mzinduko wa kitaifa wa kila jamii.

Fikara za watu katika jamii iliyoendelea hufika mbali zaidi kuliko fikara za jamii isiyofikia hatua ya juu ya maendeleo. Jamii hujiendeleza katika kujenga nadharia ambazo kusema kweli ni sehemu ya msingi wa maendeleo, na papo hapo nadharia zenyewe zikiwa ni sehemu ya mapambano au kazi.

Kwa kumalizia, itabidi kufahamu na kukumbuka kuwa mapambano yote ya mtu ni kwa ajili ya mtu na jamii. Mtu hufanya kazi daima akiwa na lengo kamili. Lengo la mtu siku zote ni kujiendeleza. Kujiendeleza kwa mtu ni kuyafanya maisha yake kuwa bora zaidi, yenye furaha, faraja na heshima itokanayo na hali ya usawa na kujitosheleza. Hayo yote hutokana na uwezo wa pekee wa mtu wa kuyatawala mazingara. Ijapokuwa kuna kuridhika katika jamii za nyakati na hatua zote za maendeleo katika vipindi mbali mbali vya historia mapambano na maendeleo ya mtu hayana mwisho. Kwa msingi huo mtu, jamii au taifa po pote duniani linayo sehemu yake ya mapambano. Maarifa yatakayotokana na mapambano hayo yatahifadhiwa katika ghala ya urithi.

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzo kuwa Afrika, kwa asili, ni nchi tajiri japokuwa watu wake ni maskini. Sababu za umaskini huo pia zimeelezwa. Baada ya yote hayo kutambulika suala linalobaki ni jamii za Kiafrika, hasa katika Afrika huru, kuchukua hatua thabiti za maendeleo ya jamii. Papo hapo ikizidi kusisitizwa kuwa maendeleo ya jamii ni matokeo ya mapambano ya mtu katika dunia na mazingara; na kwamba mapambano yote hujumuika katika kazi.

Kisayansi, kazi huwa imefanyika wakati kitu (jiwe, mtu, mnyama, na kadhalika) kimejimudu au kimesafiri umbali fulani, yaani, kutoka mahali pamoja mpaka pengine. Tafasiri hiyo ya kazi inakubalika kwa ujumla wake lakini kwa madhumuni ya mjadala wa somo hili haisaidii sana. Wanyama kama nguruwe hujimudu, hutembea, hutumia juhudi kung'oa mihogo iliyolimwa na mtu akala na kuudumisha uhai wake. Tembo huporomosha majabali na miamba ya mawe; huvunja na kung'oa magogo ya miti bila ya lengo. Katika mifano ya hapo juu 'kazi' katika maana ya mtungaji haijafanyika ingawa juhudi imefanyika. Wanyama

hao wametumia 'mitulinga'* yao lakini hawakutumia akili au maarifa.

Kazi haina budi kuleta maendeleo. 'Kazi ya maendeleo' hufanywa na mtu tu. Mtu ndiye peke yake mwenye uwezo huu wa pekee kutumia maarifa aliyojaliwa kuratibu mipango ya maendeleo yake. Katika kutekeleza mipango hiyo mtu hutumia juhudi (nguvu) na akili (mbinu na zana). Juhudi na mipango yote ya maendeleo huelekezwa kwenye mapambano na mazingara.

Nguruwe ambaye ametumia juhudi ya kufukua mihogo, kula mahindi, vitu ambavyo ni matokeo ya kazi ya mtu, hajafanya kazi ya maendeleo; ingawa juhudi yake imemsaidia kuendeleza au kudumisha, kwa muda tu, uhai wake na siyo kuyafanya maisha yake na ya vizazi vyake kuwa bora zaidi na zaidi. Kadhalika tembo, ambaye kwa kutumia mitulinga yake aliweza kuporomosha miamba ya mawe, kung'oa magogo, hajafanya kazi bali ametumia vibaya nguvu zake.

Njia ya pekee ya kuwaondoa Waafronodi katika unyonge ni kuanzisha mipango ya uchumi na ustawi wa jamii inayoweza kutoa uwezo mkubwa wa kupambana na vipengele vyote vya mazingara. Moja ya vipengele hivyo ni umaskini ambao, kwa sehemu kubwa, asili yake ni utovu wa maarifa—yaani, ujinga kwa maana iliyotolewa hapo juu. Hivyo, pambano la kwanza liwe ni kubuni mbinu na kuratibu mipango ambayo itawezesha jamii kuzalisha mali kwa wingi zaidi; na isiwe kutegemea mikopo tu ambayo mara nyingi hutumika katika kuongeza mishahara ya maafisa wa madaraja ya juu badala ya kutumika katika kuendeshea mipango ya maendeleo. Na mipango ya maendeleo ni ile inayosaidia kuendeleza kuzalisha mali kwa wingi zaidi.

Mali inayoongelewa hapa ni mazao ya chakula na biashara. Mazao mbali mbali ya chakula yatasaidia kuifanya jamii kujitosheleza na kuondokana na baa la njaa. Jamii au taifa kwa jinsi hii litakuwa na uwezo na nguvu ya kuzalisha mali zaidi; na papo hapo kuwa na uwezo wa kuhifadhi fedha yake ya kigeni ambayo imetokana na mazao ya biashara kwa kuziuzia nchi za nje. Fedha hiyo ya kigeni itakuwa ndiyo mtaji wa kununulia zana na vyombo mbali mbali vya kuendelezea shughuli za uzalishaji mali. Zana za kisasa za kilimo, yaani, mashine mbali mbali kama vile matrekta na kadhalika; zana za kuchimbulia madini mbali mbali, mishahara ya wataalam wenye ujuzi wa taaluma mbali mbali kutoka nchi zilizoendelea na shughuli nyingine nyingi zote huhi-

* Mitulinga – musuli; na kwa hiyo ina maana ya kutumia 'nguvu' bila akili.

taji pesa au mitaji.

Uwezo wa kuzalisha mali kwa wingi na kuendeleza mapambano ya maendeleo utategemea sana mipango ya jamii au taifa. Mara nyingi watu huongea juu ya mipango ya maendeleo ya uchumi katika upweke. Hayo ni makosa. Mipango ya maendeleo ya jamii lazima itazamwe katika 'jicho moja' na katika mjumuiko wa mambo mengi mengine. Kwa hiyo, kutazama mipango katika jicho moja kuna maana nyingi sana. Kwanza kabisa, taifa lazima kuweka shabaha na lengo la mipango yake ya maendeleo. Shabaha za muda mfupi na za muda mrefu nazo lazima zielewe-ke kwa taifa zima.

Pili kutazama mipango ya maendeleo katika jicho moja ni kuweza kuunganisha mipango ya uchumi, yaani, uzalishaji mali katika ujumla na mipango mingine. Mipango hiyo mingine itahusu masuala ya huduma kuwaandaa wataalam wa taaluma zote na, suala la kuendeleza utamaduni wa jamii kwa mujibu wa itikadi ya taifa. Utamaduni ndio unaoiwezesha jamii kujibainisha na jamii au mataifa mengine. Utamaduni wa kitaifa ambao pia hukuzwa kwa mwongozo wa itikadi husaidia sana kusukuma maendeleo ya aina zote ya taifa. Kinyume chake utamaduni ulioachwa kukua holela huzuia maendeleo ya uchumi, hushusha heshima ya jamii, na kadhalika.

Tatu suala la mipango ya elimu ni muhimu sana. Nchi haina budi kuwa na lengo la kujipatia wataalam wake wa kutosha. Wataalam ni watu waliojaliwa kupata maarifa ya kutosha kuhusu taaluma mbali mbali. Lengo la kuzalisha wataalam ni kuongeza uwezo wa taifa wa kuzalisha mali. Mpaka sasa mipango ya elimu imekomea katika kupanua elimu ya msingi, elimu ya sekondari na elimu ya juu kwa misingi tulioachiwa na serikali za kikoloni. Masuala ya aina ya elimu na ufafanuzi wa maana ya elimu kwa mapana na kina hayakushughulikiwa. Nchi yo yote, hasa nchi changa, haina budi kutilia mkazo elimu ya sayansi na tekinologia. Elimu ya tekinologia ndiyo elimu yenye lengo na shabaha.

Ili taifa liweze kukuza viwanda, kuendeleza shughuli za uchimbuzi wa madini, kuendeleza maarifa na elimu yenye manufaa halina budi kuwa na wataalam wake walio na maarifa ya kutosha ya kitekinologia na kisayansi.

Ingawa utaalam ni matokeo ya elimu na maarifa ya shuleni utalaam huo huwa ni wa hali ya juu sana ukiunganishwa na vipawa vya watu. Vipi na wapi taifa litaweza kugundua vipawa vya watu wake ili kuweza kuviendeleza kwa manufaa ya taifa zima?

Upangaji wa Elimu sharti uanzie katika watoto wadogo ambao bado kufikia umri wa kuanza masomo ya msingi. Na kwa muda wote watoto na vijana waelekezwe katika mikondo ya vipaji. Kufuatana na mipango ya elimu ya nchi nyingi, kadiri historia zao zinavyoonyesha watu wengi wamelazimishwa kutaalamika katika mikondo wasiyo na vipawa nayo. Pamoja na suala la elimu ya utaalamu na ya watoto wadogo kuna suala la kuwa na mipango thabiti na yenye lengo la 'mwisho' kuhusu kisomo cha watu wazima. Elimu ya watu wazima sharti iwe na shabaha ya kuwawezesha wananchi kujiingiza na kushiriki kikamilifu katika shughuli mbali mbali za kuzalisha mali katika taifa. Kisomo cha watu wazima hakina budi kuendelezwa kwa mwongozo maalum. Tabia ya hivi sasa ya kuwapa wakulima na wafanyakazi elimu isiyo na matumizi, yaani, manufaa kwa watu wenyewe na kwa taifa, ni lazima kuondokana nayo. Wafanyakazi na wakulima wengi huhudhuria zaidi masomo ya lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa. Hii ni kuendeleza kasumba. Ni kitendo cha busara kwa mpiga mashine, kwa mfano, kujiendeleza katika somo la Kiingereza na Kiswahili (kwa Tanzania) pamoja na masomo mengine yanayohusiana na utaalam wake. Kinyume chake wapiga mashine huhudhuria somo la Kifaransa (katika Tanzania) ambalo haliwezi kumwendeleza kitaalam japokuwa, bila manufaa, atakuwa amejua lugha ya Kifaransa.

Pia kuna suala la huduma kwa jamii ambalo lazima liangaliwe wakati wote wa kupanga mipango ya maendeleo. Huduma kwa jamii ni pamoja na maji, vituo vya afya, shule, vituo vya usalama, vituo vya elimu kwa watoto wadogo, njia za uchukuzi na mawasiliano, majumba ya maendeleo na starehe, mabohari na maduka ya ushirika. 'Utoaji' wa huduma hizo unawezekana tu kama watu wataamua kuishi pamoja katika miji na vijijini. Na kusema kweli sehemu kubwa ya huduma hizo zitatokana na juhudi za wananchi wenyewe. Na kwa kuwa mipango ya maendeleo ni ya watu, basi, upangaji wake utakuwa ni wa watu wenyewe wakisaidiana na wataalam.

Kuna haja pia ya kuiweka mipango hiyo kwa jinsi kwamba vipengele vya mpango mzima wa maendeleo ya taifa vinaweza kuonekana mara moja. Mbinu na utaratibu wa utekelezaji wake budi ufahamike kwa wakulima na wafanyakazi wote; na kwa viongozi wa serikali na vyama vya siasa. Wajibu wa viongozi na watumishi wa vyama na serikali lazima ufahamike pia.

Ujinga ukiwa ni sehemu moja ya mazingara ya watu ni utovu wa maarifa, ujuzi, na ufundi katika taaluma mbali mbali; pia ni

utovu wa ufumbuzi kuhusu matatizo kadha wa kadha. Ujinga ambao unaweza kuwa wa mtu binafsi, wa jamii au wa taifa, husababishwa na mambo mengi; na kwamba ujinga unaweza kuponyeka kwa muda mfupi au mrefu; na pengine ni vigumu kabisa kuponyeka. Kwa vyo vyote vile ni rahisi zaidi kufuta ujinga wa watoto kuliko ujinga mpevu wa mtu mzima au jamii. Hata hivyo ujinga wa watu wazima ukifutwa, taifa au jamii huwa imejiendeleza maradufu katika mambo mengi.

Mtu, jamii au taifa linakabiliwa na ujinga si kwa sababu ya kukosa uwezo wa kuelewa. Jamii huwa na ujinga kwa sababu jamii au taifa halijapiga hatua ya kutosha ya mapambano na mazingara yanayolikabili. Kwa hiyo, jamii mara nyingi huzingatia na kutegemea sana imani, miiko na mila badala ya kufikiria hatua maalum za mapambano ya kutatua matatizo. Ujinga usichanganywe na ubaradhuli au upumbavu ambao huwakabili watu binafsi katika kila jamii; na kwamba ubaradhuli na upumbavu ni utovu wa uwezo wa kuelewa mambo hata baada ya kuambiwa au kufundishwa.

Miaka mingi sana Wayuronodi 'wapelelezi' na wanaAfrika wengi walipoteza maisha yao kwa ugonjwa wa malaria. Hii ni kwa sababu hawakuwa wanatambua kuwa vifo hivyo vilitokana na ugonjwa wa malaria ambao huletwa na kuenezwa na mdudu mdogo sana — mbu. Leo jamii za Kiyuronodi na nyingine zilizoendelea zinafahamu kuwa hutokana na mbu na hatua muhimu zimechukuliwa za kuzuia na kuponya malaria. Kwa jinsi hii malaria leo si ugonjwa tena wa kutisha maisha ya mtu. Hata hivyo, kuna jamii katika Afrika ambazo hazina taarifa ya kutosha kuhusu malaria nazo huendelea kuamini kuwa malaria huwa ni matokeo ya mtu au ndugu kumkasirikia, kumwapiza au kumtakia maovu mwingine. Jambo hili linapotokea ndugu hukusanyika, mara nyingi saa za magharibi na alfajiri, ili kumfanyia madhehebu mgonjwa. Majani na magamba ya aina fulani ya miti, kama vile, mwembe, huchemshwa pamoja katika sufuria au chungu kikubwa. Kisha mgonjwa husogezewa kile chungu cha maji ya moto yenye kutoa mvuke. Wakati huo huo mgonjwa hufunikwa mablanketi na mashuka ili mvuke umpate barabara. Kila mwanandugu hupenga maji ya dawa kutokana na chungu hicho hicho, pande zote za dunia huku akisema: "mimi namsamehe mgonjwa huyu na iwapo huyo pepo mbaya aliyesababisha homa yake ametokana na chuki au maapizo yangu, basi, pepo huyo amwache huyo mgonjwa". Kwa kuwa watu wa jamii ya Wamanda waishio kando ya Ziwa Nyasa, katika Tanzania, wanahusika na

imani hiyo, mara nyingi huomba pepo huyo amwache mgonjwa na akimbilie huko Malawi ambako anaweza kupambana na majabali ya ajabu na kuyavunjavunja. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa fikara hizo za kufukuzia pepo Malawi ni za kijinga. Ujinga wenyewe ni utovu wa maarifa ya kijografia.

Hutokea mara nyingine mgonjwa hupata nafuu na kupona. Hii ni kwa sababu ya joto la maji ambalo husababisha mgonjwa kutokwa na jasho jingi. Matokeo ya kutokwa na jasho ni kuwa homa au joto la mgonjwa hupungua na, kwa jinsi hiyo, damu ya mgonjwa hupata nafasi ya kupambana na vijidudu vya malaria. Wakati inapotokea mgonjwa anapona imani ya jamii ni kuwa ugonjwa ulisababishwa na uadui kati ya wanandugu na kwamba kupona kwa mgonjwa kumesababishwa na maneno ya kushtakia ya wanandugu.

Imani nyingine ambayo pia ni matokeo ya ujinga ni uchawi. Baadhi ya wananchi huamini kuwa kuna wachawi wenye nguvu ya pekee. Wakati mtu anaumwa kifua kikuu ndugu zake humpeleka kwa mganga wa kienyeji ambaye pia husadikiwa kuwa ana nguvu na uwezo si wa kugangua tu bali pia kuona watu waliosababisha maradhi ya mgonjwa. Mara nyingi mgonjwa ataambiwa kuwa mmoja ya ndugu zake amemloga kwa kumkwamisha kidonge cha pamba au nywele au mfupa wa samaki na kadhalika, kooni. Hivyo, husadikiwa kuwa ndivyo vitu vinavyosababisha kukohoa kwa mgonjwa. Dawa ni kumtapisha kikatili mgonjwa.

Kwa kuwa mlozi au mchawi mara nyingi atabainiwa mmoja wa wanandugu, kwa kawaida huchaguliwa jitu lenye sura nzito, hivyo, ndugu wanaobaki huishi kwa uhasama na mfarakano. Pia kuna imani miongoni mwa jamii zetu kuwa baadhi ya watu wanaosemekana kuwa wachawi wana uwezo wa kuwafufua wafu na kuwafuga kama wanyama. Watu hao (wafugwao) huaminiwa kuwa wana nguvu ya kubeba mizigo mizito sana ambayo mtu wa kawaida hawezi kuibeba. Pia husadikiwa kuwa wanaweza kusafiri mwendo wa mbali kwa muda mfupi na kwamba mara nyingi wana uwezo wa pekee wa kufanya kazi, hasa kazi ya kulima mashamba makubwa ya mabwana zao na kuwapatia mavuno ya ajabu. Watu hao hujulikana katika sehemu fulani za Tanzania Bara kama 'ndondochi'. Vile vile inasadikiwa wachawi wana uwezo wa pekee wa kuiba 'kazi' ya mtu au watu wengine kwa kutumia 'ndumba*. Hii ina maana kuwa wakati

* Ndumba — dawa ya uchawi au uganga wa kienyeji.

majirani au ndugu wanalima kwa bidii zao zote matokeo ya kazi yao huonekana katika shamba la mchawi. Imani ya aina hii ambayo msingi wake ni ujinga hukatisha tamaa na kurudisha nyuma maendeleo ya jamii. Kadhalika mila ya kuhama nyumba na kuacha chakula chote katika nyumba hiyo kwa kuogopa maiti ya mmoja wa wanandugu aliyefia humo inapinga maendeleo. Badala ya kusaidia kuokoa maisha ya mgonjwa wananchi wanaohusika humkimbia. Chakula ambacho kingewasaidia kuendeleza uhai na maisha yao hukisusa.

Ujinga ambao hutokana na imani na miiko, kwa mfano, kuacha kula baadhi ya vyakula vya lazima vya kujenga mwili, kama vile, samaki, kuku, mayai na kadhalika, huwa si rahisi kwa jamii kuondokana nao. Moja ya vipingamizi vya maendeleo katika Tanzania ni kusita kuondokana na ile mila ya kusema hapa ni mahali walipozikwa baba na babu zangu. Kwa hiyo, ni wajibu wangu kubaki hapa kutunza makaburi. Tabia hii ya wananchi inatokana na imani ya woga kuwa wale wote waliokufa bado wanaendelea 'kuishi' na kuunganika na jamaa walio hai. Papo hapo wafu hao wanasadikiwa kuwa na nguvu na uwezo mkubwa sana. Wanaweza kuwabariki jamaa na ndugu walio hai au kuwaadhibu vikali sana. Tabia hii ni ya kusikitisha sana maana msingi wake ni ujinga; nayo hurudisha maendeleo ya jamii na ya taifa kwa kuzuia baadhi ya jamaa kujumuika na jamaa wengine kwa madhumuni ya kuunganisha nguvu na juhudi ili kuongeza uwezo wao wa kupambana kikamilifu na mazingara kwa shabaha ya kuleta maendeleo ya kuikomboa jamii au taifa kutokana na unyonge.

Ujinga utokanao na imani, miiko, mila na desturi huwa ni vigumu sana kuondokana nao. Kadhalika ujinga utokanao na kasumba za kikoloni nao huwa mgumu kutoweka upesi. Juhudi za kupambana na ujinga wa aina hii hufanikiwa tu iwapo taifa linachukua hatua za kimapinduzi. Na kwamba kwa kawaida, mafanikio makubwa huweza kufikiwa baada ya kizazi kilichoishi katika ujinga huo kumalizika. Kwa hiyo, hali hii isiwe ya kukatisha tamaa kwa wale wanaoongoza mapambano ya kuleta maendeleo katika jamii au taifa.

Kitu kingine ambacho ni sehemu ya mazingara ni mfumo na itikadi. Taifa linaweza kuchagua aina moja ya itikadi au nyingine. Lakini kwa upande wa nchi changa uchaguzi ambao ni wa busara ni kuchagua itikadi ya ujamaa. Itikadi ya ujamaa, ikiwa ni kinyume cha itikadi ya ubepari, hupigania usawa wa watu katika jamii, hukomesha unyonyaji, hujenga demokrasi na

kuondoa matabaka ya aina yote. Jamii isiyo na tabaka husemekana kuwa ina mfumo wa kijamaa. Katika jamii ya kijamaa watu hupanga mipango yote ya maendeleo, huendeleza na kusimamia utekelezaji wake kwa faida ya wanajumuiya wote. Ujamaa unaheshimu utu, haki zote za watu pamoja na suala la watu kujiunga na dini za imani yo yote mradi tu imani hizo hazipingi maendeleo ya jamii.

Itikadi ya ubepari ambayo huruhusu wachache kuwanyonya walio wengi huzuia maendeleo ya jamii. Ubepari ni udhalimu na uhasama. Itikadi hii huwagawa watu wa jamii moja katika matabaka ya wanaonyonywa, ambao ni wanyonge, na tabaka la wanyonyaji wenye hali bora ya kiuchumi na ambao, kwa sababu ya utajiri wao utokanao na kudhulumu, pia hujinyakulia madaraka ya uongozi na haki zote za kiutu katika jamii. Umma hunyimwa uhuru. Demokrasi huwa ni ndoto. Kwa ufupi, taifa lenye mpango wa uchumi wa kibepari, ambalo mfumo wake huwa ni wa kitabaka, hugawa jamii katika makundi ya wazalishaji mali ambao ni wafanyakazi na wakulima na wafanyiwa kazi ambao ni mabepari, makabaila na mabwanyenye. Kinyume chake itikadi ya ujamaa huwataka watu wote kuwa katika tabaka moja, yaani, tabaka la wakulima na wafanyakazi katika daraja zote kutegemea aina ya kazi na huduma, uwezo na utaalam wa watu wenyewe. Mfumo huu, katika maana yake halisi, yaani, usipopotoshwa kwa faida ya wachache, huwa wenyewe ni dhamana muhimu sana ya maendeleo ya haraka ya jamii.

'Maendeleo ya jamii' ni neno lenye maana pana sana, nalo ni neno la kimapinduzi. Kwanza kabisa, jamii inasemekana imeendelea kwa sababu watu wake wote wanajitosheleza kuhusu mahitaji ya lazima; kama vile nyumba nzuri, maji safi, chakula bora cha kujenga mwili, wenye afya bora. Iwapo vyakula vya aina fulani fulani kama vile nyama, samaki, mayai, matunda, sukari, chumvi, mafuta ya kupikia, na kadhalika huwa ni adimu na kwa ajili ya wachache tu wenye uwezo wa kiuchumi jamii hiyo itakuwa bado inaishi katika unyonge.

Maendeleo ya jamii huonekana pia katika huduma nyingi muhimu, kwa mfano, njia za kisasa za usafiri na mawasiliano, elimu, vituo vya afya, nguvu ya umeme na vyombo muhimu vya kurahisishia kazi. Lakini kufuatana na siasa ya 'kupanga ni kuchagua'* baadhi ya huduma hizo ingawa ni muhimu huweza tu kupatikana wakati taifa linavyozidi kusonga mbele kisayansi na

* Maneno hayo yalisemwa na Mwalimu Juliasi K. Nyerere.

kitekinologia na, kwa hiyo, kiuchumi. Vyombo vya kisasa vya kupikia, kulia, na kuhifadhia vyakula; vifaa na mapambo ya nyumbani ili kuifanya nyumba kuwa ni mahali pa kuvutia pia ni matarajio na ni sehemu ya maendeleo ya jamii. Vile vile maendeleo ya jamii huonekana katika kukua kwa utamaduni wake: nyimbo, michezo, ngoma, lugha na kadhalika.

Kitendo cha watu kukusanyika pamoja na kwa lengo moja chenyewe ni kitendo cha maendeleo kwa watu binafsi na kwa jamii nzima. Ili kuishi pamoja watu hawana budi kusahau ubinafsi na kukuza fikara za kijumuiya ili kujenga uhusiano mwema. Kuvumiliana, kusaidiana, kupendana na kujifunza kutoka kwa wengine, ni baadhi ya mambo muhimu kwa jamii ya kijamaa; na yote hayo yakitokea hueleza hatua fulani ya maendeleo ya jamii hiyo.

Jambo muhimu la kuzingatia ni kuwa taifa, bila ya kujali itikadi, linaweza kuwa na 'maendeleo' makubwa sana ingawa si ya watu. Mataifa kama Marekani, Uingereza, Italia, Ujapani, Ufaransa na Ujerumani Magharibi ambayo yanafuata itikadi ya ubepari yamepiga hatua kubwa sana ya maendeleo katika maana ya uwezo mkubwa wa kukuza uchumi na maarifa. Maendeleo hayo, ingawa (sehemu kubwa) si ya watu yana sababu za kihistoria. Hizo ni nchi za kibeberu. Ziliwanyonya watu wa nchi nyingine kwa miaka mingi zikalimbikiza mali na mitaji ya kutosha, zikatumia mali na mitaji hiyo kwa kununua utaalam wa hali ya juu zaidi. Kwa jinsi hiyo, maendeleo ya watu wa Dunia ya Tatu hayataletwa kwa njia ya kuwanyonya watu wa nchi nyingine, wala kwa misaada na mikopo, na wala si kwa mfumo wa kitabaka. Misaada na mikopo inaweza tu kuwa na maana iwapo itasaidia kusukuma maendeleo ya watu ili kuwafikisha kwenye hatua ya juu zaidi ya kujitegemea badala ya kuzifanya jamii hizo kuendelea kutegemea misaada ya mabeberu.

Nyongeza A

MSAMIATI WA MAJINA YA JAMII

1. Waafrika	Wananchi wa Afrika wakijumuika Waafronodi (kama Waafrika wa asili) na jamii zenye asili ya kigeni; Wasanodi na Wayuronodi.
2. Waafronodi	Jamii za asili za Afrika.
3. Waastranodi	Watu wa asili wa bara la Australia
4 Wabantu	Jamii za Kikansanodi zenye kuongea lugha za asili ya Kibantu. Neno hili limebuniwa na wataalam wa lugha.
5. Wahotentoti	Jamii ya Kikaprinodi iliyoishi katika sehemu ya Rasi ya huko Afrika ya kusini kabla ya Wayuronodi na Wabantu.
6. Wakalahari	Watu waishio katika sehemu ya Jangwa la Kalahari ambao huongea lugha ya Kichembe.
7. Wakansanodi	Jamii za Kiafronodi ambazo ziliishi kaskazini ya Sahara mnamo miaka c. 3000 iliyopita yaani, kabla ya jamii za Kisanodi.
8. Wakaprinodi	Jamii za Kiafronodi ambazo zilienea kusini ya Ikweta yapata miaka 3,000 iliyopita.
9. Wakichembe	Jamii za Kikaprinodi ambazo huongea lugha za kugongagonga ulimi.
10. Wakoza	Jamii ya Kinguni ambayo iliishi kusini ya Wazulu mpakani na Makaburu mpaka mnamo 1770.
11. Wakushito	Jamii za Kiafrika zinazoongea lugha zenyé asili ya Kisanodi hasa Kiarabu.

12. Walozi	Moja ya jamii za huko Zambia iishio kusini mashariki.
13. Walundo	Moja ya jamii za Zambia iishio mpakani na Katanga, jimbo la Zaire.
14. Wamarekani	Wananchi wote wa bara la Marikani ambao ni mchanganyiko wa Amarinodi na jamii za kigeni; Wayuronodi, Waafronodi, na kwa kiasi fulani Wasanodi.
15. Wamashona	Moja ya jamii za kibantu katika Zimbabwe ambayo iliishi nchini humo kabla ya Wamatabele na Wayuronodi.
16. Wamatabele	Moja ya jamii za Zimbabwe. Asili ya Wamatabele ni Unguni katika Afrika ya Kusini. Ilifika Zimbabwe baada ya 1835.
17. Wamarinodi	Jamii za asili za bara la Marekani. Jamii hizi zilijulikana kama "Wahindi Wekundu" neno ambalo mwandishi amependekeza kuliua.
18. Wamorinodi	Jamii za asili za kisiwa cha Nyuzilandi.
19. Wangoni	Jamii za Kinguni ambazo zilipata jina hilo katika Afrika ya kati zikiwa njiani kuelekea Tanzania.
20. Wanguni	Jamii za Kibantu ambazo kwa asili ni Wakansanodi. Jamii hizo ziliishi kati ya Bahari ya Hindi na milima ya Drakensberg.
21. Wanilo	Jamii za Kiafronodi zenye asili ya Kikansanodi na ambazo huongea lugha zijulikanazo kama lugha za Kinilo.
22. Wanyuzilandi	Mjumuiko wa watu wa asili wa Nyuzilandi ambao ni Wamorinodi na walowezi wa Kiyuronodi ambao waliingia Kisiwani humo kama mabeberu.

23. Wasanodi	Jamii za asili za bara la Asia.
24. Waskimonodi	Jamii za asili za Grinilendi na mara nyingi zimejulikana kama Waeskimo.
25. Wastralia	Mjumuiko wa Waastranodi ambao ni watu wa asili wa Australia na walowezi wa Kiyuronodi ambao waliingia huko kama mabeberu.
26. Wasutu	Wananchi wa Lesutu ambao kilugha ni jamii ya Kibantu.
27. Wayuronodi	Jamii za asili za bara la Yuropa au Ulaya.
28. Wazungu	Neno hili limeonekana lina kasumba ya kumtukuza mwananchi wa Ulaya kuwa yeye ni bora kuliko wengine. Hivyo, mwandishi amependekeza kulifuta kabisa na badala yake kutumia neno "Wayuronodi" ambalo lina msingi wa kijografia.

Nyongeza B

MSAMIATI WA MAJINA YA WATU

1. Daudi Livingistoni	David Livingstone
2. Chitiki	Chittick
3. Felipo-Stoku	Fellips-Stokes
4. Fransisi Kwayadi	Francois Coillard
5. Hendriki Witiboi	Hendrick Witbooi
6. Hilari	Hilary au Hilarius
7. Kalo Maksi	Karl Marx
8. Kalo Petro	Karl Peters
9. Krafu	Krapf
10. Lenini	Lenin
11. Liki	Leakey
12. Markusi Garve	Marcus Garvey
13. Mikaeli	Michael
14. Mungo Paka	Mungo Park
15. Rebumani	Rebmann
16. Roberti Mofati	Robert Moffat
17. Satoni	Sutton
18. Sesili Rodesi	Cecil Rhodes
19. Smisi	Smith
20. Vosta	Voster
21. Yohana Chilembwe	John Chilembwe

Nyongeza C

MAJINA YA NCHI YENYE ASILI YA LUGHA ZA KIGENI

KISWAHILI	LUGHA YA ASILI
Atalantiki	Atlantinc
Belini	Berlin
Boswana	Botswana
Bruseli	Brussels
Hestingi	Hastings
Ivori Kosti	Ivory Coast
Kantebari	Cantebury
Karibiani	Caribean
Kyuba	Cuba
Lesutu	Lesotho
Lisiboni	Lisbon
Londoni	London
Madagaska	Madagascar
Madina	Medina
Maka	Mecca
Malagasi	Malagasy
Marekani	America au American
Maurisiusi	Mauritius
Nazareti	Nazareth
Parisi	Paris
Pasifiki	Pacific
Trinidadi	Trinidad
Uyahudi	Israel
Vatikani	Vatican

Nyongeza D

MSAMIATI WA VYEO

Balozi	mwakilishi wa serikali ya nchi moja katika nchi nyingine.
Beberu	Mtu anayeteka nchi ya watu wengine kwa madhumuni ya kuwanyonya watu wake; pia mtu yeyote mwenye fikara kama hizo.
Bepari	Mnyonyaji ambaye hutegemea mtaji na vibarua.
Bwana	Mtu anayemiliki watu wengine kama watumwa kwa kumzalishia mali.
Bwanyenye	Mtu wa maisha ya kati ambaye anamwelekeo wa kikabaila na kibepari.
Chifu	Cheo kilichopewa kiongozi wa Kiafronodi wakati wa ukoloni. Neno hilo lina kashfa ya ukibaraka.
Kabaila	Mnyonyaji ambaye msingi wake ni ardhi na majumba ya kupangisha na ambaye hutumikisha watu kama watwana, pasipo kuwamiliki.
Kibarua	'Mfanyakazi' asiye na mwamko wa kutosha kuhusu suala la kunyonya.
Mchungaji	Padure wa Kiprotestanti. Mwandishi anapendekeza kuwaita viongozi wote wa madhehebu ya Kikristo—mapadure.
Mfalme	Mtungaji anapendekeza kulitumia neno hili kumaanisha mtawala yeyote wa jadi wa Kiyuronodi ambaye ni kabaila mkuu.
Mfanyakazi	Mtu aliyeajiriwa na ambaye ana mwamko wa juu na ambaye yumo katika mapambano ya kitabaka.
Mjamaa	Ni mtu anayeamini siasa ya usawa ambayo ni siasa yenye itikadi ya ujamaa.
Mkoloni	Mtu anayetawala nchi ya watu wengine; au mwenye tabia kama mkoloni.
Mpazi	Padure wa jadi wa Kiafronodi kabla ya ukoloni.

	madhehebu ya kigeni.
Mpinga mapinduzi	Mtu aliyejawa na ubinafsi ambaye hupigania maslahi ya wachache katika jamii.
Mtemi	Kiongozi yeyote wa jadi wa Kiafronodi kabla ya ukoloni.
Mtumwa	Mtu aliyemilikiwa na bwana kwa shabaha ya kunyonywa.
Mtwana	Mkulima chini ya kabaila.
Mwanamapinduzi	Mtu anayepigania haki za walio wengi katika jamii.
Padure (Padri)	Kiongozi wa madhehebu ya kikatoliki.
Papa	Mkuu wa Kikatoliki ambaye makao yake makuu ni Roma.
Sultani	Kiongozi yeyote wa Kisanodi Uarabuni na katika makoloni yake.

MSAMIATI WA KAWAIDA

Altare	mahali padure anapotolea sadaka.
Bosheviki	chama cha Kikomunisti cha Kirusi.
Dhana	ni fikara isiyo dhihirifu.
Dhidi	kinyume cha, kupingana na
Dola	nchi zilizo chini ya mamlaka ya mtawala au taathira ya nchi nyingine.
Dunia	sayari hii tunamoishi — maji na nchi kavu.
Fikara	wazo
Fikra	wazo. Lakini kwa sababu ya matamshi yake ya kikasumba ya Kiarabu mwandishi anapendekeza kutumia fikara.
Gundua	ona kitu hasa kwa mara ya kwanza.
Harakati	shughuli au mikikimikiki ya mapambano. Jitihada.
Itikadi	imani ya kisiasa, kwa mfano, ujamaa ni itikadi.
Itifaki	uhusiano au utaratibu wa kuendesha mambo kibalozi n.k.
Jamaa	watu wa nyumba moja. Familia.
Jamii	watu wa asili moja, kwa mfano, Wahehe, Wangoni, Wabondei au Wanyamwezi.
Kabila	neno la kashfa lililotumiwa na wakoloni kueleza jamii ya Kiafronodi. Mwandishi

Mpango	utaratibu, kwa mfano, wa kuzalisha mali, n.k.
Mpelelezi	mtu anayejifunza mazingara ya nchi au mbinu za adui.
Msingi	chanzo qanzo wa kitu.
Mwendo	umbali au hatua za kutembea.
Mwenendo	tabia, namna ya kujimudu
Nadharia	fikara ambayo ina nguvu ya kusukuma maendeleo.
Ndumba	kibuyu au kipembe n.k. cha dawa ambacho mara nyingi hutumiwa na wachawi.
Suala	tatizo, jambo muhimu linalohusu mjadala au kuchunguzwa.
Swala	mnyama; sala za msikitini.
Swali	fumbo; ulizo; au kuomba.
Tabaka	kundi; mara nyingi hutumika kueleza makundi ya kihasama katika jamii.
Uafrika	moyo wa umoja na uzalendo wa Kiafrika.
Uafronodi	moyo wa umoja wa Kiafronodi ambayo ni hatua ya mwanzo ya Uafrika.
Ubeberu	ubepari katika hatua ya juu.
Ubepari	mfumo wa kinyonyaji ambao msingi wake ni mtaji n.k.
Ubalozi	utaratibu wa nchi kuwakilishana; pia Ofisi ya balozi.
Udhanifu	sio kweli; kubunia

	amekataa kulitumia neno hili na badala yake neno jamii litumike.
Koloni	nchi inayotawaliwa na mabeberu.
Kuangusha serikali	kunatokea wakati kikundi cha wachache kinatwaa madaraka kwa nguvu kutoka kwa walio wengi au kwa wachache kwa manufaa ya wachache.
Lelemama	ngoma ya Kizaramo
Lipenga mganda	ngoma ya jamii zinazozunguka ziwa Nyasa.
Maarifa	mjumlisho wa ujuzi.
Manufaa	faida au mafanikio.
Mapambano	vita vya maneno au vya vitendo
Mapinduzi	hutokea wakati umma unatwaa madaraka ya kiserikali kutoka kwa wachache kwa manufaa ya umma,n.k.
Maslahi	manufaa.
Mazingara	mjumulisho wa mambo yanayomzunguka mtu. Vitu, mawazo, hewa, ulimwengu n.k.
Mazingira	vitu vinavyomzunguka mtu n.k. ambavyo kijografia huonekana.
Mbinu	njia au ujanja wa kufanya mambo kwa utaratibu zaidi.
Mfumo	utaratibu wa kijamii ambao kutokana na mipango yake ya uchumi unaweza kuwagawa watu katika matabaka ya wanyonyaji na wanaonyonywa au kuondoa matabaka.
Mkataba	mapatano baina ya watu au serikali.

Udugu	uhusiano katika jamii ambao unawafanya watu wajione ndugu au wamoja.
Ujamaa	mfumo wa jamii ambao hauruhusu matabaka wala unyonyaji.
Ujima	ni mfumo wa jamii usio wa kitabaka. Huonekana katika jamii ambazo kiteknologia hazijaendelea sana.
Ujinga	utovu wa maarifa na ujuzi.
Ukabaila	mfumo wa jamii ambao huruhusu unyonyaji; na ambao msingi wake ni ardhi na majumba ya kupangisha.
Ukoloni	mpango wa mabeberu kutawala nchi nyingine kwa shabaha ya kuwanyonya watu wake.
Ulimwengu	dunia pamoja na sayari zote na anga n.k.
Unyonge	hali duni; udhaifu.
Unyonyaji	kupunja au kutumia nguvu na jasho la wengine kwa faida ya mtu binafsi.
Unyarubanja	ukabaila kama ulivyoendeshwa huko Bukoba katika Tanzania.
Utumwa	mfumo wa jamii ambao unaruhusu kisheria mtu au kikundi cha watu kuwamiliki wengine na kuwanyonya.
Utwana	hali ya unyonge inayowapata wakulima maskini chini ya kabaila.
Wakakasadi	neno lililotumiwa na wakoloni kuwaeleza watu weupe. Neno hili lina kasumba ya kumfanya mtu mweupe kuonekana bora zaidi kuliko mtu mweusi kwa sababu ya rangi yake. Mwandishi anapendekeza kuliua kabisa neno hili.

Wanigrodi	neno la kashfa lililotumiwa na wakoloni kuwaeleza watu weusi wa Afrika na kuonyesha kuwa ni watu duni. Maneno hayo yote mwandishi ameyapiga marufuku.
Wavambo	moja ya jamii za Kibantu huko Namibia.
Wazo	fikara iliyodhihirifu zaidi kuliko dhana.

Kimetolewa na Tanzania Publishing House, S.L.P. 2138, Dar es Salaam
na Kupigwa Chapa na Printpak Tanzania Ltd., Dar es Salaam.

Kwa karne kadhaa wakoloni na wabaguzi wa rangi wamekuwa wakieneza fikara mbaya kwamba "Waafrika hawakuwa na historia" mpaka watu kutoka nchi za mbali walipoingia na kufanya biashara nasi au kututawala. Kwa wakoloni maana ya "historia" ni matukio ya kale na ya sasa ya Ulaya au yanayowahusu Wazungu, binafsi au kitaifa.

Wasomi wengi Waafrika kwanza waliikubali tafsari hii ya "historia", wakaisoma, wakaitetea na kuieneza. Historia ya Tanzania, kwa mfano, kwao ingekuwa kwanza historia ya Waarabu kwenye pwani ya Afrika ya Mashariki mpaka kuingia kwa utawala wa Wajerumani na Waingereza. Mengineyo juu ya Tanzania yasingeitwa historia wacha kusomeshwa.

Historia ya Mapambano ya Mwafrika kinachambua vizuri sana tatizo hili la "utovu wa historia ya Mwafrika" na hata kutupilia mbali maneno yaliyotumiwa kama vile "manegro, bushmen n.k." ambayo yamejaa kasumba ya kashfa dhidi ya Waafrika. Lakini zaidi ya hayo kitabu hiki kina uchambuzi madhubuti wa kudhoofishwa kwa maendeleo ya kijamii – kiuchumi ya Waafrika na wageni na jinsi gani Waafrika wanaweza kujikomboa kikamilifu.

Katika safu ya vitabu vya historia, *Historia ya Mapambano ya Mwafrika* ni kitabu cha lazima.

TANZANIA PUBLISHING HOUSE DAR ES SALAAM